

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Saba – Tarehe 19 Mei, 2015

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, jana kipindi cha saa tano asubuhi, Ndugu yetu Mwandishi wa Habari na Mtangazaji wa TBC, Kanda ya Kati alikuwa kazini. Bahati mbaya afya yake ikabadilika ikabidi akimbizwe kwenye dispensary yetu hapa. Walipojaribu kumsaidia kule hali ikaonekana inazidi kuwa mbaya akakimbizwa kwenye hospitali ya Mkao. Kwa bahati mbaya, saa tano usiku akawa ameaga dunia. Huyu kijana wetu anaitwa Samwel Chamlomo. Kwa hiyo, naomba tusimame dakika moja tumkumbuke kwa sababu alikuwa mwenzatu hapa.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge walismama kwa dakika moja kumkumbuka Ndugu Samwel Chamlomo)

SPIKA: Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi, amen. Ahsante, Katibu.

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na maoni ya

Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

SPIKA: Ahsante. Wale nitakaowaita kuwasilisha Hati zinazofuata watazisoma zote kama zilivyo, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI (ELIMU):

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 (*The General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Local Government Authorities for the Financial Year ended 30th June, 2014*).

Taarifa ya majibu ya Mpango Kazi ya Utekelezaji wa Hoja na Mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 (*The Responses and Action Plan for Implementation of Recommendations issued by the Controller and Auditor General Regarding Accounts of Local Government Authorities for the Financial year ended 30th June, 2014*).

Taarifa ya Majibu ya Mpango Kazi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2014.

Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

SPIKA: Ahsante. Naomba mjue tuko Bungeni hamuwezi kuwa mnacheka tu kwa nguvu, kumbe ni Tundu Lissu analeta matatizo. Yuko kule analeta matatizo mimi namuona. Mheshimiwa Tundu Lissu tunasema unaleta matatizo huko. Haya tunaendelea, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 (*The Annual General Report on the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Central Government for the Year ended 30th June, 2014*).

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Public Authorities and other Bodies for the Financial Year 2013/2014*).

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Financial Statements of Development Projects for the Year ended 30th June, 2014*).

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi wa Ufanisi Maalum kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Machi, 2014 (*The General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Financial Statements of Development Projects for the Year ended 30th June, 2014*).

Majumuisho ya Mpango Mkakati wa kujibu Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Wizara, Idara za Serikali na Mikoa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kitabu cha I na II (Volume I na II).

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Udhibiti wa Mifumo ya Mazingira katika Sekta ya Madini Tanzania kwa Mwaka 2015 (*A Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit on the Environmental Control Systems in the Mining Sector in Tanzania for the Year 2015*).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII):

A Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit Report on the Management of Demand Forecasting and Distribution of Essential Medicines and Medical Suppliers of Health Facilities in Tanzania for the Year 2014.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI:

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ufanisi wa Usimamizi wa Matengenezo ya Majengo ya Serikali kwa Mwaka 2015 (*A Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit Report on the Management of Government Buildings Maintenance in Tanzania for the Year 2015*).

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

A Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit on Provision of Extension Services of Farmers in Tanzania, Ministry of Agriculture, Food Security and Cooperatives and Prime Minister's Office, Regional Administration and Local Government Authorities for the Year 2015.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi wa Menejimenti ya Mipango Miji nchini Tanzania wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya Mwaka 2014 (*A Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit Report on Management of Urban Planning in Tanzania, The Ministry of Lands Housing and Human Settlement Development and Prime Minister's Office, Regional Administration and Local Government for the Year 2014.*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyowatangazia nadhani kwenye briefing na baadaye humu ndani kwamba leo tutakuwa na mgeni Rais wa Msumbiji.

Kwa hiyo, tukimaliza kipindi cha Maswali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais atasoma hotuba yake ya makadirio kwa muda wa dakika 45 halafu nitaahirisha kikao cha Bunge, tutakwenda kuwangoja wageni pale halafu kwenye saa tano na nusu tunaingia na mgeni Rais wa Msumbiji na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hoja ya kuwakaribisha wageni hawa ilishatolewa jana na ikapitishwa.

Baada ya yeye kulihutubia Bunge, tutasitisha shughuli, nadhani mnajua tofauti ya kusitisha na kuahirisha. Kwa hiyo, kutakuwa na kupiga picha pale na makundi mbalimbali halafu picha ya mwisho na Wabunge wote. Baada ya hiyo picha, Wabunge mnarejea ndani tunaendelea na taarifa za Kamati na za Upinzani. Kwa hiyo, tutakuwa tumekamilisha kipindi cha asubuhi halafu mchana tutaendelea na mjadala wa Wizara hii na kuhitimisha. Muda mwingi nimeutumia kusoma taarifa nyingi kwa hiyo, maswali yanaweza kubakia kwa sababu muda hautoshi, Katibu.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 43

Kuugawa Mkoa wa Morogoro

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA aliuliza:-

Mkoa wa Morogoro ni kati ya Mikoa mikubwa nchini uliobaki bila kugawanywa hivyo kuzorotesha maendeleo ya Mkoa na kusababisha umaskini kwa wananchi:-

(a) Je, ni lini Serikali itatangaza kuugawa Mkoa huo kwa kuzingatia maombi na mapendekezo ya RCC ya tangu mwaka 2013?

(b) Je, ni lini Serikali itaridhia mapendekezo ya kugawa Jimbo la Kilombero kuwa Majimbo mawili ili kusogezwa huduma kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Aloyce Kiwanga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo mapya ya utawala ikiwemo Mkoa na Wilaya huanzishwa kwa kuzingatia Sheria ya Uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya mpya (*the Regional and District Establishment Procedures Act No. 4, 1992*). Sheria hii imetaja vigezo na hatua za kufuata ili kuanzisha Mikoa na Wilaya mpya.

Mheshimiwa Spika, suala la kugawa Mkoa wa Morogoro liliibuliwa katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kilichokutana tarehe 10 Januari, 2014. Katika kikao hicho, ilipendekezwa uanzishwe Mkoa mpya wa Kilombero na kuagiza mchakato wa kitaalam ufanyike pamoja na kuwasilisha mapendekezo hayo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Hadi sasa, pendeleko hili halijapitishwa katika vikao vya kisheria ili kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi kwa kuzingatia vigezo na maoni ya vikao hivyo vya kisheria. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro imekwishaandaa Rasimu ya Andiko la Kugawa Mkoa ambayo itapelekwa kwenye vikao vya kisheria vya Serikali za Vijiini, Baraza la Madiwani, Kamati za Ushauri za Wilaya na Kamati za Ushauri ya Mkoa kama taratibu zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, pendeleko la kugawa Mkoa wa Morogoro litatekelezwa baada ya kukamilika kwa taratibu za vigezo hivyo kwa mujibu wa sheria na baada ya Mheshimiwa Rais kuridhia pendeleko hilo la kuzingatia Ibara ya 2(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kugawa Majimbo ya Uchaguzi uko chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hadi sasa mapendekezo ya kugawa Jimbo la Kilombero yameshapitishwa kwenye vikao vyote vya kisheria vya ngazi ya chini vikiwemo Kamati ya Mipango na Fedha, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa RCC. Hivyo, maamuzi ya kugawa Jimbo hilo yatafanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo ndiyo yenye dhamana ya kugawa Majimbo ya uchaguzi kwa mujibu wa sheria.

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Mkoa wa Morogoro mchakato kama alivyojibu ni kweli na kwa kuwa katika vikao RCC mara nyingi kumetokea ubishani kati ya Wilaya ya Ulanga ambapo Wilaya hiyo inatakiwa iwe na Wilaya mbili, Jimbo la Ulanga Mashariki na Ulanga Magharibi lakini inaonekana kuna mgogoro na wananchi wa Lupilo washaamua kwamba wao wanataka kubaki Ulanga Magharibi.

Je, Serikali sasa haioni kwamba kuna haja ya kwenda kule Ulanga kukaa na wananchi ili wamalize mgogoro wao kati ya Majimbo haya mawili, Wabunge wawili, Mheshimiwa Celina Kombani na Mheshimiwa Mponda ili sisi watu wa Morogoro tupate Mkoa kwa sababu tunateseka na ukubwa mkoa huo?

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kweli utaratibu wa kugawa Jimbo la Kilombero unaafanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi lakini nashukuru sasa kwa kuwa ofisi ya Mkoa imeshafanya taratibu zote na tuna imani kwamba Jimbo la Kilombero litagawiwa kutokana na vigezo vilivyotimizwa, ahsante.

SPIKA: Kwa hiyo? Mheshimiwa naomba ujibu swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Mheshimiwa Spika, kwanza, suala la kukamilisha taratibu za kuugawa Mkoa wa Morogoro kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi na kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amekiri kwamba bado kuna tatizo liko kule ndani, lakini taratibu zetu ni kwamba mpaka ninyi wenyele mlioko

pale mnactaka mabadiliko hayo mridhie mabadiliko hayo. Kwa hiyo, bado jukumu hilo liko ndani ya Mkoa wa Morogoro kupitia vikao vyake lakini kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameonyesha kwamba liko tatizo na kwamba linahitaji pia labda sisi tuingilie, basi nitawasiliana na Katibu Tawala wa Mkoa leo ili tuone umuhimu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda kuona jambo hilo pale Ulanga na zile Wilaya za Waheshimiwa Wabunge wawili ili sasa tupate muafaka wa namna ya kuugawa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, kwa kuwa amekiri kwamba mchakato huu wa Jimbo umeendelea vizuri na bado wenye mamlaka kugawa Jimbo ni Tume ya Uchaguzi, tuendelee kusubiri maamuzi ya Tume ya Uchaguzi wanavyo vigezo na wana mapitio ambayo wanajiridhisha ili wakisharidhika waweze kuridhia basi tuendelee kusubiri hilo. Kwa kuwa wao ndiyo wenye mamlaka na sisi hatuna uwezo wa kuwataka wafanye hilo kwa haraka, naamini jambo hili litaenda vizuri.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Uratibu na Bunge).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERNA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini nataka tu niongeze majibu katika swali la nyongeza. Mheshimiwa Mbunge amesema baada ya Mkoa kukamilisha kupitia vigezo vyote na taratibu zote kuwa tayari, ana uhakika sasa Jimbo lile limegawanya.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka record vizuri katika Bunge lako Tukufu, naomba kusema kwamba Tume ya Uchaguzi itapokea mapendekezo hayo, lakini bado Tume ya Uchaguzi inatakiwa kujithibitishia na kufanya ukaguzi yakinifu kuthibitisha yale yote yatakayokuwa yamepelekwa katika Tume na hatimaye kupitia vile vigezo na ndipo itakapoweza kutamka kwamba Jimbo hili sasa linaweza kugawanywa. Napenda kulifanya Bunge lako lielewe kwamba mchakato ukishaisha kwenye ngazi ya Mkoa siyo kwamba sasa tayari kila kitu kimeshatokea. Kwa hiyo, waendelee kusubiri, Tume ya Uchaguzi kama ilivyosema na sisi tulivyotoa taarifa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutayapitia hayo maombi yote na tutafanya kazi hiyo kwa usawa na kwa kuzingatia mahitaji halisi na vigezo vilivywewka na Serikali.

SPIKA: Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt Mbassa, safari hii Mheshimiwa Dkt. Mbassa uko very active. (Kicheko)

Na. 44

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari wa Pili (MMES II)

MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA (K.n.y. MHE. CHTISTOWAJA G. MTINDA) aliliza:-

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari wa Pili (MMES II) ulioanza mwaka 2011/2012-2015/2016 unalenga kutoa Tshs.25,000/= kwa mwaka kwa kila mwanafunzi wa shule za sekondari za Serikali nchini:-

(a) Je, mpango huo umefanikiwa kwa kiasi gani nchi nzima?

(b) Je, mpaka sasa Halmashauri ya Wilaya ya Singida imeshapokea kiasi gani cha fedha tangu mpango huo uanzé?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), Serikali hutenga fedha za ruzuku ya uendeshaji kwa shule za sekondari kwa kiwango cha shilingi 25,000 kwa mwanafunzi kwa mwaka. Serikali imefanikiwa kutekeleza mpango huu kwa kuweza kutoa fedha kila mwaka kulingana na makusanyo na kuimarisha upatikanaji wa vitabu hadi kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu. Mfano, mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali ilitoa shilingi bilioni 33.2 sawa na shilingi 22,736.63 kwa mwanafunzi kwa mwaka. Mwaka wa fedha 2012/2013 zilitolewa shilingi bilioni 22.4 sawa na shilingi 14,750 kwa mwanafunzi kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango huu, Serikali inashirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo. Mchango wa Serikali kifedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ni pamoja na ujenzi wa nyumba za Walimu, maabara, vyumba vya madarasa, ununuvi wa madawati, ukarabati wa majengo na ruzuku ya uendeshaji. Tangu mwaka 2011 hadi sasa, Halmashauri ya Wilaya ya Singida imeshapokea fedha za uendeshaji kwa shule za sekondari jumla ya shilingi bilioni 1.02.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango huu, Serikali hivi sasa imeamua kutenga asilimia 50 kwa shule za sekondari na asilimia 40 kwa shule za msingi ya fedha ya uendeshaji kwa shule kwa kununua vitabu kwa pamoja badala ya kuzipeleka shulenii ili Wakuu wa Shule wanunue vitabu. Kwa hiyo, kiasi kinachotolewa katika Halmashauri kinakuwa pungufu ya kile kilichotengwa kwa ajili ya ununuvi wa vitabu.

SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa Dkt. Mbassa.

MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika majibu ya msingi inaonekana pesa hizi zinazopelekwa katika Halmashauri hii ya Ikingu ambayo sasa ina Majimbo mawili haziwezi kutosheleza na hazijatosheleza mahitaji ya shule. Mheshimiwa Waziri anawahakikishiaje sasa kwamba katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 pesa hii itapelekwa kwa ukamilifu wake?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa mazingira ya pesa hizi ni sawasawa na mazingira yaliyoko katika Wilaya ya Biharamulo na Halmashauri nyingine zote ziwazo kwani mpango huu umekuwa haueleweki vizuri sana kwa Walimu. Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha hizi kwa ukamilifu wake, kwani zinapotolewa na wafadhili zinatolewa kwa ukamilifu na siyo kwa upungufu? Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Mheshimiwa Spika, mgao wa Wilaya ya Ikingi unakwenda kama mgao wa Halmashauri yenyewe ya Ikingi pamoja na kwamba Halmashauri hiyo imegawiwa kutoka Singida Vijiji kwa sababu fedha zile zinakwenda kwenye shule. Kwa hiyo, bado Wilaya ya Ikingi ilikuwa na shule zake hata kama ilikuwa ndani ya Wilaya ya Singida bado shule zilizoko ndani ya Wilaya ya

Ikingu sasa zimetengwa na fedha hiyo inapelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ikingu, kwa hiyo, mgao unaenda.

Mheshimiwa Spika, suala la mgao huu kueleweka vizuri kwa Walimu, utaratibu huu ulishatolewa na uko wazi lakini si tu Walimu mpaka Kamati za Shule kwa shule za msingi au Bodi kwa shule za sekondari. Fedha hizi zinapopelekwa zimegawiwa kwenye mgao. Kwa fedha za sekondari zimegawiwa katika maeneo mawili, asilimia 50 ya fedha yote lazima inunue vitabu vile ambavyo Walimu wanahitaji kuvitumia kwa ufundishaji. Asilimia 50 nyingine ni ya vifaa vingine vyta ufundishaji pamoja na eneo la michezo. Kwa hiyo, mgao huu uko wazi na masharti fedha hii inapoletwa lazima iandikwe kwenye ubao wa matangazo ili pia hata wanafunzi waone mgao umefika na mgao huo uko kwenye zile asilimia.

Mheshimiwa Spika, lakini ambacho tumekifanya sasa, kwa kuwa tumegundua sehemu kubwa ya Walimu wanaingia kwenye matatizo makubwa ya matumizi ya fedha ya ununuvi wa vitabu vyta shulenii na kwa kuwa vitabu hivyo sasa havipatikani shulenii, tumeamua ku-centralize ile 50% ya sekondari na 40% ya shule za msingi kununua vitabu centrally na kuwapelekea vitabu. Jambo hili ndiyo limetuletea mafanikio sasa ya kupunguza uwiano wa mwanafunzi na kitabu na hali itaendelea tukichanganya na fedha ambayo tunaweka kwenye bajeti ya Wizara, sasa hivi uwiano wa kitabu na mwanafunzi unaendelea kuimarika. Malengo yetu, kitabu kimoja kwa mwanafunzi katika kila somo na itawezekana.

SPIKA: Tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, kwa niaba yake Mheshimiwa Esther Bulaya.

Na. 45

Wanawake Kushiriki katika zoezi la Kupanda Miti

MHE. ESTHER A. BULAYA (K.n.y. MHE. AMINA N. MAKILAGI) aliuliza:-

Wanawake ni kiungo katika familia na wamekuwa wakifanyiwa vitendo vyta ukatili wakati wa kutafuta kuni za kupikia:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kushirikisha wanawake katika suala la upandaji miti ili waepukane na adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta kuni?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wanawake wanaotumia kuni kwa muda mrefu na kipelekeea macho yao kuwa mekundu na hivyo kupata tatizo la ukatili wa kuuawa kwa imani za kishirikina?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua adha wanayopata wanawake hususani walioko vijijini katika kutafuta nishati ya kuni na pia madhara wanayoyapata wanawake kutookana na

moshi wa kuni ikiwemo matatizo ya macho kuwa mekundu na hivyo kusababisha baadhi yao kuwawa kwa imani za kishirikina katika baadhi ya Mikoa nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na matatizo hayo, Serikali imechukua hatua za kushirikisha wanawake na jamii kwa ujumla katika upandaji miti kwa lengo la kuongeza misitu. Serikali ilianzisha kampanya ya kitaifa ya upandaji miti mwaka 1998 ambapo Halmashauri zote nchini zinatakiwa kupanda miti milioni moja na nusu kila mwaka kwa kushirikisha taasisi na wananchi wote ikiwemo wanawake.

Mheshimiwa Spika, vilevile kupitia utekelezaji wa mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji wa mwaka 2006, taasisi za umma na binafsi na wananchi wote kwa ujumla wakiwemo wanawake pia wanahimizwa kuanzisha maeneo ya mashamba ya miti kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa.

Aidha, kupitia tuzo ya Rais ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kupanda na kutunza miti, wananchi wote wakiwemo wanawake wamepewa fursa ya kushikiri kupanda miti ili kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, kupitia miradi ya kuhifadhi mazingira inayotekeliza nchini, wanawake wanaelimishwa, wanahamasishwa na kuwezeshwa kutumia majiko banifu na sanifu. Aidha, Serikali imeendelea kusisitiza matumizi ya nishati mbadala kama vile mafuta ya taa, gesi, samadi, makapi ya mazao na nishati ya jua. Serikali pia imeendelea kusimamia uamuza wake wa mwaka 2012/2013 wa kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani katika vifaa vya gesi na umeme ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

SPIKA: Ahsate. Mheshimiwa Esther Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri Masele kwa majibu yake mazuri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa sababu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) tunajua ina programu kwenye Magereza ya kuhamasisha ujenzi wa majiko banifu ambayo yanatumia kiasi kidogo cha kuni. Tunawajua akina mama wa Tanzania na wa Mkoa wa Mara kwa ujumla, kwanza wanapenda utunzaji wa mazingira lakini wamejiunga kwenye vikundi mbalimbali. Je, Serikali kupitia Ofisi ya Mazingira, kupitia vikundi vya akina mama, ina mkakati gani wa kuwasaidia ili na hawa akina mama waweze kimiliki hayo majiko banifu na waweze kutumia kiasi kidogo cha kuni ili waweze kutunza mazingira?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nilikuwa nataka kujua, kumekuwa na mabadiliko ya tabia nchi kwa kasi lakini kwa mujibu wa sheria, Ofisi ya Mazingira inapaswa kutoa Ripoti ya Mwaka ya Mazingira kila baada ya miaka miwili. Hivi tunavyoongea, Ofisi ya Mazingira imekaa miaka sita bila kutoa taarifa hiyo na imetoea mwaka jana. Nataka njue, ni sababu gani za msingi zilizopelekea wamevunja sharia kwa kutotoa Taarifa ya Mazingira kwa mujibu wa sheria?

SPIKA: Haya, naomba majibu kwa kifupi, muda umeisha.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyooleza kwenye majibu ya msingi Serikali inahamasisha wananchi wakiwemo wanawake kutumia majiko banifu na mimi naunga mkono jitihada za wanawake wa Mkoa wa Mara za kutengeneza majiko haya.

Mheshimiwa Spika, malengo makuu ya Serikali ni kuondokana kabisa na matumizi ya mkaa pamoja na kuni na ndiyo maana kuna msukumo mkubwa kabisa wa kuelekeza nishati

vijiji pamoja na matumizi ya nishati ya gesi na hivyo tuna mpango pia wa kuhakikisha kwamba sehemu zote zenye mikusanyiko mikubwa ikiwemo baa, magereza, hoteli na taasisi nyingine waelekee kwenye kutumia majiko ya gesi ili kupunguza kabisa matumizi ya mkaa na kuni ili kuendelea kutunza mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli ripoti hii imetoka kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Kwa kweli sina majibu sahihi ya kusema kwa nini haikutoka huko nyuma lakini nachoweza kusema kwamba ripoti hii imetoka na tutaendelea kufuata sheria kutoa ripoti hii kwa wakati.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mkosamali, swali kwa kifupi!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ni kweli tunatamani mazingira yatunzwe na yaendelee kuwa vizuri lakini sasa hivi Kibondo na maeneo mengine ya Kanda ya Ziwa, Wizara ya Maliasili wamepandisha ushuru wa mkaa kutoka Sh.3,000 kwenda Sh.15,000. Kwa hiyo, hawa akina mama wananyanyaswa sana, wanakamatwa na Polisi na kupigwa. Haiwezekani mtu wa kijiji aliye Sh.15,000 kwa gunia la mkaa. Tunaomba majibu ya Serikali juu ya jambo hili, *it is an impossible thing*, haiwezekani!

SPIKA: Lakini si wamepandisha kwenu huku? Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, kama ni jambo la kuwapongeza watu wa Kasulu hili ni mojawapo, ni jambo zuri sana. Mkaa unasababisha uharibifu mkubwa sana wa mazingira, mkaa ndiyo umesababisha ukataji wa miti hovyo, matokeo yake ndiyo tunapata mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanababisha mabadiliko ya mifumo ya hali ya hewa katika uso wa dunia na ndiyo tunapata mafuriko na madhara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la msingi hapa ningeshauri wananchi watumie nishati mbadala na haya majiko...

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Naomba mnisikilize.

SPIKA: Hapa tunajibu maswali hatuko sokoni, Waziri endelea kujibu swali.

MBUNGE FULANI: Gesi iko wapi sasa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie majibu.

SPIKA: Wewe endelea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Yako majiko yanauzwa Sh.25,000 yanayotumia mkaa kidogo sana ambapo unaweza ukauza jogoo wawili tu ukanunua hilo jiko.

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Kwa utafiti tuliofanya inaonyesha kwamba majiko ya gesi bado bei yake ni nafuu. Kwa hiyo, naomba niendelee kusisitiza kwamba matumizi ya mkaa hatuya-encourage kwa sababu yanaharibu vyanzo vya misitu. (Makofii)

SPIKA: Umejibu vizuri Mheshimiwa Waziri, sasa mlikuwa mnauliza swali la nini kama hamtaki majibu. (Makofii)

Sasa tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu)

SPIKA: Midomo hiyo, hakuna maendeleo kwa midomo.

Na. 46

Uharibifu wa Mazingira Mkao wa Mbeya

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA aliuliza:-

Mkao wa Mbeya umezungukwa na milima ambayo ndiyo chanzo cha maji Mkoani humo lakini kumekuwa na tabia za makusudi za kuchoma moto misitu ovyo kwenye misitu inayozunguka milima hiyo na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na vyanzo vya maji.

Je, Serikali ina mpango gani endelevu wa kuzuia uharibifu huo unaoendelea mara kwa mara?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uchomaji moto misitu katika milima inayozunguka Mkao wa Mbeya kutokana na shughuli za kilimo, ufugaji, uwandaji, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na kadhalika na hivyo kusababisha uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji katika milima hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongeza kwa uharibifu wa vyanzo vya maji nchini, Serikali ilipitisha mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji unaoelekeza Halmashauri zote nchini kudhibiti uchomaji wa misitu katika maeneo yao ikiwemo katika Mkao wa Mbeya. Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania imeendelea kuchukua hatua katika kusimamia uhifadhi wa misitu ya Mlima Mbeya kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu ya Mlima Mbeya kwa wananchi wa Kata kumi zinazozunguka misitu hiyo kwa kuwashirikisha viongozi wa ngazi zote za Serikali Mkoani Mbeya;

(ii) Kuandaa miche ya miti na kipanda katika meneo yaliyoathiriwa ili kurejesha uoto wa asili katika maeneo hayo;

(iii) Kutengeneza barabara za kuzuia moto katika maeneo ya misitu hiyo yanayoathiriwa mara kwa mara na moto; na

(iv) Kuanzisha miradi ya vipato mbadala kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka misitu hiyo kama vile ufugaji nyuki na kilimo cha matunda.

Mheshimiwa Spika, ili kupata ufumbuzi wa kudumu Serikali ilizindua mpango endelevu wa uhifadhi wa msitu wa Mlima Mbeya mwezi Machi, 2015. Utekelezaji wa mpango huu unashirikisha wadau mbalimbali pamoja na wananchi wanaozunguka msitu huo. Lengo la mpango huu ni kuhakikisha changamoto zinazokabili msitu wa Mlima Mbeya zinapatiwa ufumbuzi ikiwemo matatizo ya uchomaji moto.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, swali la nyongeza.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza pamoja na majibu yanayoridhisha sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mbeya geographically ni wa milima, misitu, *fertile soil* pamoja na *green land* lakini cha ajabu ni kwamba bado hali ya mazingira hairidhishi pamoja na kwamba Mkuu wa Mkoa aliweza kuunda na kuzindua Kamati ya Mazingira miezi minne iliyopita. Nilikuwa nataka tu kujua nini mkakati wa Serikali katika kuwapatia fungu wana Mbeya katika mapambano haya ya utunzaji wa mazingira?

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna ule mradi wa *Tanzania Strategic Cities Project* kwenye udhibiti wa taka ngumu. Jiji la Mbeya tumeshajenga dampo la kisasa kabisa pale Nsalaga lakini bado halijaanza kutumika kwa ajili ya *sanitary landfill*. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kujua tu Serikali italeta lini mitambo hii pamoja na zile gari zake ili udhibiti huu wa taka ngumu katika kutunga mazingira uanze?

Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba majibu. Ahsante.

SPIKA: TAMISEMI mtakuwa na sehemu ya kujibu? Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa kwa kazi nzuri anayofanya ya kuwatafutia maendeleo wananchi wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, katika swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanjelwa, katika mradi huu wa taka ambaa ameueleza, kimsingi tunashirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha kwamba tunatunza mazingira. Mradi huu katika utekelezaji wake tunashirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhakikisha kwamba vifaa vyote vinavyohusika ili mradi huu uweze kuanza vinapatikana kupita kwenye bajeti ya Halmashari. Wajibu wa Ofisi ya Makamu ya Rais katika miradi hii ni ku-coordinate zaidi.

Mheshimiwa Spika, natumaini kwamba Mheshimiwa Mwanjelwa atashirikiana na Madiwani wenzake katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhakikisha kwamba mradi huu unaanza mara moja.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, sehemu ya pili.

WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, nataka nichukue fursa hii kwanza kulipongeza sana Jiji la Mbeya kwa kuanzisha mradi mkubwa sana wa dampo

ambao kwa bahati nzuri mimi nimetembelea na vifaa vya mradi ule vinaanza kuingia mwezi wa saba na vikishaingia, vitaanza kufungwa na kuanza kutumika. Kwa hiyo, nataka niwashukuru sana TAMISEMI pamoja na Jiji la Mbeya na ningeshauri sana miji mingine mikubwa iige mfano wa Jiji la Mbeya wa kutenga fedha kwenye bajeti zao kwa ajili ya miradi mikubwa kama hii.

SPIKA: Ahsante. Twende sasa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, kwa niaba yake Mheshimiwa Ismail Rage.

Na. 47

**Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
Kuchelewasha Utoaji wa Mizigo Bandarini**

MHE. ISMAIL A. RAGE (K.n y. MURTAZA A. MANGUNGU) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa mwongozo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kurahisisha utoaji mizigo bandarini.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali kwa wadau wa bandari ikiwemo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji mizigo bandarini. Mionganoni mwa miongozo iliyokwishatolewa na Serikali, ni pamoja na kuanzisha Kamati Maalum ya Kushughulikia Uboreshaji wa Shughuli za Bandari (*Port improvement Committee*) ambayo hukutana kila baada ya wiki mbili. Kamati hii inaundwa na wadau wote wanaohusika na utoaji mizigo bandarini kama vile Mamlaka ya Bandari (TPA), TRA, Kampuni ya Upakuaji wa Mizigo Bandarini (TICTS), Umoja wa Mawakala wa Forodha (TAFFA), Tasisi zote za Serikali zinazohusika na utoaji wa vibali kwa bidhaa ziingiazo nchini na wamiliki wa sehemu za kuhifadhi mizigo nje ya bandari (*internal container depots*).

Mheshimiwa Spika, hatua zingine ni pamoja na utaratibu wa kufanya kazi na kutoa mizigo bandarini kwa saa 24 pamoja na siku za Jumamosi, uanzishwaji wa bandari za nchi kavu (*inland container depots scheme*) kwa walipa kodi wakubwa, sambamba na kuidhinisha utoaji wa mizigo ndani ya saa 24. Aidha, utaratibu wa kufanya tathmini ya muda unaotumika kutoa mizigo bandarini kila baada ya miezi mitatu pamoja na kuanzisha mifumo mipya ya forodha kama vile TANCIS (*Tanzania Customs Integrated Systems*) imesaidia sana kujenga mazingira ya kurahisisha utoaji mizigo bandarini.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi kwa pamoja zimesaidia sana kurahisisha utoaji wa mizigo bandarini na hivi sasa wastani wa mizigo kukaa bandarini ni chini ya siku tisa ikililinganishwa na siku 21 mwaka 2008 na wastani wa siku 11 mwaka 2013.

SPIKA: Mheshimiwa Rage, swalii la nyongeza.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu ya hekima na yanayoelewaka.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ucheleweshaji ninaolalamikia hapa wakati mwingine ni kwa sababu ya TRA, Bandari na TICTS lakini anayekuja kuadhibiwa ni mto mzingo. Kwa nini hii gharama isiwe shared kuliko kumtupia burden yote mwenye mzingo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sasa hivi tuna matatizo ya ajira lakini bado tuna makampuni ya kigeni yanayofanya *clearing* pale bandarini. Je, hatuoni ni wakati muafaka sasa kazi hii ikafanywa na Watanzania peke yake?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Spika, kwanza lazima nikubali kwamba pamoja na utaratibu ambao tumejaribu kuweka na uwepo wa hii system mpya TANCIS, utaratibu wa *pre-arrival declaration system* ambapo unapitia kwa wakala wako kabla mzingo haujafika ili taratibu ziwe zimeanza, unakusudia kufanya siku nne au tano mzingo ule uwe umetoka. Mheshimiwa Rage (Rais Mstaifu wa Simba) amesema kwamba wakati mwingine ucheleweshaji unatokana na mifumo yenye kuwa haina ufanisi mkubwa, ni kweli. Wizara yangu imeielekeza TRA na hili naomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania walifahamu, kuweka mfumo ambao unakuwa na haki kwa pande zote mbili. Kwa hiyo, kama ikionekana kwamba kweli wewe umeweka *pre-assessment declaration form* yako na hakuna tatizo katika *form* yako, ulikuwa unatakiwa mzingo wako uwe umetoka ndani ya siku nne, tano, sita, siku 10 bado haujatoka kwa sababu ya matatizo ya mtandao, hili ni jambo ambalo lazima dhamana ibebwe na wale ambao wameshindwa kutekeleza wajibu wao. Kwa hiyo, naomba liendelee kwa sababu kuna utaratibu wa mteja kulalamika na kupatiwa haki yake, hili tutalifanyia kazi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hili la pili ni kwamba yule mteja mwenyewe anachagua wakala wa kumwakilisha pale. Kwa hiyo, kama *clearing and forwarding agents* ni ya wageni lakini wewe kwa nafsi yako umeona ndiye atakusaidia ku-clear mzingo wako mapema hukatazwi kukubaliana naye. Hata hivyo, sasa hivi tuna usajili wa *Clearing and Forwarding Agents (CFAs)* ambao ni wazawa wengi tu na wana uwezo mkubwa. Kwa hiyo, nashauri muwatumie hawa wazawa ili nao waendelee kujenga uwezo na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali la Wizara ya Afya, Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 48

Vipaumbele vya Sekta ya Afya

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Sekta ya Afya imeingizwa katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN):-
Je, nini vipaumbele vya sekta hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa unaanza kutekelezwa katika sekta ya afya katika mwaka huu wa fedha 2015/2016. Mpango huu unalenga kutekeleza na kutimiza malengo yaliyoainishwa katika muda mfupi, kwa maana ya *short time period* na mkakati wa BRN uliana kutekelezwa mwaka 2012 kwa lengo la kuongeza kasi ya utekelezwaji wa vipaumbele vya kitaifa ili kufikia malengo yaliyowekwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya sekta ya afya katika Matokeo Makubwa Sasa ni vinne, navyo ni vifuatavyo:-

Moja, utendaji wa kufikia malengo (*performance management*) wa vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi za Halmashauri yaani hospitali, vituo vya afya na zahanati katika Mikoa 11 ya kipaumbele. Mikoa hiyo ni Kagera, Shinyanga, Tabora, Singida, Katavi, Kigoma, Geita, Mwanza, Simiyu, Pwani na Dar es Salaam. Vigezo viliviyotumika kwa kupata Mikoa hii ya kipaumbele ni kuwa na upungufu mkubwa katika mifumo ya utoaji huduma za afya katika Mikoa hiyo. Pia kuwepo kwa majoribio ya kuboresha mifumo ya utoaji wa afya kwa Mikoa miwili ya Pwani na Dar es Salaam.

Mbili, ni kuboresha kiwango cha Idara za watumishi wa Afya na Ustawi wa Jamii katika Mikoa tisa ya kipaumbele ambayo ni Kagera, Shinyanga, Tabora, Singida, Katavi, Kigoma, Geita, Simiyu na Rukwa. Kigezo kilichotumika kupata Mikoa hii ya kipaumbele ni kuwepo kwa upungufu mkubwa chini ya kiwango cha kitaifa kwa wafanyakazi hao wa sekta ya afya katika Mikoa hiyo.

Tatu, ni upatikanaji wa dawa muhimu, vitendanishi na vifaa vinginevyo vya matumizi katika hospitali za Halmashauri, vituo vya afya na zahanati kwa nchi nzima.

Mwisho, ni afya ya uzazi, mama na mtoto katika Mikoa mitano ya kipaumbele. Mikoa hiyo yenye kipaumbele ni Kigoma, Geita, Mwanza, Simiyu, na Mara. Kigezo kilichotumika hapa kupata Mikoa ya kipaumbele ni kuwepo kwa idadi kubwa ya vifo vya mama na watoto wachanga juu ya kiwango cha kitaifa.

SPIKA: Mheshimiwa Kabati swalii la nyongeza.

MHE. RITA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo ya nyongeza mawili. Nimshukuru pia Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Mkoo wetu wa Iringa uko katika Mikoa ya vipaumbele vya BRN lakini umekuwa na shida sana hasa kutoekana na ufinyu wa bajeti za hospitali zetu za Rufaa na Mkoo na kusababisha kuwa na madeni makubwa sana ya maji, umeme, dawa na ukosefu wa vifaa tiba. Je, ni lini Serikali itakuwa na mpango wa kuanzisha akaunti maalum ya afya ya Mikoa au kuzi-ring-fence zile fedha za OC?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, katika utelekezaji wa Matokeo Makubwa Sasa, Serikali ina mpango wa kupunguza vifo vya mama na mtoto lakini Mkoo wetu wa Iringa bado kuna ukosefu mkubwa sana wa magari katika hospitali zetu zote za Wilaya na Mkoo pia. Pia kumekuwa na ukosefu wa magari kwa ajili ya kusambazia chanjo ya mtoto na mama. Je, ni lini Serikali sasa itatekeleza ahadi yake ya kutuletea magari katika hospitali zetu zote za Wilaya na Mkoo? Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII): Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Wizara ya Afya iliona umuhimu mkubwa wa kutafuta namna nyingine ya kuongeza uwepo wa fedha kwenye sekta hii ili kuweza kutoa tiba stahili. Mpango ambao tunao sasa ni ule wa Bima ya Afya ambapo pia kazi inayofanya ni kuona ni namna sahihi ya kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kutoa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya hospitali zetu kuanzia zahanati mpaka hospitali zetu za Mikoa ili kuongeza pia utoaji wa dawa na huduma nyingine kwenye eneo hili. Kwa hiyo, mkakati wa kuanzisha mfuko wa tiba, tumeanza na hiyo lakini hatujaishia kwenye ngazi ya Taifa tu tumeshuka mpaka kwenye ngazi ya jamii ambako tumeendelea kuhamasisha kwa pamoja na Ofisi ya Waziri Mkoo, kuwa na Mfuko wa Jamii (CHF) ambapo wananchi huchangia na wanapochangia kiwango ambacho Halmashauri ya Wilaya kinakusanya Bima ya Afya nao wanaweka top up ya asilimia 100 ya mchango ule ili kuweza kuongeza kiwango cha upatikanaji wa dawa na tiba kama ambavyo tumeeleza.

Mheshimiwa Spika, suala la kukosekana kwa usafiri wa magari ya ambulances kwenye maeneo yetu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa pamoja na Ofisi ya Waziri Mkoo, TAMISEMI, ambako hospitali hizi ziko kwenye maeneo ya Ofisi ya Waziri Mkoo, TAMISEMI, tumetenga bajeti kwa pamoja na Wizara ya Afya. Taarifa ambazo tunazo sasa, walishawahi kuagiza magari 50, ambayo bado hayajafika na yatakapofika yataanza kusambazwa lakini kwa ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkoo, TAMISEMI nayo katika mipango yake huwa tunanunua ambulance. Kwa hiyo, tutaona mahitaji ili kubaini Mkoa wa Iringa tunaweza kupeleka ngapi kwa ajili ya huduma hizo.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu.

Na. 49

Sheria ya Haki za Wazee

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU aliuliza:-

(a) Je, Serikali itawasilisha lini Bungeni Sheria ya Haki za Wazee ikiwa ni pamoja na haki ya matibabu kama ilivyokwishaahidi?

(b) Je, ni kwa nini Serikali inashindwa kusimamia kauli zake katika suala la matibabu kwa wazee ambao wananyanyapaliwa kupata huduma hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Henry D. Shekifu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa haki za wazee ikiwa ni pamoja na kutungwa kwa sheria itakayosimamia haki za wazee nchini kote. Tangu mwaka 2007, Wizara ilipitia hatua mbalimbali ili kupata idhini ya kutungwa kwa Sheria ya Haki za Wazee. Hatua mojawapo ilikuwa ni kupeleka rasimu kwenye Kabineti Sekretarieti ambayo nayo ilitoa mapendekezo ya kuongeza vipengele kadhaa ikiwemo kupata maoni ya wadau muhimu.

Mwezi Aprili, 2012, maoni ya wadau yalipatikana na hivyo kuwezesha kupatikana kwa rasimu itakayopelekwa kwenye Kabineti Sekretarieti ili kupata idhini ya kutungwa kwa Muswada wa Sheria hiyo. Serikali inatarajia kuwasilisha Muswada wa Sheria hii Bungeni katika mwaka ujao wa fedha wa mwaka 2015/2016.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika kuhudumia wazee wote nchini, Wizara inaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Mji na Vijiji ili kuhakikisha kwamba wazee wanapatiwa vitambulisho vinavyothibitisha umri wao, kitu ambacho mara nyingi kinachangia wazee kupata usumbufu usio wa lazima pindi wanapohitaji huduma za matibabu. Aidha, Wizara inaboresha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Shekifu, swali la nyongeza.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutangaza kwamba kuanzia mwaka kesho, Serikali inachukua jukumu la kuwashudumia wazee. Naomba Serikali yetu ilione hilo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tatizo la wazee ni la muda mrefu na hata ukiangalia majibu yanaonyesha suala hili lilianza kushughulikiwa kuanzia mwaka 2007 mpaka leo. Nina uhakika hata tungefanya nini, bila sheria mahsusii itakayowashughulikia wazee suala hili haliwezi kupata msisitizo. Sasa nauliza, Serikali imeahidi, ni kweli, je, wanatuhakikisha nini kwamba sasa mwaka ujao ndiyo utakuwa wa mwisho na Serikali itawajibika kwa kutoleta sheria?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wako wazee wa kundi la waliokuwa watumishi wa Serikali, kiwango cha chini cha pensheni ni Sh.50,000/= sawa na dola 25 na kwa bahati mbaya wazee hawa ni wale ambao wametumikia Taifa hili muda mrefu na ni wazee sana sasa. Serikali inatamka nini kuhusu kupandisha kima cha chini cha pensheni kilingane angalau na mahitaji ya wazee ya kuishi? (Makofii)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la pili hili la pensheni. Hili jambo tumeshalizungumza hapa Bungeni mara kadhaa na Serikali ilichosema kwamba ni kweli pensheni kwa sasa hivi ni ndogo hasa kwa wale wazee ambao hawakuwahi kuchangia ama walichangia kwa kiasi kidogo sana. Kwa hiyo, ni lazima tutambue kwamba kama tunalipa pensheni sasa hivi kadri tunavyopandisha maana yake tunailipa ile pensheni kwa watu ambao hawakuchangia pensheni ile. Kwa hiyo, inatokana na michango ya wale ambao wamechangia hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba tathmini hii ni ya kitaalam, inafanywa na vyombo vya pensheni na Serikali na tunaendelea kuifanyia kazi kwa lengo la kuhakikisha kwamba kwa namna yoyote ile inayowezekana tuweze kunyanya kale ka-pensheni kidogo kwa wazee hawa ili na wao waweze kuishi miaka yao ya mwisho wakiwa na uwezo mkubwa zaidi. Hata hivyo, tunaendelea kusema ni jambo la kitaalam, linahitaji tathmini kubwa ili kutokuharibu uwezo wa kulipa pensheni wanaochangia sasa utakapofika muda wao wa kulipwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Kwa kifupi sehemu ya kwanza ya swali maana muda umekwisha kabisa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII): Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Shekifu kwa namna ambavyo anafuatilia hata pale kwenye Halmashauri yake kwa sababu leo hii tukiwa tunaendelea na kuandaa Muswada wa Sheria na kufikia hatua ya kuwa na sheria ya kuendelea kuwahudumia wazee hawa na inawezekana pia tukafikia hatua ambayo Zanzibar wameifikia, hospitali ya Wilaya ya Lushoto wamekwenda mbali sana. Kwanza wamefungua Dirisha Maalum kwa ajili ya kuwahudumia wazee lakini pili, wametenga Daktari kwenye dirisha lile anayehudumia wazee wakati wote. Tatu, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto wamemudu kuandikisha na kupiga picha na kutoa vitambulisho kwa wazee zaidi ya 3,000, ni maendeleo makubwa sana. Kwa hiyo, jitihada hizi ni nzuri na Wilaya nyininge zote nchini ziige utaratibu ambao tayari wameufikia Halmashauri ya Lushoto ili wazee hawa wasipate matatizo kwenye maeneo yetu. Jambo hili kila Halmashauri ikizingatia na zikatekeleza utaratibu huu kama Lushoto, tunaweza tukaondoa mgogoro, mgongano na matatizo tunayoyapata kuwahudumia wazee wetu nchini kote.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dokta Goodluck Joseph Ole-Medeye.

Na. 50

Fidia kwa Wananchi Waliopisha Ujenzi wa Barabara

MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE MEDEYE aliuliza:-

Mwaka 2012 Serikali iliwapa taarifa wakazi wa Kata ya Oldonyosambu kuondoa maendelezo yote kwenye eneo la akiba ya barabara ya Arusha – Namanga kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007, na uthamini wa mali za wananchi hao ulifanyika Juni, 2013 lakini hakuna mwananchi hata mmoja amelipwa fidia. Vivyo hivyo mwaka 2013 taarifa kama hiyo ilitolewa kwa wakazi wa Kata ya Mateves kuondoa maendelezo kwenye eneo lililochukuliwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya Arusha – Babati lakini bado uthamini haujafanya ili walipwe fidia:-

(a) Je, ni lini wananchi wa Oldonyosambu na Mateves watalipwa kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria ya Barabara Na. 13 ya 2007?

(b) Kwa kuwa malipo ya fidia ya mali ya wananchi inayochukuliwa na Serikali kwa maslahi ya umma ni sharti la Kikatiba, je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kuwa wananchi watakaoathirika na utwaaji wa ardhi yao kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa siku zijazo watalipwa kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Goodluck Joseph Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Arusha – Namanga ni barabara kuu inayohudumiwa na Wizara yangu kuititia Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*). Barabara hii imekuwepo tangu enzi za ukoloni na imetambuliwa na Sheria ya Barabara, Cap. 167 ya mwaka 1967 na mabadiliko yake kuititia Sheria Na. 13 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, mali za wananchi wa kijiji cha Oldonyosambu zilizoathiriwa wakati wa ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga zilifanyiwa tathmini, jumla ya shilingi milioni mia mbili themanini na moja na senti hamsini zinahitajika kulipa fidia kwa wananchi 55 ambaao ndiyo waliathirika. Wizara yangu inapitia nyaraka husika ili wananchi hao walipwe fidia zao kwa mujibu wa sheria kwani barabara iliwaafuata. Kwa wananchi ambaao wako ndani ya hifadhi ya barabara, hawatalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na TANROADS kwa wakazi wa Kata ya Mateves kuhusu kuondoa maendelezo kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Arusha – Babati kwa sababu hakuna eneo liilohitaji kwa ajili ya upanuzi wa barabara hii. Aidha, katika Kata ya Mateves hakuna wananchi walioathirika wakiwa nje ya hifadhi ya barabara kwa mujibu wa sheria kwa sababu hakuna eneo liilotwaliwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya Arusha – Babati.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba malipo stahiki ya fidia yanalipwa kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na.13 ya mwaka 2007, kabla maeneo ya wananchi kutwaliwa kwa ajili ya miradi ya barabara.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Ole-Medeye, swali la nyongeza.

MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa majibu ya sehemu ya kwanza ya swali langu, wamekiri kuwepo kwa wananchi walioathirika na wanastahili kulipwa fidia. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi kama ilivyorekebishwa mwaka 2004, fidia ya ardhi baada ya uthamini kukamilika thamani ile inakoma baada ya miezi sita kupita, kwa maana nyingine ni kwamba lazima upitie upya uthamini uliokuwa umeufanya baada ya kila miezi sita. Tokea Juni, 2013 uthamini ule ulipofanyika hadi leo imeshapita karibu miezi 18 ikiwa na maana kwamba thamani uliyoitaja ya shilingi mia mbili themanini na moja siyo thamani halisi ya fidia inayotakiwa kulipwa, ni lini fidia hiyo italipwa kwa kuzingitia sheria?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Waziri anasema kwamba wananchi wa Mateves hawakufuatwa na barabara. Siku ya Alhamisi wiki iliyopita, mimi nikiwa nimefuatana na mwakilishi wa Meneja wa Mkoa wa TANROADS, tulikwenda eneo la Mateves. Mbele ya viongozi wa Kata hiyo, mwakilishi yule alikiri kwamba barabara ile imeingia ndani ya eneo la wananchi kwa mita saba na nusu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kanuni ambazo Waziri wa Ujenzi alitunga mwaka 2009, kanuni ya 29 inasema ifuatavyo, kwa ruhusa nayo naomba niisome.

"Where the Minister is satisfied that certain land would be required in future for the construction of public roads, he shall consult the Minister responsible for Land for the purposes of preservation of that land. The land preserved pursuant to sub-regulation (1), shall not be subject for any private development. And for, upon consultation with Minister responsible for land, the Minister shall take all measures to procure acquisition of that reserved land, including measures to compensate person who lawfully claim interest to that land".

Mheshimiwa Spika, sasa kama wananchi wa Mateves wamefuatwa kwa mita saba na nusu...

SPIKA: Punguza swali lako limekuwa refu mno.

MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, naomba Waziri asema ni lini anawalipa fidia wananchi wa Mateves ambao barabara ya Arusha – Babati imewafuata.

SPIKA: Waziri wa Ujenzi, naomba ujibu kwa kifupi.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama alivyozungumza yeye, ame-quote Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 pamoja na mabadiliko yake lakini pia kuna Sheria ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, kuna Sheria ya Maendeleo ya Vijiji ya mwaka 2007 lakini pia kuna Sheria Na.13 ya mwaka 2007 ambazo zote zinazungumzia juu ya road reserve.

Mheshimiwa Spika, katika jibu letu la msingi tumeeleza kwamba kuna wananchi 55 ambao watalipwa shilingi milioni mia mbili themanini na moja na hayo ndio tunaendelea nayo. Taratibu za kulipa fidia kwa wananchi wote wanaofuatwa na barabara, Mheshimiwa Medeye anafahamu. Huwa inafanywa *evaluation* na watu wa Wizara ya Ardhi na *evaluation* hii ilifanywa wakati yeye akiwa Naibu Waziri wa Ardhi. Ikimalizika kufanywa *evaluation* ndipo processes hizi zinafanya kwa ajili ya kulipa *compensation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Medeye, kwa wale ambao wamefuatwa na barabara, kwa mujibu wa sheria watalipwa fidia yao kama tulivyojibu kwenye swali la msingi.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali la linalofuata, Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa niaba yake Mheshimiwa Herbert Mntangi.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, kwanza tunatambua kwamba Mheshimiwa Zabein Mhita amefiwa na mume wake. Kwa hiyo, tuombe roho ya marehemu ipate rehema kwa Mungu na apumzike kwa amani.

Na. 51

**Kupandishwa Hadhi Barabara ya
Ntundwa – Hurui – Kashi**

MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.n.y. MHE. ZABEIN M. MHITA) aliuliza:-

Mwaka 2010, Mheshimiwa Rais aliahidi barabara ya Ntundwa – Hurui – Kash itachukuliwa na TANROADS kwa kuwa barabara hii inatoka Mkoa wa Dodoma mpaka Mkoa wa Manyara; na barabara hiyo mpaka sasa haijapandishwa hadhi pamoja na kuwa suala hili limefikishwa kwenye vikao vya Road Board Mkoa:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ieleweke kuwa barabara zote nchini, ziwe chini ya TAMISEMI au TANROADS ziko chini ya mamlaka ya Rais.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi ilipokea maombi ya kupandishwa hadhi barabara ya Ntundwa – Hurui – Kash kuwa barabara ya Mkoa. Kufuatia maombi haya, Kamati ya kitaifa ya kupanga barabara katika madaraja stahiki ilifanya ukaguzi na uchambuzi wa maombi hayo kwa kuzingatia Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na kujiridhisha kuwa barabara hiyo haikidhi vigezo vya kupandishwa hadhi kuwa barabara ya Mkoa. Hivyo, barabara ya Ntundwa – Hurui – Kash itaendelea kubakia kuwa barabara ya Wilaya na itahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya husika kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

SPIKA: Mheshimiwa Mntangi swali la nyongeza.

MHE. HERBERT J. MTANGI: Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kusema kwamba Wizara haina mamlaka ya kufuta ahadi ya Mheshimiwa Rais. Kwa msingi huo basi, ni vigezo gani ambavyo havijakamilishwa na kama kweli Halmashauri ya Wilaya ile ya Kondoa imefahamishwa vigezo hivyo ili iweze kuchukua hatua za haraka kuvikamilisha na kuweza kupandisha hadhi barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa upandishaji wa barabara unasaidia Halmashauri nydingi kuweza kutumia vizuri Mfuko wa Barabara, hasa kwa kuweza kufungua barabara nydingi zaidi katika maeneo ya kata na vijiji na Wilaya ya Muheza pia imefanya hivyo na ina maombi yake. Je, ni lini Kamati ya Taifa itafika pia Muheza kufanya ukaguzi wa vigezo kwa barabara ilizoomba zipandishwe daraja?

SPIKA: Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kama tunavyosema hii Kamati ya Kitaifa ipo kwa mujibu wa sheria kuweza kufanya uhakiki wa vigezo vile vilivyopendekezwa na mamlaka za chini. Kwa hiyo, hatusemi kwamba tunakuwa tunafuta ahadi ya Rais, ndiyo maana tumeleka kwenye jibu la msingi kwamba barabara zote hizi ni za Rais lakini tumeziweka kwenye madaraja kulingana na sheria ili ziweze kuhudumiwa na mamlaka ya TAMISEMI au ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, vigezo ambavyo viliifanya barabara hii isiweze kupitishwa, kwanza, inaweza ikakidhi vigezo vilivyoandikwa kwenye sheria lakini barabara inatakiwa isiwe barabara kitanzsi. Inaweza kuwa inatoka point A kwenda point B lakini inazunguka, kwa sababu kuna barabara tayari yenye hadhi. Au isiwe sambamba yaani iko parallel, barabara zote zinalekeea upande mmoja. Kwa hiyo, ndiyo sababu zilifanya barabara hii ishindwe kukidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili kuhusu Kamati kufika Muheza, ni kwamba Kamati hii inapitia barabara zote katika nchi nzima kwa hiyo hata Muheza itafika.

SPIKA: Ahsante. Swali la mwisho, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed.

Na. 52

Majengo ya Ubalozi Yanayomilikiwa na Serikali

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED aliuliza:-

Je, ni majengo mangapi ya Ubalozi na yako nchi zipo ambayo yanamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Balozi zake zilizoko nje ambazo Serikali imepata hati miliki?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Jimbo la Ole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayo jumla ya majengo 97 ya Balozi zetu zilizoko katika nchi mbalimbali duniani. Kati ya majengo hayo 88 yana hati na 9 hayana hati.

Mheshimiwa Spika, majengo 88 yenye hati yapo katika Balozi zifuatazo ambazo ni London - 8, Harare - 8, Nairobi - 2, Kigali - 1, Kinshasa - 3, Lusaka - 11, Maputo - 3, Tokyo - 2, Roma - 1, Lilongwe - 5, Ottawa - 5, Berlin - 1, Pretoria - 7, Geneva - 1, Bujumbura - 3, Cairo - 4, Washington - 6, Kampala - 4, New York - 4, Stockholm - 3, Brussels - 2, Adis Ababa - 2 na Paris - 2.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inaendelea kushirikiana na Balozi zetu kufuatalilia upatikanaji wa hati kwa majengo ambayo hayana hati. Aidha, napenda kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge katika utoaji wa hati inategemeana na sheria za nchi husika na pia makubaliano kati ya nchi na nchi.

SPIKA: Mheshimiwa Rajab swalii la nyongeza.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimuulize Naibu Waziri maswali mawili madogo tu ya nyongeza. La kwanza, ni kutaka kujua hizi nchi tisa ni zipi ambazo hadi leo hatujapata hati za majengo yao?

Mheshimiwa Spika, mwezi wa pili Kamati yangu ilikuwa Uganda na katika mazungumzo yetu na Balozi, moja ya mambo ambayo aliyazungumza na kuyalalamikia ni kukosekana kupatiwa hati kwa nyumba ambayo imetelekezwa iliyoko mlima Kilolo na ile ya Kitanga. Hapa Waziri amesema kwamba Kampala tayari wana hati za nyumba nne wakati kuna nyumba mpaka mwezi wa pili Kampala hazijapatiwa hati, je, ukweli hasa uko wapi katika hili?

SPIKA: Naomba Naibu Waziri ujibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WAARDHI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA): Mheshimiwa Spika, katika swalii la kwanza alitaka kujua hayo majengo tisa yako katika nchi zipi na napenda kumjibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa London – Uingereza tunalo jengo moja, Kigali – Rwanda liko moja, Beijing – China liko moja, New Delhi - India liko Moja, Rome – Italy liko moja, Cairo moja, Khartoum mawili na The Hague mawili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uganda ameeleza kuwa yako majengo mawili, moja liko mlima Kilolo na lingine Kitanga na kwamba haya nayo hayana hati. Naomba Mheshimiwa Mbunge aniachie nilifuatilie suala hili lakini kwa takwimu na kumbukumbu ambazo tunazo hivi sasa sisi haya masuala hayapo. Kwa sababu labda walibadilishana majengo kwa

upande wa Kampala Uganda na sisi kwa upande wa Tanzania inawezekana kuna taratibu mbalimbali za mchakato wa kiserikali zimekuwa zikichukua muda mrefu, tutalifuatilia.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tuna tatizo la muda, tunaendelea.

Naomba nitangaze shughuli za kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Anna Abdallah, anawatangazia Wajumbe wake kwamba saa nane mchana watakuwa na kikao ukumbi namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa nane watakuwa na kikao ukumbi namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa nane mchana na siyo saa saba, kutakuwa na kikao chao katika ukumbi namba 136, Hazina House.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia tutakuwa na wageni, baada ya Waziri wa Nchi kusoma hotuba yake dakika 45 tutaahirisha kazi ya Bunge ili tuweze kuwapokea wageni. Ninji Wabunge wengine wote mtabaki humu ndani, watakaotoka nje kwenda kuwapokea wageni ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Wajumbe wa Tume ya Huduma ya Bunge, Wenyevitit wa Kamati za Kudumu za Bunge au Makamu Wenyevitit. Kwa hiyo, ni hao wachache watatoka pale nje kumpokea mgeni. Baada ya kusema hivyo, Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 - Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano)

SPIKA: Mheshimiwa Mtoa hoja, dakika 45,

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, WAKATI WA KWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa ndani ya Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 na malengo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, naomba kutoa hoja kwamba ...

SPIKA: Wanaotoka waondoke kimya kimya.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda niwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa James Daudi Lembeli kwa kupokea na kuchambua taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na pia

kujadili na kupidisha malengo na makadirio ya mapato na matumizi kwa ofisi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa shukrani kwa Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse kwa upande wa Mazingira na Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu kwa upande wa Muungano, kwa ushirikiano wao wa dhati na michango yao katika kuboresha hoja hii ninayoiwasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha hoja yangu, napenda kutumia fursa hii ya kipekee kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake makini katika Awamu ya Nne ya utawala wa Serikali. Mafanikio yaliyopatikana ni matokeo ya uwezo na umakini katika uongozi wake. Ni ukweli ulio dhahiri kuwa, nchi yetu imepata mafanikio ya kiuchumi na kijamii katika kipindi chake cha uongozi. Tanzania imezidi kutambulika kimataifa hasa katika kuchangia juhudzi za kuleta amani katika Bara la Afrika. Napenda pia kutumia nafasi hii, mimi binafsi na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Mazingira na Naibu Waziri – Ofisi ya Makamu wa Rais, kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupa dhamana ya kuratibu masuala ya Muungano na kusimamia hifadhi ya mazingira nchini katika kipindi cha uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini na wa hekima ambao umewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa masuala ya Muungano na usimamizi wa hifadhi ya mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa Bunge hili Tukufu kwa kazi nzuri ambayo limeifanya kwa kipindi chote cha uongozi wako. Vilevile, nakupongeza wewe binafsi, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara ya hali ya juu katika kutimiza majukumu na wajibu wake kwa wananchi wa Tanzania. Nakupongeza pia kwa kuliwakilisha vizuri Bunge na nchi yetu katika Mabunge ya Jumuiya mbalimbali, hususan kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Bunge la SADC. Tunakuombea kila la kheri na mafanikio katika majukumu makubwa uliyonayo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii sasa kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Grace Puja na Mheshimiwa Dkt. Innocent Sebba, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawataki utekelezaji mzuri wa majukumu yao mapya na kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni, ambazo zimetoa tathmini ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na malengo na mwelekeo kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, niwatakie Mawaziri wote watakaofuata kila jema na ufanisi katika kazi hii inayotukibili.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi kwa ujumla, kwa kifo cha Mheshimiwa Kapt. John Damiano Komba, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi, kilichotokea mwezi Februari, 2015. Aidha, natoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla, kwa kuwapoteza ndugu zao na mali kutohana na matukio ya ajali za barabarani na maafa ya mafuriko yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Vifo na majanga yaliyotufika ni pigo kubwa kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu. Tutawakumbuka kwa juhudzi zao na tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, pamoja na malengo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya kazi zetu, ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Mpango wa Taifa wa wa miaka mitano, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015, Malengo ya Milenia; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania; Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kujielekeza katika masuala ya Muungano na nitafanya mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 na malengo ya mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015, Ibara ya 184, imetoa maelekezo yanayohusu kuendeleza Muungano wetu ambayo uhalisia wa utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

Moja, tulitakiwa kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Jitihada za Ofisi katika kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa mambo ya Muungano ziliendelezwa kwa kufuutilia utatuzi wa masuala ya hisa za SMZ zilizokwu katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na mgawanyo wa faida ya Benki Kuu; malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili; uchimbaji wa mafuta na gesi asili na usajili wa vyombo vya moto.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya hisa za SMZ zilizokwu katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki SMT na SMZ, baada ya kuangalia mawasiliano yanayofanywa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na iliyokuwa Bodi ya Sarafu Afrika Mashariki kwa pamoja zimekubaliana kuwashirikisha Wanasheria Wakuu wa SMT na SMZ ili watoe ushauri wa kisheria kabla ya Waraka uliotayarishwa kupelekwa kwenye kikao cha pamoja cha SMT na SMZ na kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, sekta za fedha zinaendelea kujadili kuhusu malalamiko ya wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili kwa kuangalia vipengele na masharti yatakayofanya SMZ na SMT kukubaliana kutumia mfumo mmoja wa malipo, kwa walipa kodi waliopo Zanzibar, jambo ambalo litasaidia kuondoa manung'uniko kwa wafanyabiashara na hili nalo lipo katika hatua za mwisho za kumalizika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba suala la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia limekubalika kuondolewa katika mambo ya Muungano, bado SMT na SMZ zinaendelea na mawasiliano ya jinsi kazi ya uchimbaji wa mafuta na gesi itakavyofanywa kwa kuzingatia sheria za hapa nchini na zile za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, fursa iliyotokea ya kutunga Katiba Mpya ya nchi yetu, imetoa wasaa mzuri wa kuyapa hadhi ya Kikatiba masuala mengi ya Muungano ambayo Serikali zetu za SMT na SMZ zilishakubaliana na mustakabali wa uendeshaji wake. Baadhi ya mambo hayo yaliyopata hadhi ya Kikatiba ni suala la ushirikiano na uhusiano wa Zanzibar na Taasisi za Kikanda na Kimataifa kwa mambo yanayohusu Zanzibar ambayo ni Ibara ya 76. Uwezo wa SMZ kukopa ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (Ibara ya 261) ambapo utaratibu huu utarahisisha upatikanaji wa mikopo kwa maendeleo na ustawi wa Zanzibar. Suala lingine ni ajira kwa wananchi wa pande zote mbili za taasisi za Muungano ambapo

Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Mambo ya Muungano imepewa jukumu la kusimamia uwepo wa uwakilishi wa pande zote mbili za Muungano (Ibara 128 (1) (f) na 128 (3) na kutiliwa mkazo na Ibara 150 (4) iliyoweka wazi uzingatiaji wa uwakilishi wa pande mbili za Muungano kwa nafasi za uteuzi.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kwamba mchakato huu utakapokamilika na kama Katiba Inayopendekezwa itakubaliwa na wananchi, changamoto nyngi za Muungano zitakuwa zimepatiwa ufumbuzi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tuliloagizwa ni uratibu wa masuala ya kiuchumi, kijamii na kisheria na mambo yanayohusiana na Katiba katika Muungano kwa faida ya pande mbili za Muungano. Ofisi ya Makamu wa Rais imeratibu masuala ya kiuchumi na kijamii yanayotekelvezwa kimuungano. Imeratibu gawio la fedha la asilimia 4.5 kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kusaidia kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii. Gawio hilo hujumuisha misaada ya kibajeti, fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania na Kodi ya Mishahara (PAYE) kwa wafanyakazi wa taasisi za Muungano. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, SMZ ilipokea Sh.27,681,808,403/= kati ya Sh.44,039,608,000/= zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, Sh.7,137,882,543/= ni gawio la kibajeti kwa SMZ, Sh.15,750,000,000/= ni fedha za kodi ya mishahara, Sh.1,243,925,860/= ni fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Sh.3,200,000,000/= ni gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, SMZ imepokea Sh.350,000,000/= ikiwa ni deni la fedha zilizotumiwa na SMZ wakati wa uzinduzi wa maadhisho ya sherehe za Muungano.

Mheshimiwa Spika, ofisi pia inaratibu miradi ya kiuchumi na kijamii inayolenga kuboresha elimu, afya, masoko, maji, mazingira pamoja na usafiri na usafirishaji inayotekelvezwa Tanzania Bara na Zanzibar ambayo inafadhiliwa na Serikali kwa kushirikiana na wahisani wa maendeleo. Miradi hiyo ni pamoja na utekelezaji wa malengo ya kazi za TASAF III yanayoendelea kufanyika kwa mafanikio katika pande zote mbili za Muungano. Mpango wa kunusuru Kaya Maskini umetekelvezwa kwa kaya zipatazo 1,000,000 na Halmashauri 159 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Tanzania Zanzibar. Mpango huu unafaidisha watu wapatao milioni saba ambao ni karibu asilimia 15 ya Watanzania wote.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mazungumzo yamezidi humu ndani.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA NA MUUNGANO): Mheshimiwa Spika, miradi mengine ni ile ya Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo na Kuendeleza Sekta ya Mifugo. Miradi hii imestawisha hali za maisha ya wakulima na wafugaji walio chini ya mradi huu kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wenye tija, kipato na uhakika wa chakula. Kwa mwaka huu wa fedha, programu hii imekamilika na Serikali iko katika hatua za maandalizi ya Awamu ya II ya program hii.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Awamu ya II ya Programu inayoendeshwa na Mfuko wa Changamoto za Milenia umepangwa kutekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar kwenye miradi ya sekta za nishati. Programu inalenga kuboresha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa kukarabati mfumo wa umeme katika Mji Mkongwe Zanzibar na katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara; kujenga uwezo wa kitaasisi kwa TANESCO na ZECO; na kukuza sekta ya nishati kwa kushirikisha sekta binafsi kwa Zanzibar pekee.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) pia unatekeleza kazi zake Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa upande wa Tanzania Bara zoezi la upimaji wa ardhi limezalisha viwanja 8,091 katika Halmashauri za Njombe, Babati na Tunduma pamoja na Manispaa za Iringa, Morogoro, Kinondoni na Arusha.

Kwa upande wa Zanzibar, upimaji umefanywa kwenye Shehia za Limbani, Jang'ombe na Welezo ambapo viwanja 4,130 vilipimwa na Vijiji vya Kiungoni, Chwaka, Chokocho na Nungwi vilipimwa na viwanja 4,307 vimepatikana. Mpango huu unaendelea na zoezi la uratibu wa kutoa hati za kimila kwa wamiliki wa mashamba pamoja na urasimishaji wa biashara katika baahi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Kifedha Vijiji – (MIVARF) yenye dola za Marekani milioni 169.5 una lengo la kupunguza umaskini na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi endelevu, kwa kuziwezesha kaya maskini za vijiji, katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuongeza kipato na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, kazi zilizotekelzeza chini ya Programu hii ni pamoja na: ukarabati wa kilomita 369 za barabara kati ya kilomita 555.3 zilizopangwa katika Halmashauri 18 za Tanzania Bara na Zanzibar; ujenzi wa masoko na maghala manne (4) na matatu (3) yamekarabatiwa; vikundi vya wajasiriamali 102 vya Zanzibar na 294 vya Tanzania Bara vimeunganishwa na masoko; kuwezesha benki za wananchi kupanua wigo wa huduma kwa jamii maskini za vijiji na kukuza ufanisi wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Spika, ili taasisi za Muungano ziweze kufanya kazi kwa ufanisi na kusogeza huduma kwa wananchi, jitihada za kujenga au kuanzisha ofisi za kudumu kwa upande wa Zanzibar ziliendelea. Mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uhamiaji imemaliza ujenzi wa jengo la Makao Makuu Zanzibar na kulizindua rasmi tarehe 25 Aprili, 2015. Aidha, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imewekwa katika jengo la zamani la Uhamiaji na imefungua matawi yake katika Wilaya zote za Zanzibar. Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Kamisheni ya Nguvu za Atomiki zimepata Ofisi za Kudumu huko Maruhubi Zanzibar na Taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inaendelea na Awamu ya II ya ujenzi wa jengo la taasisi hiyo huko Buyu Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tuliloagizwa na Ilani ni kuelimisha umma kuhusu Muungano. Katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano kupitia majarida, vipeperushi na fulana zenye ujumbe wa Muungano zilizogawiwa kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu Zanzibar, Iringa, Mbeya na Dodoma. Aidha, Ofisi inakamilisha Toleo la Pili la Kitabu cha taarifa ya mafanikio ya miaka 50 ya Muungano, sambamba na kukamilisha kitabu cha mafanikio ya masuala ya Muungano katika Awamu ya Nne kwa ajili ya kuelimisha umma. Pamoja na hayo, semina za elimu ya Muungano kwa wananchi zilifanywa huko Zanzibar. Ofisi kwa kushirikiana na Makumbusho ya Taifa imetoe elimu ya Muungano kwa wanafunzi 1,500 wa shule za msingi za Mkoa wa Dar es Salaam na kuandaa onesho la Muungano wakati wa maadhimisho ya miaka 51 ya Muungano pamoja na kutoa elimu kwa watumishi 80 (Maafisa Viingo) wa Wizara na Taasisi za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ilani imetuagiza pia kukuza ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano. Katika kulitekeleza hili, ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umeratibiwa. Katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu, Wizara na taasisi zisizo za Muungano za SMT na SMZ hushirikiana katika kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya sera, utaalamu na wataalamu, ushiriki katika masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa, utafiti na ziara za mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, vikao vitano (5) vya ushirikiano vimefanyika katika sekta zinazosimamia masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; utumishi katika Jamhuri ya Muungano; uchukuzi; biashara na masuala ya utawala bora.

Masuala yaliyojadiliwa katika sekta hizo ni pamoja na changamoto na mikakati ya ukusanyaji wa mapato katika mamlaka za Serikali za Mitaa; uwiano wa fedha zinazolipwa na huduma wanazopatiwa wananchi; uzoefu katika kuzuia na kupambana na rushwa na maadili ya viongozi wa umma.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine yaliyojadiliwa yanahusu nafasi za ajira katika taasisi za Muungano; kufungua Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Zanzibar na mikakati ya kudhibiti bidhaa zisizo na viwango na bandari zisizo rasmi ambazo zimekuwa mwanya wa kuitisha biashara na wahamiaji haramu, majahazi yasiyosajiliwa na vitendo vingine viovu.

Mheshimiwa Spika, malengo kwa mwaka 2015/2016 kwa upande wa Idara ya Muungano. Ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni, utaratibu na miongozo ya kitaifa, ikiwa ni pamoja na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika kulitekeleza hilo, Ofisi itaandaa na kuitisha kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kutafakari njia muafaka za kushughulikia masuala ya Muungano. Kikao hicho kitatanguliwa na kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ, kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ na vikao vinne (4) vya Sekretarieti ya SMT na SMZ.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya kudumisha Muungano wetu, Ofisi itaendelea kuelimisha umma kuhusu Muungano, kuongeza ufanisi katika uratibu wa utekelezaji wa miradi ya jamii inayolenga kuinua kipato kwa kaya masikini Mijini na Vijiji kwa lengo la kuziinua kiuchumi na kushajiisha Wizara au taasisi zisizo za Muungano zenye kazi zinazoshabihiana SMT na SMZ kuendeleza mashirikiano kwa nia ya kukuza ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha bajeti ukurasa wa 17 kinaelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne katika kipindi cha mwaka 2005-2015.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa upande wa Muungano, naomba sasa nijielekeze kwa upande wa hifadhi endelevu ya mazingira kwa kuititia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 na utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 194 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010 – 2015, inaelekeza Serikali kutekeleza masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira hapa nchini. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya uchaguzi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulielekezwa kuimarisha zoezi la Kitaifa la kupanda miti pamoja na miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji kwa mwaka 2006 kwa kuhimiza upandani wa miti milioni 1,500,000 kwa mwaka kwa kila Halmashauri ya Wilaya. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi imepokea taarifa ya upandaji miti kutoka Mikoa 22 inayobainisha kwamba miti milioni 217,301,650 ilipandwa na kati ya hiyo, miti 181,720,849 imestawi, sawa na asilimia 83.63 ya miti iliypandwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zilizopanda miti na kustawi kwa zaidi ya asilimia 80 ni 39 kama zinavyoonekana katika kitabu cha bajeti, Ibara ya 40, ukurasa wa 19. Mikoa

ambayo Halmashauri zake hazijawasilisha taarifa za upandaji miti kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni Manyara, Kagera na Geita.

Mheshimiwa Spika, mashindano ya tuzo ya Rais ya kuhifadhi vyano vya maji, kupanda na kutunza miti yameendelea kuhamasishwa nchini katika ngazi za Kaya hadi Mkoo. Makundi mengine ni shule za msingi na sekondari; vyuo vya mafunzo/utafiti; taasisi za Kijeshi na taasisi/vikundi vya uhamasishaji na uwekezaji. Tuzo hii hutolewa kila baada ya miaka miwili (2) na mara ya mwisho tuzo ilitolewa mwaka 2014 na itatolewa tena mwaka 2016 wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Ilani imetuelekeza pia kwamba tuvielekeze Vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitunge Sheria Ndogo za Hifadhi ya Misitu. Ofisi iliendelea kuhimiza Wilaya na Manispaa kutunga Sheria Ndogo za Hifadhi ya Misitu, Tathmini ya Mazingira na Usafi wa Mazingira. Katika mwaka huu wa fedha, Halmashauri za Njombe, Kalambo, Mpanda, Uvinza, Kasulu, Kibondo, Kishapu na Sengerema zilifanikisha kutunga sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, lingine tuliloagizwa ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira katika vyano vya maji na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa usafi katika fukwe. Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira limeendelea kuhimiza utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 na Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyano vya Maji na Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa nchini. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na SUMATRA na Serikali ya Norway, linatekeleza mpango wa dharura wa kukabiliana na uchafuzi wa mazingira baharini. Ofisi inakamilisha taratibu za kuridhia marekebisho ya Mkataba wa Nairobi na Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi unaotokana na shughuli zinazofanyika nchi kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo lingine tulitakiwa tuchukue hatua ya kuandaa sera na kutunga sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa mazingira. Kwa kushirikiana na Wizara za Nishati na Madini, Sera ya Nishati nchini imetungwa ili kuhakikisha matumizi ya nishati mbadala yanazingatiwa. Aidha, ofisi inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na baadaye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kwa lengo la kufanya mazingatio ya matumizi ya nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, pia tuliagizwa kupunguza gharama za vifaa vya nishati mbadala ili wananchi wanaojenga nyumba za kisasa vijijini watumie nishati hiyo badala ya kuni na mkaa wa miti. Serikali imeendelea kusimamia punguze la Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa asilimia 18 katika vifaa vya gesi na umeme ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Aidha, gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijijini zimeshushwa ili kuwafanya watu wengi zaidi vijijini kuweza kuunganisha umeme kwenye nyumba zao na katika maeneo yao ya biashara. Matumizi ya nishati inayotokana na kinyesi cha mifugo (*biogas*) na umeme nuru (*solar energy*) yanaendelea kuhamasishwa.

Mheshimiwa Spika, tuliagizwa kuimarisha usimamizi wa viwanda na biashara ili kutochafua mazingira. Katika kulitekeleza hili, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilifanya tathmini ya athari kwa mazingira kwenye viwanda vya MM Integrated Steel Mills Ltd; BIDCO Oil & Soap Ltd; Murzah Oil Mills Ltd; Auto Mech Limited; OK Plastic Limited; Basic Elements Ltd na Twiga Cement vyote ya Dar es Salaam. Viwanda vingine ni Azam Fruit and Juices Industry na Rhino Cement Mkoani Pwani; Tanga Cement; Nilecanth Ltd; Afritex Ltd na PPTL Mkoani Tanga; 21st Century Textile Mills, Morogoro; na Sunflag Textile Mill – Arusha.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi hilo la ukaguzi, amri za katazo zilitolewa kwa viwanda vinne (4); amri za kusitisha shughuli zilitolewa kwa viwanda vitatu (3) na viwanda vingine vilipewa onyo na kutozwa faini. Maeneo mengine yaliyofanyiwa ukaguzi ni kama yalivyotajwa kwenye Kitabu cha Bajeti, Ibara ya 49 - 51, ukurasa wa 25.

Mheshimiwa Spika, Ilani ilituagiza kutekeleza Mradi wa Vijiji vya Mfano vya Hifadhi ya Mazingira (Eco-Villages). Awamu ya Pili ya Mradi wa Vijiji vya Mfano unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya kwa gharama ya takribani shilingi bilioni 16 inaendelea. Fedha hizo ziligaisha kwa taasisi tano zinazotekeleza miradi hiyo ambayo ni Community Forest Pemba - EURO 1,250,000; Heifer Nederland katika Wilaya ya Igunga - EURO 2,132,480; ONGAWA katika Milima ya Usambara Mashariki - EURO 1,364,449; Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijiji Dodoma - EURO 1,999,802 na mradi ulioko Wilaya ya Arumeru - EURO 1,796,262. Miradi hii inatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Mheshimiwa Spika, Ilani ilituagiza kufanya tathmini ya athari za kimazingira katika miradi ya maendeleo. Katika mwaka huu wa fedha jumla ya miradi 870 ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira. Kati ya miradi hiyo, 596 ni miradi ya sekta mbalimbali na 274 ni minara ya mawasili. Katika kipindi hiki, miradi 640 ilipatiwa hati (*Environmental Impact Assesment Certificates*).

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya mazingira katika maeneo maalum. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Baraza liliuftilia na kufanya tathmini ya hali ya mazingira katika Wilaya tatu (3) za Kilolo, Mufindi na Kilombero ambazo zimo ndani ya eneo la lindimaji la Kihansi. Aidha, Baraza lilitribu Programu ya Binadamu na Mazingira Hai (*Man and Biosphere Reserve*) na kufanikiwa kukamilisha mchakato uliopelekeza kuingiza hifadhi za Jozani Chwaka Bay kwa Zanzibar na Saadani Tanzania Bara katika mtando wa Hifadhi Hai wa Dunia (*World Network of Biosphere Reserves*). Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Baraza litakamilisha andiko la miradi miwili ambayo imeshawasilishwa kwenye Bodi ya Mfuko wa Mazingira Duniani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza utekelezaji wa maagizo ya Ilani ya Uchaguzi, naomba sasa nijielekeze katika utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa mwaka fedha 2014/2015 ambayo Idara ya Mazingira ilijipangia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, sambamba na utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, ofisi ilitekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, elimu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Elimu ya uhamasishaji wa umma imekuwa ikitolewa kwa njia mbalimbali katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa, Maadhimisho ya Kimataifa ya Tabaka la Ozone za kila mwaka. Aidha, Ofisi imeendelea kusambaza nakala za Mpango Kazi wa Taifa wa Mazingira wa mwaka 2013-2018 kwa nia ya kukuza uelewa kwa wadau na kwa mwaka wa fedha 2015 -2016, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Hali ya Mazingira nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ripoti ya Hali ya Mazingira nchini ya mwaka 2014 imekamilika, kuchapishwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 22 Aprili, 2015 na Mheshimiwa Dkt. Mohammed Ghalib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa ujumla, ripoti imeonesha kuendelea kuwepo kwa uharibifu wa mazingira nchini pamoja na juhudzi zinazoendelea kufanywa. Aidha, ripoti imebainisha kuwepo kwa changamoto mpya za mazingira hususan taka zinazotokana na vifaa vya umeme na kielektroniki, viumbe vamizi vigeni, viumbe vilivyo fanyiwa mabadiliko ya kinejetiki na biofuel na kubainisha mbinu ya kupambana na hayo. Katika kipindi cha mwaka wa

fedha ujao, ofisi itaendelea kusambaza ripoti hii na kuelimisha na kuhamasisha umma jinsi ya kukabiliana na changamoto zilizobainishwa.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya athari za mazingira kimkakati. Pamoja na kufanya tathmini ya athari kwa mazingira, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira imeelekeza pia kufanyika kwa tathmini ya mazingira kimkakati katika uandaaji wa Sera, Miswada, Kanuni, Mipango Mikakati au Programu kabla ya utekelezaji wake. Katika kipindi cha mwaka 2014/2015, jumla ya mipango 12 ya tathmini ya mazingira kimkakati ilisajiliwa. Kati ya mipango hiyo, jumla ya ripoti sita za tathmini ya mazingira kimkakati zilipitishwa kwa ajili ya utekelezaji kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 29 - 32 wa kitabu chetu cha bajeti. Ripoti sita zilizobakia zitaendelea kuandaliwa na kukamilishwa pamoja na kukamilishwa kwa mwongozo wa mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa mifuko ya plastiki. Katika kuhakikisha kwamba uchafuzi wa mazingira kutokana na mifuko ya plastiki unadhibitiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau, imeandaa Rasimu ya Kanuni Mpya ya Mifuko ya Plastiki inayoongeza unene wa mifuko kutoka maikroni 30 hadi kufikia maikroni 50. Mifuko yenye unene chini ya mikroni 50 haitaruhusiwa kuzalishwa, kuingizwa nchini wala kutumika. Katika mwaka mwaka 2015/2016, ofisi itaendelea kuwasiliana na Umoja wa Watengenezaji wa Mifuko ya Plastiki kuhusu kuwekeza katika sekta ya urejelezaji (*recycling*) wa mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Maadhimisho haya hufanyika kila tarehe 05 Juni ya kila mwaka. Kwa mwaka huu 2015, maadhimisho hayo yatafanyika Mkoani Tanga. Aidha, kauli mbiu ya mwaka huu ni Ndoto Bilioni Saba, Dunia Moja, Tumia Rasilimali kwa Uangalifu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Manzingira. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, jitihada za kuhakikisha Mfuko wa Taifa wa Mazingira unaanza kufanya kazi zimeendelea. Majadiliano kuhusu maeneo ya kupata vyanzo vya fedha kwa ajili ya Mfuko yanaendelea ambapo hadidu za rejea za Mtaalam Mwelekezi na Kikosi Kazi cha Kisekta kubaini vyanzo vya fedha vya Mfuko huo zimeandaliiwa. Pamoja na hatua hiyo, Baraza limefungua Akaunti ya Mfuko na kufanya mawasiliano na washirika wa maendeleo, juu ya uanzishwaji wa Mfuko huo ili waweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Environment Facility-GEF*). Kupitia Mfuko huo, ofisi imeratibu miradi saba (7) chini ya usimamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (*UNDP*) yenye thamani ya dola za Marekani 480,507. Miradi hiyo inatekelezwa katika maeneo ya Wilaya ya Kusini (Makunduchi) Zanzibar na katika Mikoa ya Iringa (Pawaga, Kalenga na Isimani), Arusha (Longido), Pwani (Rufiji), Mwanza (Magu) na Morogoro (Uluguru).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2015/2016 mpaka 2018/2019, Serikali imetengewa jumla ya Dola za Marekani milioni 29.09 kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia. Miradi tisa inayolenga kwenye maeneo ya Hifadhi ya Bioanuai, Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi Endelevu wa Ardhi imeibuliwa kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, vituo vya huduma kwa wasafiri na wasafirishaji. Ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika barabara kuu nchini, katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Ofisi kwa kushirikiana na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali itaanda utaratibu wa ujenzi wa vituo vya kupumzikia wasafiri na wasafirishaji wanaotumia barabara kuu nchini. Vituo hivyo vitasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuongeza usalama kwa kuepusha ajali zinazosababishwa

na uchovu wa madereva. Ofisi kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuhamasisha sekta binafsi na jamii kwa ujumla kuwekeza katika ujenzi wa vituo hivi muhimu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira. Mikataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai. Ofisi imeendelea kuratibu kuridhiwa kwa Itifaki ya Nagoya inayohusu upatikanaji na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki na itifaki ya ziada ya Nagoya Kuala-Lumpur, inayohusu uwajibikaji kisheria dhidi ya athari zinazotokana na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa. Ofisi itaendelea kusimamia uridhiaji huo mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikataba wa Nairobi unaohusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, kazi kubwa kwenye Mikataba huu ni kukamilisha taratibu za kuridhia Marekebisho ya Mikataba wa Nairobi na Itifaki ya Udhhibit wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 25, ukurasa wa 22 wa kitabu cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, Mikataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Kyoto. Madhumuni ya Mikataba huu ni kushirikisha nchi zote duniani ili joto la dunia lisongezeke kwa zaidi ya nyuzijoto mbili juu ya kiwango cha sasa. Tanzania inaendelea kuandaa ripoti ya maeneo maalum yatakayochangia kupunguza uzalishaji wa gesi joto, kazi ambayo inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Oktoba 2015.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi ya upunguzaji wa gesi joto, itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi za Afrika ya Mabadiliko ya Tabianchi (CAHOSCC) na Ofisi ya Makamu wa Rais ili kumsaidia Mheshimiwa Rais kukamilisha kazi zake vizuri, ilisaidia kuratibu mikutano minne ikiwa ni pamoja na ule ulioitishwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Septemba 2014 huko Newyork. Maeleo kamili ya kazi zilizofanyika wakati wa Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Kamati ya CAHOSCC yanaonekana kwenye ukurasa wa 38 hadi 41.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuhuisha masuala ya mazingira Serikalini imeendelea kutekelezwa. Katika kipindi hiki mafanikio ya miradi ya mabadiliko ya tabia nchi iliyotekelvezwa kwenye Wilaya za Igunga, Misenyi, Mbinga na huku Nungwi Zanzibar yameandikwa na kusambazwa nchini kwa nia ya kueneza elimu iliyopatikana katika maeneo hayo ili kuhamasisha wananchi walioathirika na mabadiliko ya tabianchi kuandaa na kutekeleza miradi ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda, kuna mikataba mingine ikiwemo; Mikataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa; Mikataba wa Montreal kuhusu kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozone; Mikataba Stockhom wa kudhibiti Kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu ambapo mikataba yote inafanyiwa kazi ndani ya ofisi yetu na itaendelea kufanyiwa kazi katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 51 hadi 53 wa kitabu unaonesha mafanikio ya sekta ya mazingira katika kipindi hiki cha Awamu na Nne ya Serikali. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira, changamoto zifuatazo zimejitokeza:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na wadau wengine walioanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kutotekelvezwa matakwa ya sheria

kikamilifu badala yake wanachukulia kuwa utekelezaji wa sheria hii ni jukumu la Ofisi ya Makamu wa Rais na peke yake.

Mheshimiwa Spika, masuala ya utawala. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi imeendelea kuwawezesha watumishi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Maelezo kamili yanaonekana katika ukurasa wa 55 mpaka 58 kwenye kitabu cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, shukrani na hitimisho. Napenda kutoa shukrani zangu kwa Mawaziri wenzangu, Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Waziri wa Nchi mwenye dhamana ya Mazingira na Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano na utendaji wao thabiti na makini katika kutekeleza majukumu ya Ofisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Watendaji Wakuu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Bwana Saazi Bundara Salula, Katibu Mkuu, Mhandisi Angelina Elias Madete, Naibu Katibu Mkuu na Mhandisi Bonaventure Thobias Baya, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Nawashukuru na kuwapongeza pia Wakuu wa Idara na Vitengo na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa juhud zao za dhati katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Vilevile, napenda kuwashukuru wale wote walioituwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita na kufanikisha kuandaan mipango ya mwaka wa fedha 2015/2016 na hivyo kustawisha hoja ambayo nimeiwasilisha hapa leo.

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri iliyofanywa na wote niliowashukuru hapo juu isingewezekana bila uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. Mohammed Ghalib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uongozi wake makini na hekima ndivyo vimewezesha mafanikio yaliyopatikana katika masuala ya Muungano na usimamizi wa hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii ya kipekee, kuwashukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa ambayo yameshiriki katika kusaidia ufanikishaji wa shughuli zetu, nazo ni kama zinavyoonekana katika kitabu chetu cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye maombi ya fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Ili Ofisi ya Makamu wa Rais iweze kutekeleza ipasavyo malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka 2015/2016 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 26 - Makamu wa Rais. Ofisi inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.5,079,085,000/= fedha za Matumizi ya Kawaida. Kiasi hicho kinajumuisha fedha za Mishahara Sh.1,480,676,000/= na fedha za Matumizi Mengineyo Sh.3,598,412,000/=

Mheshimiwa Spika, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais. Ofisi inaombwa kuidhinishiwa jumla ya Sh.38,077,215,000/= zikijumuisha fedha za Matumizi ya Kawaida Sh.33,558,368,000/= na fedha za Maendeleo Sh.4,518,847,000/=. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Sh.3,200,337,000/= Mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Sh.30,358,031,000/= Matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, fedha za Matumizi Mengineyo zinajumuisha Sh.22,400,000,000/= gawio kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; Sh.3,592,326,000/= ruzuku kwa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kiasi kinachosalia cha Sh. 4,365,705,000/= ni fedha za Matumizi Mengineyo za Idara na Vitengo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa upande wa Fedha za Maendeleo zinajumuisha Sh.3,500,000,000/= fedha za ndani na Sh.1,018,847,000/= fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofii)

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, WAKATI WA KUWASILISHA BUNGENI
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA
2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/15; na malengo kwa mwaka wa fedha 2015/16, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2015/16.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kuwashukuru kwa dhati, Waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa **Jason Samson Rweikiza (Mb.)**, na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa **James Daudi Lembeli (Mb.)** kwa kupokea na kuchambua taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/15, na pia kujadili na kupitisha malengo na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2015/16. Vilevile, natoa shukrani kwa Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani, Mhe. Mchungaji **Israel Natse (Mb.) (Mazingira)** na Mheshimiwa **Tundu Antiphas Lissu (Mb.) (Muungano)** kwa ushirikiano wao wa dhati na michango yao katika kuboresha hoja hii ninayoiwasilisha leo hapa bungeni.

3. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuwasilisha hoja yangu, napenda kutumia fursa hii ya kipekee kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake makini katika Awamu ya Nne ya utawala wa Serikali. Mafanikio yaliyopatikana ni matokeo ya uwezo na umakini wake katika uongozi. Ni ukweli ulio dhahiri kuwa, nchi yetu imepata mafanikio ya kiuchumi na kijamii katika kipindi chake cha uongozi. Tanzania imezidi kutambulika kimataifa hasa katika kuchangia juhudzi za kuleta amani katika Bara la Afrika na kusimamia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi wa Afrika ya Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, napenda kutumia nafasi hii, mimi binafsi na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Mazingira na Naibu Waziri – Ofisi ya Makamu wa Rais, kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupa dhamana ya kuratibu masuala ya Muungano na hifadhi ya Mazingira nchini katika kipindi cha uongozi wake.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa **Dkt. Mohammed Gharib Bilal**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini na wa hekima ambao umewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika masuala ya Muungano na usimamizi wa hifadhi ya Mazingira nchini.

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutoa pongezi za dhati kwa Bunge lako tukufu kwa kazi nzuri ambayo limeifanya kwa kipindi chote cha uongozi wako. Nitumie nafasi hii

kukupongeza wewe binafsi, kwa kuliongoza Bunge letu tukufu kwa busara ya hali ya juu katika kutimiza majukumu yake na wajibu kwa wananchi wa Tanzania. Nakupongeza pia kwa kuliwakilisha vizuri Bunge na nchi yetu katika Mabunge ya jumuiya mbalimbali, hususan kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Bunge la SADC. Tunakuombea kila la kheri na mafanikio katika majukumu makubwa uliyonayo.

6. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii sasa kuwapongeza Mheshimiwa **Dkt. Grace Pujah (Mb)** na Mheshimiwa **Dkt. Innocent Seba (Mb)** kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawatakia utekelezaji mzuri wa majukumu yao mapya ya kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

7. Mheshimiwa Spika, nawashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni, ambazo zimetoa tathmini ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/15 na malengo na mwelekeo kwa mwaka wa fedha 2015/16. Aidha, niwatakie Mawaziri wote watakaofuata kila jema na ufanisi katika kazi hii inayotukabili.

8. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, naunganana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi, kwa kifo cha Mheshimiwa **Kapt. John Damiano Komba**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi, kilichotokea mwezi Februari, 2015. Aidha, natoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla, kwa kuwapoteza ndugu zao na mali kutohana na matukio ya ajali za barabarani na maafa ya mafuriko na mvua kubwa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Vifo na majanga yaliyotufika ni pigo kubwa kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu. Tutawakumbuka kwa juhudhi zao, na tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

9. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, pamoja na malengo kwa mwaka wa fedha 2015/16.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15, UTEKELEZAJI WA MAELEKEZO YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 – 2015 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2015/16

10. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2010 – 2015); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2010 - 2015; Malengo ya Maendeleo ya Milenia; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II); Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997; na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004.

11. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Makamu wa Rais iliweza kutekeleza kazi zilizokuja zimelempewa katika uratibu wa masuala ya Muungano na ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano; na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya usimamizi wa Mazingira hapa nchini. Utekelezaji ulifanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

II. MASUALA YA MUUNGANO

12. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi kupitia hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15 iliahidi mambo kadhaa, ambayo utekelezaji wake umeendana na maagizo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015 kama yalivyo kwenye Ibara ya **184**. Uhalsia wa utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano

13. **Mheshimiwa Spika**, jithada za Ofisi za kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa mambo ya Muungano ziliendelezwa kwa kufuatalia utatuzi wa masuala ya Mahusiano ya Kifedha baina ya SMT na SMZ. Masuala hayo ni pamoja na: hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki; mgawanyo wa faida ya Benki Kuu; malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili; uchimbaji wa mafuta na gesi asili; na usajili wa vyombo vya moto.

14. **Mheshimiwa Spika**, sekta za fedha za SMT na SMZ baada ya kuangalia mawasiliano yaliyofanya baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na iliyokuwa Bodi ya sarafu ya Afrika Mashariki, kwa pamoja, zimekubaliana kuwashirikisha Wanasheria Wakuu wa SMT na SMZ watoe ushauri wa kisheria kabla ya Waraka uliotayarishwa kupelekwa kwenye kikao cha pamoja cha SMT na SMZ.

15. **Mheshimiwa Spika**, sekta za fedha zinaendelea kujadiliana kuhusu malalamiko ya wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili kwa kuangalia vipengee na masharti yatakayofanya SMZ na SMT kukubaliana kutumia mfumo mpya wa malipo, kwa walipo kodi waliopo Zanzibar, jambo ambalo litasaidia kuondoa manung'uniko kwa wafanyabiashara.

16. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba suala la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia limekubalika kuondolewa katika mambo ya Muungano, bado SMT na SMZ zinaendelea na mawasiliano ya jinsi kazi ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi itakavyofanya kwa kuzingatia sheria za hapa nchini na zile za kimataifa.

17. **Mheshimiwa Spika**, fursa iliyotokea ya kutunga Katiba Mpya ya nchi yetu imetoe wasaa mzuri wa kuyapa hadhi ya kikatiba masuala mengi ya Muungano ambayo Serikali zetu za SMT na SMZ zilikubaliana na mustakabali wa uendeshwaji wake. Baadhi ya mambo hayo ni; suala la ushirikiano na uhusiano wa Zanzibar na Taasisi za Kikanda na Kimataifa kwa mambo yanayohusu Zanzibar, Ibara ya **76**; uwezo wa SMZ kukopa fedha ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (Ibara ya 261) ambapo utaratibu huu utarahisisha upatikanaji wa mikopo kwa maendeleo na ustawi wa Zanzibar. Suala jengine ni ajira kwa wananchi wa pande zote mbili katika taasisi za Muungano, ambapo Tume ya Uhusiano na Uratibu wa mambo ya Muungano imepewa jukumu la kusimamia uwepo wa uwakilishi wa pande zote mbili za Muungano, (Ibara 128 (1) (f) na 128 (3), na kutiliwa mkazo katika Ibara 150 (4) iliyoweka wazi uzingatiaji wa uwakilishi wa pande mbili za Muungano kwa nafasi za uteuzi.

18. **Mheshimiwa Spika**, ni matumaini yetu kwamba, mchakato huu utakapokamilika, na kama Katiba inayopendekezwa itakubaliwa na wananchi, changamoto nyingi za Muungano zitakuwa zimepatiwa ufumbuzi.

Uratibu wa Masuala ya Kiuchumi, Kijamii na Kisheria na Mambo Yanayohusiana na Katiba katika Muungano kwa faida ya pande mbili za Muungano

19. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamo wa Rais ikiwa ndie Mratibu Mkuu wa masuala ya kiuchumi na kijamii yanayotekelawa ki-muungano, imeratibu gawio la fedha la asilimia 4.5 kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kusaidia kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii. Gawio hilo hujumuisha misaada ya kibajeti, fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania na Kodi ya Mishahara (PAYE) kwa

wafanyakazi wa taasisi za Muungano. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, SMZ ilipokea shilingi **27,681,808,403/=** kati ya shilingi **44,039,608,000/=** zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo shilingi **7,137,882,543/=** ni gawio la kibajeti kwa SMZ, shilingi **15,750,000,000/=** ni fedha za Kodi ya Mishahara, shilingi **1,243,925,860/=** ni fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na shilingi **3,200,000,000/=** ni gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, SMZ imepokea shilingi **350,000,000/=** ikiwa ni deni la fedha zilizotumiwa na SMZ wakati wa uzinduzi wa maadhisho ya miaka **50** ya Muungano.

20. Mheshimiwa Spika, miradi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi kiuchumi na kijamii imeendelea kuibuliwa. Utekelezaji wa miradi inayolenga kuboresha elimu, afya, masoko, maji, mazingira pamoja na usafiri na usafirishaji unaimarishwa ili kujenga jamii ya watanzania wenyе uwezo wa kupambana na umaskini. Baadhi ya miradi ambayo hufadhliliwa na Serikali kwa kushirikiana na wahisani wa maendeleo ni pamoja na utekelezaji wa malengo ya kazi za TASAF III yanayoendelea kufanyika kwa mafanikio katika pande zote mbili za Muungano. Mpango wa kunusuru Kaya Maskini umetkelezwa kwa kaya zipatazo **1,000,000** za Halmashauri **159** za Tanzania Bara na Wilaya zote za Tanzania Zanzibar. Mpango huu unafaidisha watu wapatao milioni **7** ambaо ni karibu asilimia **15** ya Watanzania wote. Malipo yaliyofanyika kwa kaya za walengwa ni shilingi **41,989,439,745/=** kwa upande wa Tanzania Bara na shilingi **240,205,767/=** kwa Zanzibar. Fedha hizo zinatumika katika kuboresha maisha ya watoto katika kaya zilizofaidika kwa kupatiwa lishe bora, elimu na afya, na pia kutoa fursa za ajira za muda. Aidha, Mpango huu una malengo ya kuinua hali ya maisha kuitia uwekaji wa akiba na kuwekeza kwenye shughuli za kiuchumi.

21. Mheshimiwa Spika, miradi mengine ni ile ya programu ya kuimarisha Huduma za Kilimo na kuendeleza Sekta ya Mifugo (ASDPL/ ASSP) Miradi hii imestawisha hali za maisha ya wakulima na wafugaji walio chini ya mradi huu, kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wenyе tija, kipato na uhakika wa chakula. Kwa mwaka huu wa fedha, Programu hii imekamilika na Serikali iko katika hatua za maandalizi ya awamu ya pili ya programu.

22. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Awamu ya pili ya Programu inayoendeshwa na Mfuko wa Changamoto za Milenia (MCA-T) umepangwa kutekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar, kwenye miradi ya Sekta za Nishati. Programu inalenga kuboresha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa kukarabati mfumo wa umeme katika mji mkongwe Zanzibar na katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara; kujenga uwezo wa kitaasisi kwa TANESCO na ZECO; na kukuza Sekta ya nishati kwa kushirikisha sekta binafsi kwa Zanzibar pekee.

23. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) unatekeleza kazi zake Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa upande wa Tanzania Bara zoezi la upimaji wa ardhi limezalisha viwanja **8,091** katika Halmashauri za Njombe, Babati, na Tunduma, pamoja na Manispaa za Iringa, Morogoro, Kinondoni na Arusha. Kwa upande wa Zanzibar, upimaji umefanywa kwenye shehia za Limbani, Jang'ombe na Welezo, ambapo viwanja **4,130** vilipimwa, na Vijiji vya Kiungoni, Chwaka, Chokocho na Nungwi vilipimwa na viwanja **4,307** vimepatikana. Mpango huu unaendelea na zoezi la uratibu wa kutoa hati za kimila kwa wamiliki wa mashamba pamoja na urasimishaji wa biashara katika baadhi ya Halmashauri.

24. Mheshimiwa Spika, Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Kifedha Vijiji – (MIVARF) yenye dola za Marekani milioni **169.5** unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA). Lengo la Mpango huu ni kupunguza umaskini na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi endelevu, kwa

kuziwezesha kaya maskini za vijijini, katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuongeza kipato na usalama wa chakula.

25. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15 kazi zilizotekelawa chini ya programu hii ni pamoja na: ukarabati wa kilomita **369** za barabara, kati ya kilomita **555.3** zilizopangwa katika Halmashauri **18** za Tanzania Bara na Zanzibar; ujenzi wa masoko na maghala manne (**4**) na matatu (**3**) yamekarabatiwa; vikundi vya wajasiriamali **102** vya Zanzibar, na **294** vya Tanzania Bara vimeunganishwa na masoko; kuwezesha benki za wananchi (Community Banks) kupanua wigo wa huduma kwa jamii maskini za vijijini; na kukuza ufanisi kwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo.

26. Mheshimiwa Spika, ili taasisi za Muungano ziweze kufanyakazi kwa ufanisi na kusogeza huduma kwa wananchi, jithada za kujenga au kuanzisha Ofisi za kudumu kwa upande wa Zanzibar ziliendelea. Mwaka wa fedha 2014/15, Idara ya Uhamiaji imemaliza ujenzi wa jengo la Makao Makuu Zanzibar, na kulizindua rasmi tarehe 25 Aprili, 2015. Aidha, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imewekwa katika jengo la zamani la uhamiaji na imefungua matawi yake katika wilaya zote za Zanzibar. Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Kamisheni ya Nguvu za Atomiki (TAEC) zimepata Ofisi za Kudumu huko Maruhubi Zanzibar, na taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la taasisi hiyo huko Buyu Zanzibar.

Kuelimisha Umma kuhusu Muungano

27. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano kuitia majarida, vipeperushi, na fulana zenye ujumbe wa Muungano zilizogawiwa kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu Zanzibar, Iringa, Mbeya na Dodoma. Aidha, Ofisi inakamilisha toleo la pili la Kitabu cha taarifa ya mafanikio ya miaka **50** ya Muungano, sanjari na kukamilishwa kwa kitabu cha mafanikio ya masuala ya Muungano katika Awamu ya Nne, kwa ajili ya kuelimisha umma. Pamoja na hayo, semina za elimu ya Muungano kwa wananchi zilifanywa huko Zanzibar. Ofisi kwa kushirikiana na Makumbusho ya Taifa imetoe elimu ya Muungano kwa wanafunzi **1500** wa shule za msingi za Mkoa wa Dar es Salaam, na kuandaa onesho la Muungano wakati wa maadhimisho ya miaka **51** ya Muungano pamoja na kutoa elimu kwa watumishi **80** (Maafisa Viungo) wa Wizara na Taasisi za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano

28. Mheshimiwa Spika, ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umeratibiwa. Katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu, wizara na taasisi zisizo za Muungano za SMT na SMZ hushirikiana katika kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya sera, utaalamu na wataalamu, ushiriki katika masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa, utafiti na ziara za mafunzo.

29. Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, vikao vitano (**5**) vya ushirikiano vimefanya katika sekta zinazosimamia masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; utumishi katika Jamhuri ya Muungano; Uchukuzi; Biashara, na masuala ya utawala bora. Masuala yaliyojadiliwa katika sekta hizo ni pamoja na changamoto na mikakati ya ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; uwiano wa fedha zinazolipwa na wananchi na huduma zinazotolewa; uzoefu katika kuzuia na kupambana na rushwa; na maadili ya viongozi wa umma.

30. Mheshimiwa Spika, masuala mengine yaliyojadiliwa yanahusu nafasi za ajira katika Taasisi za Muungano; kufungua Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Zanzibar; na mikakati ya kudhibiti bidhaa zisizo na viwango, na bandari zisizo rasmi ambazo

zimekuwa mwanya wa kupitisha biashara na wahamiaji haramu, majahazi yasiyosajiliwa na vitendo vingine viovu.

MALENGO YA MWAKA 2015/2016

31. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/16 Ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya kitaifa, ikiwa ni pamoja na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi. Ofisi inalenga kwenye kuongeza ufanisi katika uratibu wa shughuli za Muungano, na kudumisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa manufaa ya Watanzania wote.

32. Mheshimiwa Spika, katika kulitekeleza hilo, Ofisi itaandaa na kuitisha kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kutafakari njia muafaka za kushughulikia masuala ya Muungano. Kikao hicho kitatanguliwa na kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ, kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ na vikao vine **(4)** vya Sekretarieti ya SMT na SMZ.

33. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyengine ya kudumisha Muungano wetu, Ofisi itaendelea kuelimisha umma kuhusu Muungano kupitia redio, luninga, magazeti, majarida, vipeperushi, semina na maonesho ya kitaifa; kuongeza ufanisi katika uratibu wa utekelezaji wa miradi ya jamii inayolenga kuinua kipato kwa kaya masikini Mijini na Vijiji kwa lengo la kuziinua kiuchumi; na kushajiiha wizara au taasisi zisizo za Muungano zenyne kazi zinazoshabihiana SMT na SMZ kuendeleza mashirikiano kwa nia ya kukuza ustawi wa Watanzania.

MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2005 HADI 2015

34. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi 2015 Serikali imekuwa na mafanikio katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Mafanikio hayo ni pamoja na kukua kwa demokrasia nchini; kuimarika kwa ulinzi na usalama; amani na mshikamano; na uhuru wa kuabudu na kuishi popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuundwa kwa Kamati ya Pamoja SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano. Kamati hii imeshughulikia hoja **15** za Muungano ambapo hoja **11** zimefanyiwa kazi kwa mafanikio na kutatta changamoto za Muungano.

35. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Nne ya Serikali, ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano umeimarika baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na hivyo kuimarisha na kuendeleza uhusiano baina ya wananchi wa pande mbili za Muungano.

36. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, ujenzi wa Ofisi na makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Tunguu Zanzibar na jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, Mtaa wa Luthuli Dar es Salaam umefanyika. Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu yamejengwa Zanzibar, Awamu ya kwanza ya Jengo la Sayansi ya Bahari huko Buyu, Zanzibar imekamilika, pamoja na majengo yaliyoainishwa katika Ibara ya **26** ya Kitabu hiki.

37. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza masuala ya Muungano, zipo changamoto zilizojitokeza ambazo ni: utatuzi wa hoja za Muungano kwa pande mbili zenyne mifumo tofauti ya sheria; suala la uelewa wa jamii kuhusu masuala ya Muungano; na ufinyu wa bajeti.

III. HIFADHI ENDELEVU YA MAZINGIRA

MAELEKEZO YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 – 2015 NA UTEKELEZAJI WAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

38. **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya **194** ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2010 – 2015, inaelekeza Serikali kutekeleza masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira hapa nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15 hali halisi ya utekelezaji wa llani hiyo ni kama ifuatavyo:-

"Kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti pamoja na miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Viongozi wa vitongoji, mitaa, vijiji na kata watakiwe kuikagua mara kwa mara miti iliyopandwa ili kuhakikisha inakua. Aidha, miti ipandwe katika maeneo ya shule, barabara, zahanati za vijiji, vituo vya afya na makazi ya watu. Wakuu wa maeneo hayo wahakikishe lengo la kupanda miti linafanikiwa".

39. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza maelekezo haya, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2006 kwa kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti milioni **1.5** kwa mwaka, kwa kila Halmashauri ya Wilaya. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imepokea taarifa za Mikoa **22** kuhusu miti iliyopandwa na kumea kwa mwaka wa fedha 2013/14. Taarifa hizo zinaonesha kuwa miti **217,301,650** ilipandwa na kati ya hiyo miti **181,720,849** imestawi, sawa na asilimia **83.63** ya miti iliyopandwa. **Kiambatisho Na.1** ni taarifa za upandaji miti kitaifa kwa mwaka 2013/14.

40. **Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zilizopanda miti na kustawi kwa zaidi ya asilimia **80** ni **39** ambazo ni **Wilaya za Mbanga, Ilaje, Kyela, Mbeya Vijiji, Siha, Iringa, Kilwa, Ruangwa, Butiama, Musoma, Ranya, Ludewa, Njombe, Makete, Makambako, Wanging'ombe, Uyui, Ulanga, Gairo, Kilombero, Msalala, Kishapu, Shinyanga Vijiji, Shinyanga Mjini, na Maswa, Misungwi, Ukerewe, Mwanza jiji, Ilemela, Newala, Nanyumbu, Mtwara vijiji, Manispaa ya Sumbawanga, Arusha, Meru, Longido, Monduli, Karatu na Kilindi**. Mikoa ambayo Halmashauri zake hazijawasilisha taarifa za upandaji miti kwa mwaka 2013/14 ni: Manyara, Kagera na Geita. Naipongeza Mikoa ambayo wilaya zake zimevuka lengo la upandaji miti, nahimiza mikoa mingine kuongeza juhudhi ili kulinda mazingira ya nchi yetu.

41. **Mheshimiwa Spika**, mashindano ya Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti yameendelea kuhamasishwa nchini katika ngazi za Kaya, Vijiji, Kata, Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa na Mikoa. Makundi mengine ni shule za msingi na sekondari; Vyuo vya Mafunzo/Utafiti; Taasisi za Kijeshi; na Taasisi/Vikundi vya uhamasishaji, uwekezaji na uvezeshaji. Utoaji wa tuzo hii umeimarisha upandaji wa miti nchini. Tuzo hii hutolewa kila baada ya miaka miwili **(2)** na itatolewa tena mwaka 2016 wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, kitaifa. Orodha ya washindi na aina ya Tuzo walizopata zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2** cha Kitabu hiki.

"Serikali za Vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitunge sheria ndogo za hifadhi ya misitu"

42. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi iliendelea kuhimiza Wilaya na Manispaa kutunga sheria ndogo za hifadhi ya misitu, tathmini ya mazingira na usafi wa mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2014/15, Halmashauri za Njombe, Kalambo, Mpanda, Uvinza, Kasulu, Kibondo, Kishapu, na Sengerema zilitunga sheria ndogo za kusimamia utunzaji wa Mazingira katika maeneo yao.

"Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira katika vyanzo vya maji na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa usafi katika fukwe"

43. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuhamasisha na kuhimiza utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi ya Mwaka 2004, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, na Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa nchini.

44. Mheshimiwa Spika, Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imeendelea kuratibu na kutekeleza Mkakati wa Usimamizi wa Mazingira ya Pwani kwa kukamilisha taarifa ya tathmini ya Matumbawe ambayo itasaidia kuweka mikakati ya kuhifadhi maeneo yanayohitaji uangalizi zaidi. Aidha, Baraza limeanza utekelezaji wa mpango wa dharura wa kukabiliana na uchafuzi wa mazingira baharini (Marine Contingency Plan), kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), unaofadhiliwa na Serikali ya Norway.

45. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kukamilisha taratibu za kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Nairobi na Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, kutohana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Kuridhiwa kwa marekebisho ya Mkataba na Itifaki yake yatachangia katika jithada za miradi hii ya kuhakikisha kuwa uchafuzi wa fukwe za nchi yetu unapungua.

“Serikali ichukue hatua ya kuandaa sera na kutunga sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa Mazingira”

46. Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara za Nishati na Madini, Maliasili na Utalii, Kilimo na Mifugo, pamoja na Tume ya Mipango, inaandaa mpango wa kuongeza matumizi ya nishati mbadala, mfano gesi asilia, ili kupunguza matumizi ya mkaa wa miti katika miji mikubwa, kwa kuanza na jiji la Dar-es-Salaam. Maandalizi ya mpango huu ni sehemu ya juhudhi za Ofisi za kupunguza uharibifu wa mazingira na kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini inaendelea kukamilisha Sera ya Uendelezaji wa Nishati nchini ili kuhakikisha matumizi ya nishati mbadala yanaenda sanjari na sera na mipango ya taifa ya kujiletea maendeleo endelevu. Katika mwaka 2015/16, Ofisi itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 itakayosisitiza matumizi ya nishati mbadala ili kuhifadhi mazingira. Aidha, baada ya mapitio ya Sera, Ofisi itaendelea na kupitia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

“Serikali kupunguza gharama za vifaa vya nishati mbadala ili wananchi wanaojenga nyumba za kisasa vijijini watumie nishati hiyo badala ya kuni na mkaa wa miti”

47. Mheshimiwa Spika, kama nilivvolarifu bunge lako tukufu mwaka jana, Serikali imeendelea kusimamia uamuvi wa kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani, kwa asilimia **18** katika vifaa vya gesi na umeme, ili wananchi waweze kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na hivyo kunusuru mazingira yetu. Aidha, gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijijini zimeendelea kubaki shilingi **27,000/=** tu na hivyo kuwafanya watu wengi zaidi vijijini kuunganisha umeme. Aidha, washirika wa Maendeleo, yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wameendelea kuchangia jithada za Serikali kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala, mfano: nishati itokanayo na kinyesi cha mifugo (biogas) na umeme nuru (solar energy).

“Serikali iimarishe usimamizi wa viwanda na biashara ili kutochafua mazingira”

48. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira iliendelea kufanya ukaguzi wa viwanda, biashara na migodi ili shughuli hizo zisichafue mazingira na kuhimiza uzingatiaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na ufuatiliaji wake. Jumla ya viwanda **15** vilifanyiwa ukaguzi wa Mazingira. Viwanda hivyo ni: MM Integrated Steel Mills Ltd; BIDCO Oil & Soap Ltd; Murzah Oil Mills Ltd; Auto Mech Limited; OK

Plastic Limited; Basic Elements Ltd; na Twiga Cement vya Dar es Salaam. Viwanda vingine ni: Azam Fruit and Juices Industry; na Rhino Cement mkoani Pwani; Tanga Cement; Nilecanth Ltd; na Afritex Ltd; na PPTL mkoani Tanga; 21st Century Textile Mills, Morogoro; na Sunflag Textile Mill – Arusha.

49. Mheshimiwa Spika, katika zoezi hilo la ukaguzi, amri za katazo (Environmental Protection Orders) zilitolewa kwa viwanda vinne (**4**); amri za kusitisha shughuli (Stop Orders) zilitolewa kwa viwanda vitatu (**3**); na viwanda vingine vilipewa onyo na kutozwa faini kwa uchafuzi wa mazingira. Aidha, Baraza lilikagua eneo la Vingunguti ambako viwanda vilikuwa vinatiririsha majitaka kwenye Mto Msimbazi. Ukaguzi ulifanyika pia katika eneo la dampo la Pugu Kinyamwezi na maelekezo yalitolewa ya hatua za kuchukua.

50. Mheshimiwa Spika, viwanda na maeneo mengine yaliyofanyiwa ukaguzi wa mazingira na kupewa onyo ni pamoja na: Kiwanda cha Royal Soap and Detergents na Carmel Concrete Plant vilivyopo eneo la viwanda la Mabibo; Mwambao wa fukwe za Kunduchi kuhusu ukongoaji wa meli chakavu; shughuli za gereji katika makazi, eneo la Tabata Kinyerezi – Manispaa ya llala; na maeneo ya uchimbaji mchanga holela Bunju, Kigamboni – Gezaulole na Ubungo nyuma ya majengo ya Shirika la Viwango Tanzania. Amri za kusitisha shughuli za uchimbaji katika maeneo hayo zilitolewa.

51. Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa mazingira ulifanyika pia katika eneo la ujenzi wa mtambo wa kusafisha majitaka wa Mnazi Bay mkoani Mtwara. Baraza lilibaini kasoro na kutoa amri ya kusitisha ujenzi wa bomba la kutiririsha majitaka kutoka kwenye mtambo kwenda bahaarini. Aidha, TPDC walielekezwa eneo ambalo majitaka yanaweza kumwagwa bila kuathiri viumbe bahari.

"Kutekeleza Mradi wa Vijiji vya Mfano vya Hifadhi ya Mazingira (Eco-Villages)"

52. Mheshimiwa Spika, kama niliviyolitaarifu Bunge lako tukufu mwaka jana, awamu ya pili ya Mradi wa Vijiji vya Mfano (Eco-villages) unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya, ulianza kutekelezwa mwaka 2013/14 katika Kanda za Maeneo ya Pwani na Ukanda wa Chini; Maeneo ya Miinuko yenye mvua nyingi kiasi; na Maeneo ya Kanda Kame kwa gharama ya takriban shilingi bilioni **16**. Miradi hii ni muhimu katika kuonyesha mbinu zilizo bora za kuhahikisha shughuli za wananchi za kiuchumi na kijamii haziathiriwi na mabadiliko ya tabianchi. Taasisi tano (**5**) zinashiriki katika utekelezaji wa miradi mitano (**5**). Taasisi hizo ni: Community Forest Pemba (CFP) inayotekeliza Mradi Kisiwani Pemba kwa gharama ya EURO **1,250,000**; Heifer Nederland katika Wilaya ya Igunga kwa gharama ya EURO **2,132,480**; ONGAWA – Ingeniería para el katika Milima ya Usambara Mashariki kwa gharama ya EURO **1,364,449**; Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - Dodoma kwa gharama ya EURO **1,999,802**; na Instituto Oikos Onlus Associazione katika Wilaya ya Arumeru kwa gharama ya EURO **1,796,262.50**. Miradi hii inatarajiwaa kutekelezwa kwa kipindi cha miezi **48** hadi **54** kuanzia mwaka 2014.

"Kufanya Tathmini ya Athari za Kimazingira Katika Miradi ya Maendeleo"

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, jumla ya miradi **870** ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Kati ya Miradi hiyo, 596 ni miradi ya sekta mbalimbali na **274** ni minara ya mawasiliano. Katika kipindi hiki, miradi **640** ilipatiwa Hati ya TAM (Environmental Impact Assesment - EIA Certificates). Baraza liliatuilia miradi **121** katika mikoa ya Mbeya, Katavi na Morogoro, ambapo miradi **42** ni migodi, **13** ni viwanda,

56 ni vituo vya mafuta, hoteli mbili (2), mashamba matatu (3) na mingine minane (8) ya barabara, hospitali na duka la vipuri.

54. Mheshimiwa Spika, Baraza lilipokea maombi ya wataalamu binafsi **229** na makampuni **38** ili kusajiliwa kufanya TAM na Ulagazi wa Mazingira, baada ya uhakiki, wataalamu binafsi **108** na makampuni **25** yamesajiliwa. Napenda kutumia fursa hii kuwasihii wataalam wote wa Mazingira nchini kuzingatia ipasavyo maadili ya kazi yao na maelekezo ya sheria, ili kwa pamoja tuweze kutunza mazingira yetu. Vile vile, maofisa wa Mazingira **35** walipatiwa mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15 NA MALENGO YA MWAKA 2015/16

55. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, sanjari na utekelezaji wa maelekezo ya llani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015, Ofisi ilitekeleza yafuatayo:-

Elimu ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

56. Mheshimiwa Spika, elimu kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira hutolewa katika maadhisho ya Siku ya Mazingira Duniani tarehe 1-5 Juni; maadhisho ya Siku ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa tarehe 17 Juni; na Maadhisho ya Kimataifa ya Tabaka la Ozoni tarehe 15-16 Septemba za kila mwaka kwa kutumia hotuba za viongozi, vipeperushi, mabango, machapisho na vitabu vyenye ujumbe kuhusu masuala ya mazingira. Aidha, Ofisi imeendelea kusambaza nakala za Mpango Kazi wa Taifa wa Mazingira (National Environmental Action Plan - NEAP) wa mwaka 2013-2018 kwa Wizara na Mikoa yote na wadau wengine nchini kwa ajili ya kukuza uelewa wao, kuhusu majukumu waliyonayo katika kuhifadhi na kusimamia mazingira. Kwa mwaka wa fedha 2015/16 Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira.

Ripoti ya Hali ya Mazingira Nchini

57. Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Ripoti ya Pili ya Hali ya Mazingira Nchini ya mwaka 2014, imekamilika, kuchapishwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 22 Aprili, 2015 na Mheshimiwa **Dkt. Mohammed Gharib Bilal**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa ujumla, Ripoti imeonesha kuendelea kuwepo kwa uharibifu wa mazingira nchini pamoja na juhudzi zinazoendelea kufanya. Aidha, Ripoti imebainisha kuwepo kwa changamoto mpya za mazingira hususan, taka zinazotokana na vifaa vya umeme na kielektroniki, viumbe vamizi vigeni, viumbe vilivyo fanyiwa mabadiliko ya kijenetiki na biofueli, na kubainisha mbinu ya kupambana na hayo. Katika kipindi cha mwaka 2015/16, Ofisi itaendelea kusambaza Ripoti hii na kuelimisha na kuhamasisha umma jinsi ya kukabiliana na changamoto zilizobainishwa. Ripoti hii pia itawasilishwa Bungeni.

Tathmini za Athari kwa Mazingira Kimkakati

58. Mheshimiwa Spika, pamoja na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM), Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 imeelekeza pia kufanya kwa Tathmini ya Mazingira Kimkakati (Strategic Environmental Assessment-SEA) katika uandaaji wa sera, miswada, kanuni, mipango, mikakati au programu mbalimbali kabla ya utekelezaji wake. Katika kipindi cha mwaka 2014/15 jumla ya mipango kumi na mbili (12) ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati ilisajiliwa. Kati ya mipango hiyo, jumla ya Ripoti sita (6) za Tathmini ya Mazingira Kimkakati ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji.

59. Mheshimiwa Spika, Ripoti za Tathmini zilizoidhinishwa ni: Mpango wa Ukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania –

SAGCOT); Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Mfumo wa Usafirishaji Tanzania (Comprehensive Transport System Development Master Plan in Tanzania); Mpango wa Uendelezaji wa Eneo la Pwani la Jiji la Dar es Salaam (Waterfront City Development Plan at the Coastal area of Dar es Salaam City); Mpango wa Uendelezaji wa Mji wa Kisasa katika eneo la Tengeru, Wilaya ya Meru, mkoani Arusha (Tengeru Satellite Town Development, Meru District, Arusha Region); Mpango wa Uendelezaji wa Mji wa Kisasa katika eneo la Themsi ya Simba Arusha (Satellite Town Development at Themsi ya Simba Arusha District, Arusha Region); na Mpango Kabambe wa Ukanda Maalum wa Uwekezaji Bagamoyo (Bagamoyo Special Economic Zone Master Plan, 2015).

60. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Ripoti za Tathmini ya Mazingira Kimkakati kwa ajili ya mipango sita (**6**) zitaendelea kuandaliwa na kukamilishwa. Mipango iliyopangwa ni:- Mpango wa Uendelezaji wa Mji wa Kisasa katika eneo la Kibada Kigamboni (Kibada Satellite City Development, Temeke District, Dar es Salaam); Mpango wa Uendelezaji Nishati-Kimiminika Tanzania (Liquid Bio-energy Development in Tanzania); Mpango wa Uendelezaji na Mapitio ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Mikoa ya Mtwara na Ruvuma (Development and Review of the Current strategic development plans for Mtwara na Ruvuma Regions); Tathmini ya Usimamizi, Uchimbaji na Uendelezaji wa Mradi wa Maji ya Ardhini katika eneo la Kimbiji (Comprehensive Ground Water Assessment, Supervision of drilling works, development of aquifer monitoring system and evaluation of environmental impact for the Kimbiji aquifer); Mpango Kabambe wa Mafuta na Gesi (Oil and Gas Master Plan); na Mpango Kabambe wa Mfumo wa Usambazaji wa Nishati Tanzania (Power system Master Plan in Tanzania).

61. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Ofisi inakamilisha Mwongozo wa uandaaji wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati ambao utatumia na sekta na taasisi za Serikali katika kufanya tathmini hizo. Aidha, ninapenda kutumia fursa hii kuzikumbusha wizara na taasisi za Serikali kuzingatia maelekezo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kwa kuandaa ripoti za Tathmini za Mazingira Kimkakati sanjari na maandalizi ya sera, miswada, kanuni, mipango, mikakati au programu katika wizara au taasisi husika.

Hifadhi ya Mazingira katika Maeneo Maalum

62. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilifuatilia na kufanya tathmini ya hali ya mazingira katika Wilaya tatu (**3**) za Kilolo, Mufindi na Kilombero ambazo zimo ndani ya eneo la lindimaji la Kihansi. Aidha, Baraza lilitribu Programu ya Binadamu na Mazingira Hai (Man and Biosphere Reserve), na linaendelea na mchakato wa kuingiza hifadhi za Jozani, Chwaka Bay na Saadani katika mtandao wa Hifadhi hai wa dunia (World Network of Biosphere Reserves). Mafanikio mengine katika kipindi hiki ni: - Kukamilika kwa Taarifa ya hali ya Mazingira katika Mifumo Ikolojia ya Bwawa la Mtera; kukamilika kwa Taarifa ya hali ya Milima ya Kanda ya Magharibi na Nyanda za juu kusini; na kukusanya taarifa zitakazosaidia kuandaa Taarifa ya Pwani.

Udhibiti wa Mifuko ya Plastiki

63. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba uchafuzi wa mazingira kutokana na mifuko ya plastiki unadhibitiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau, imeandaa Rasimu ya kanuni mpya ya mifuko ya plastiki inayoongeza unene wa mifuko kutoka maikroni **30** na kufikia maikroni **50**. Mifuko yenye unene chini ya mikroni **50** haitaruhusiwa kuzalishwa, kuingizwa nchini wala kutumika. Chini ya Kanuni hii baadhi ya bidhaa za plastiki (Polyethylene materials) zitaendelea kutumika kwa ajili ya shughuli muhimu viwandani; kama vile viwanda vya maziwa, na usindikaji wa vyakula. Aidha, Ofisi imewasiliana na Umoja wa Watengenezaji wa Mifuko ya Plastiki - (Plastic Manufacturers Association of Tanzania – PMAT) kuhusu uwekezaji katika eneo la urejelezaji mifuko ya plastiki. Katika mwaka 2015/16 Ofisi kupitia

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira itaendelea kusimamia kanuni inayoruhusu matumizi ya mifuko ya plastiki yenyne unene kiasi cha maikroni **30** na kusitiza wafanya biashara kutokugawa mifuko hiyo bure. Vile vile, Ofisi itaendelea kuelimisha wadau juu ya umuhimu wa udhibiti wa taka za mifuko ya plastiki na kuhimiza matumizi ya mifuko mbadala.

Vituo vya Huduma Kwa Wasafiri na Wasafirishaji

64. Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika barabara kuu nchini, katika kipindi cha mwaka 2015/16, Ofisi kwa kushirikiana na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali itaandaa utaratibu wa ujenzi wa vituo vya huduma kwa wasafiri na wasafirishaji wanaotumia barabara kuu nchini. Vituo hivyo vitasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuongeza usalama kwa kuepusha ajali zinazosababishwa na uchovu wa madereva. Ofisi kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha sekta binafsi na jamii kwa ujumla kuwekeza katika ujenzi wa vituo hivi muhimu. Vituo hivi vitaanza kujengwa katika barabara za Dar es Salaam hadi Tunduma; Dar es salaam hadi Mwanza; na Dar es salaam hadi Mtwara.

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani

65. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yameendelea nchini, Ofisi imewasiliana na Mikoa yote Tanzania Bara kuwakumbusha kuanza maandalizi hayo katika maeneo yao. Maadhimisho hayo hufanyika tarehe **05 Juni** ya kila mwaka. Kwa mwaka huu 2015, maadhimisho hayo yatafanyika Mkoani Tanga. Kaulimbiu ya mwaka huu ni **Ndoto Bilioni Saba. Dunia Moja. Tumia Rasilimali kwa Uangalifu. (Seven Billion Dreams. One Planet. Consume with Care)**.

Mfuko wa Taifa wa Mazingira

66. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, jitihada za kuhakikisha Mfuko wa Taifa wa Mazingira unaanza kufanya kazi zimeendelea. Majadiliano na wadau kuhusu maeneo ya kupata vyanzo vya fedha kwa ajili ya Mfuko yanaendelea. Aidha, Hadidu za rejea za Mtaalam Mwelekezi na Kikosi Kazi cha Kisikta kubaini vyanzo vya fedha vya Mfuko zimeandaliwa. Pamoja na hatua hiyo, Ofisi imefungua Akaunti ya Mfuko na kufanya mawasiliano na Washirika wa Maendeleo, juu ya uanzishwaji wa Mfuko huo, ili waweze kuchangia.

Mfuko wa Mazingira wa Dunia (Global Environment Facility-GEF)

67. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Miradi midogo inayofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia chini ya usimamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP). Chini ya Mfuko huu, miradi midogo saba (**7**) ya jamii, yenyne thamani ya Dola za Marekani **480,507** inatekelezwa. Miradi hiyo inalenga: kuimarisha uwezo wa jamii katika kuhimili mabadiliko ya Tabianchi; kuhifadhi ardhi; kukuza matumizi endelevu ya maliasili; kupunguza umaskini; na kuhifadhi bioanuai na mazingira kwa ujumla. Miradi inatekelezwa katika maeneo ya Wilaya ya Kusini (Makunduchi) Zanzibar na katika mikoa ya Iringa (Pawaga, Kalenga na Isimani), Arusha (Longido), Pwani (Rufiji), Mwanza (Magu) na Morogoro (Uluguru). **Kiambatisho Na.3** cha Kitabu hiki ni Miradi midogo ya hapa nchini inayo fadhiliwa na GEF.

68. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2014 - 2018, Serikali imetengewa jumla ya Dola za Marekani milioni **29.09** kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF). Kikao cha wadau cha kupitia maandiko ya miradi na kugawa fedha hizo kilifanyika mwezi Machi, 2015, ambapo zaidi ya miradi **26** ilichambuliwa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Kitaifa ya Uendeshaji ya GEF kwa ajili ya maamuzi. Katika ya miradi hiyo, jumla ya miradi tisa (**9**) inayohusu Hifadhi ya Bioanuai, Mabadiliko ya Tabianchi, na Usimamizi Endelevu wa Ardhi imepitishwa na kuwasilishwa katika Sekretariati ya Mfuko wa Mazingira wa Dunia kwa hatua zaidi. **Kiambatisho Na.4** ni Miradi iliyopitishwa kufadhiliwa na GEF. Katika mwaka 2015/16, Ofisi itaendelea

kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi inayoendelea kutekelezwa chini ya ufadhilli wa mfuko huu. Aidha, Ofisi itaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka katika Mfuko wa Mazingira wa Dunia.

Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira

Mikataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba huu kwa kufanya yafuatayo: Kushirikiana na wadau kuandaa Ripoti ya Tano ya Mikataba na kuiwasilisha Sekretarieti ya Mikataba; Kuratibu mapitio ya Mpango Mkakati wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai kulingana na Mpango Mpya wa Kimataifa wa mwaka 2011 hadi 2020; Kushiriki, kuandaa na kusambaza kwa wadau taarifa ya maamuzi ya Mkutano wa **12** wa nchi wanachama wa Mikataba wa Bioanuai; na kuendelea kukamilisha taratibu za kuridhia Itifaki ya Nagoya inayohusu Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida Zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki (The Nagoya Protocol on Access and Benefit Sharing of Genetic Resources). Vilevile, Ofisi itaendelea kuratibu uridhiaji wa Itifaki ya Ziada ya Nagoya Kuala-Lumpur, inayohusu Uwajibikaji Kisheria Dhidi ya Athari zitokanazo na Matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa (Nagoya-Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress to the Cartagena Protocol on Biosafety).

Mikataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi

70. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imeendelea kukamilisha taratibu za kuridhia Marekebisho ya Mikataba wa Nairobi, na Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Aidha, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya na Mamlaka za Mabonde kwa kuhimiza utekelezaji wake. Kazi hii itaendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/16.

Mikataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Kyoto

71. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15 Ofisi imeendelea kutekeleza shughuli za mabadiliko ya tabianchi. Moja ya majukumu muhimu ni kushiriki kikamilifu katika majadiliano ili kupata Mikataba mpya wa mabadiliko ya tabianchi ambao unatarajiwa kupitishwa mijini Paris mwezi Desemba, 2015. Madhumuni ya Mikataba huu ni kushirikisha nchi zote duniani kuhakikisha kuwa shughuli za maendeleo hazisababishi joto la dunia kuongezeka kwa zaidi ya nyuzijoto mbili (**2oC**) juu ya kiwango cha sasa, ili kuepuka madhara ya mabadiliko ya tabianchi kwa binadamu na viumbe wengine. Aidha, Mikataba utatoa fursa kwa nchi ambazo tayari zinaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kupewe fedha, teknolojia na kujengewa uwezo wa kuhimili mabidiliko ya tabianchi katika nyanja zote.

72. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba mwaka 2014, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano wa ishirini wa nchi wanachama wa Mikataba wa Mabadiliko ya Tabianchi huko Lima, Peru. Maamuzi muhimu ya Mkutano huu ni makubaliano ya kila nchi kuandaa na kuwasilisha maeneo maalumu yatakayokuwa ni mchango wa nchi husika katika juhudzi za dunia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (Intended Nationally Determined Contributions – INDCs). Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kushirikiana na wadau, inafanya mchanganuo wa maeneo muhimu yatakayokuwa ni mchango wa Tanzania katika juhudzi za dunia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kazi hii ya kuandaa INDCs inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu, na kuwasilishwa kwenye Sekretarieti ya Mikataba.

73. Mheshimiwa Spika, Ofisi imekuwa na jukumu la kumsaidia Mheshimiwa Rais, akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi za Afrika ya Mabadiliko ya Tabianchi (Committee of African Heads of State and Government on Climate Change – CAHOSCC). Ofisi imendaa na kuratibu Mikutano minne (4) ya Kamati hiyo ambayo imefanyika chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Rais, ikiwa ni pamoja na Mkutano Maalumu wa viongozi wakuu wa nchi duniani, kuhusu mabadiliko ya tabianchi ulioitishwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwezi Septemba, 2014. Katika kipindi cha uenyekiti wa CAHOSCC Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira alikuwa Katibu wa Kamati hiyo.

74. Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Mazingira wa Nchi za Afrika (The African Ministerial Conference on Environment – AMCEN) tangu Septemba, 2012 na jukumu hili limeekoma Machi, 2015. Katika kipindi hiki Tanzania kupitia Waziri wa Nchi, wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira imesimamia majukumu ya kutoa miongozo ya usimamizi wa Mazingira katika Bara la Afrika, na kuhakikisha kuwa mahitaji ya msingi ya binadamu yanapatikana na yanakuwa endelevu. Katika kutekeleza majukumu haya, AMCEN imeendelea kutoa miongozo kuhusu masuala ya Mazingira ikiwemo utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Hifadhi ya Mazingira.

75. Mheshimiwa Spika Ofisi imeratibu maandalizi ya Programu maalum ya Bara la Afrika ya Mabadiliko ya tabianchi, (High Level Work Programme on Climate Change Action in Africa – WPCCAA) chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Rais. Programu hii imepitishwa na Mkutano wa Umoja wa Afrika mwezi Januari, 2015 na itakuwa dira ya kuongoza nchi za Afrika katika kushughulikia changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

76. Mheshimiwa Spika, kazi ya kuhuisha masuala ya mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sera na mipango ya maendeleo ya Serikali imeendelea kutekelezwa. Katika mwaka 2014/15, mafanikio ya miradi ya mabadiliko ya tabianchi iliyotekelizwa Zanzibar na kwenye Wilaya za Igunga, Misenyi, Mbinga, yameandikwa na kusambazwa nchini kwa nia ya kueneza elimu iliyopatikana katika maeneo mengine, ili kuhamasisha wananchi walioathirika na mabadiliko ya tabianchi, kuandaa na kutekeleza miradi kama hiyo ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Vile vile, Mradi umeendesha mafunzo ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa Maafisa 18, Madiwani 16, na viongozi wa vijiji 80 wa halmashauri hizo.

77. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani ya Bahari ya Hindi Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kutokana na kuongezeka kwa kina cha bahari. Mradi huu unaotekelizwa katika Wilaya za Bagamoyo, Rufiji, Pangani; na Zanzibar. Katika kipindi hiki, Ofisi imetua mafunzo kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa maafisa 80 kutoka wilaya hizo na Zanzibar. Aidha, kupitia mradi huu Ofisi imeweka wasimamizi wa Mradi katika maeneo unakotekelezwa na kuwapatia usafiri na vitendea kazi.

78. Mheshimiwa Spika, Serikali imefikia makubaliano na Shirika la Umoja wa Mataifa la Huduma za Miradi (United Nations Office for Project Services –UNOPS) ya kufanya upembuzi yakinifu na kuajiri Mkandarasi wa kujenga kuta za bahari za Pangani - Tanga, Kisiwa Panza - Pemba na Kilimani – Unguja. Aidha, katika maeneo ya jiji la Dar es Salaam, hatua za awali kuhusu maandalizi ya ujenzi wa ukuta wa bahari zitaanza mwaka huu katika maeneo ya Ocean Road na Kigamboni (Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Dar es Salaam), sehemu zilizoharibika kutokana na kuongezeka kwa kina cha bahari, na ukarabati wa baadhi ya miundombinu ya majitaka katika manispaa za Jiji la Dar es Salaam.

79. Mheshimiwa Spika, ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, Ofisi imeendelea kutoa mafunzo kwa vikundi vya jamii ya wavuvi na maafisa wa Halmashauri za Manispaa za

Temeke, Kinondoni, Ilala na Jiji la Dar es Salaam, juu ya teknolojia za nishati mbadala, na utunzaji wa mazingira ya pwani dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Mpango Kazi wa Kuhuisha masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi katika eneo la Pwani ya Dar es Salaam unaandaliwa.

80. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, kazi zifuatazo zitatekelezwa katika miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi: kuendelea kuchimba visima vipyta **17** na kujenga mifumo sita (**6**) ya uvunaji wa maji ya mvua Bagamoyo; kupanda mikoko katika Wilaya za Rufiji na Kinondoni, ili kuzuia mmomonyoko wa fukwe za bahari; na kuanza ujenzi wa kuta za bahari za Pangani na Dar es Salaam. Aidha, maeneo mengine ambako shughuli zitatekelezwa ni pamoja na Kisiwa Panza, Mnazi Mmoja na Kilimani –Zanzibar.

81. Mheshimiwa Spika, chini ya Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi Ofisi kwa kushikiana na Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika zimeandaa mikakati na mipango ya kisekta ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi (National Adaptation Plans-NAP). Ofisi pia, inatekeleza mpango wa kujenga uwezo katika juhudhi za upunguzaji wa gesijoto kwa kuzingatia maeneo ambayo yataleta maendeleo endelevu, hasa kuititia upatikanaji wa teknolojia na fedha kutoka katika mifuko ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, kama vile Green Climate Fund na mashirika ya kimataifa. Mpango huu ambaao unafadhiliwa na UNDP unasadia pia kuweka misingi imara ya kuwa na uwezo wa kuandaa mipango ya kupunguza gesi joto zinazosababisha mabadiliko ya tabianchi, bila kuathiri maendeleo ya nchi (Nationally Appropriate Mitigation Actions -NAMAs).

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame

82. Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Usimamizi Endelevu wa Ardhi Nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imepitia Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame, ili uendane na Mkakati wa Miaka **10** (2008 - 2018) wa utekelezaji wa Mkataba. Aidha, Taarifa ya hali ya uharibifu wa Ardhi nchini imeandaliwa na kuelekeza mbinu bora za kunusuru maeneo yaliyoharibiwa. Miongozo ya kuhuisha Programu ya Taifa ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame katika Sera na Mipango ya kisekta imeandaliwa; Vile vile, Ripoti ya Tano ya utekelezaji wa Mkataba na Kitabu cha Mbinu Bora za Usimamizi Endelevu wa Ardhi vimeandaliwa.

83. Mheshimiwa Spika, Ofisi inaendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi miwili ya kupunguza uharibifu wa mazingira ya ardhi katika miinuko ya milima mkoani Kilimanjaro (Reducing Land Degradation on the Highlands of Kilimanjaro Regions). Shughuli zilizo fanyika ni: kutoa mafunzo kwa wadau **900** katika masuala ya kisheria, kibashara na matumizi endelevu ya kuni na mkaa; Ujenzi wa matangi **10** ya maji; na uchimbaji wa mifereji tisa (**9**) na makinga maji. Mradi mwingine ni wa kuhuisha masuala ya usimamizi endelevu wa misitu ya miombo katika Mikoa ya Tabora na Katavi. Wananchi wamewezeshwa kuwa na shughuli mbadala za kuongeza kipato kama ufugaji wa kuku wa kienyeji, ufugaji nyuki, kusindika matunda pori. Vile vile, Mradi umefadhili kikundi cha Akiba na Mikopo – Mbola Uyui ili kuwasaidia wananchi kuweka akiba na kupata mikopo. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa vikundi vyta ufugaji nyuki na mizinga ya kisasa **310**.

84. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/16 Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za kupambana na kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame, na kutekeleza miradi chini ya Mkataba huu.

Mkataba wa Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni Angani

85. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya kitaifa ya kuondokana na matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la hewa ya Ozoni angani. Katika kutekeleza Programu hiyo, mafanikio yaliyopatikana ni:- Mapitio ya mpango wa kuondokana na matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni, inayofadhiliwa na UNDP na UNIDO; na kusambaza jumla ya vifaa **389** vya kuhudumia majokofu, viyoyozi na mitambo ya kupoozea viwandani katika Chuo cha Ufundi cha Arusha; Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam; VETA-Kigoma; VETA-Moshi; VETA Kihonda-Morogoro; VETA-Chang'ombe; VETA-Mgulani (JKT); VETA YMCA - Dar es Salaam; Taasisi ya Teknolojia Karume; Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya; Chuo cha Uvuvi Nyegezi - Mwanza; Chuo cha Uvuvi Mbegani-Bagamoyo; Chuo cha Taifa cha Usafirishaji; na Chuo cha Mafunzo ya Ubaharia - Dar es Salaam.

86. **Mheshimiwa Spika**, warsha ya mafunzo iliyoshirikisha Mafundi **50** wa Majokofu, Viyoyozi na Mitambo ya kupozea viwanda, kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo ilifanyika Jijini Arusha. Washiriki walitoka Mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Dodoma, Morogoro na Singida. Aidha, takwimu za mwaka za ungingizaji na matumizi ya kemikali na bidhaa zenyenye kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni angani zilikuusanya na taarifa kuwasilishwa Sekretariati ya Mkataba. Takwimu hizo zinaonesha kupungua kwa matumizi ya kemikali nchini kwa asilimia **85.7** ukilinganisha na mwaka 1996.

87. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 16 Septemba, 2014, Tanzania iliungana na nchi nyiningine duniani kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Ozoni. Maadhimisho haya yaliifanyika mjini Dodoma ambapo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais -Mazingira alitoa Tamko kwa wanahabari kutoka vyombo vya habari nchini kuhusu umuhimu wa Tabaka la Ozoni kwa afya na mazingira.

88. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba huu nchini kwa kutekeleza kazi zifuatazo:- kukuza uelewa wa jamii kuhusu utekelezaji wa Mkataba na udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la Ozoni; Kuendesha mafunzo ya wadau juu ya utekelezaji wa sheria na kanuni za kusimamia kemikali hizo; kutekeleza Mpango wa kitaifa wa kupunguza/kusitisha matumizi ya kemikali aina ya Hydrochlorofluorocarbons - HCFCs kwa kufuata ratiba iliyowekwa na Mkataba; kukusanya takwimu za ungingizaji na matumizi ya kemikali hizo nchini na kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mkataba kwenye Sekretarieti ya Mkataba.

Mkataba wa Stockholm wa Kudhibiti Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu (Persistent Organic Pollutants)

89. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2014/15, mapitio ya Mpango wa Taifa wa utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm yaliifanyika, ili kubainisha hali ya kemikali hizo nchini na hatua zinazochukuliwa kudhibiti athari zake. Kazi hii ilihuisha kukusanya takwimu za kemikali zinazodhibitiwa na Mkataba huu katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Shinyanga na Mwanza. Vile vile, ukaguzi ulifanyika katika maeneo yaliyoharibiwa na kemikali hizo katika mikoa ya Arusha na Morogoro. Aidha, mafunzo ya kukuza uelewa wa jamii kuhusu usimamizi bora wa kemikali hizo, yaliifanyika jijini Dar es Salaam. Mafunzo hayo yaliyoshirikisha wataalamu **55** kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Kilimo, Misitu na Maliasili – Zanzibar; Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO); Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Zanzibar; Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali; Shirika la Usambazaji wa Umeme Tanzania bara (TANESCO); Chuo Kikuu cha Ardhi; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa

Mazingira; na Ofisi ya Makamu wa Rais. Utafiti umebainisha kuwa kemikali mpya zilizoongezwa kwenye Mkataba zipo nchini.

90. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na UNEP imeanzisha mtandao wa kupeana taarifa unaojumuisha wadau wote wanaosimamia Kemikali nchini. Mtandao huo unajulikana kama *Chemicals Information Exchange Network - CIEN*. Wataalam **25** kutoka Wizara, Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali walipatiwa mafunzo ya kukusanya na kupeana taarifa zinazohusu kemikali, kupitia mtandao huu. Mtandao huu unalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa kutumia tovuti yenye anwani www.estis.net/sites/cien-tanza. Tovuti hii ina taarifa zinazohusu sera, sheria, mikakati na Miongozo kutoka taasisi zinazohusika na usimamizi endelevu wa matumizi ya kemikali nchini.

91. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2015/16, Ofisi itakamilisha mapitio ya Mpango wa Taifa wa utekelezaji wa Mkataba; na itatoa elimu na kukuza uelewa kwa wadau kuhusu madhara kwa afya na mazingira yanayosababishwa na kemikali za awali na zile mpya zinazodhibitiwa na Mkataba. Aidha, itahamasisha matumizi ya kemikali mbadala zilizopo; itachapisha na kusambaza nakala za Mpango huo kwa wadau; na kuandaa ripoti ya utekelezaji wa Mkataba huu, na kuiwasilisha Sekretarieti ya Mkataba.

Mkataba wa Basel kuhusu Udhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu Bainya ya Nchi na Nchi na Mkataba wa Bamako unaozuia Uingizaji wa Taka za Sumu Barani Afrika

92. Mheshimiwa Spika, kupitia mkataba huu, Ofisi imefanya utafiti kuhusu usimamizi endelevu wa matairi chakavu na yaliyokwisha muda wa kutumika. Utafiti huu ulifanyika ili kubainisha changamoto na hatua za kudhibiti taka hizo; Warsha ya kubadilishana uzoefu katika usimamizi wa taka za matairi ilifanyika Dar es Salaam na wadau **30** walishiriki Ufutiliaji na ukaguzi wa tani **3000** za taka hatarishi za betri chakavu za magari ulifanyika, na kibali kutolewa kwa kampuni ya TANKO ya Dar es Salaam, kusafirisha taka hizo kwenda nchini Korea kwa ajili ya urejelezaji. Aidha, ufutiliaji na ukaguzi wa tani **200** za taka hatarishi za vifaa vya umeme na elektroniki ulifanyika na kibali kilitolewa kwa Kampuni ya OK Plastic Ltd, ya Dar es Salaam kusafirisha taka hizo kwenda Ubeligiji kwa ajili ya urejelezaji.

93. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba iliyotajwa.

MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2005 HADI 2015

94. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia hifadhi ya mazingira nchini, mafanikio yafuatayo yamepatikana katika kipindi hiki katika kusimamia utekelezaji Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 :-

Kanuni 25 na Miongozo 10 vimeandalila. Aidha, Miongozo ilivoandalila inatumika katika kuandaa Mipango Kazi ya Mazingira katika ngazi ya Wizara na Serikali za Mitaa ili kupunguza uharibifu wa mazingira nchini. Mafanikio mengine ni kutolewa kwa Ripoti mbili (2) za Hali ya Mazingira nchini ambapo Ripoti ya kwanza ilitolewa mwaka 2008 na ya pili mwaka 2014. Ripoti hizi zimeonesha kuendelea kuwepo kwa uharibifu wa mazingira nchini, pamoja na juhudhi zinazoendelea kufanyika. Aidha, Ripoti ya mwaka 2014 imebainisha kuwepo kwa changamoto mpya za mazingira. Ripoti hizi ni muhimu katika kuandaa mipango ya maendeleo.

95. Mheshimiwa Spika, Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imendelea kusimamia na kuhakikisha kwamba Miradi ya maendeleo inafanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Miradi ilifanyiwa Tathmini za Athari kwa Mazingira na

vyeti vya TAM **1,846** vilitolewa. Hatua hizi zimesaidia kupunguza athari kwa mazingira na hivyo kuchangia maendeleo endelevu.

96. Mheshimiwa Spika, jumla ya viwanda **935**, migodi mikubwa na ya kati **121**, vituo vya mafuta **161**, mahoteli ya kitalii **74**, mashamba makubwa matatu (**3**) yalifanyiwa ukaguzi, na hatua za kisheria kuchukuliwa, ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

97. Mheshimiwa Spika, katika kuoanisha maendeleo endelevu na kupunguza umaskini, Baraza liliandaa Agenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mazingira. Vilevile, tathmini ya hali ya milima imeandaliwa kwa Kanda za Kusini, Magharibi na Nyanda za Juu Kusini. Taarifa hizi zimesaidia kuainisha maeneo ambayo yanahitaji uhifadhi maalumu. Elimu ya hifadhi ya mazingira kwa umma imetolewa kupitia maadhisho na maonesho ya Siku ya Mazingira Afrika; Siku ya Mazingira Duniani; Siku ya Utumishi wa Umma; Siku ya Wakulima Nanenane na Siku ya Ozoni Duniani. Aidha, elimu ilitolewa pia kwa kutumia njia zifuatazo: vipeperushi, mabango na vitini; magari ya matangazo, televisheni, redio na makala kwenye magazeti; na maonesho ya matumizi ya majiko banifu. Vilevile, elimu kuhusu uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira na TAM imetolewa kwa Maafisa Mazingira wa Serikali za Mitaa katika Mikoa yote ya Tanzania bara. Elimu inayoendelea kutolewa imechangia katika utekelezaji wa Sheria ya Mazingira na kuongeza uelewa wa jamii na hivyo kupunguza uharibifu wa Mazingira.

98. Mheshimiwa Spika, Serikali imepitisha mikakati miwili (**2**) kwa lengo la kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji, mazingira ya ardhi na misitu. Mkakati hiyo ni: Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2006; na Mkakati wa Hatua za Haraka za kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka 2008. Hatua hizi zimesaidia kuimarisha hifadhi ya mabonde na vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti imetolewa mara tatu. Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji Miti inayozitaka kila Halmashauri nchini kupanda miti **1,500,000** kila mwaka imeendelea kutekelezwa. Kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2015 Ofisi ya Makamu wa Rais ilipokea taarifa za upandaji miti kutoka mikoani, zinazoonesha kuwa miti **1,491,870,192** ilipandwa na kati ya hiyo miti **1,139,473,928** imestawi, sawa na asilimia **76.2**.

99. Mheshimiwa Spika, uratibu wa utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira imewezesha kuandaliwa kwa Mipango na Programu ifuatayo:- Mpango kazi wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2013-2018); Mpango wa Taifa wa Kusimamia Kemikali Zinazodumu kwa Muda Mrefu katika Mazingira wa mwaka 2007; Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ya Mwaka 2007; Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame; na Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ucaa Unaotokana na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu. Aidha, Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mkakati wa Mawasiliano wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi imeandaliwa na inaendelea kutekelezwa.

100. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira, changamoto zifuatazo zimejitokeza:- Sekta, Serikali za Mitaa na wadau wengine walioainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kutotekeleza matakwa ya Sheria kwa ukamilifu wakidhani kuwa, utekelezaji wa Sheria hii ni jukumu la Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza pekee; Sekta na Serikali za Mitaa kutohuisha na kutekeleza kikamilifu masuala ya mazingira katika Mipango na bajeti zao; Ufinyu wa bajeti unaosababisha kutotekelezwa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa, katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na Serikali za Mitaa; Uhaba wa watumishi na vitendea kazi katika kusimamia masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira katika sekta zote; Uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya hifadhi

na usimamizi wa Mazingira; Athari za mabadiiko ya Tabianchi; Kukosekana kwa takwimu sahihi za mazingira na kwa wakati; na hali ya umaskini katika jamii.

IV. MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

101. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imeendelea kuwawezesha watumishi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika kipindi hiki, watumishi **66** waliwezesha kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi, yanayohusiana na taaluma zao, ili kuongeza ujuzi mbalimbali na uwezo katika utendaji wa kazi. Aidha, Ofisi imejaza nafasi za ajira mpya **15**; kuwapandisha vyeo watumishi **29**; na kuwabadilisha kada watumishi wawili (**2**) wenye sifa. Taarifa za watumishi wa Ofisi zimehakikiwa na kuboreshwa kwa kutumia mfumo wa taarifa za watumishi na mishahara (Human Capital Management Information System).

102. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki maslahi, stahili na haki za watumishi zimeendelea kutolewa kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, taratibu na Miongozo iliyotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi imeendelea kutekeleza Mfumo wa Wazi wa mapitio na tathmini ya utendaji kazi wa watumishi (Open Performance Review Appraisal System - OPRAS).

103. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa 2014/15 Ofisi imeendelea kuimarisha na kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kufanikisha upatikanaji wa vitendea kazi kwa kuzingatia uwezo kifedha. Aidha, ukamilishwaji wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, Awamu ya Pili, lilitopo Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam pamoja na Ofisi na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Tunguu Zanzibar umesimamiwa kikamilifu. Aidha, Mradi wa Jengo la Ofisi za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, eneo la Regent Estate, Dar es Salaam unaendelea kukamilisha maandalizi ya michoro ya ujenzi, na pia kukamilisha mazungumzo ya kujenga jengo hilo kwa kushirikiana na mbia.

104. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2014/15 Ofisi iliendelea kuzingatia misingi ya utawala bora, demokrasia na ushirikishwaji wa watumishi mahala pa kazi katika kupanga na kutekeleza majukumu ya Ofisi, kuititia vikao viwili (**2**) vya Baraza la Wafanyakazi pamoja na vikao vya Idara na Vitengo.

105. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki Ofisi imeimarisha mahusiano, ushirikiano na mshikamano kwa watumishi wake na watumishi wa Ofisi nyingine za Serikali kuititia michezo ya SHIMWI iliyofanyika Morogoro na SHIMUTA iliyofanyika Tanga. Aidha, watumishi wameshiriki kikamilifu katika mazoezi ya viungo, ili kuimarisha afya zao na kuwajengea ukakamavu na hatimaye kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

106. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2015/16 Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu iliyo kabidhiwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo iliyowekwa katika Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi itaendelea kutathmini utendaji kazi wa watumishi kwa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi kwa watumishi (Open Performance Review and Appraisal System – OPRAS). Aidha, kumbukumbu za watumishi zitaendelea kuboreshwa kwa kutumia Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Mishahara (Human Capital Management Information System), pamoja na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kutekeleza shughuli zilizopangwa.

107. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2015/16 Ofisi itaendelea kuratibu utoaji wa elimu ya UKIMWI kwa watumishi wake na kuwashawishi kupima afya zao kwa hiyari, kuwapatia ushauri nasaha na utoaji huduma kwa watumishi watakaobainika kuwa na maambukizi. Aidha, Ofisi

itendelea kuwapatia watumishi stahili, maslahi na haki zao ikiwa ni pamoja na kuwapandisha vyeo na kuwathibitisha kazini, kwa kuzingatia sifa na miundo inayotawala kada zao, na kuwapatia vitendea kazi. Nafasi mpya za ajira thelathini na moja (**31**) zinatarajiwa kujazwa kwa kuzingatia ikama itakayoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

108. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Ofisi itasimamia ukarabati wa jengo kuu la Ofisi lililopo Mtaa wa Luthuli na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais yaliyopo Oysterbay – Dar es Salaam, Kilimani Dodoma na Wete Pemba. Aidha, Ofisi za Baraza zitafanyiwa ukarabati mdogo ili kuboresha mazingira ya kazi katika majengo yaliyopo.

VI. SHUKRANI NA HITIMISHO

109. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mawaziri wenzangu, Mheshimiwa Mhandisi **Dkt. Binilith Satano Mahenge (Mb.)**, Waziri wa Nchi mwenye dhamana ya Mazingira, na Mheshimiwa **Stephen Julius Masele (Mb.)**, Naibu Waziri – Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano na utendaji wao thabiti na makini, katika kutekeleza majukumu ya Ofisi.

110. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Watendaji Wakuu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, **Bw. Sazi Bundara Salula** - Katibu Mkuu, Mhandisi **Angelina Elias Madete** – Naibu Katibu Mkuu, na Mhandisi **Bonaventure Thobias Baya** - Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Nawashukuru na kuwapongeza pia Wakuu wa Idara na Vitengo, na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa juhud zao za dhati, katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Vile vile, napenda kuwashukuru wale wote walioituwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na kufanikisha kuandaan mipango ya mwaka wa fedha 2015/16 na hivyo kustawisha hoja ambayo nimeiwasilisha hapa leo.

111. Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii ya kipekee, kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi, kwa mwaka wa fedha 2014/15. Baadhi ya nchi na Mashirika ya Kimataifa yafuatayo yameshiriki katika kusaidia ufanikishaji wa shughuli zilizolengwa:- Serikali ya Marekani; Serikali ya Norway; Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Umoja wa Nchi za Ulaya (EU); Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF); Benki ya Dunia (IDA); Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA); Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA); World Wildlife Fund (WWF); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); International Institute of Tropical Agriculture – (IITA); Taasisi ya Kimataifa Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE); na Sekta Binafsi. Napenda kuwaomba washirika wa maendeleo kuendelea kushirikiana nasi mwaka wa fedha 2015/16 katika kufikia malengo yaliyowekwa ya kuhifadhi Mazingira na kudumisha Muungano wetu.

VII. MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2015/16

112. Mheshimiwa Spika, ili Ofisi ya Makamu wa Rais, iweze kutekeleza ipasavyo malengo yaliyoelezwa katika Hotuba hii, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka 2015/16 kama ifuatavyo:

FUNGU 26: MAKAMU WA RAIS

113. Mheshimiwa Spika, Ofisi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **5,079,085,000/=** fedha za Matumizi ya Kawaida kwa ajili ya Fungu hilo. Kiasi hicho kinajumuisha fedha za Mishahara shilingi **1,480,676,000/=** na fedha za Matumizi Mengineyo shilingi **3,598,409,000/=**

FUNGU 31: OFISI YA MAKAMU WA RAIS

114. Mheshimiwa Spika, Ofisi inaombwa kuidhinishiwa jumla ya shilingi **38,077,215,000/=** zikijumuisha fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi **33,558,368,000/=** na fedha za Maendeleo shilingi **4,518,847,000/=**. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha shilingi **3,200,337,000/=** Mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais; na shilingi **30,358,031,000/=** Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Matumizi Mengineyo zinajumuisha shilingi **22,400,000,000/=** gawio kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; shilingi **3,592,326,000/=** ruzuku kwa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na kiasi kinachosalia cha shilingi **4,365,705,000/=** ni fedha za Matumizi Mengineyo za Idara na Vitengo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa upande wa fedha za Maendeleo zinajumuisha shilingi **3,500,000,000/=** fedha za ndani; na shilingi **1,018,847,000/=** fedha za nje.

115. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja.

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono. Kama nilivyosema, sasa hivi tuna mgeni itabidi niahirishhe kikao ili tumkaribishe mgeni wetu halafu tutarejea baadaye. Kwenye meza zenu kuna earphones, Channel 0 ni Portugese – Kiswahili; Channel 1 ni Kiswahili – Portugese; Channel 2 ni English. Tumependa tuwe na *simultaneous translation* yaani msikie wakati anazungumza badala ya kuzungumza kisha tupate tafsiri. Kwa hiyo, naomba tu hivyo vifaa viweze kufanya kazi, inawezekana visifanye kazi, kama havifanyi kazi kila mtu akae hivyo hivyo tu, tutamsimulia baadaye, tafadhali. Msianze Mwongozo wa Spika, havisemi, aah, please mnyamaze hivyo hivyo. (Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba wale niliowaomba waende kumpokea mgeni watoke. Waheshimiwa Wabunge wengine ingependeza zaidi mkakaa hapa lakini mnawenza kuongea kidogo kidogo humu ndani ama kwenda kunawa mikono, si hoja, lakini tukibakia humu ndani itakuwa vizuri zaidi.

Kwa hiyo, ninaahirisha kikao cha Bunge mpaka saa 5.30. Ninaahirisha kwa hiyo msimame tu.

(Saa 05.01 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Saa 05. 30 Asubuhi)

(Saa 5.49 asubuhi Bunge lilirudia)

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaambia, leo tumepata bahati ya kufikiwa na mgeni. Mgeni huyu ni Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi. Tunayo furaha sana kumpokea Mheshimiwa Rais katika Ukumbi wetu wa Bunge Dodoma, mahali ambapo Bunge linakaa. (Makofi)

Ninachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuamua kumpanga mgeni wetu huyu aje pia kutusalimia sisi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mkae.

Kwa heshima kubwa kabisa, ninamwalika mgeni wetu aweze kulihutubia Bunge, Mheshimiwa Rais! (Makofi)

HON. FILIPE JACINTO NYUSI - PRESIDENT OF REPUBLIC DE MOZAMBIQUE: Honourable Anne Semamba Makinda, Speaker of the National Assembly of the United Republic of Tanzania,

Honourable Jakaya Kikwete, President of the United Republic of Tanzania, Members of the Diplomatic Corp Accredited to the United Republic of Tanzania, Ladies and Gentlemen,

I am very honoured to address you and through you the people of the Republic of Tanzania, to whom we convey the most cordial greetings of the people from your sister country of the Republic of Mozambique. (Applauses)

Let me first of all express, on behalf of my delegation and indeed on my own behalf, our profound satisfaction and gratitude for the warm reception and hospitality accorded to us by the people and government of the United Republic of Tanzania since our arrival in the beautiful and historic capital, Dar es Salaam, then Zanzibar and now, here in Dodoma, the political capital of this sister country.

Upon arrived in this country, indeed, we felt we were at home, for this is a reunion with the same mother land, the same people who side by side with the Mozambican people have written the history of our emancipation.

This is our first state visit after inauguration as the President of the Republic of Mozambique on 15th January 2015, following general, Presidential, Parliamentary and Provincial Assembly Elections held on 15th October, 2014.

We have chosen to visit the United Republic of Tanzania first, because we keep and preserve, very fondly, historic friendly, solidarity and cooperation ties we have always maintained with the people and government of this country, not only before and during the national liberation struggle, but also throughout the building and consolidation process of Mozambique's Independence.

We are here, therefore to reaffirm our unwavering desire to continue consolidating further the friendly and sisterly bonds sown by Mwalimu Nyerere, Eduardo Mondlane, Samora Machel and followed by our successive Presidents both in Tanzania and in Mozambique. All this is for the sake of welfare and sustainable development of our two sister countries and peoples. (Applauses)

In our country, the wise and almost prophetic words, delivered by Mwalimu Nyerere, during the year of our independence, when he visited us and, I quote: "Mozambique is in the high sea" end of quote, are still remembered. With these words Mwalimu wanted to warn us on the difficulties and hiccups/cliffs we would have to face to achieve the desired development by all Mozambicans, without any distinction, after attaining political independence. (Applauses)

These words from the speech of Late Mwalimu Nyerere, which were immediately studied in school books in our country, are still cherished by our history and they always come up, as on a daily basis we recall the advice we received when we were still less than a year after independence.

We have come to the land of Mwalimu Nyerere to say the high sea is being crossed. Each hiccup or bottleneck has received adequate treatment. The new cycle we are leading, we have chosen that the crossing will only be possible when all of us sail on the same boat, in peace, harmony and national unity. (Applauses)

Were doing all we can so that no Mozambican attempts to travel on a different boat, because torments lying ahead should be tackled collectively and the input of every Mozambican is important so that its effect does not impact in the way that the enemies of our people, including poverty in the first place, would desire.

The boat whose rudder is under our responsibility, accept and must carry all Mozambicans, without distinction of religious belief, political, sex, race or any kind of discrimination and embracing one another singing peace, waving national unity and social harmony, enjoy together the fruits of freedom. This is one of the lessons learned from this school, Tanzania, where we always come to re-energize and re-invigorate ourselves. We are willing to share our experience which results from our journey in the democratic process in Mozambique.

Your Excellencies, Ladies and Gentlemen, our visit to this House of the People, the National Assembly of the Republic of Tanzania, constitutes a very special occasion to consolidate our bilateral relations and, in particular, our efforts aimed enhancing cooperation and exchange of experience in the exercise of democratic rule. (Applauses)

As I have mentioned early on, the Republic of Mozambique has held on 15 October 2014, for the fifth consecutive time, its Presidential, Parliamentary and Provincial Assembly Elections from which this government and the Honorable MPs that accompany us in this delegation emerged. They represent the 250 MPs that our National Assembly comprises.

The National Assembly is here represented because we also want this occasion to be used, to encourage bilateral cooperation and exchange of experiences between the two legislatures and oversight bodies of governance exercise in our two countries.

We have followed with keen interests the activities of this National Assembly and in particular, the patriotic and sovereign spirit in which you have discussed and built consensus on different matters of national interest. We want, therefore, to benefit from that experience, especially, during this phase when Mozambique focuses on the consolidation of national identity, and democratic governance.

Just like here, in Mozambique the National Assembly plays a critical role in enacting national laws and in the oversight to governing activities. But the main responsibility rests on the legitimate incarnation and presentation of the desires of the people. This is where we derive our respect and our commitment to work for common good.

In this regard, since we started our governing activities in Mozambique we have worked with the National Assembly to deepen and consolidate national unity, the rule of law, the culture of accountability, fight on corruption, reciprocal oversight of day to day activities and, above all, in the approval of the Government Five Year Programme and National Budget, including its respective implementation. These tasks help us to cross the high sea.

Our National Assembly has been experiencing positive and encouraging developments. But we want its performance increasingly strengthened through interaction and networking with other National Assemblies, like this one, because out of this engagement and combination of synergies, bilateral and, indeed regional responses for common challenges will emerge, for the welfare and progress of our two countries and the region.

We are of the view that MPs from two countries have a patriotic duty to promote and cement the prevailing historical and friendly coexistence between our countries, free movement of people, goods and services and particularly, entrenching cross border development as a key factor for prevention and elimination of territorial conflicts. (Applauses)

In our official conversations with the government of the United Republic of Tanzania we have expressed our openness to sign bilateral agreements that enable our relevant authorities to extend the length of stay of our citizen in each of the countries as a way to cement our friendly ties and territorial contiguity. (Applauses)

We have brought along in this visit, the institution responsible for promoting the economy in Mozambique so that, with Tanzanian business people they can develop business partnerships and, in this way, entrepreneurs from both countries can share benefits arising from the use of opportunities, generating wealth and developing existing economic potential in the two countries. (Applauses)

It is high time that our historic sisterhood and brotherhood, is not only translated into political speeches of ours, but should also be turned into actions that go a long way in consolidating our historic relation through concrete acts of solidarity, sharing of historic, social and economic values.

We are happy with the exchange programmes we are developing with Tanzania in the areas of basic and higher education, tourism, among others, particularly local government, as it is this kind of exchanges that will yield and multiply the seeds of our friendship, solidarity, peaceful coexistence and interaction between future generations of both countries. (Applauses)

We count on the cooperation on each and every one of the MPs in promoting harmonious and peaceful exchanges and interactions between our countries and peoples. (Applauses)

We should jointly commit ourselves as we look for solutions to common problems arising from illegal migration, transnational and cross boarder crime, international terrorism, maritime, piracy and other forms of international extremism. These and other challenges can only be overcome, through a combination of efforts between governments and Legislatures like National Assemblies and other stakeholders in neighbouring States and the region. (Applauses)

Your Excellencies, Members of Parliament, Ladies and Gentlemen, let me once again reiterate our personal commitment and of my government in furthering our historical friendly, solidarity and cooperation relations for the benefit of our two countries and peoples. (Applauses)

In this regard, we invite Tanzanian people through you, Honourable MPs, to actively participate in the building and consolidation of unity and understanding between our two peoples, and side by side, in peace and commit to the development of our contiguous resources for the benefit of our two countries and peoples. (Applauses)

Thank you very much, karibuni Msumbiji. Ahsante sana. (Makofi)

(*Hapa Wabunge fulani walishangilia kwa
kuimba na kupiga makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Huyu aliyejewa anaimbisha ni Mwenyekiti wa Chama cha Urafiki kati ya wananchi wa Msumbiji na wananchi wa Tanzania. Kwa hiyo, aliyoafanya hapa siyo ajali ndivyo ilivyo. (Makofii)

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Msumbiji - Rais Filipe Jacinto Nyusi, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kayanza Peter Pinda - Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri kutoka Serikali ya Msumbiji na viongozi mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mabalozi, wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Kwa niaba ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote, ninapenda Mheshimiwa Rais kukupongeza kwa dhati kwa kuchaguliwa kwako kuwa Rais wa watu wa Msumbiji. Tunakupongeza sana kwa sababu uchaguzi ulifanyika hivi juzi, lakini kwa heshima umependa kuja Tanzania kwa mara yako ya kwanza na kuja kulihutubia Bunge. (Makofii)

Hii ni heshima kubwa sana kwa nchi yetu na ni heshima kubwa sana kwetu sisi Wabunge. Ninadhani hujakosea kwa sababu kupitia kwetu sisi umewasalimia Watanzania wote. Sisi Bunge letu linapoendeshwa nchi nzima inaona, inasikia, kwa hiyo, wamekuona na wamekusikia, maneno yako matamu uliyoyasema hakika umegusa nyoyo za Watanzania walio wengi. (Makofii)

Mheshimiwa Rais hii ni ziara yako ya kwanza nje ya Msumbiji tangu uchaguliwe kuwa Rais wa Taifa hili kubwa. Aidha, wewe umeweka historia ya kuwa Rais wa Kwanza wa Msumbiji kulihutubia Bunge la Jamhuri ya Tanzania, ahsante sana. (Makofii)

Ninaomba kutumia fursa hii kukushukuru kwa dhati kwa heshima kubwa uliyolipa Bunge hili la Kumi na wananchi wa Tanzania kwa ujumla, kwa kuja kulihutubia Bunge siku hii ya leo. Kitendo hiki siyo tu cha kihistoria, bali ni kielelezo cha udugu na ushirikiano uliopo baina nchi zetu mbili. (Makofii)

Kwa niaba ya Wabunge wote, ninakushukuru sana kwa mara nyingine tena kwa heshima hii kubwa uliyotupa.

Mheshimiwa Rais, wananchi wa Tanzania na Msumbiji wamekuwa na uhusiano wa karibu wa kindugu hata kabla ya Uhuru wa nchi hizi mbili. Aidha, Serikai za awamu zote za nchi zetu, tangu uongozi wa waasisi wa Mataifa haya, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Samora Machel, zimechukua hatua madhubuti kukuza uhusiano wa kidiplomasia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. (Makofii)

Ama hakika ziara yako hapa nchini na uamuzi la kulihutubia Bunge hili siku ya leo ni kielelezo cha jitihada za kukuza na kuendeleza uhusiano huo wa kihistoria. (Makofii)

Mheshimiwa Rais na wageni waalikwa, katika Medani ya za Kibunge, Mabunge ya nchi zetu mbili yamekuwa na ushirikiano wa karibu wa muda mrefu. Mabunge yetu ni wanachama wa Jukwaa la Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC Parliamentary Forum), Bunge la Afrika pamoja na Chama cha Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola (Commonwealth Parliamentary Association).

Kupitia vyama hivi, Mabunge haya mawili yamekuwa yakishiriki kwenye mikutano, semina, makongamano na warsha kuhusu masuala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kijinsia. Aidha, kumekuwa na ziara za mara kwa mara za mafunzo baina ya Mabunge yetu haya

mawili, zikuhusisha Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge. Tutaendelea kukuza uhusiano huu kwa faida ya vyombo hivi viwili vya uwakilishi wa watu.

Mheshimiwa Rais, hivi sasa aliyekuwa Spika wa Bunge la Msumbiji anagombea Urais wa Bunge la Afrika. Kwa hiyo, hata huko tunashirikiana kuhakikisha anapata Urais huo. Mimi nilipogombea Urais wa SADC Parliamentary Forum, Msumbiji ilikuwa tusimame pamoja, lakini niliposema mimi ninasimama, walijiondoa wakaniachia nafasi. (Makofii)

Spika wa Msumbiji ni dada yangu, rafiki yangu, ni rafiki yetu mkubwa sana. Kwa hiyo, ninapenda kuhitimisha kwa mara nyingine tena kwa kukushukuru sana kwa kuja Dodoma na kulihutubia Bunge letu na kupitia Bunge hili wananchi wote wa Tanzania. Aidha, ninakushukuru kwa hotuba yako fasaha, iliyoelezea dira, mwelekeo na vipaumbele vya Serikali yako kwa siku zijazo. Ninakutakia kila la heri na mafanikio katika safari yako uliyoianza ya kuwaletea maendeleo Wananchi wa Msumbiji. (Makofii)

Mwisho, ninayo heshima kukukabidhi baadaye kule nje zawadi ya picha ya Ukumbi wa Bunge hili Tukufu ikiwa ni kumbukumbu muhimu ya ziara na hotuba yako hapa Bungeni. Zawadi hiyo ni kama itakavyoonekana kwenye screen hapo juu. Mgeni hawezি kuona screen huku nyuma, lakini tutampa. Zawadi hiyo ipo inaonesha Ukumbi wetu. Toka nchi yetu ipate Uhuru, hili ndiyo Bunge letu la kwanza kabisa la Tanzania kuwa na Ukumbi wake na sehemu yake ni hii ya kwanza kabisa. Kwa hiyo, nitakukabidhi rasmi zawadi hiyo huko nje wakati tunapiga picha. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima kubwa sana, ninashukuru kwa kunisikiliza na ninamshukuru sana mgeni wetu. Ahsanteni sana. (Makofii)

Kwa sababu ni Vikao vya Bunge kila wakati tuna taratibu zetu. Kwa hiyo, baada ya kusema haya yote, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasema leo siyo siku yake, kwa hiyo, mumwone kama alivyo, asije akaharibu utamu ulioletwa na mgeni na wengine hapa sasa kuna majoto majoto haya wakaongeza na mengine. (Kicheko)

Kwa hiyo, amesema leo yeye hayumo amemaliza na kwa sababu hiyo basi, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa saba mchana. (Makofii)

(Hapa Maandamano ya Spika, Rais wa Msumbiji
Mhe. Filipe Jacinto Nyusi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya
Mrisho Kikwete walitoka Ukumbini)

(Saa 6.20 mchana Bunge lilitishwa hadi saa 7.00 mchana)
(Saa 7.00 mchana Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016
Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano)**

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Na kama mtakavyokumbuka, hapo mapema Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano) kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ilishasomwa na Mheshimiwa Waziri Samia Suluhi.

Sasa namwomba Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, aje atusomee Hotuba yake. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Rweikiza. Mheshimiwa Rweikiza karibu!

TAARIFA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za 99 na ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

NAIBU SPIKA: Kwa makubaliano yetu ya jana, utakumbuka Mwenyekiti ni dakika ishirini. Ahsante.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu ya Kamati kuhusiana na uchambuzi wa bajeti kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mafungu mawili chini ya ofisi hii ambayo ni Fungu 26 - Makamu wa Rais na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Samia Suluhi Hassan, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), mnamo tarehe 6 Mei, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) inahusika na majukumu ya Kitaifa ikiwemo kuratibu mambo yote ya Muungano na ushirikiano, katika mambo yote yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka 2014/2015, Kamati ilitaka kujua mambo makuu mawili yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

(ii) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ilitoa ushauri, mapendeleko na maoni yenye lengo la kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wa ofisi hii.

Ushauri wa Kamati ulitekelezwa. Mifano ya uzingatiaji huo ni kama ushauri ufuatao:-

Kwanza, Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu na faida ambazo zinatokana na Muungano kwa pande zote mbili ili kuwawezesha wananchi kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano huu kwa masilahi mapana ya nchi yetu na kwa kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetekeleza ushauri wa Kamati kwa kutoa elimu kwa umma kupitia vipeperushi, mabango na fulana zenyenje ujumbe kuhusu Muungano zilizokabidhiwa kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Zanzibar, Iringa, Mbeya na Dodoma. Aidha, inakamilisha Toleo la Pili la Kitabu cha Taarifa ya Mafanikio ya miaka 50 ya Muungano kwa ajili ya kuelimisha umma pamoja na kuelimisha wanafunzi 1500 wa shule za msingi za Mkoa wa Dar es Salaam na kutoa elimu kwa watumishi 80 wa Wizara na Taasisi za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pili, Ofisi ya Makamu wa Rais iendelee kuratibu ushirikiano katika Mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar, kupitia vikao vya kisekta kila inapohitajika ili kuimarisha ushirikiano huu wa kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa inaonyesha kuwa, ofisi hii imetekeleza ushauri huu kwa kuhimiza Taasisi zisizo za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kukutana ili kujadili masuala yanayohusu sekta zao. Ofisi iliandaa ratiba ya vikao vya ushirikiano na kusambazwa kwa pande mbili za Muungano. Hadi kufikia Machi 2015 vimefanyika vikao vinne vya ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati ambaa upo katika hatua za utekelezaji. Mfano wa ushauri huo ni pamoja na:-

Moja, pamoja na kuwa baadhi ya kero za Muungano kama vile suala la Hisa za Zanzibar zilizokuwa kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, mafuta na gesi, mgawanyo wa fedha za wafadhili, malalamiko ya wafanyakishara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili wanapopelea bidhaa zao Tanzania Bara na Akaunti ya Pamoja ya Fedha, zipo katika hatua mbambali za kushughulikiwa na Serikali zote mbili.

Kamati inashauri kuwa, kwa kuwa Serikali yetu ipo katika mchakato wa utungaji wa Katiba Mpya na Wabunge wote wa Bunge hilo Tukufu na Wajumbe wa Bunge hilo, ni vyema kupitia mchakato huo watakapofikia katika eneo hilo, watafakari kwa kina namna ya kumaliza kero hizo kwa lengo la kuimarisha na kudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Katiba limejadili Rasimu ya Katiba na maeneo mengine yenye changamoto za Muungano yameibuliwa na kujadiliwa kwa lengo la kuzitatua na mengine yameondolewa katika Mambo ya Muungano.

Baadhi ya hoja zilizokuwemo ambazo zitapatiwa ufumbuzi kupitia Katiba Inayopendekezwa ni pamoja na:-

Suala la utafiti na uchimbaji wa gesi asilia ambalo limeondolewa katika Orodha ya Mambo ya Muungano, Ibara ya 74(3). Aidha, Katiba Inayopendekezwa imeimarisha utekelezaji wa masuala ya Muungano na utatuza wa changamoto zake kwa kuunda Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Mambo ya Muungano, Sura ya 9.

Mbili, Serikali ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Zanzibar zifanye mazungumzo na mmiliki wa jengo lililo jirani na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa lengo la kulinunua kwa kuimarisha usalama wa ofisi na Makazi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zimeanza mazungumzo na mmiliki wa jengo la ghorofa linaloendelea kujengwa nyuma ya Makazi ya Makamu wa Rais. Ushauri wa Kamati ambao haukutekelezwa:-

Serikali iongoze bajeti ya kutosha na kutoa kwa wakati fedha zinazoidhinishwa ili kuwezesha Ofisi ya Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Katika kuripoti utekelezaji wa ushauri huo, mtoa hoja alijulisha Kamati kuwa suala la bajeti ndogo na kutolewa fedha kwa wakati bado ni tatizo linalokwamisha utekelezaji wa kazi zinazopangwa katika ofisi hii.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 bajeti iiliyopangwa kwa Ofisi hii haitoshalezi na hadi kufikia Machi 2015 ni asilimia 28 tu ya bajeti ndiyo iliyotolewa kwa Ofisi kwa ajili ya kushughulikia Mambo ya Muungano. Aidha, bajeti imezidi kuwa finyu kwani ukomo wa bajeti mwaka 2015/2016 umezidi kushuka kwa asilimia nane.

Tatu, Serikali iendelee kuwajengea uwezo Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais ili waweze kutekeleza majukumu yao na kuleta tija katika Ofisi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), imeandaa Mpango wa Mafunzo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Hata hivyo, utekelezaji wake umekuwa mdogo kutokana na kutopatika kwa fedha zilizopangwa kwa ajili ya mafunzo hayo. Changamoto zinazoikabili Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano):-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), inayoratibu masuala yote ya Muungano na Ushirikiano katika Mambo yasiyo ya Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, katika utekelezaji wa majukumu yake inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ufinyu wa bajeti.

(ii) Magari yanayotumika katika Ofisi ya Makamu wa Rais kuisha muda wake na hivyo kuongeza gharama za matengenezo.

(iii) Fedha za mchango wa kibajeti kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenda katika Serikali ya Mapinduzi kujumlishwa katika Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipeleka fedha katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya shughuli za kibajeti na kugharimia masuala mbalimbali ya maendeleo na kijamii.

Kwa kufanya hivyo, Fungu 31 huoyesha kuwa limetengewa fedha nydingi wakati kiuhalisia Fungu hilo linatengewa fedha kidogo sana na kusababisha majukumu mengi ya msingi katika Ofisi hii kushindwa kutekelezwa kwa ufanisi.

Nne, kukamilika kwa Jengo la Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu Zanzibar na hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Tunguu Zanzibar, umesababisha gharama za uendeshaji kama vile kulipia bili za umeme, maji na mahitaji mengine; hivyo, kuhitaji kuongezeka kwa bajeti ili kukidhi mahitaji hayo.

Tano, kuchekelawa kukamilika kwa mazungumzo ya kununua jengo la ghorofa lililojengwa karibu na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu Zanzibar. Katika eneo ambapo kumejengwa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais iliyopo Tunguu Zanzibar, kuna jengo la ghorofa la mtu binafsi. Jengo hilo ni refu kiasi cha kumuwezesha mmiliki wa jengo hilo, kuona shughuli zote zinazofanyika katika Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais; jambo ambalo siyo sahihi kiusalama.

Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kufanya mazungumzo na mmiliki wa jengo hilo la ghorofa ili kulinunua, lakini mazungumzo hayo hayajafikia hatua za kuridhisha.

Maoni na ushauri; kufuatia Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati wakati wa kupitia na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2015/2016, kama yalivyowasilishwa kwa kila Fungu pamoja na changamoto zinazoikabili zilizobainika wakati wa uchambuzi huo, Kamati inashauri yafuatayo ili kuboresha utendaji wa ofisi hii:-

(i) Serikali itenye bajeti ya kutosha na kutoa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati kwa ajili ya ofisi hii, kwani ilibainika dhahiri wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2014/2015 kuwa, fedha zilizotengwa kwa mwaka huo ni asilimia 28 tu ndiyo iliyokuwa imetolewa hadi kufikia Machi 2015.

(ii) Kwa kuwa magari yanayotumiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais yamekwisha muda wake wa matumizi, Kamati inashauri Serikali itenye bajeti ya kutosha kwa ajili ya kununua magari mapya ili kuepuka gharama za matengenezo ya mara kwa mara ya magari yaliyokwisha muda wake.

(iii) Kwa kuwa mazungumzo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na mmiliki wa jengo linalojengwa karibu na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais kuhusu kununua jengo hilo hayajakamilika, Kamati inashauri Serikali hizo ziongeze kasi ya mazungumzo hayo na kufikia mwafaka kwa lengo la kuhakikisha usalama wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais.

(iv) Kwa kuwa Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais inajumuisha fedha za mchango wa kibajeti kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, hivyo kufanya Fungu hilo kuonekana lina fedha nydingi, lakini kwa uhalisia fedha zinazobaki kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii baada ya kutoa fedha zinazokwenda Zanzibar ni kidogo sana na hazikidhi mahitaji ya Ofisi hii. Kamati inashauri Serikali kuandaa Fungu jipya kwa ajili ya fedha za mchango wa kibajeti kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (Makofifi)

Tano, kwa kuwa sherehe za maadhimisho ya Muungano zinazofanyika Kitaifa kila mwaka zinatoa elimu kwa wananchi kuhusu Muungano, lakini inaonyesha hamasa inafanyika zaidi katika ngazi za Taifa; Kamati inashauri maadhimisho haya yahamasishwe na kufanyika katika ngazi za Wilaya na Mikoa ili kuwawezesha wananchi wengi hasa wa vijiji, kushiriki na kupata elimu sahihi ya Muungano kwa lengo la kuwezesha kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano wetu adhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), inaomba fedha kwa mwaka 2015/2016 kwa Mafungu 26 na 31 kama ilivyoolezwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) alipokuwa anawasilisha hoja yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa fedha kwa mwaka 2015/2016. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa, umesaidia kufanikisha kukamilisha kwa Taarifa hii kwa wakati.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Dkt. Thomas Kashililah - Katibu wa Bunge, Ndugu Charles Mloka - Mkurugenzi wa Idara ya Kamati na Ndugu Athumani Hussein - Mkurugenzi Msaidizi, kwa kusaidia kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, ninamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano mkubwa aliounyesha kwa Kamati wakati wa kuchambua na kujadili Mpango wa Bajeti ya Ofisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofi)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGUE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS- MUUNGANO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5), (9) na 117 (11) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Katikakutekeleza majukumuya Kamati kuhusiana na uchambuzi wa Bajeti, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mafungu mawili chini ya Ofisi hii ambayo ni :-

- (i) Fungu 26 - Makamu wa Rais; na
- (ii) Fungu - 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Samia

S. Hassan (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano mnamo tarehe 6 Mei, 2016

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wake, Kamati ilizingatia majukumu ya Ofisi hii kwamujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, rejea nyingine muhimu katika kufuatilia utekelezaji wa mpango na bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilikuwa ni tangazo la serikali la mgawanyo wa majukumu ya Wizara, Tangazo Na. 494 la tarehe 17 Desemba, 2010 (*Assingment of Ministerial Responsibilities, Government Notice No. 494 of 17th December, 2010*).

Mheshimiwa Spika, rejea hizo kwa ujumla zinaonesha kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano inahusika na majukumu ya kitaifaikiwemokuratibu mambo yote ya Muungano na Ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Ofisi hii inahusika na usimamizi wa uhifadhi wa mazingira hapa nchini. Kwa mantiki hiyo ni ofisi muhimu kwa mustakabali wa Muungano wetu adhimu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Ofisi hii ni kiungo muhimu katika kuimarisha, kuendeleza na kudumisha muungano adhimu wa iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya watu wa Zanzibari ulioasisiswi na waasisi wa Taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.

Mheshimiwa Spika, Kupitia Muungano huu wananchi wa pande zote mbili wamenufaika na maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni yaliyofikiwa kwa kipindi chote cha miaka Hamsini na moja. Ni jambo lisilopingika kuwa Muungano huu wa kipekeeumekuwa wa kuigwa Afrika na duniani kote.

MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, katika kupitia taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ilitaka kujua mambo makuu mawili yafuatayo:-

- (i) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015; na
- (ii) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu uchambuziwa Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati kwa keleza yaliyobainika katika mambo hayo kama ifuatavyo:-

Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati ilitoa ushauri, mapendekezo na maoni yenye lengo la kuimairisha na kuboresha utendaji kazi wa ofisi hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi na mwengine unaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Ushauri wa Kamati Uliotekelezwa

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyowasilishwa mbele Ya Kamati imeonesha kuwa yapo maoni na ushauri uliozingatiwa na kufanyiwa kazi na Serikali. Mifano ya uzingatiaji huo ni kama ushauri ufuatao:-

- (i) **Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu na faida ambazo zinazotokana na Muungano kwa pande zote mbili ili kuwawezesha wananchi kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano huu kwa maslahi mapana ya nchi yetu na kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.**

Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza ushauri wa Kamati kwa kutoa elimu kwa Umma kupitia vipeperushi,mabango na fulana zenye ujumbe kuhusu Muunganozilizogawiwa kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu Zanzibar,Iringa,Mbeya na Dodoma.Aidha inakamilisha toleo la pilii la kitabu cha taarifa ya mafanikio ya miaka 50 ya muungano kwa ajili ya kuelimisha Umma pamoja na kuelimisha wanafunzi 1500 wa shule za msingi za mikoa ya Dar es salaam na kutoa elimu kwa watumishi 80 wa wizara na Taasisi za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- (ii) **Ofisi ya Makamu wa Raisiendelee kuratibu ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia vikao vya kisekta kila inapohitajika ili kuimarisha ushirikiano huu wa kihistoria.**

Mheshimiwa Spika,Taarifa inaonesha kuwa Ofisi hii imetekeleza kwa kuhimiza Taasisi zisizo Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kukutana ili kujadili masuala ya yanayohusu Sekta zao.Ofisi iländaa ratiba ya vikao vya ushirikiano na kusambazwa kwa pande mbili za Muungano.Hadi kufikia Machi,2015 vimefanyika vikao vinne vya ushirikiano ,vikao vya Utumishi wa Umma vilifanyika tarehe 11na 12 Disemba 2014 Dar es salaam.kikao kati ya OWM-TAMISEMI na OR-TMIM,Zanzibar kilifanyika tarehe 22-23 Januari 2015 Morogoro,Kikao cha utawala Bora kilifanyika tarehe 5 Februari 2015 Dar es salaam na kikao cha Uchukuzi kilifanyika tarehe 18 Februari,2015 mkoani Tanga.

Ushauri wa Kamati ambao upo katika hatua za utekelezaji

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa ushauri uliotekelizwa, upo ushauri ambao bado upo kwenye mchakato wa utekelezaji. Mfano wa ushauri huo ni pamoja na:

- i) **Pamoja na kuwa baadhi ya kero za Muungano kama vile suala la Hisa za Zanzibar zilizokuwa kwenye bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, mafuta na gesi ,mgawanyo wa fedha za wafadhli, malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili wanapoleta bidhaa zao Tanzania Bara na Akaunti ya pamoja ya fedha zipo katika hatua mbalimbili za kushughulikiwa na Serikali zote mbili, Kamati inashauri kuwa kwa kuwa Serikali yetu iko katika mchakato wa utungaji wa Katiba Mpya na Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu ni Wajumbe wa Bunge hilo, ni vyema kupitia mchakato huo watakapofikia katika eneo hilo watafakari kwa kina namna ya kuzimaliza kero zote kwa lengo la kuimarisha na kudumisha Muungano wetu.**

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa Bunge la Katiba limejadili Rasimu ya Katiba na maeneo mengi yenye changamoto za Muungano yameibuliwa na kujadilwa kwa lengo la kuzitatua na mengine yameondolewa katika mambo ya Muungano. Baadhi ya hoja zilizokuwepo ambazo zitapatiwa ufumbuzi kupitia Katiba Inayopendekezwa ni pamoja na; Suala la utafiti na uchimbaji wa Gesi asilia,ambalo limeondolewa katika orodha ya Mambo ya Muungano, Ibara ya 74(3). Aidha Katiba Inayopendekezwa imeimarisha utekelezaji wa masuala

ya Muungano na utatuzi wa changamoto zake kwa Kuunda Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Mambo ya Muungano, (Sura ya Tisa).

- ii) **Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zifanye mazungumzo na mmiliki wa jengo lililo jirani na Ofisi ya makamu wa Rais kwa lengo la kulinunua kwa kuimarisha usalama wa ofisi na makazi hayo**

Mheshimiwa Spika, Taairifa ya Serikali inaonyesha kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibarzimeanza mazungumzo na mmiliki wa jengo la gorofa linaloendelea kujengwa nyuma ya makazi ya makamu wa Rais.

Ushauri wa Kamati ambao haujatekelezwa

- i) **Serikali iongeze bajeti ya kutosha na kutoa kwa wakati fedha zinazoidhinishwa ili kuwezesha Ofisi ya Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

Mheshimiwa Spika, katika kuripoti utekelezaji wa ushauri huo, mtoa hoja alijulisha Kamati kuwa Suala la bajeti ndogo na kutotolewa fedha kwa wakati bado ni tatizo linalokwamisha utekelezaji wa kazi zinazopangwa katika Ofisi hii. Katika Mwaka wa fedha 2014/2015 bajeti iliyopangwa kwa Ofisi hii haitoshelezi na hadi kufikia mwezi Machi 2015 ni asilimia 28 tu ya bajeti ukuondoa fedha zilizopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ndiyo iliyotolewa kwa ofisi kwa ajili ya kushughulikia mambo ya Muungano. Aidha bajeti imezidi kuwa finyu kwani Ukomo wa bajeti wa Mwaka 2015/2016 umezidi kushuka kwa asilimia 8.

- iii) **Serikali iendelee kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais ili waweze kutekeleza majukumu yao na kuleta tija katika ofisi na Taifa kwa ujumla**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano imeandaa mpango wa mafunzo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 Hata hivyo utekelezaji wake umekuwa mdogo kutokana na kutopatikana kwa fedha zilizopangwa kwa ajili ya mafunzo hayo.

Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015

Mheshimiwa Spika, Wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilitaka kujiridhisha na mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ilijidhinishwa kwa Mwaka 2014/2015.Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 6 Mei, 2015 ilionesa kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha umekuwa si wa kuridhisha kwani kiasi cha fedha kilichopokelewa na ofisi hii kutoka Hazina ni asilimia 28 tu ya bajeti yote. Mchanganuo wa fedha zilizotengnwa na zilizopokelewa ni kama ifuatavyo:-

- i) Fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ni Shilingi **55,574,700,000/=**. Hadi kufikia Machi 2015 imepokea shilingi **33,605,818,195/=** sawa na asilimia 60.5
- ii) Fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo Ofisi ilitengewa Shilingi **6,562,746,000/=**. Hadikufikia Machi 2015 imepokea Shilingi **2,254,148,325/=** sawa na asilimia 34.3.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano inayoratibu masuala yote ya Muungano na ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i) Ufinyu wa bajeti

Bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuwezesha kugharamia utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ni ndogo hivyo, kutokidhi mahitaji halisi ya uendeshaji wa majukumu ya Ofisi hii.

ii) Magari yanayotumika Katika Ofisi ya Makamu wa Rais kuisha Muda wake na hivyo kuongeza gharama za matengenezo.

Magari mengi yanayotumiwa na watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais yameisha Muda wake wa Matumizi kisheria hivyo huhitaji matengenezo ya mara kwa mara jambo ambalo linaongeza gharama za matengenezo.

iii) Fedha za Mchango wa Kibajeti kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenda katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujumuishwa katika Fungu 31(Ofisi ya Makamu wa Rais)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipeleka fedha katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya shughuli za kibajeti na kugharamia masuala mbalimbali ya maendeleo na kijamii. Kwa Kufanya hivyo, Fungu 31 huonyesha kuwa linatengewa fedha nyingi wakati kiuhalisia Fungu hilolinatengewa fedha kidogo sana na kusababisha majukumu mengi ya msingi katika ofisi hii kushindwa kutekelezeka kwa ufanisi.

iv) Kukamilika kwa Jengo la Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu Zanzibar na hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania huko Tunguu Zanzibar kumesababisha gharama za uendeshaji kama vile kulipia bili za Umeme, Maji na mahitaji mengine hivyo kuhitaji kuongezeka kwa bajeti ili kukidhi mahitaji hayo.

v) Kuchelewa kukamilika kwa mazungumzo ya Kununua Jengo la Ghorofa ililojengwa Karibu na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Tunguu Zanzibar.

Katika eneo ambapo Ofisi na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais iliyopo Tunguu Zanzibar kuna jengo la ghorofa karibu sana na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Jengo hilo ni refu kiasi cha kumwezesha mmiliki wa jengo hilo kuona shughuli zote zinazofanyika katika Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais jambo ambalo sio sahihi kiusalamu.Kamati yangu ilitoa Maoni na Ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kufanya mazungumzo na mmiliki wa jengo hilo la ghorofa ili kulinunua lakini mazungumzo hayajafikia hatua za kuridhisha.

MAONI NA USHAURI

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati wakati wa kupitia na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2015/2016 kama yaliviyowasilishwa kwa kila fungu pamoja na changamoto zilizobainika wakati wa uchambuzi huo,Kamati ina shauri kama yafuatayo ili kuboresha utendaji wa Ofisi hii:

- i) Serikali itenge bajeti ya kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa wakati kwa ajili ya Ofisi hii kwani ilibainika dhahiri wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka fedha 2014/2015 kuwa fedha zilizotengwa kwa mwaka huo ni asilimia 28 tundiyo iliyokuwa imetolewa hadi kufikia Machi,2015.
- ii) Kuwa magari mengi yanayotumiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais yamekwisha muda wa matumizi kwa mujibu wa sheria,Kamati inashauri Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya kununua magari mapya ili kuepuka gharama za matengenezo ya mara kwa mara ya magari yaliyokwisha muda wake.
- iii) Kwa kuwa Mazungumzo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na mmiliki wa jengo lililojengwa karibu na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais kuhusu kununua jengwa hilo hayajakamilika ,Kamati inashauri Serikali hizo ziongeze kasi ya mazungumzo hayo na kufikia muafaka kwa lengo la kuhakikisha usalama ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais.
- iv) Kwa kuwa Fungu 31:Ofisi ya Makamu wa Rais linajumuisha fedha za mchango wa kibajeti kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hivyo kulifanya Fungu hilo kuonekana lina fedha nyingi lakini kwa uhalisi fedha zinazobaki kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii baada ya kutoa Fedha zinazoenda Zanzibar ni kidogo sana na hazikidhi mahitaji ya Ofisi hii,Kamati inashauri Serikali kuandaa Fungu jipya kwa ajili ya fedha za mchango wa kibajeti kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
- v) Kwa kuwa Sherehe za Maadhimisho ya Muungano zinazofanyika kitaifa kila mwaka yanatoa elimu kwa wananchi kuhusu Muungano lakini inaonesha hamasa inafanyika zaidi katika ngazi ya taifa, Kamati inashauri maadhimisho haya yahamasishwe na kufanyika katika ngazi za wilaya na Mikoa ili kuwezesha wananchi wengi hasa wa vijiji kushiriki na kupata elimu sahihi ya Muungano wetu kwa lengo lakuwawezesha kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano wetu adhimu.

MAOMBI YA FEDHA NA MALENGO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, Ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano inaomba fedha kwa mwaka 2014/2015 kwa muhtasari kwa mafungu 26 na 31 kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano alipokuwa anawasilisha hoja yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

- i) Mhe. Jasson S. Rweikiza, Mb, - Mwenyekiti

ii)	Mhe. Gosbert B. Blandes, Mb	-	M/ Mwenyekiti
iii)	Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mb	-	Mjumbe
iv)	Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	-	Mjumbe
v)	Mhe. Nimrod Elirehema Mkono, Mb	-	Mjumbe
vi)	Mhe. Halima J. Mdee, Mb	-	Mjumbe
vii)	Mhe. Fakharia K. Shomar, Mb	-	Mjumbe
viii)	Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb	-	Mjumbe
ix)	Mhe. Ali Khamis Seif, Mb	-	Mjumbe
x)	Mhe. Felix Francis Mkosamali, Mb	-	Mjumbe
xi)	Mhe. Abdallah Sharia Ameir, Mb	-	Mjumbe
xii)	Mhe. Mustapha B. Akunaay, Mb	-	Mjumbe
xiii)	Mhe. Mariam Reuben Kasembe, Mb	-	Mjumbe
xiv)	Mhe. Tundu A. Mughwai Lissu, Mb	-	Mjumbe
xv)	Mhe. Deogratias A. Ntukamazina, Mb	-	Mjumbe
xvi)	Mhe. William M.Ngeleja, Mb	-	Mjumbe
xvii)	Mhe. Nyambari C.M.Nyangwine,Mb	-	Mjumbe
xviii)	Mhe. Ramadhan Haji Saleh	-	Mjumbe
xix)	Mhe. Zahra Ali Hamad	-	Mjumbe
xx)	Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	-	Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, Ndg. Charles J. Mloka, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati na Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru ndugu Matamus Fungo nandugu Maria Mdulugu, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato naMatumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rweikiza na ninashukuru sana kwa kuniachia muda kidogo.

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa niaba yake anakuja Mheshimiwa Ester Bulaya. Karibu sana Mheshimiwa Ester Bulaya kutusomea Taarifa ya Kamati yenu!

MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, kwa niaba ya Kamati, tunatoa pole kwa Ofisi ya Rais (Mazingira), kwa kupotelewa na Mkurugenzi wa Mazingira, Bwana Robert ambaye alipoteza maisha alipokuwa katika ziara ya kimafunzo nchini Marekani. Nawapa pole sana kwa niaba ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yote iingie kwenye Hansard kutokana na muda.

Kabla ya yote, ninawashukuru vijana wote wa Tanzania wa Mkoa wa Mara kwa kuniamini nilipopata fursa ya kuwawakilisha katika Bunge lao hili Tukufu. Kipekee, nawashukuru

vijana wa Mara na Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi, kwa kuniamini na wakiendelea kuniamini, ninaamini nitapata fursa ya kuitumikia nchi yangu katika miaka mitano ijayo. Ahsante. (Makofii)

Taarifa ya Kamati ya Bunge la Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(9), Toleo la Mwaka 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Fungu 31, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Makadirio ya Mapato ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, mnamo tarehe 30 Aprili 2015, Kamati ilikutana katika Ukumbi wa Benki Kuu Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu ya Rais (Mazingira) pamoja na Wataalamu wake na kupokea Taarifa ya Ofisi kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa majadiliano ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015: Wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, ilitoa ushauri katika maeneo mbalimbali kwa Ofisi ya Baraza la Taifa la Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, japokuwa kuna maeneo ambayo Serikali haijatekeleza ipasavyo kutokana na ufinyu wa bajeti kama ilivyoainishwa hapo chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kamati kuendelea kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya ofisi hii hasa kwa Idara ya Mazingira (NEMC), kwa miaka mitatu mfululizo; 2011/2012, 2012/2013 na 2013/2014, bado Serikali imieendelea kutenga fedha kidogo, ambapo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya shilingi 7,764,000,000/= zilitengwa kwa ajili ya Idara ya Mazingira na Vitengo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika hali halisi, fedha hizi hazitoshelezi mahitaji ya msingi katika kutekelezaa shughuli za uhifadhi wa Mazingira nchini. Aidha, Kamati inasikitishwa na Serikali kutotenga Fungu Maalum kwa ajili ya mgao wa kibajeti unaopelekwa katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ili fedha zinazotengwa kwa ajili ya mazingira zijulikane wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudia; Kamati inasikitishwa na Serikali kutotenga Fungu Maalum kwa ajili ya mgao wa kibajeti unaopelekwa katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ili fedha zinazotengwa kwa ajili ya mazingira zijulikane wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza ili kuwe na maendeleo endelevu katika sekta zote, ni lazima suala la mazingira lipewe kipaumbele kwa kutengewa bajeti ya kutosha, hasa kwa kuzingatia kuwa suala la Mazingira ni suala mtambuka. Mipango mingi inayopangwa na Serikali haiwezi kufanikiwa iwapo mazingira yatakuwa yameharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatenga pesa kidogo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni ya pili kwa umuhimu baada ya Ofisi ya Rais. Fedha kidogo zinazotengwa haziwiani na kazi za Idara hii, umuhimu wa Sekta yenye na uzito wa Ofisi.

Kamati inalipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, ambalo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeweza kubomoa nyumba 24 zilizojengwa kinyume cha Sheria katika kingo za mito na fukwe za Bahari ya Hindi, kurudisha mito iliyoathirika katika hali yake ya asili na hivyo kuondoa athari kubwa za kimazingira zinazoweza kutokea.

Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba nyumba zote zilizojengwa kinyume cha sheria katika kingo za mito na fukwe za bahari zinabomolewa. Kamati inaitaka Serikali kutoa taarifa ya kina kuhusu nyumba zilizobomolewa, katika plot zippi, zinamilikiwa na nani na pia itoe taarifa ya nyumba ambazo hazijabomolewa, katika plot zippi, wamiliki wake ni akina nani na kwa nini hazijabomolewa. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba, watu wote waliojenga mabondeni wanahamishwa na kuyaacha mazingira hayo vizuri ili kuepusha athari ambazo zinatokea na zitakazoendelea kutokea. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali kwa kuanda Kanuni mpya ya mifuko ya plastiki iliyoongeza unene wa mifuko kufikia mikroni 50 na kwamba mifuko yenye unene chini ya mikroni 50 haitaruhusiwa kuingizwa nchini wala kutumika. Kanuni hii inaendeleza viwango bora vya mifuko ya plastiki katika mazingira, vilivyowekwa katika Jumuia ya Afrika Mashariki, vilivyopitishwa mwaka 2012. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuelimisha wananchi na wadau juu ya umuhimu wa udhibiti wa taka za plastiki na kukuza matumizi ya mifuko mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Ofisi ya Makamu wa Rais - Fungu 31, iliidhinishiwa shilingi 62,137,446,000/=, ambapo kati ya hizo, mishahara ilikuwa shilingi 2,258,948,000/= na shilingi 55,574,700,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, kiasi hicho kinajumuisha shilingi 44,039,608,000/= kwa ajili ya mgao wa kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na fedha za ruzuku za NEMC shilingi 3,770,949,000/. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Ofisi ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi 34,048,048,486/= kwa ajili matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 54.7 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya shilingi 62,137,446,000/=.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, ziliidhinishwa jumla ya shilingi 6,562,746,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,500,000,000/= zilikuwa ni fedha za ndani na Shilingi 2,062,746,000 zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2015, jumla ya shilingi 2,254,148,325/= zilikuwa zimetolewa, ambapo fedha za ndani ni shilingi 1,050,000,000/= na za nje ni shilingi 1,204,148,325/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kukabiliwa na ufinyu wa bajeti, bado imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

- (i) Kuendelea kutoa elimu ya hifadhi ya usimamizi wa mazingira kwa umma kuitia warsha, maadhisho na maonesho na njia mbalimbali.
- (ii) Kuendelea kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira chini ya ufadhili wa DANIDA na CANADA (CIDA).
- (iii) Kuratibu na kutekeleza Mikataba minne ya Kimataifa ya Mazingira ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, ufinyu wa bajeti umeendelea kuwa changamoto kubwa inayosababisha kutotekelezwa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa.

Aidha, changamoto nyingine ambazo zimeendelea kuikabili Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ni pamoja na uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuihimiza Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kuweka, kuimarisha na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa kutumia fedha kidogo wanayopata katika bajeti, lakini pia kwa fedha inayotokana na Miradi mbalimbali ambayo huandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuandaa Bajeti ya mwaka 2015/2016, Kamati ilijulishwa kwamba, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yamezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mkakati wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II) na Maoni na Mapendekezo ya Bunge wakati wa kujadili Mpango wa Bajeti ya Ofisi hii ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa zimegawanywa kulingana na vipaumbele vya majukumu ya Ofisi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Hivyo basi, kiasi cha shilingi 37,296,617,000/= katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 kinaombwa kwa ajili ya Fungu 31. Kiasi hiki kinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida shilingi 32,777,770,000/= na fedha za matumizi ya maendeleo shilingi 4,518,847,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha matumizi ya kawaida kinajumuisha fedha za mgao wa asilimia 4.5 ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shilingi 22,400,000,000/=; hivyo, Idara ya Mazingira imetengewa kiasi cha shilingi 4,365,705,000/= na shilingi 3,326,210,000/= ni fedha za ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya shilingi 4,518,847,000/= zimetengwa ambazo zinajumuisha fedha za ndani shilingi 3,500,000,000/= na fedha za nje shilingi 1,018,847,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii na kupitia Kifungu kwa Kifungu. Japokuwa Kamati hairidhishwi na kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili maombi hayo yenye jumla ya shilingi 37,296,617,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuujadili kwa kina Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Kamati inatoa maoni na ushauri ufuataao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote Kamati inasikitishwa sana kwa jinsi Serikali isivyotoa kipaumbele kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa kuitengea bajeti ndogo kila mwaka. Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) imeshuka kutoka shilingi 62,137,446,000/= mwaka 2014/2015 hadi shilingi 37,296,617,000/= mwaka 2015/2016. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuyapa Mazingira uzito unaostahili kwa kuongeza Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira hasa katika Sekta za Kilimo, Misitu, Mifugo, Nishati, Maji na kadhalika, inasikitisha kuona Serikali yetu bado hajatoa kipaumbele katika suala la mazingira. Ni ukweli usiofichika kwamba, ili kuwa na maendeleo endelevu, lazima uhifadhi wa mazingira upewe kipaumbele. Hii itawezekana endapo tu Serikali itatambua umuhimu huu na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, kwa mwaka ujao wa fedha 2015/2016, Idara ya Mazingira imetengewa jumla ya shilingi 7,691,915,000/= zinazojumuisha fedha za ruzuku kwa Baraza (NEMC) shilingi 3,326,210,000/. Bajeti hii ni ndogo kwa Idara na Baraza lake kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hasa kwa kuzingatia kwamba, hawana vitendea kazi vya kutosha kama vile magari, ambayo ni muhimu kwa ajili ya ukaguzi hasa katika maeneo ya viwanda na migodi. Pamoja na hayo, bajeti hii ni ndogo sana ikilinganishwa na gharama kubwa zinazotumika katika kulinda maeneo ya fukwe na kingo za mito hususan pale ambapo inahusisha kubomoa majengo yaliyojengwa katika maeneo hayo hasa kinyume cha Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inapendekeza kwamba, kuwe na fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo Fungu 31, kujumuisha mgao wa kibajeti wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwa zinazoidhinishwa chini ya Fungu 31, ni pesa nyingi kulinganishwa na zinazobaki kwa ajili ya Mazingira. Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kuipatia Idara ya Mazingira na Baraza lake Fungu la pekee ili kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Idara ya Mazingira kijulikane wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya maoni ya Kamati hii kwa Ofisi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ilikuwa ni Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kamati inatoa ushauri huu kwa kuzingatia kwamba, mara nyingi fedha za nje huwa hazitolewi kwa wakati na hivyo kukwamisha Miradi mingi.

Kamati inafarijika kuwa ushauri wa Kamati umezingatiwa ambapo kwa mwaka ujao wa fedha (2015/2016), Serikali imetenga fedha za ndani shilingi 3,500,000,000/=, ikilinganishwa na shilingi 1,018,847,000/= fedha za nje. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za ndani za kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto kubwa ya Idara ya Mazingira ni uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya mazingira hasa Sheria ya Mazingira Namba 20 ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kuhusu kuwepo kwa ujenzi usiofuata sheria katika maeneo ya fukwe na kingo za mito. Hali hii inasababishwa na wananchi aidha kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Sheria ya Mazingira ama kukaidi sheria hiyo. Ujenzi huu hasa katika kingo za mito, unaathiri mazingira ya asili na mito ikiwa ni pamoja na kupindisha mikondo ya mito. Hali hii ni ya hatari kwani imekuwa ikitababishwa mafuriko kwa pande ambazo mito imemelekezwa na hivyo kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba, nyumba zote zilizojengwa kinyume cha Sheria katika kingo za mito na fukwe za bahari, zibomolewe na kurudisha mito iliyoathirika katika hali yake ya asili ili kuondoa athari kubwa za kimazingira zinazoweza kutokea. Kamati inataka kujua maendeleo ya zoezi la uchunguzi wa hati za nyumba zilizojengwa kinyume cha sheria na maendeleo ya kesi mbalimbali zilizofunguliwa dhidi ya Baraza. Aidha, pale ambapo imebainika kwamba, waliojenga katika maeneo tuliyoyataja kwa kupewa vibali

kama vile hati na kadhalika kinyume cha sheria, waliohusika na vitendo hivi vya kifisadi vya kutoa vibali au hati, wakamatwe na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni dhahiri kwamba wananchi wengi bado hawana uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na faida zake hususan wakati huu ambapo kuna changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi. Athari mbalimbali zimeendelea kutokea kutokana na uharibifu wa mazingira.

Vitendo vya kuharibu vyanzo vya maji, ukataji hovyo wa miti na utupaji hovyo wa taka vinafanyika kwa kiasi kikubwa kutokana na ukosefu wa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira mionganini mwa wananchi. Kamati inaishauri, Serikali itenye fedha za kutosha ili kuiwezesha Idara ya Mazingira kuendesha Programu ya Elimu kwa Umma itakayoleta mafanikio. Kamati inashauri Serikali kutambua umuhimu wa elimu hii na kuongeza bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Oktoba 2006, Serikali ilitoa agizo la kupiga marufuku uingizaji, utengenezaji, uuzaaji na matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene chini ya mikroni thelathini. Agizo hili lilitrudiwa tena mwezi Agosti 2013. Aidha, Serikali iliahidi kuchukua hatua ya kupiga marufuku kabisa matumizi ya mifuko hiyo ya plastiki ili kulinda mazingira. Hata hivyo, ni dhahiri kabisa agizo hilo halijatekelezwa kwani mazingira yetu yameendelea kuchafuliwa na mifuko hiyo hususan maeneo ya mijini na kwenye fukwe za Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza agizo lake na kuvisimamia Kanuni ya Kudhibiti Matumizi ya Mifuko ya Plastiki ya Mwaka 2014 mapema iwezekanavyo ili kuondoa tatizo hili sugu la uchafuzi wa mazingira ambalo linaitia aibu nchi yetu. Sanjari na hilo, ni pendekezo la Kamati kwamba Serikali isimamie usafi wa mazingira kwa kudhibiti utupaji taka ovyo. Vilevile elimu ya utunzaji au usafi wa mazingira, iwekwe kwenye mitaala katika shule za misingi ili kuwajengea wanafunzi utamaduni wa kuwa na mazingira safi na yaliyohifadhiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali za Mitaa zimeendelea kuwa na mwitikio mdogo katika hifadhi na utunzaji wa Mazingira, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kufuatilia utungaji na utekelezaji wa Sheria Ndogo za Hifadhi ya Misitu ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba yote yaingie katika Hansard. Kwa niaba ya Kamati, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. (Makofii)

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA
BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015;
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI
KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA OFISI HIYO
KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1.1 Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(9) Toleo la Mwaka 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira (**Fungu- 31**), kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

1.2 Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge (2013) Kifungu namba 6(8) na 7 (1)kuwa ni pamoja na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na kuchambua Bajeti ya Ofisi hii; kuisimamia na kuishauri kuhusu utekelezaji wa majukumu yake.

1.3 Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza jukumu hilo, mnamo tarehe 30/04/2015 Kamati ilikutana katika ukumbi wa Benki Kuu Dar ES Salaam na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) pamoja na wataalam wake, na kupokea Taarifa ya Ofisi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

1.4 Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti hiyo, pamoja na mambo mengine, Kamati ilipata fursa ya kujadili:-

- 1.4.1 Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais(Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 na malengo yanayoombewa fedha kwa Mwaka wa 2015/2016.
- 1.4.2 Muhtasari wa kazi zilizotekelawa na Idara ya Mazingira na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
- 1.4.3 Utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2014/2015; na
 - 1.4.4 Mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

2.0 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI ULIOTOLEWA WAKATI WA MAJADILIANO YA BAJETI KWA MWAKA WA 2014/2015

2.1 Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa 2014/2015, Kamati ilitoa ushauri katika maeneo mbali mbali kwa Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)

2.2 Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitalidi kuzingatia ushauri wa Kamati japokuwa kuna maeneo ambayo Serikali haijayatekeleza ipasavyo kutohana na ufinyu wa bajeti kama inavyoainishwa hapa chini:-

- **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuendelea kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya Ofisi hii hasa kwa Idara ya Mazingira na NEMC kwa miaka mitatu mfululizo (**2011/2012; 2012/2013 na 2013/14**), bado Serikali imeendelea kutenga fedha kidogo ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa **2014/2015** jumla ya shilingi **7,764,143,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Idara ya Mazingira na vitengo chini ya ofisi ya Makamu wa Rais. Katika hali halisi fedha hizi hazitoshelezi mahitaji ya msingi katika kutekeleza shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Aidha kamati inasikitishwa na Serikali kutenga fungu maalum kwa ajili ya mgao wa Kibajeti unaopelekwa katika

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili fedha zinazotengwa kwa ajili ya mazingira zijulikane wazi.

- **Mheshimiwa Spika**, Kamati inasistiza ili kuwe na maendeleo endelevu katika sekta zote ni lazima suala la mazingira lipewe kipaumbele kwa kutengewa bajeti ya kutosha hasa kwa kuzingatia kuwa suala la mazingira ni mtambuka.

Mipango mingi inayopangwa na Serikali haiwezi kufanikiwa iwapo mazingira yatakuwa yameharibika. Mipango mizuri kama ya ujenzi wa miundombinu, Kilimo Kwanza, uchimbaji wa madini, gesi pamoja na ufuaaji wa umeme unaotokana na maji n.k haiwezi kufanikiwa kama mazingira hayako salama. Kamati inaipongeza Sekta ya madini kwa ushirikiano wake na Sekta ya Mazingira na kuzitaka Sekta nyengine zitoe ushirikiano kwa Ofisi ya makamu wa Rais Mazingira katika kupanga na kutekeleza miradi mbali mbali ili kuyalinda mazingira ya kuyafanya yawe endelevu.

- **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatenga pesa kidogo Kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni ya pili kwa umuhimu baada ya Ofisi ya Rais. Fedha kidogo zinazotengwa haziwiani na Kazi za Idara hii, umuhimu wa sekta yenewe lakini pia na uzito wa Ofisi.
- **Mheshimiwa Spika**, Kamati inalipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambalo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi limebomoa nyumba 24 zilizojengwa kinyume cha Sheria katika kingo za mito na fukwe za bahari ili kurudisha mito iliyoathirika katika hali yake ya asili na hivyo kuondoa athari kubwa za kimazingira zinazoweza kutokea. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba nyumba zote zilizojengwa kinyume cha sheria katika kingo za mito na fukwe za bahari zinabomolewa. Kamati inaitaka Serikali kutoa taarifa ya kina kuhusu nyumba zilizobomolewa ni katika plot zippi zinamilikiwa na nani na pia itoe taarifa ya nyumba ambazo hazijabomolewa ziko katika plot zippi wamiliki wake ni akina nani na kwa nini hazijabomolewa.
- Aidha kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba watu wote waliojenga mabondeni wanahamishwa na kuyaacha mazingira hayo vizuri ili kuepusha maafa yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali kwa kuandaa Kanuni mpya ya mifuko ya plastiki iliyongeza unene wa mifuko kufikia mikroni 50 na kwamba mifuko yenyе unene chini ya mikroni 50 haitaruhusiwa kuzalishwa na kuingizwa nchini wala kutumika. Kanuni hii inaendana na viwango bora vya vya mifuko ya plastiki katika mazingira vilivyowekwa katika Jumuia ya Afrika Mashariki vilivyopitishwa mwaka 2012. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuelimisha wananchi na wadau juu ya umuhimu wa udhibiti wa taka za plastiki na kukuza matumizi ya mifuko mbadala.

Mheshimiwa Spika, Kamati, imefurahishwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali za kudhibiti uchafuzi wa Mazingira katika barabara kuu nchini kwa kuandaa mradi wa ujenzi wa vituo vya kupumzikia wasafiri na wasafirishaji wanaotumia barabara kuu nchini. Vituo hivi vitasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuongeza usalama kwa kuepusha ajali zinazosababishwa na uchovu wa madereva. Kamati inaihimiza Serikali kuanza kutekeleza mradi huu haraka iwezekananvyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia na kuyafanya kazi maoni yanayotolewa na Kamati hii ili kazi ya kutunza na kuhifadhi mazingira ifanikiwe kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2014/2015

3.1 MATUMIZI YA KAWAIDA

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Ofisi ya Makamu wa Rais **Fungu 31** iliidhinishiwa Shilingi **62,137,446,000/=** ambapo kati ya hizo mishahara ilikuwa shilingi **2,258,948,000/=** na shilingi **55,574,700,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Aidha, kiasi hicho kinajumuisha shilingi **44,039,608,000/=** kwa ajili ya mgao wa kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na fedha za ruzuku za NEMC shilingi **3,770,949,000/=** Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Ofisi ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi **34,048,048,486/=** kwa ajili matumizi ya kawaida sawa na asilimia **54.7** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya shilingi **62,137,446,000/=**.

3.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 ziliidhinishwa jumla ya Shilingi **6,562,746,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo; kati ya fedha hizo shilingi **4,500,000,000/=** zilikuwa ni fedha za ndani na Shilingi **2,062,746,000/=** zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015 jumla ya Shilingi **2,254,148,325/=** tu zilikuwa zimetolewa ambazo za ndani ni **1,050,000,000/=** na za nje ni **1,204,148,325/=**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuacha kutegemea sana misaada toka nje na badala yake ianze kujenga uwezo wake wa ndani, kwa kuwa imedhihirika kwamba misaada ya wafadhili haina uhakika wa kupatikana kwa wakati.

4.0 MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

4.1 MAFANIKIO

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kukabiliwa na ufinyu wa bajeti, bado imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

- i) Kuendelea kutoa elimu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa umma kuitia warsha; maadhimisho; maonesho na njia mbalimbali;
- ii) Kuendelea kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira chini ya ufadhili wa DANIDA na CANADA CIDA. Kwa kipindi hiki Ofisi imeweza kuandaa mwongozo wa kuanzisha mfuko wa mazingira, mwongozo wa kusimamia fedha za mfuko wa mazingira na kuandaa utaratibu wa kuendesha Baraza la usuluhishi la Mazingira.
- iii) Kuratibu na kutekeleza Mikataba minne (4) ya Kimataifa ya Mazingira ikiwa ni pamoja na Mkataba wa mabadiliko ya Tabianchi.
- iv) Kuandaa Ripoti ya pili ya Hali ya Mazingira nchini na kutoa kwa wananchi kwa mujibu wa Sheria ya usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Jumla ya nakala 2400 zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau. Aidha Kamati inaishauri Serikali kutoa nakala za kutosha kwa lugha ya Kiswahili kwa kutumia fedha za ndani badala ya kusubiri misaada ya wahisani.

- v) Kuendelea kuratibu, kusimamia na kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya Mazingira kwa kufanya kaguzi katika viwanda na shughuli za uzalishaji zaidi ya 70 na kubomoa ujenzi uliokiuka Sheria katika maeneo ya mikondo ya mito na mikoko Jijini Dar es Salaam;
- vi) Kuendelea kusajili wataalam wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na ukaguzi wa Mazingira na kukagua miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa inatekeleza matakwa yaloainishwa kwenye hati za TAM.

4.2. CHANGAMOTO

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoolezwa hapo awali, pamoja na mafanikio yaliyopatikana ufinyu wa bajeti umeendelea kuwa changamoto kubwa inayosababisha kutotekelawa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa.

Aidha, changamoto nyingine ambazo zimeendelea kuikabili Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ni pamoja na:-

- 4.2.1 Uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya uhifadhi wa Mazingira; na mabadiliko ya Tabianchi
- 4.2.2 Kukosekana kwa takwimu sahihi za mazingira kwa wakati;
- 4.2.3 Mwitikio mdogo wa Serikali za Mitaa katika hifadhi na utunzaji wa mazingira.

4.3 Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuihimiza Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuweka, kusimamia na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

- (i) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa kutumia fedha kidogo wanayopata katika bajeti, lakini pia kwa fedha inayotokana na miradi mbalimbali ambayo huandika;
- (ii) Kuboresha ukusanyaji wa takwimu kwa kutoa mafunzo na vifaa kwa waratibu wa mazingira wa sekta mbalimbali na maafisa mazingira wa Serikali za Mitaa; na
- (iii) Kuendelea kuhamasisha Serikali za Mitaa kuhuisha masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo.

5.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

5.1 Mheshimiwa Spika, katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2015/2016, Kamati ilijulishwa kwamba makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yamezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka 5, Mkakati wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II), na maoni na mapendeleko ya Bunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa 2014/2015.

5.2 Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa zimegawanywa kulingana na vipaumbele vyatia majukumu ya Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Hivyo basi, fedha kiasi cha shilingi **37,296,617,000/=** katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 zinaombwa kwa ajili ya Fungu **31**. Kiasi hiki kingjumuisha fedha za matumizi ya kawaida shilingi **32,777,770,000/=** na fedha za matumizi ya maendeleo shilingi **4,518,847,000/=**.

5.3 Mheshimiwa Spika, kiasi cha matumizi ya kawaida kinajumuisha fedha za mgao wa asilimia **4.5** ya bajeti kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shilingi **22,400,000,000/=** hivyo Idara ya Mazingira imetengewa kiasi cha shilingi **4,365,705,000/=** na shilingi **3,326,210,000/=** ni fedha za ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

5.4 Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya shilingi **4,518,847,000/=** zimetengwa ambazo zinajumuisha fedha za ndani shilingi **3,500,000,000/=** na fedha za nje shilingi **1,018,847,000/=**.

5.5 Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii na kupitia Kifungu kwa Kifungu. Japokuwa Kamati haikuridhishwa na kiasi kidogo cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira, naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili maombi hayo yenye jumla ya shilingi 37,296,617,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kuujadili kwa kina Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

6.1 Mheshimiwa Spika, awali ya yote Kamati inasikitishwa sana kwa jinsi Serikali isivyotoa kipaumbele kwa Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kwa kuitengea bajeti ndogo kila mwaka. Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira imeshuka kutoka shilingi **62,137,446,000/=** mwaka 2014/2015 hadi shilingi **37,296,617,000/=** mwaka 2015/2016. Hata hivyo Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuyapa Mazingira uzito unaostahili kwa kuongeza bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira.

Mheshimiwa Spika, kutopteka na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira hasa katika sekta za kilimo, misitu, mifugo, nishati, maji n.k, inasikitisha kuona kwamba Serikali yetu bado hajatoa kipaumbele katika suala la mazingira. Ni ukweli usiofichika kwamba ili kuwa na maendeleo endelevu lazima uhifadhi wa mazingira upewe kipaumbele. Hii itawezekana endapo tu Serikali itatambua umuhimu huu na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi wa Mazingira.

6.2 Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoolezwa hapo awali, kwa mwaka ujao wa fedha 2015/2016, Idara ya Mazingira imetengewa jumla ya **Tsh 7,691,915,000=** zinazojumuisha fedha za ruzuku kwa Baraza (NEMC) **Tsh 3,326,210,000**. Bajeti hii ni ndogo kwa Idara na Baraza lake kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hasa kwa kuzingatia kwamba hawana vitendea kazi vya kutosha kama vile magari ambayo ni muhimu kwa ajili ya ukaguzi hasa katika maeneo ya viwanda na migodi.

Pamoja na hayo, bajeti hii ni ndogo sana ikilinganishwa na gharama kubwa zinazotumika katika kulinda maeneo ya fukwe na kingo za mito hususan pale ambapo inahusisha kubomoa majengo yaliyojengwa katika maeneo hayo kinyume cha Sheria;

Mheshimiwa Spika, Aidha Kamati inapendekeza kwamba, kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Fungu 31 hujumuisha mgao wa kibajeti wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa chini ya **Fungu 31** ni pesa nyingi kulinganisha na zinazobaki kwa ajili ya Idara ya Mazingira, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione

umuhimu wa kuipatia Idara ya Mazingira na Baraza lake Fungu la pekee ili kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Idara ya Mazingira kijulikane wazi.

6.3 Mheshimiwa Spika, Moja ya maoni ya Kamati hii kwa Ofisi kwa Mwaka wa fedha **2013/2014**, ilikuwa ni Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kamati ilitoa ushauri huu kwa kuzingatia kwamba mara nyingi fedha za nje huwa hazitolewi kwa wakati na hivyo kukwamisha miradi mingi. Kamati inafarijika kuwa ushauri wa Kamati umezingatiwa ambapo, kwa Mwaka ujao wa fedha **2015/2016**, Serikali imetenga fedha za ndani Tsh. **3,500,000,000/=** ikilinganishwa na **1,018,847,000/=** fedha za nje. Hii ni dalili nzuri.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za ndani za kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyokusudiwa;

6.4 Mheshimiwa Spika, Moja ya changamoto kubwa ya Idara ya Mazingira ni uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya mazingira hasa Sheria ya Mazingira namba 20 ya Mwaka 2004. Sheria hii inasema wazi kwamba itakuwa ni makosa kufanya shughuli zifuatazo bila kupata kibali cha Waziri mwenye dhamana ya mazingira:-

- Kujenga jengo au umbile lolote kwenye fukwe za bahari, ziwa, ukingo wa mto au bwawa;
- Kufukua/kutoboa fukwe na kingo za mito;
- Kuchepusha au kuzuia mito;
- Kufanya shughuli za kudumu za kibanadamu(ujenzi wa nyumba)ndani ya mita 60 kutoka baharini au kwenye kingo za mito ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha ulinzi wa mazingira na utunzaji wa bahari au kingo za mito.

Mheshimiwa Spika, waheshimiwa wabunge ni mashahidi kuhusu kuwepo kwa ujenzi usiofuata Sheria katika maeneo ya fukwe na kingo za mito. Hali hii inasababishwa na wananchi aidha kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Sheria ya Mazingira ama kukaidi Sheria hiyo. Ujenzi huu hasa katika kingo za mito unaathiri mazingira ya asili ya mito ikiwa ni pamoja na kupindisha mikondo ya mito. Hali hii ni ya hatari kwani imekuwa ikisababisha mafuriko kwa pande ambazo mito imeelekezwa na hivyo kuharibu mazingira;

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba nyumba zote zilizojengwa kinyume cha Sheria katika kingo za mito na fukwe za bahari zibomolewe na kurudisha mito iliyothirika katika hali yake ya asili ili kuondoa athari kubwa za kimazingira zinazoweza kutokea; Kamati inataka kujua maendeleo ya zoezi la uchunguzi wa hati za nyumba zilizojengwa kinyume cha sheria na maendeleo ya kesi mbali mbali zilizofunguliwa dhidi ya Baraza.

Aidha, pale ambapo imebainika kwamba waliojenga katika maeneo tuliyoyataja kwa kupewa vibali kama vile hati n.k kinyume cha Sheria, waliohusika na vitendo hivi vyta kifisadi vyta kutoa vibali au hati wakamatwe na kufikishwa katika vyombo vyta Sheria.

6.5 Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni dhahiri kwamba wananchi wengi bado hawana uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na faida zake hususan wakati huu ambapo kuna changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi.

Athari mbalimbali zimeendelea kutokea kutokana na uharibifu wa mazingira. Vitendo vyta kuharibu vyanzo vyta maji, ukataji ovyo wa miti na utupaji ovyo wa taka ni vitendo

vinavyofanyika kwa kiasi kikubwa kutokana na ukosefu wa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira mionganoni mwa wananchi;

Kamati inaishauri, Serikali itenye fedha za kutosha ili kuiwezesha Idara ya Mazingira kuendesha programu ya elimu kwa umma itakayoleta mafanikio. Kamati inashauri Serikali kutambua umuhimu wa elimu hii na kuongeza bajeti hii;

6.6 Mheshimiwa Spika, Mnamo Oktoba 2006, Serikali ilitoa agizo la kupiga marufuku vingizaji, utengenezaji, uuzaji na matumizi ya mifuko ya plastiki yenyne unene chini ya mikroni thelathini (30). Agizo hili lilirudiwa tena mwezi Agosti 2013. Aidha Serikali iliahidi kuchukua hatua ya kupiga marufuku kabisa matumizi ya mifuko laini ya plastiki ili kulinda mazingira. Hata hivyo, ni dhahiri kabisa agizo hilo halijatekelezwa kwani mazingira yetu yameendelea kuchafuliwa na mifuko hiyo hususan maeneo ya mijini na kwénye fukwe za bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza agizo lake na kuisimamia kanuni ya Kudhibiti Matumizi ya Mifuko ya Plastiki ya mwaka 2014 mapema iwezekanavyo ili kuondoa tatizo hili sugu la uchafazi wa mazingira ambalo linaitia aibu nchi yetu.

Sanjari na hilo, ni pendekezo la Kamati kwamba Serikali isimamie usafi wa mazingira kwa kudhibiti utupaji taka ovyo. Vilevile elimu ya utunzaji/usafi wa mazingira iwekwe kwenye mitaala katika shule za misingi ili kuwajengea wanafunzi utamaduni wa kuwa na mazingira safi na yaliyohifadhiwa vizuri;

6.7 Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali za Mitaa zimeendelea kuwa na mwitikio mdogo katika hifadhi na utunzaji wa Mazingira, Kamati inaendelea kushauri Ofisi ya Makamu wa Rais-mazingira kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI kufuatilia utungaji na utekelezaji wa Sheria Ndogo za hifadhi ya misitu, hifadhi ya vyanzo vya maji, tathmini ya mazingira na usafi wa mazingira. Kamati inazipongeza Halmashauri zilizoanza kutunga na kutekeleza Sheria Ndogo hizo na kutoa msisitizo kwa Halmashauri nyingine kuiga mfano huo. Halmashauri zilizotunga Sheria Ndogo zinazohusu mazingira ni Manispaa ya Moshi, Jiji la Mwanza, Halmashauri za Wilaya ya Njombe, Babati, Singida Vijijini, Iramba, Bahi, Mbeya Vijijini na Mpanda; Kamati inaishauri Serikali itafute namna mpya ya kuhimiza suala la usafi wa Mazingira badala ya utaratibu uliozoleka wa kutenga siku moja kwa mwezi kwa ajili ya kufanya usafi wa Mazingira.

Kuna haja ya kubadili mkakati ili tuwe na utamaduni wa kila siku au mara kwa mara na kuwe na motisha kwa ajili ya Halmashauri/Manispaa zitakazoshinda kwa utunzaji Mazingira. Kamati inapendekeza pia kuwe na utaratibu wa kutoa hati chafu kwa Halmashauri au Manispaa zilizofanya vibaya katika utunzaji wa Mazingira.

6.8 Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mgongano wa kimamlaka katika baadhi ya sekta na Idara ya Mazingira. Kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo ambayo huhifadhiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kama vile maeneo ya hifadhi za misitu, fukwe na vyanzo vya maji. Hata hivyo, bado mamlaka nyingine za Halmashauri na Wizara kwa kutumia Sheria zao zinaendelea kutoa vibali kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile ujenzi kandokando ya mito na fukwe za bahari. Ni rai ya Kamati kwamba kwa kuwa Mamlaka hizi zote zipo chini ya Serikali moja, zishirikiane kwa pamoja kuondoa migongano ya matumizi ya ardhi inayoendelea kukua kwa kasi nichini; Kamati inaishauri Serikali iweke mfumo wa mawasiliano ya moja kwa moja katika ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na maafisa Mazingira wa sekta na Halmashauri ili kurahisisha utekelezaji wa sheria.

Aidha, Maafisa Mazingira wa sekta na Halmashauri washirikishwe katika kutoa maamuzi ya mipango ya matumizi ya Ardhi na maamuzi mbali mbali ya kisekta. Ofisi ya Makamu wa Rais ishirikiane na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili utekelezaji wa miradi mbali mbali uweze kuzingatia masuala ya Mazingira. Kamati inaiagiza Serikali ifuatilie utekelezaji wa

masharti yaliyotolewa kwa mradi wa Dar ES Salaam Rapid Transport (DART) wakati walipopewa hati ya Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) kama yamezingatiwa.

6.9 Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa suala la mabadiliko ya tabianchi limeendelea kuleta athari nyingi ikiwa ni pamoja na ukame na mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini na duniani kote. Kamati inashauri Serikali kuendelea kukuza weledi kuhusu tatizo hili na jinsi ya kukabiliana nalo kwa wananchi wote ikiwa ni pamoja na kuhamasisha upandaji miti na kuzuia kilimo kisichofuata utaratibu katika miinuko kinachosababisha maporomoko ya ardhi na mmomonyoko wa udongo.

Aidha, Kamati inashauri Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi ianzishwe ili itoe mwongozo kwa Serikali, Taasisi na mashirika mbalimbali kuhusu uhuishaji wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya maendeleo. Vile vile Kamati inaishauri Serikali kuanzisha kituo cha "Climate Change Early Warning System" ili kuchukua tahadhari na kuwaandaa wananchi kukabiliana na majanga yanayobashiriwa kutokea.

6.10 Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia kikamilifu ufungaji wa mgodi wa Dhahabu wa Resolute. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya kusimamia ukarabati wa mazingira baada ya kufunga mgodi zinasimamiwa kikamilifu na kuwepo uwazi kujua kiasi kilichotengwa na matumizi yake.

7.0 HITIMISHO

7.1 Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati, napenda kumshukuru Mhe. Dkt. Binilith Satano Mahenge, (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Naibu Waziri Mhe. Stephen Masele; Ndugu Sazi M. Salula - Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Wataalamu wote wa Ofisi hii na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa ushirikiano, ushauri na utaalamu wao ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

7.2 Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa busara, ushirikiano na kujituma kwao bila kuchoka kwa kupitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti inayoombwa na hivyo kufanikisha Taarifa hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. James Daudi Lembeli, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdulkarim E. Hassan. Shah, Mb-M/M/Kiti
3. Mhe. Zakia Hamdani Meghji, Mb Mjumbe
4. Mhe. Sylvester Mhoja Kasulumbayi , Mb "
5. Mhe.SusanLimbweniKiwanga, Mb "
6. Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa,Mb "
7. Mhe. Muhamad Amour Chomboh, Mb "
8. Mhe. Michael Lekule Laizer, Mb "
9. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb "
10. Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb "
11. Mhe. Amina Andrew Clement, Mb "
12. Mhe. John John Mnyika, Mb "
13. Mhe. Salim Hassan Turky, Mb "
14. Mhe. Abuu Hamoud Jumaa, Mb "
15. Mhe. Kisyeri Werema Chambiri, Mb "
16. Mhe. Al-Shymaa John Kwegyr, Mb "
17. Mhe. Dkt Henry Daffa Shekifu, Mb "

18.	Mhe.MwanaKhamis KassimSaid, Mb	"
19.	Mhe. Waride Bakar Jabu, Mb	"
20.	Mhe. Clara Diana Mwatuka, Mb	"
21.	Mhe. Haji Khatibu Kai, Mb	"
22.	Mhe.Benedict Ole Nangoro, Mb	"
23.	Mhe. Dkt Dalaly Kafumu, Mb	"
24.	Mhe. Dkt Grace Kihwaya Puja, Mb	"

7.3 Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Charles Mloka, Katibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili kwa kuratibu shughuli za Kamati kwa ufasaha na kufanikisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao uliovezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

7.4 Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, na kwa kuzingatia kwamba hoja kubwa ya Kamati ni ufinyu wa bajeti usiotosheleza utekelezaji wa malengo katika Idara ya Mazingira kwa miaka mitatu mfululizo (2013/14- 2015/16); na kwa kuwa jambo hili sasa linashughulikiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge Bajeti, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ninakushukuru sana kwa usomaji mahiri wa Taarifa hiyo ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, lakini naomba nitambue uwepo wa Mheshimiwa Habib Mnyaa, ambaye kwa muda mrefu hakuwepo hapa Bungeni. (Kicheko/Makofij)

Sasa naomba nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa Tundu Lissu, dakika 20!

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, naomba nitoe Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Naomba nifanye hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa mwisho wa maisha ya Bunge la Kumi ambalo umeliongoza tangu tulipokuchagua mwezi Novemba 2010. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa Ibara ya 65 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, maisha ya kila Bunge yatakuwa ni muda wa miaka mitano, unaoanza tarehe ambapo Bunge jipya limeitishwa kukutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na kuisha tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge kwa ajili ya kuwezesha Uchaguzi Mkuu mwininge wa kawaida kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha miaka mitano katika maisha ya chombo muhimu katika nchi kama Bunge ni muda mwafaka kufanya tathmini ya kazi ambazo tumezifanya kama Wabunge na majukumu ambayo tumeyatekeleza. Siyo busara kujisemea ama kujisifu kwa kazi ambazo nimezifanya ndani ya Bunge lako Tukufu na majukumu ambayo nimeyatekeleza kama Mbunge, Mnadhimu Mkuu na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu

kuhusu masuala ya Muungano na masuala ya Katiba na Sheria. Hilo ninawaachia wapiga kura na wananchi wangu wa Jimbo la Singida Mashariki ambaeo leo wamewakilishwa vyema na viongozi mbalimbali wa chama chao cha ukombozi wa Kata zote za Jimbo langu na wengine nje ya Jimbo ambaeo wanafaa zaidi kutoa hukumu juu ya utendaji kazi wangu wa kazi za Kibunge. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo naomba niwashukuru kwa moyo wangu wote kwa kunipa heshima kubwa ya kuwatumikia wao na Watanzania wengine katika Bunge lako Tukufu. Ni matumaini yangu kwamba imani yao kubwa kwangu katika miaka hii mitano ya maisha ya Bunge hili la Kumi haikuwa ya bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hawajasahau, lakini siyo vibaya kuwakumbusha Makamanda wangu kwamba, huu ni mwaka wa kukamilisha ile kazi tulioianza Januari 2008, tukaifanya vizuri Oktoba 2010 na kufaulu kwa kiwango cha kihistoria kilichoishangaza Tanzania mwezi Desemba 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni yetu ya mwaka jana, tuliliambia Bunge lako Tukufu kwa mchanganuo wa mgawanyo wa mapato mbalimbali ya Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar kwamba Muungano huu ni kielelezo cha unyonyaji na ukandamizaji mkubwa ambaeo nchi ndogo ya Zanzibar imefanyiwa na nchi kubwa ya Tanganyika. Ni mfano wa jinsi ambavyo nchi moja kubwa ya Kiafrika imeweza kuigeuza nchi nyingine ndogo ya Kiafrika kuwa koloni lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulionyesha kwenye maoni yetu jinsi ambavyo kwa miaka mingi Zanzibar imepunjwa katika mgawanyo wa misaada na mikopo ya kibajeti inayopatikana kwa jina la Jamhuri ya Muungano. Ndiyo maana mwaka 2013 Kamati ya Kudumu ya Bunge lako Tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala iliishauri Serikali hii ya CCM kuangalia upya utaratibu wa mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotoka kwa wafadhili.

Aidha, Kamati iliishauri kwamba, Serikali itolee uamuzi mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha yaliyowasilishwa Serikalini tangu mwaka 2006 na kuwasilishwa tena mwaka 2010 kuhusu utaratibu wa mgao wa fedha za Serikali zote mbili. (Makofii)

Serikali hii ya CCM ilijibu ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuahidi kwamba, Serikali zetu mbili bado zinaendelea kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Ndiyo kusema kwamba karibu miaka kumi baada ya Tume ya Pamoja ya Fedha kupendekeza utaratibu mpya wa mgawanyo wa mapato ya Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar, bado Serikali hii sikuwa inaendelea na mchakato wa kushughulikia mapendekezo hayo!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujibu ushauri wa Kamati, Serikali hii ya CCM ililiambia Bunge lako Tukufu vilevile kwamba kwa utaratibu ulivyo sasa, mgawo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa misaada na mikopo ya kibajeti inayotolewa na nchi wafadhili na Mashirika ya Kimataifa ni asilimia 4.5. Hata hivyo, tulionyesha kwa kutumia takwimu zilizoletwa Bungeni na Waziri wa Fedha kwamba hata kwa Makadirio ya mwaka wa fedha 2013/2014, Zanzibar iliikuwa imetengewa asilimia 2.8 tu ya misaada na mikopo ya kibajeti iliyoitoka kwa wafadhili wa nje. Kiasi hicho kilipungua hadi kufikia takribani asilimia 2.2 katika Makadirio ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti mwaka wa fedha 2014/2015 na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016, iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais mwezi uliopita, kati ya shilingi bilioni 44 zilizoidhinishwa na Bunge mwaka jana kwa ajili ya kupelekwa Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar kama mgawo wa Zanzibar wa misaada ya kibajeti na mikopo, ni shilingi bilioni 27.68 ndizo zilizopelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015.

Kiasi hiki hakitofautiani sana na shilingi bilioni 27.19 za misaada ya kibajeti na mikopo zilizopelekwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika mwaka wa fedha fg2013/2014. Hata hivyo, uchunguzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti unaonyesha kwamba, takwimu hizi za Serikali hii ya CCM zinapotosha ukweli wa hali halisi kwa kiasi kikubwa. Kwamba takwimu sahihi zinaonyesha kiasi kilichotolewa kama mgawo wa Zanzibar wa mikopo nafuu na misaada ya kibajeti ni kidogo kwa karibu mara tatu kiasi cha shilingi bilioni 27.68 kilichotajwa kwenye Taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa aya ya 3.3.2(b) ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), imeratibu gawio la fedha la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya kusaidia kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii. Gawio hilo hujumuisha misaada ya Kibajeti, fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, faida ya Benki Kuu na Kodi ya Mishahara (PAYE). Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2015, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipokea shilingi bilioni 27.681 kati ya shilingi bilioni 44 zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 7.137 ni Gawio la Kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na shilingi bilioni 15.75 ni fedha za Kodi ya Mishahara, shilingi bilioni 1.2 ni fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na shilingi bilioni 3.2 ni gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imepokea shilingi milioni 350 ikiwa ni deni la fedha zilizotumiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 50 ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbe kile ambacho Serikali hii ya CCM hukieleza kila mwaka kuwa ni mgawo wa Zanzibar wa fedha za misaada ya kibajeti na mikopo yenyenye masharti nafuu, kinajumuisha pia fedha za ndani zinazojumuisha makato ya mishahara ya wafanyakazi, fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na hata mchango wa Sherehe za Kitaifa kama Muungano! Kama mgao halisi wa Zanzibar kutokana na misaada ya kibajeti na mikopo nafuu ni shilingi bilioni 7.137 kama inavyoonyeshwa kwenye Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti, maana yake ni kwamba kiasi kilichotolewa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika mwaka huu wa fedha ni pungufu kwa takribani asilimia 74 ukilinganisha na fedha iliyoolewa mwaka jana, assuming takwimu za mwaka jana hazikuchakachuliwa kama za mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, whether tunatumia takwimu zilizochakachuliwa na zinazoonyesha Serikali ya Mapinduzi imepata shilingi bilioni 27 kama mgawo wake wa misaada ya kibajeti na mikopo yenyenye masharti nafuu katika mwaka huu wa fedha au takwimu zinazoonyesha kiasi halisi kuwa ni shilingi bilioni 7.137, nyaraka nyingine zilizowasilishwa Bungeni na Serikali hii ya CCM zinaashiria kwamba, Zanzibar imendelea kupunjwa mapato yake halali kwa sababu ya Muungano huu. Katika Maelezo ya Waziri wa Fedha akiwasilisha Mapendekezo ya Mfumo wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Waheshimiwa Wabunge tarehe 29 Aprili, 2015, Bunge lako Tukufu liliambiwa kwamba, hadi kufikia Machi 2015, kiasi cha shilingi bilioni 1,583 kilipokelewa kama misaada ya kibajeti na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia takwimu zilizochakachuliwa za shilingi bilioni 27, hii ina maana kwamba, mgawo wa Zanzibar kutokana na fedha zilizotoka nje na Taasisi za Maendeleo za Kimataifa ni takribani asilimia 1.7 tu, wakati Tanganyika imechukua shilingi bilioni 1,555 au asilimia 98.3 ya fedha zote zilizokuja mwaka huu wa fedha kwa jina la Tanzania. Kwa upande mwingine, kwa kutumia takwimu zinazoonyesha kiasi halisi kuwa shilingi bilioni 7.137, mgao wa Zanzibar wa misaada ya kibajeti na mikopo yenyenye masharti nafuu kwa mwaka huu ni

asilimia 0.45 tu! Kiasi kilichobaki, yaani shilingi bilioni 1,575.863 au asilimia 99.55 ya fedha zote za misaada ya kibajeti na mikopo ya masharti nafuu imebaki Tanganyika! (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Zanzibar ingepata mgawo wa asilimia 4.5 ambao tumekuwa tunaambibiwa na Serikali hii ya CCM, basi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ingepaswa kupokea jumla ya shilingi bilioni 71.235 kama fedha za misaada ya kibajeti na mikopo yenye masharti nafuu. Kwa sababu ya muundo wa Muungano kama ulivyo sasa, Zanzibar imepokea shilingi bilioni 7.137 kati ya shilingi bilioni 71.325 ya fedha zake halali katika mwaka huu wa fedha. Hii ni asilimia 10 tu ya fedha ambazo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipaswa kupokea kama misaada ya kibajeti na mikopo yenye masharti nafuu. Shilingi bilioni 64.098 au asilimia 90 ya fedha zilizobaki imechukuliwa na Serikali ya Tanganyika ambayo kwa maneno ya Spika Emeritus Msekwa, ndiyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya Serikali hii ya CCM kuhusu mgawo wa Zanzibar kwa misaada ya kibajeti na mikopo yenye masharti nafuu kwa mwaka unaokuja wa fedha 2015/2016, hayana nafuu yoyote kwa Zanzibar. Kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti, katika mwaka wa fedha 2015/2016, mgao wa misaada na mikopo ya kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar unakadiriwa kuwa shilingi bilioni 22.400. Katika kipindi hicho, kwa mujibu wa Maelezo ya Waziri wa Fedha, misaada ya kibajeti na mikopo ya masharti nafuu inayokadiriwa kuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano itakuwa shilingi bilioni 1,888.178. Kwa maana hiyo, mgawo unaopendekezwa kwa Zanzibar ni takribani asilimia 1.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Zanzibar ingepata mgawo wa asilimia 4.5 kama ambavyo imezungumzwa kwa miaka mingi na Serikali hii ya CCM, basi makadirio ya mgawo wake yangekuwa shilingi bilioni 84.968. Kwa hiyo, kwa mapendekezo haya, Zanzibar itapoteza kwa Tanganyika shilingi bilioni 62.568, au asilimia 73.6 ya fedha zake halali. Katika mazingira haya na kwa takwimu hizi, ni watu wenye masilahi katika unyonyaji huu pekee ndiyo wanaoweza kubishia ukweli wa kauli ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Maalim Seif Shariff Hamad, kwamba, Mfumo wa Muungano uliopo sasa hauinufaishi Zanzibar na hivyo haukulaliki kwa Wazanzibari. Koti la Muungano kama liliuyo sasa linabana sana. Wakati umefika tushone koti jipy kwa mujibu wa mahitaji ya zama hizi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni yetu ya mwaka 2014 tulionyesha kwamba hali ni mbaya zaidi kuhusiana na fedha za misaada na mikopo isiyokuwa ya kibajeti. Katika eneo hili tulionyesha kwamba, Zanzibar imekuwa haipati mgawo wowote wa fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo zikijumuisha misaada na mikopo ya Basket Fund na misaada na mikopo ya miradi. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, fedha hizo zilituwa takribani shilingi bilioni 2,692 na zote zilitumika kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Tanganyika. Maelezo ya Waziri wa Fedha yanaonyesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mikopo na misaada ya Miradi ya Maendeleo ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 2,019.43. Ijapokuwa maelezo hayo hayaonyeshi ni kiasi gani cha fedha hizo kilipatikana, ni wazi kwamba, kiasi chochote kitakachokuwa kimepatikana, kitakuwa kimetumika kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni hiyo hiyo kwa mikopo yenye masharti ya kibiashara, ambayo katika mwaka wa fedha 2014/2015, ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 1,320. Maelezo ya Waziri wa Fedha yanasema hadi kufikia Machi 2015, Serikali ilipokea mkopo wa dola milioni 300, sawa na shilingi bilioni 514 kutoka Benki ya Maendeleo ya China. Kama tulivyotabiri mwaka 2014, kwa sababu ya muundo wa Muungano wetu, kwenye fedha hizi Zanzibar haikupata kitu chochote. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaamini kwamba dhana iliyojengwa kwa muda mrefu na Serikali hii ya CCM kwamba Zanzibar ina haki

ya kupatiwa mgawo hata kama ni kwa kupunjwa sana, wa fedha za mikopo ya masharti nafuu na misaada ya kibajeti, lakini haina haki ya kupata mgawo wowote wa fedha za mikopo ya masharti ya kibiashara na misaada ya Miradi ya Maendeleo ni sababu kubwa ya dhuluma inayotendewa Zanzibar katika mgawo wa fedha na mapato mengine yanayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana hii haina msingi wowote Kikatiba na kisheria. Ukweli ni kwamba, mgawanyo wa fedha na mapato ya Muungano ambao umejengwa kwa msingi wa dhana hii unakuuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ni kinyume na masharti ya Makubaliano ya Muungano ya Mwaka 1964. Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ambayo imeorodhesha Mambo ya Muungano inaonyesha kwamba, Mikopo na Biashara ya Nchi za Nje na Mambo yote yanayohusika na fedha na sarafu kwa ajili ya malipo yote halali, fedha za kigeni na usimamizi wa mambo yanayohusika na fedha za kigeni ni mojawapo ya mambo 22 ya Muungano. Hali hii imekuwa hivyo tangu Makubaliano ya Muungano yaliposainiwa tarehe 22 Aprili, 1964.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba yetu hajatenganisha kati ya mikopo ya masharti nafuu ambayo Zanzibar ina haki ya kupata mgao na mikopo yenyeye masharti ya kibiashara, ambayo Zanzibar haina haki ya kupatiwa mgao. Mikopo ya masharti ya aina zote ni mambo ya Muungano na Zanzibar ina haki na imekuwa na haki tangu mwaka 1964 kwa mujibu wa Katiba, ya kupata mgawo wa mikopo hiyo. (Makofii)

Msimamo ni huo huo kwa misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo. Katiba yetu hajatenganisha kati ya misaada ya kibajeti ambayo Zanzibar inastahili kugawiwa na ile isiyokuwa ya kibajeti ambayo Zanzibar haistahili kupata mgao. Kwa vile misaada yote inayotoka kwa washirika wa maendeleo inakuja kama fedha za kigeni, basi inaangukia katika kipengele cha mambo ya Muungano kinachohusiana na mambo yote yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yote halali, fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yote yanayohusika na fedha za kigeni. Kwa sababu hiyo, Zanzibar ilistahili na bado inastahili kupata mgawo wa fedha za misaada ya aina zote, iwe ya kibajeti ama isiyokuwa ya kibajeti. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2014 Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge lako Tukufu ilitoa agizo kwamba, Serikali iweke utaratibu wa kutoa taarifa na elimu kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na wananchi kwa ujumla, juu ya namna na kiasi gani cha fedha Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaichangia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Kamati iliagiza kwamba taarifa kuhusu fedha zote zinazopelekwa Zanzibar kupitia Hazina au mamlaka yoyote, ziwasilishwe Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa ajili ya kumbukumbu na kuujulisha umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo hilo la Bunge lako Tukufu halijatekelezwa. Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2014/2015 haina tofauti yoyote na taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa kila mwaka na Ofisi ya Makamu wa Rais. Kama ilivyokuwa mwaka 2014 na miaka mingine yote ya nyuma, Taarifa ya mwaka huu haionyeshi kiasi chochote cha fedha kilichotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutoka fungu la mikopo na misaada ya Miradi ya Maendeleo ambayo siyo ya kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya mwaka huu haionyeshi fedha yoyote iliyotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama mgawo wa Zanzibar kutoka kwenye fungu la mikopo yenyeye masharti ya kibiashara na wala hakuna taarifa yoyote kuhusu fedha zote zinazopelekwa Zanzibar kupitia Hazina au mamlaka yoyote ya Jamhuri ya Muungano. Kwa kifupi, agizo la Bunge lako Tukufu limepuuzwa na Serikali hii sikivu ya CCM! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, badala yake, Serikali hii ya CCM imekuja na *blah blah* zake za miaka yote ili kuwapumbaza wajinga na kuwadanganya wasioelewa. Hivi ndivyo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anavyoolezea utekelezaji wa agizo hilo la Bunge. Serikali ina utaratibu wa kutoa taarifa kuhusu fedha zinazopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Bunge na machapisho mbalimbali kuhusu Muungano. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuhakikisha kuwa, taarifa hizo zinapatikana na kuwajulisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima zote kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hoja siyo kwamba Kamati ya Bunge ilikuwa hajui kuwa Serikali ina utaratibu wa kutoa taarifa kwa Bunge kuhusu fedha zinazopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hoja ya msingi ni kwamba, Kamati haikuridhika na utaratibu huo. Hoja ya msingi ni kwamba utaratibu wa sasa wa utoaji wa taarifa za fedha za Muungano na mgawanyo wake unaficha unyonyaji na dhuluma kubwa inayofanyiwa Zanzibar katika mgawanyo wa fedha na mapato mengineyo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni yetu ya mwaka jana, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu ilitaka Serikali hii ya CCM ilete mbele ya Bunge lako Tukufu takwimu za fedha zote zilizopokelewa na Serikali kama misaada na mikopo ya kibajeti kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita na sehemu ya fedha zilizolipwa kwa Zanzibar kama gawio lake katika kipindi hicho. Kama tulivyosema katika maoni yetu hayo, takwimu hizo ni muhimu ili Watanzania na hasa Wazanzibari, waweze kufahamu kama Zanzibar imekuwa ikipata sehemu yake halali ya mapato ya Jamhuri ya Muungano yanayotokana na misaada na mikopo ya kibajeti. (Makofij)

Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitoa ahadi kwa Bunge lako Tukufu kwamba angeleta takwimu hizo. Hajafanya hivyo! Maelezo yake hayana takwimu zozote za mgawanyo wa mapato ya Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar za kipindi chochote. Katika mazingira haya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itasemehewa na wapenda haki wote kwa kuamini kwamba, takwimu hizi zinafichwa kwa sababu zina ushahidi wa dhuluma kubwa ambayo Zanzibar na Wazanzibari wamefanyiwa na Serikali ya Tanganyika, ambayo ndiyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa miaka yote ya Muungano huu. Kama maneno yetu haya siyo ya kweli, basi Serikali hii ya CCM na ithubutu kuthibitisha uongo wetu kwa kutoa takwimu za mgawanyo wa mapato yote ya Muungano kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyoahidi kuzileta Bungeni. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo lingine la Bunge lako Tukufu ambalo limepuuzwa na Serikali hii ya CCM linahusu hisa za Zanzibar katika iliyokuwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki ambayo ilivunjwa mwaka 1966 pale nchi wanachama wake zilipoanzisha Benki Kuu zao. Kwa sababu ya masuala ya sarafu na fedha kufanywa mambo ya Muungano...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu, dakika 20 zimeisha!

MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba maelezo mengine yaliyobaki yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge. (Makofij)

MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO), MHESHIMIWA TUNDU A.M. LISSU (MB.) KUHUSU MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)
KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika,

Huu ni mwaka wa mwisho wa maisha ya Bunge la Kumi ambalo umeliongoza tangu tulipokuchagua mwezi Novemba 2010. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa ibara ya 65 ya **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977**, "... maisha ya kila Bunge yatakuwa ni muda wa miaka mitano ... unaoanza tarehe ambapo Bunge jipya limeitishwa kukutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na kuisha tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge kwa ajili ya kuwezesha Uchaguzi Mkuu mwingine wa kawaida kufanyika."

Kipindi cha miaka mitano katika maisha ya chombo muhimu katika nchi kama Bunge ni muda muafaka kufanya tathmini ya kazi ambazo tumezifanya kama Wabunge na majukumu ambayo tumeyatekeleza. Si busara kujisemea ama kujisifu kwa kazi ambazo nimezifanya ndani ya Bunge lako tukufu na majukumu ambayo nimeyatekeleza kama Mbunge, Mnadhimu Mkuu na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu kuhusu masuala ya Muungano na masuala ya Katiba na Sheria. Hilo ninawaachia wapiga kura na wananchi wangu wa Jimbo la Singida Mashariki – ambao leo wamewakilishwa vyema na viongozi mbali mbali wa chama chao cha ukombozi wa Kata zote za Jimbo letu – na wengine nje ya Jimbo ambao wanafaa zaidi kutoa hukumu juu ya utendaji wangu wa kazi za kibunge.

Kwa leo naomba tu niwashukuru kwa moyo wangu wote kwa kunipa heshima kubwa ya kuwatumikia wao na Watanzania wengine katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba imani yao kubwa kwangu katika miaka hii mitano ya maisha ya Bunge hili la Kumi haikuwa ya bure. Najua hawajasahau, lakini si vibaya kuwakumbusha makamanda wangu, kwamba huu ni mwaka wa kukamilisha ile kazi tulioianza Januari 2008, tukaifanya vizuri Oktoba, 2010 na kufaulu kwa kiwango cha kihistoria kilichoishangaza Tanzania mwezi Desemba ya mwaka jana.

MGAWANYO WA MAPATO YA MUUNGANO

Mheshimiwa Spika,

Katika Maoni yetu ya mwaka jana tuliliambia Bunge lako tukufu – kwa mchanganuo wa mgawanyo wa mapato mbali mbali ya Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar - kwamba "... Muungano huu ni kielelezo cha unyonyaji na ukandamizaji mkubwa ambao nchi ndogo ya Zanzibar imefanyiwa na nchi kubwa ya Tanganyika. Ni mfano wa jinsi ambavyo nchi moja kubwa ya Kiafrika i[me]weza kuigeuza nchi nyingine ndogo ya Kiafrika kuwa koloni lake."

Tulionyesha kwenye Maoni yetu jinsi ambavyo kwa miaka mingi Zanzibar imepunjwa katika mgawanyo wa misaada na mikopo ya kibajeti inayopatikana kwa jina la Jamhuri ya Muungano. Ndio maana mwaka 2013 Kamati ya Kudumu ya Bunge lako tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala iliishauri Serikali hii ya CCM kuangalia upya "utaratibu wa mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotoka kwa wafadhili...." Aidha, Kamati iliishauri kwamba "Serikali itolee uamuzi mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha yaliyowasilishwa Serikalini tangu mwaka 2006 na kuwasilishwa tena mwaka 2010 kuhusu utaratibu wa mgao wa fedha za Serikali zote mbili."

Serikali hii ya CCM ilijibu ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuahidi kwamba "Serikali zetu mbili bado zinaendelea kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha." Ndio kusema kwamba karibu miaka kumi baada ya Tume ya Pamoja ya Fedha kupendekeza utaratibu mpya wa mgawanyo wa mapato ya Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar, bado Serikali hii sikivu inaendelea na 'mchakato' wa kushughulikia mapendekezo haya!

MIKOPO YA MASHARTI NAFUU NA MISAADA YA KIBAJETI

Mheshimiwa Spika,

Katika kujibu ushauri wa Kamati, Serikali hii ya CCM illiambia Bunge lako tukufu vile vile kwamba, kwa utaratibu ulivyo sasa, mgawo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa misaada na mikopo ya kibajeti inayotolewa na nchi wafadhili na mashirika ya kimataifa ni asilimia 4.5. Hata hivyo, tulionyesha – kwa kutumia takwimu zilizoletwa Bungeni na Waziri wa Fedha - kwamba hata kwa makadirio ya mwaka wa fedha 2013/2014, Zanzibar ilikuwa imetengewa asilimia 2.8 tu ya misaada na mikopo ya kibajeti iliyoleta kwa wafadhili wa nje. Kiasi hicho kilipungua hadi kufikia takriban asilimia 2.2 katika makadirio ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika,

Kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti Mwaka wa Fedha 2014/15 na Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/16 iliyowasilishwa mbele ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge lako tukufu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais mwezi uliopita, kati ya shilingi bilioni 44.039 zilizoidhinishwa na Bunge mwaka jana kwa ajili ya kupelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama mgawo wa Zanzibar wa misaada ya kibajeti na mikopo, ni shilingi bilioni 27.681 ndizo zilizopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015.

Kiasi hiki hakitofautiani sana na shilingi bilioni 27.190 za misaada ya kibajeti na mikopo zilizopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika mwaka wa fedha 2014/15. Hata hivyo, uchunguzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti unaonyesha kwamba takwimu hizi za Serikali hii ya CCM zinapotosha ukweli wa hali halisi kwa kiasi kikubwa. Kwamba takwimu sahihi zinaonyesha kiasi kilichotolewa kama mgawo wa Zanzibar wa mikopo nafuu na misaada ya kibajeti ni kidogo kwa karibu mara tatu kiasi cha shilingi bilioni 27.681 kilichotajwa kwenye Taarifa.

Kwa mujibu wa aya ya 3.3.2(b) ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti:

“Ofisi (ya Makamu wa Rais – Muungano) imeratibu gawio la fedha la asilimia 4.5 kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kusaidia kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii. Gawio hilo hujumuisha Misaada ya Kibajeti (GBS), fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, faida ya Benki Kuu na Kodi ya Mishahara (PAYE). Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, [Serikali ya Mapinduzi Zanzibar] ilipokea shilingi 27,681,808,403/= kati ya shilingi 44,039,608,000/= zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, shilingi 7,137,882,543/= ni Gawio la Kibajeti kwa [Serikali ya Mapinduzi Zanzibar] na shilingi 15,750,000,000/= ni fedha za Kodi ya Mishahara, shilingi 1,243,925,860/= ni fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na shilingi 3,200,000,000/= ni gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, [Serikali ya Mapinduzi Zanzibar] imepokea shilingi 350,000,000/= ikiwa ni deni la fedha zilizotumiwa na [Serikali ya Mapinduzi Zanzibar] wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya sherehe za miaka 50 ya Muungano.”

Kumbe, Mheshimiwa Spika, kile ambacho Serikali hii ya CCM hukieleza kila mwaka kuwa ni mgawo wa Zanzibar wa fedha misaada ya kibajeti na mikopo yenye masharti nafuu kinajumuisha pia fedha za ndani zinazojumuisha makato ya mishahara ya wafanyakazi, fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na hata mchango wa sherehe za kitaifa kama Muungano! Kama mgawo halisi wa Zanzibar kutokana na misaada ya kibajeti na mikopo nafuu ni shilingi bilioni 7.137 kama inavyoonyeshwa kwenye Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti, maana yake ni kwamba kiasi kilichotolewa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika mwaka huu wa fedha ni pungufu kwa takriban asilimia 74 ukilinganisha na fedha iliyotolewa mwaka jana, assuming takwimu za mwaka jana hazikuchakachuliwa kama za mwaka huu.

Mheshimiwa Spika,

Whether tunatumia takwimu zilizochakachuliwa zinazoonyesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imepata shilingi bilioni 27.681 kama mgawo wake wa misaada ya kibajeti na mikopo yenyenye masharti nafuu katika mwaka huu wa fedha, au takwimu zinazoonyesha kiasi halisi kuwa ni shilingi bilioni 7.137, nyaraka nyingine zilizowasilishwa Bungeni na Serikali hii ya CCM zinaashiria kwamba Zanzibar imeendelea kupunjwa mapato yake halali kwa sababu ya Muungano huu.

Katika Maelezo ya Waziri wa Fedha Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (MB) Akiwasilisha Mapendeleko ya Mfumo wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/16 kwa Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dar es Salaam, mnamo tarehe 29 Aprili, 2015, Bunge lako tukufu liliambiwa kwamba “[h]adi kufikia Machi, 2015 kiasi cha shilingi bilioni 1,583 kilipokelewa ...” kama misaada ya kibajeti na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Kwa kutumia takwimu zilizochakachuliwa za shilingi bilioni 27.681, hii ina maana kwamba mgawo wa Zanzibar kutohuna na fedha zilizotoka nchi za nje na taasisi za maendeleo za kimataifa ni takriban asilimia 1.7 tu, wakati Tanganyika imechukua shilingi bilioni 1,555.319, au asilimia 98.3 ya fedha zote zilizokuja mwaka huu wa fedha kwa jina la Tanzania. Kwa upande mwingine, kwa kutumia takwimu zinazoonyesha kiasi halisi kuwa shilingi bilioni 7.137, mgawo wa Zanzibar wa misaada ya kibajeti na mikopo yenyenye masharti nafuu kwa mwaka huu ni asilimia 0.45 tu! Kiasi kilichobaki, yaani shilingi bilioni 1,575.863 au asilimia 99.55 ya fedha zote za misaada ya kibajeti na mikopo ya masharti nafuu imebaki Tanganyika!

Mheshimiwa Spika,

Kama Zanzibar ingepata mgawo wa asilimia 4.5 ambaa tumekuwa tunauambiwa na Serikali hii ya CCM, basi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ingepaswa kupokea jumla ya shilingi bilioni 71.235 kama fedha za misaada ya kibajeti na mikopo yenyenye masharti nafuu. Kwa sababu ya muundo wa Muungano kama ulivyo sasa, Zanzibar imepokea shilingi bilioni 7.137 kati ya shilingi bilioni 71.235 ya fedha zake halali katika mwaka huu wa fedha. Hii ni asilimia 10 tu ya fedha ambazo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipaswa kupokea kama misaada ya kibajeti na mikopo yenyenye masharti nafuu. Shilingi bilioni 64.098 au asilimia 90 ya fedha zilizobaki imechukuliwa na Serikali ya Tanganyika ambayo, kwa maneno ya Speaker Emeritus Msekwa, ndiyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika,

Mapendeleko ya Serikali hii ya CCM kuhusu mgawo wa Zanzibar kwa misaada ya kibajeti na mikopo yenyenye masharti nafuu kwa mwaka unaokuja wa fedha 2015/16 hayana nafuu yoyote kwa Zanzibar. Kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti, katika mwaka wa fedha 2015/16 “... mgao wa misaada na mikopo ya kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ...” unakadirisha kuwa shilingi bilioni 22.400. Katika kipindi hicho, kwa mujibu wa Maelezo ya Waziri wa Fedha, misaada ya kibajeti na mikopo ya masharti nafuu inayokadirisha kuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano itakuwa shilingi bilioni 1,888.178. Kwa maana hiyo, mgawo unaopendekezwa kwa Zanzibar ni takriban asilimia 1.9.

Kama Zanzibar ingepata mgawo wa asilimia 4.5 kama ambavyo imezungumzwa kwa miaka mingi na Serikali hii ya CCM, basi makadirio ya mgawo wake yangekuwa shilingi bilioni 84.968. Kwa hiyo, kwa mapendeleko haya, Zanzibar itapoteza kwa Tanganyika shilingi bilioni 62.568, au asilimia 73.6 ya fedha zake halali. Katika mazingira haya, na kwa takwimu hizi, ni watu wenye maslahi katika unyonyaji huu pekee ndio wanaoweza kubishia ukweli wa kauli ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Maalim Seif Shariff Hamad, kwamba: “Mfumo (wa Muungano) uliopo sasa hauinufaishi Zanzibar na hivyo haukulaliki kwa Wazanzibari. Koti la Muungano kama liliivo sasa linabana sana. Wakati umefika tushone koti jipya kwa mujibu wa mahitaji ya zama hizi.”

MISAADA ISIYOKUWA YA KIBAJETI NA MIKOPO YA KIBIASHARA

Mheshimiwa Spika,

Katika Maoni yetu ya mwaka jana tulionyesha kwamba "... hali ni mbaya zaidi kuhusiana na fedha za misaada na mikopo isiyokuwa ya kibajeti." Katika eneo hili tulionyesha kwamba Zanzibar imekuwa haipati mgawo wowote wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikijumuisha misaada na mikopo ya Basket Fund na misaada na mikopo ya miradi. Katika mwaka wa fedha 2013/14, fedha hizo zilikuwa takriban shilingi bilioni 2,692 na zote zilitumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tanganyika.

Maelezo ya Waziri wa Fedha yanaonyesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2014/15, 'mikopo na misaada ya miradi maendeleo' ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 2,019.43. Ijapokuwa Maelezo hayo hayaonyeshi ni kiasi gani cha fedha hizo kilipatikana, ni wazi kwamba kiasi chochote kitakachokuwa kimepatikana kitakuwa kimetumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tanganyika.

Hali ni hiyo hiyo kwa 'mikopo yenye masharti ya kibiashara', ambayo, katika mwaka wa fedha 2014/15, ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 1,320. Maelezo ya Waziri wa Fedha yanasema: "Hadi kufikia Machi 2015, Serikali ilipokea mkopo wa dola milioni 300 (sawa na shilingi bilioni 514) kutoka Benki ya Maendeleo ya China (CDB)." Kama tulivyotabiri mwaka jana, kwa sababu ya muundo wa Muungano wetu, kwenye fedha hizi "Zanzibar hai[ku]pata kitu chochote."

DHANA POTOFU

Mheshimiwa Spika,

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaamini kwamba dhana iliyojengwa kwa muda mrefu na Serikali hii ya CCM kwamba Zanzibar ina haki ya kupatiwa mgawo - hata kama ni kwa kupunjwa sana – wa fedha za mikopo ya masharti nafuu na misaada ya kibajeti, lakini haina haki ya kupata mgawo wowote wa fedha za mikopo ya masharti ya kibiashara na misaada ya miradi ya maendeleo ni sababu kubwa ya dhuluma inayotendewa Zanzibar katika mgawo wa fedha na mapato mengine yanayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano.

Dhana hii haina msingi wowote kikatiba na kisheria. Ukweli ni kwamba mgawanyo wa fedha na mapato ya Muungano ambaa umejengwa kwa msingi wa dhana hii unakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ni kinyume cha masharti ya Makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964. Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ambayo imenorodhesha Mambo ya Muungano inaonyesha kwamba 'Mikopo na Biashara ya Nchi za Nje'; na 'Mambo yote yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali; ... fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusika na fedha za kigeni' ni mojawapo ya mambo 22 ya Muungano. Hali hii imekuwa hivyo tangu Makubaliano ya Muungano yaliposainiwa tarehe 22 Aprili, 1964.

Mheshimiwa Spika,

Katiba yetu haijatenganisha kati ya mikopo ya masharti nafuu – ambayo Zanzibar ina haki ya kupata mgawo – na mikopo yenye masharti ya kibiashara, ambayo Zanzibar haina haki ya kupatiwa mgawo. Mikopo ya masharti ya aina zote ni Mambo ya Muungano na Zanzibar ina haki, na imekuwa na haki tangu mwaka 1964, kwa mujibu wa Katiba, ya kupata mgawo wa mikopo hiyo.

Msimamo ni huo huo kwa misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo. Katiba yetu haijatenganisha kati ya misaada ya kibajeti – ambayo Zanzibar inastahili kugawiwa - na ile isiyokuwa ya kibajeti, ambayo Zanzibar haistahili kupata mgawo. Kwa vile misaada yote

inayotoka kwa washirika wa maendeleo inakuja kama fedha za kigeni, basi inaangukia katika kipengere cha Mambo ya Muungano kinachohusiana na ‘mambo yote yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali ... fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yote yanayohusika na fedha za kigeni.’ Kwa sababu hiyo, Zanzibar ilistahili, na bado inastahili, kupata mgawo wa fedha za misaada ya aina zote, iwe ya kibajeti ama isiyokuwa ya kibajeti.

MAAGIZO YA BUNGE YAMEPUUZWA

Mheshimiwa Spika,

Mwaka jana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge lako tukufu ilitoa agizo kwamba “Serikali iweke utaratibu wa kutoa taarifa/elimu kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi kwa ujumla kuhusu namna na kiasi gani cha fedha Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaichangia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.” Aidha, Kamati iliagiza kwamba “taarifa kuhusu fedha zote zinazopelekwa Zanzibar kupitia Hazina au mamlaka yoyote, ziwasilishwe Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa ajili ya kumbukumbu na kuujulisha umma wa Watanzania.”

Agizo hilo la Bunge lako tukufu halijatekelezwa. Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2014/15 haina tofauti yoyote na Taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa kila mwaka na Ofisi ya Makamu wa Rais. Kama ilivyo kuwa mwaka jana na miaka mingine yote ya nyuma, Taarifa ya mwaka huu haionyesi kiasi chochote cha fedha kilichotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutoka fungu la ‘mikopo na misaada ya miradi ya maendeleo’ ambayo sio ya kibajeti.

Taarifa ya mwaka huu haionyesi fedha yoyote iliyotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama mgawo wa Zanzibar kutoka kwenye fungu la ‘mikopo yenye masharti ya kibiashara.’ Na wala hakuna taarifa yoyote kuhusu ‘fedha zote zinazopelekwa Zanzibar kupitia Hazina au mamlaka yoyote’ ya Jamhuri ya Muungano. Kwa kifupi, agizo la Bunge lako tukufu limepuuzwa na Serikali hii sikivu ya CCM!

Badala yake, Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya CCM imekuja na blah blah zake za miaka yote ili kuwapumbaza wajinga na kuwadanganya wasioelewa. Hivi ndivyo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais anavyoolezea ‘Utekelezaji’ wa agizo hilo la Bunge: “Serikali ina utaratibu wa kutoa taarifa kuhusu fedha zinazopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Bunge na machapisho mbali mbali kuhusu Muungano. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuhakikisha kuwa, taarifa hizo zinapatikana na kuwajulisha wananchi.”

Kwa heshima zote kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hoja sio kwamba Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilikuwa hajui kuwa Serikali ina utaratibu wa kutoa taarifa kwa Bunge kuhusu fedha zinazopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hoja ya msingi ni kwamba Kamati haikuridhika na utaratibu huo. Hoja ya msingi ni kwamba utaratibu wa sasa wa utoaji wa taarifa za fedha za Muungano na mgawanyo wake unaficha unyonyaji na dhuluma kubwa inayofanyiwa Zanzibar katika mgawanyo wa fedha na mapato mengine ya Muungano.

Mheshimiwa Spika,

Katika Maoni yetu ya mwaka jana, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu iliitaka Serikali hii ya CCM “... ilete mbele ya Bunge lako tukufu takwimu za fedha zote zilizopokelewa na Serikali kama misaada na mikopo ya kibajeti kwa kipindi cha miaka kumi iliopita na sehemu ya fedha hizo zilizolipwa kwa Zanzibar kama gawio lake katika kipindi hicho.” Kama tulivyosema katika Maoni yetu hayo, “takwimu hizo ni muhimu ili Watanzania, na hasa Wazanzibari, waweze kufahamu kama Zanzibar imekuja ikipata sehemu yake halali ya mapato ya Jamhuri ya Muungano yanayotokana na misaada na mikopo ya kibajeti.”

Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitoa ahadi kwa Bunge lako tukufu kwamba angeleta takwimu hizo. Hajafanya hivyo. Maelezo yake hayana takwimu zozote za mgawanyo wa mapato ya Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar za kipindi chochote. Katika mazingira haya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itasemehewa na wapenda haki wote kwa kuamini kwamba takwimu hizo zinafichwa kwa sababu zina ushahidi wa dhuluma kubwa ambayo Zanzibar na Wazanzibari wamefanyiwa na Serikali ya Tanganyika – ambayo ndiyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano – kwa miaka yote ya Muungano huu. Kama maneno yetu haya sio ya kweli basi Serikali hii ya CCM na ithubutu kuthibitisha uongo wetu kwa kutoa takwimu za mgawanyo wa mapato yote ya Muungano ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliahidi kuzileta Bungeni.

HISA ZA ZANZIBAR BODI YA SARAFU YA AFRIKA MASHARIKI

Mheshimiwa Spika,

Agizo lingine la Bunge lako tukufu ambalo limepuuzwa na Serikali hii ya CCM linahusu hisa za Zanzibar katika iliyokuwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (*East African Currency Board*) ambayo ilivunjwa mwaka 1966 pale nchi wanachama wake zilipoanzisha Benki Kuu zao. Kwa sababu ya masuala ya sarafu na fedha kufanywa mambo ya Muungano kufuatia Makubaliano ya Muungano, hisa za Zanzibar zilichukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, yaani Serikali ya Tanganyika iliyovaa joho la Tanzania.

Suala la fedha za Zanzibar katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki limekuwa mojawapo ya ‘kero’ sugu za Muungano kwa sababu Serikali ya Jamhuri ya Muungano, aka Serikali ya Tanganyika imekataa kuirudishia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar fedha zake halali. Visingizio vinavyotumiwa na Serikali hii ya CCM kukataa kurudisha fedha za Wazanzibari ni vingi na vimekuwa vinabadilika badiliya kutegemea mazingira na wakati.

Kwa mfano, mwezi Januari 2013, Mheshimiwa Waziri wa Nchi alitoa kauli ifuatayo mbele ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu suala hili: “*Katika Kikao cha Kamati ya Pamoja ya [Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania] na [Serikali ya Mapinduzi Zanzibar] ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika tarehe 14 Januari 2013 imeelezwa kwamba Mawaziri wa Fedha wa [Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania] na [Serikali ya Mapinduzi Zanzibar] wamepatiwa nyaraka madalum zenye taarifa za siri na wamekubaliana kujadili suala hili mwezi Februari, 2013 baada ya kuzipitia nyaraka hizo.*”

Hata hivyo, baada ya mwaka huo kumalizika bila ufumbuzi wa suala hilo, mwaka jana Mheshimiwa Waziri wa Nchi alikuja na maelezo hayo hayo kuhusu fedha hizo za Zanzibar. Kwa maneno yake mwenyewe, hisa za Zanzibar katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki ni mojawapo ya “*kero zilizobaki katika orodha ya mambo ya kutafutiwa ufumbuzi....*” Kwa sababu hiyo, “... masuala ya Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na mgawanyo wa faida ya Benki Kuu yapo katika ngazi ya Mawaziri wa Fedha wa (Serikali ya Jamhuri ya Muungano) na (Serikali ya Mapinduzi Zanzibar) kwa hatua za majadiliano.”

Mwaka huu Mheshimiwa Waziri wa Nchi amekuja na hadithi tofauti. Kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Kamati iliagiza kwamba “*Wajumbe wa Bunge la Katiba watumie fursa ya Bunge la Katiba kuzimaliza kero za hisa za Zanzibar zilizokuwa kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki....*” Majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi yanadhihirisha ubabaishaji mkubwa na ukwepaji hoja ambao umetumika kuendeleza dhuluma dhidi ya Zanzibar katika suala hili:

“*Bunge la Katiba limejadili Rasimu ya Katiba, na maeneo mengi yenye changamoto za Muungano yameibuliwa na kujadiliwa kwa lengo la kuzitatua na mengine kuondolewa kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Baadhi ya hoja zilizokuwepo ambazo zitapatiwa ufumbuzi kupitia Katiba Inayopendekezwa ni pamoja na suala la utafiti na*

uchimbaji wa mafuta na gesi asili, ambalo limeondolewa katika orodha ya mambo ya Muungano, ibara ya 74(3). Aidha, Katiba Inayopendekezwa imeimarisha utekelezaji wa masuala ya Muungano na utatuzi wa changamoto zake kwa kuunda Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Mambo ya Muungano (Sura ya Tisa). Ni matumaini yetu kuwa, kupitia Tume hiyo changamoto za Muungano zilizopo zitapatiwa ufumbuzi na maamuzi yatakayopatikana yatatambulika kikatiba."

Maneno haya yametoka katika sehemu ya Taarifa iliyoandikwa 'Utekelezaji', lakini Mheshimiwa Waziri wa Nchi hajasema neno hata moja kuhusu hisa za Zanzibar katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, ambalo ndio lilikuwa agizo la Bunge! Hata hivyo, kwingineko katika Taarifa yake, Waziri wa Nchi amerudia majibu yake ya mwaka jana na mwaka juzi kuhusu suala hili: "Miongoni mwa masuala yanayofuatiliwa ni pamoja na Hisa za [Serikali ya Mapinduzi Zanzibar] zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na mgawanyo wa faida ya Benki Kuu...."

Majibu ya aina hii yanathibitisha wazi kwamba Serikali hii ya CCM haina nia wala uwezo wa kutatua kero za Muungano ambazo zimeisibu Zanzibar tangu mwaka 1964. Kwa vile yenye ni zao la Muungano huu wa kinyonyaji, CCM haiwezi kutatua kero hizi za Muungano na ikabaki salama. Ndio maana waasisi wake waliobaki – kama akina Mzee Hassan Nassoro Moyo – ambao wametambua dhuluma za Muungano huu kwa Zanzibar na kudiriki kuzzungumzia hadharani wanafukuzwa uanachama badala hoja zao kusikilizwa kwa makini na kujibiwa.
KATIBA INAYOPENDEKEZWA NA KUISHI KWA MATUMAINI!!!!

Mheshimiwa Spika,

Baada ya Serikali hii ya CCM kushindwa kutatua 'ker za Muungano', sasa imepata kisingizio kingine cha kuwafanya Wazanibari waendelee kuishi kwa matumaini: Katiba Inayopendekezwa. Hivyo basi, kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, "... Katiba Inayopendekezwa imeimarisha utekelezaji wa masuala ya Muungano na utatuzi wa changamoto zake kwa kuunda Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Mambo ya Muungano.... Ni matumaini yetu kuwa, kupitia Tume hiyo changamoto za Muungano zilizopo zitapatiwa ufumbuzi na maamuzi yatakayopatikana yatatambulika kikatiba."

Kwingineko katika Taarifa hiyo tunakumbushwa kwamba matumaini hayo yamejengwa katika msingi wa mchanga: "Kupitia mchakato wa kuandika Katiba mpya, changamoto nyingi za Muungano zimejadiliwa na baadhi ya hoja zilizokuwepo zitapatiwa ufumbuzi kupitia Katiba Inayopendekezwa **baada ya kupitishwa**.... Vile vile, uanzishwaji wa Tume ya Usimamizi na Uratibu wa Mambo ya Muungano ... itajenga misingi imara ya kikatiba ya utekelezaji wa mambo ya Muungano na kuyapa nguvu ya kisheria maamuzi mbali mbali yatakayotolewa na Tume hii."

Mheshimiwa Spika,

Kwa wale wanaofikiria kwamba kuanzishwa kwa Tume ya Mambo ya Muungano - kama inavyopendekezwa na Katiba Inayopendekezwa – kutakuwa ni mwarobaini wa kero za Muungano, ni vyema wakatafakari historia ya zaidi ya miaka thelathini ya Tume nyingine ilioanzishwa na Mabadiliko ya Tano ya Katiba ya sasa, yaani Tume ya Pamoja ya Fedha. Tume hiyo ilipewa jukumu, *inter alia*, la "kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo ya Serikali hizo."

Baada ya kutamkwa na Katiba mwaka 1984, Tume ya Pamoja ya Fedha haikutungiwa ya kuitekeleza mpaka mwaka 1996; na baada ya hapo Tume yenyewe haikuteuliwa hadi mwaka 2003, karibu miaka ishirini baada ya kuundwa rasmi kikatiba. Na tangu kuteuliwa miaka kumi na mbili iliyopita, mapendekezo yake muhimu kuhusu mgawanyo wa fedha na mapato ya Muungano na uchangiaji wa gharama zake yamekuwa yakipuuza na Serikali hii ya CCM. Kwa mfano, mwezi Agosti, 2006, Tume hiyo ilianda Mapendekezo ya Tume Kuhusu Vigezo vya Kugawana Mapato na Kuchangia Gharama za Muungano. Kwa mujibu wa waraka huo wa Tume, "... mapato yanayotokana na vyanzo vya Muungano yanakidhi matumizi ya Muungano na kuwa na ziada ya kutosha. Takwimu zinaonyesha kuwa kiasi kidogo cha mapato hayo kimekuwa kinagharimia matumizi ya Muungano.

Aidha, uchambuzi wa Tume ya Pamoja ya Fedha ulionyesha kuwa "... kiasi kikubwa cha ziada ya mapato ya Muungano kimekuwa kinatumika kugharimia mambo yasiyo ya Muungano." Kwa sababu hizo, Tume ilipendekeza kwamba uwekwe utaratibu utakaowezesha kutenganisha mapato na matumizi ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Siku kama ya leo mwaka jana, miaka nane baada ya Tume kutoa mapendekezo yake, Mheshimiwa Waziri wa Nchi aliliambia Bunge lako tukufu kwamba "Serikali zetu mbili bado zinaendelea kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha."

Na kama inavyofahamika, hadi sasa Akaunti ya Pamoja ya Fedha "... ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili... kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa Mambo ya Muungano" haijafunguliwa, yapata miaka thelathini na moja baada ya kuamriwa hivyo na Katiba. Kutokana na kushindikana kufunguliwa huko, kwa miaka yote hii, bajeti ya Muungano imekuwa ndio bajeti ya Tanganyika, kinyume na maelekezo ya Katiba.

KURA YA MAONI HEWA!!!

Mheshimiwa Spika,

Kuna sababu nyininge zaidi ya historia ya Serikali hii ya CCM kushindwa kutatua kero za Muungano: hakuna uhakika wowote kwamba Katiba Inayopendekezwa itakuwa ndiyo Katiba Mpya ya Tanzania. Suala kubwa hapa ni je, kutakuwa na kura ya maoni kuhalalisha Katiba Inayopendekezwa? Kwa kauli za viongozi wote wa Serikali hii ya CCM, kuanzia Rais Jakaya Kikwete, Waziri Mkuu na Waziri wa Katiba na Sheria, jibu la swali hili ni ndio. Hata hivyo, viongozi hawa hawa ndio waliokuwa mstari wa mbele kuwaaminisha wananchi kwamba kura ya maoni ingefanyika tarehe 30 Aprili iliyopita, licha ya kila mwenye macho ya kuona na akili ya kufikiria kusema kwamba kura ya maoni kwa tarehe hiyo ilikuwa ni ndoto ya mchana!!!! Kwa sababu hiyo, kauli za viongozi hawa haziaminiki tena.

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, hata kama Tume ya Uchaguzi itakamilisha jukumu lake la kuandikisha wapiga kura nchi nzima, bado hakutakuwa na uhakika wa kufanyika kwa kura ya maoni kuhalalisha Katiba Inayopendekezwa. Tatizo la msingi hapa ni matakwa ya Sheria ya Kura ya Maoni, 2013. Sheria hiyo imeweka utaratibu mgumu wa uendeshaji wa kura ya maoni, ambapo kila hatua inayotakiwa kuchukuliwa haiwezekani kuahirishwa wala kuongezewa muda.

Kwa mfano, ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kupokea Katiba Inayopendekezwa, Rais anatakiwa – kwa Amri iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali na baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar – kuielekeza Tume ya Uchaguzi kuendesha kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa. Amri ya kura ya maoni inatakiwa kufanua kipindi cha kampeni na kipindi ambacho kura hiyo ya maoni inatakiwa kufanyika. Rais Kikwete alikwishatoa Amri kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Kura ya Maoni. Rais hana mamlaka yoyote, kwa mujibu wa

Sheria hii, wa kutengua Amri yake au kutoa Amri mpya ili kuwezesha kura ya maoni kufanyika kwa tarehe nyingine tofauti na tarehe iliyo tangazwa kwenye Amri ya kwanza.

Pili, ndani ya siku saba baada ya kuchapishwa kwa Katiba Inayopendekezwa, Tume inatakiwa kuandaa swalii la kura ya maoni na kulichapisha katika Gazeti la Serikali. Na ndani ya siku kumi na nne baada ya kuchapisha swalii hilo, Tume inatakiwa kutoa Taarifa ya kufanyika kwa kura ya maoni, itakayoeleza kipindi cha kuhamasisha na kuelimisha umma juu ya kura hiyo na siku ya kura ya maoni. Na kila msimamizi wa kura ya maoni anatakiwa, ndani ya siku ishirini na moja baada ya kuchapishwa kwa Taarifa ya Tume, kuwajulisha wananchi katika Jimbo lake la Uchaguzi kuhusu utaratibu wa kufanyika kwa kura ya maoni. Aidha, Tume inatakiwa kutoa elimu kwa umma juu ya Katiba Inayopendekezwa kwa muda wa siku sitini tangu Katiba Inayopendekezwa ilipochapishwa.

Tume ilikwishaandaa na kuchapisha swalii la kura ya maoni na ilikwishatoa Taarifa ya kura ya maoni na ratiba yake nzima. Tume haina mamlaka yoyote, kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni, ya kutengua Taarifa yake na kutoa Taarifa nyingine, au kuweka ratiba nyingine badala ya ratiba iliyokwishatolewa. Vile vile, Tume haiwezi kujiongezea muda wa kutoa elimu kwa umma juu ya Katiba Inayopendekezwa; au kujipa muda mwengine kwa vile muda uliowekwa na Sheria haukutumika ipasavyo. Kwa upande wao, wasimamizi wa kura ya maoni hawana mamlaka yoyote kisheria ya kuongeza au kuongezewa muda wa kutoa taarifa kwa umma chini ya kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika,

Tume ya Uchaguzi haina mamlaka yoyote kisheria kuongeza muda kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kuendesha elimu kwa umma juu ya Katiba Inayopendekezwa baada ya muda wa awali uliowekwa kwa ajili hiyo kupita. Kwa kifupi, Mheshimiwa Spika, hakuna uwezekano kisheria wa kurudia tena hatua zozote muhimu ambazo zilikwischachukuliwa kwa ajili ya kufanyika kwa kura ya maoni iliyokuwa imepangwa tarehe 30 Aprili, 2015. Hakuna uwezekano kisheria wa kuongeza muda kwa hatua zozote ambazo muda wake ulikwishapita.

Kwa sababu hizi, hakuna kufanyika kura ya maoni juu ya Katiba Inayopendekezwa kwa mujibu wa Sheria ya Kura ya Maoni kama ilivyo kwa sasa. Na hadi sasa, Serikali hii ya CCM haijaleta Muswada wowote wa marekebisho ya Sheria hiyo ili kuwezesha kufanyika kwa kura ya maoni siku za usoni. Kama ilivyo kuwa kwa ahadi ya kura ya maoni ya tarehe 30 Aprili, Serikali hii ya CCM inadanganya Watanzania kuwa kutakuwa na kura ya maoni wakati kila mwenye akili timamu anajua hilo haliwezekani bila kwanza kuwa na mazingira wezeshi ya kisheria. Inataka Watanzania, hasa Wazanzibari ambaa ndio wamekuwa victims wakubwa wa Muungano, waendelee kuishi kwa matumaini kwamba kero za Muungano zitatafutiwa dawa wakati hakuna dawa ya kero hizo bila mabadiliko ya muundo wa Muungano.

Mheshimiwa Spika,

Historia yote ya Muungano inathibitisha ukweli mmoja mkuu: 'kerou za Muungano' – hasa uchangiaji wa gharama na mgawanyo wa mapato yake - zinatokana na muundo wa Muungano. Bila kutatua tatizo la muundo, kero hizo hazitatatuliwa na hatimaye Muungano wenyewe utakufa. Kabla ya kutishwa na 'kuufyata' Dodoma wakati wa Bunge Maalum, Baraza la Wawakilishi Zanzibar lilitambua ukweli huu. Kama ilivyo iambia Tume ya Mabadiliko ya Katiba, "rasilmali za Muungano ziwe ni milki ya pande mbili za Muungano; na rasilmali hizo ndio zitumike katika uendeshaji wa Mamlaka za Muungano. Ugawaji wa rasilmali ufanywe kwa uwiyano maalum utakaokubaliwa kwa pamoja na pande mbili za Muungano."

HITIMISHO: MUUNGANO WA DHATI AU WA KIINI MACHO???

Mheshimiwa Spika,

Kwa yeote mwenye macho ya kuona na akili ya kufanya tafakuri juu ya Muungano, hawezi kukanusha maneno ya aliyejewa Spika wa Bunge lako tukufu, Mheshimiwa Pius Msekwa, kwamba 'Muungano huu ni kiini macho tu.' Kauli hiyo ilitolewa na Speaker Emeritus Msekwa katika mada yake Hali ya Muungano aliyoiwasilisha katika semina juu ya Miaka Thelathini ya Muungano iliyofanyika Tanga mwaka 1994.

Speaker Emeritus Msekwa alisema kwamba, chini ya Muungano huu, Zanzibar ilikabidhi sehemu muhimu ya mamlaka yake (mahusiano ya nchi za nje, ulinzi na usalama, uraia, kodi na ushuru wa forodha, sarafu, nguvu kuu za kuendeshea uchumi na mengineyo) kwa Tanganyika; na kisha Tanganyika ikajigeuza jina na kujita Jamhuri ya Muungano. Kwa maneno yake, "kwa jinsi mambo yalivyo sasa, Zanzibar inaonekana kama vile ni '**invited guest**' (mgeni mwalikwa) katika Muungano huu."

Ili kuthibitisha kwamba Speaker Emeritus Msekwa hakuwa anatunga hadithi za mambo yasiyokuwepo, mwaka huo huo, msomi mashuhuri wa Kiafrika, hayati Profesa Ali A. Mazrui aliandika katika gazeti *The Sunday Nation* la Kenya kwamba kwa sababu ya Muungano, Zanzibar imepoteza kila kitu chake muhimu, wakati Tanganyika imebadilika jina tu na kuwa Tanzania, huku ikiwa na mamlaka zaidi.

Mheshimiwa Spika,

Kauli za Speaker Emeritus Msekwa na Hayati Profesa Mazrui juu ya Muungano wetu zilikuwa za kweli mwaka 1994, na bado ni za kweli leo, yapata miaka ishirini na moja baadae. Muungano wetu umebakia ni wa jina tu. Ndio maana hata Baraza la Wawakilishi Zanzibar, katika maoni yake kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, lilitaka 'kuwa na Muungano wa dhati', yaani "... Muungano wa kweli, hata kama ni kwa maeneo machache, kwa dhati ya wanasiwa na Watanzania kwa ujumla."

Kwa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Muungano 'wa dhati' na 'wa kweli' ni ule ambao kuna "... Mamlaka ya Zanzibar huru na Mamlaka ya Tanganyika huru ndani ya Muungano, (na) Mamlaka ya Muungano iwekwe wazi – maeneo yake, uwezo au nguvu zake, na utendaji wake. Mambo yote hayo yawekwe wazi na mipaka yake." Kwa vile mambo haya hayapo kwa sasa, na hayajawahi kuwekwa wazi tangu mwaka 1964, ni wazi kwamba Muungano huu sio wa 'kweli' wala wa 'dhati' na, kwa maneno ya Speaker Emeritus Msekwa, ni kiini macho!

Mheshimiwa Spika,

Kwa kumalizia, tunaomba kurudia maneno tuliyoyasema katika Maoni yetu ya mwaka jana kuhusu mgawanyo wa fedha na mapato ya Muungano: "... [K]wa sababu ya Muungano huu, uhusiano kati ya Tanganyika na Zanzibar ni uhusiano wa kinyonyaji. Kwa sababu hiyo, huu ni uhusiano wa kikoloni. Ni uhusiano kati ya 'himaya' ya Tanganyika na 'koloni' lake la Zanzibar. Himaya za kikoloni huwa zinadhibiti masuala yote ya ulinzi na usalama, mambo ya nje na uhusiano wa kimataifa, uraia, kodi, fedha, sarafu na benki kuu ya makoloni yao. Na himaya za kikoloni huwa zinatumia nguvu na udhibiti wao wa masuala haya kuyanyonya makoloni yao kiuchumi, kuyadidimiza kijamii na kuyatawala kisasa. Hivi ndivyo ambavyo imekuwa kwa mahuasiano kati ya Tanganyika na Zanzibar tangu kuzaliwa kwa Muungano huu tarehe 26 Aprili, 1964."

Mheshimiwa Spika,

Kama kuna mwenye tafsiri tofauti na tafsiri hii ya takwimu za mgawanyo wa fedha na mapato ya Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar basi na aiweke hadharani tafsiri yake hiyo na kutukanusha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru sana kwa kuwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano).

Muda uliobaki ni mdogo sana kuweza kumwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Tutafanya shughuli hiyo jioni ya leo tutakaporudi.

Mwisho, naomba niwatambue Wageni wa Mheshimiwa Tundu Lissu, ambao wanatoka kule Singida, Jimbo la Singida Mashariki. Naomba msimame wote pale mlipo wale wageni wetu kutoka Singida! (Makofi)

Karibuni sana Bungeni. Naambiwa baadhi yenu mnatoka kule Matare, baadhi mnatoka Mahambe, niliwahi kulelewa kidogo kwenye maeneo hayo. Nawashukuruni sana wazee wangu. Ahsanteni sana na karibuni sana. (Makofi)

Baada ya maneno hayo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

(Saa 8.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Wabunge wana kawaida ya kulaumu kwamba Waheshimiwa Mawaziri hawapo, leo Mawaziri wapo, Wabunge ndiyo hawapo! (Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Mheshimiwa Mchungaji Natse, karibu sana kwa hotuba yako!

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE - MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kulihutubia Bunge pamoja na Watanzania kwa ujumla. Pili, ninaishukuru familia yangu kwa kunipa moyo na kunifanya niweze kazi hii ya Kibunge kwa ufanisi zaidi. Ninawashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Karatu, kwa kunipa ushirikiano mkubwa kwa kipindi chote cha miaka mitano hadi sasa na kwa imani waliyonayo kwangu kama mwakilishi wao. Ninatoa pia pongezi zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mboge, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ndani na nje ya Bunge, Watanzania wanaona tumaini kubwa kutoka Upinzani. Nitoe pia pongezi kwa viongozi wakuu wa vyama vinavyounda UKAWA; Wenyeviti na Makatibu Wakuu pamoja na Sekretarieti. Kazi yao nzuri imeendelea kufuta machozi ya Watanzania wakiwa na matumaini ya kuuondoa utawala wa kifisadi wa CCM ifikapo Oktoba 2015, kwani mbadala wake ambao wamekuwa wakiuomba kwa muda mrefu sasa umepatikana.

Katika llani ya CCM ya mwaka 2010, kifungu cha 34, kinachoainisha masuala ya wanyamapori na misitu, llani imeonesha umuhimu wa wanyamapori na misitu unazidi kuongezeka, siyo tu katika kuvutia watalii, pia katika kutunza mazingira. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010 - 2015), Serikali ya CCM ilisema kwenye llani yake kufanya yafuatayo; nitasoma machache tu:-

- (a) Kuendelea kuelekeza nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha na kuvuna maliasili ya Taifa kwa manufaa ya Taifa letu.
- (b) Kuzipa Serikali za Mitaa nguvu zaidi kuwawezesha wananchi kumiliki na kunufaika na rasilimali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la Majukumu ya Wizara (*Assignment of Ministerial Responsibilities Notice*) la mwezi Januari 2011, majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yameainishwa kama ifuatavyo:-

Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Hifadhi ya Mazingira; kufuatilia na kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, kutatua changamoto zinazohusiana na uharibifu wa mazingira ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali na maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma katika llani ya CCM juu ya uhifadhi wa mazingira nchini na ukasoma pia katika Mwongozo wa Kiwizara majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Raisi Mazingira, utaona kama upo mkakati wa kuhakikisha suala la kimazingira nchini linafanyiwa kazi kwa kuzingatia taaluma na weledi, kuhakikisha nchi inakuwa salama katika utunzaji wa mazingira na kuwawezesha uchumi kukua, ikizingatiwa kuwa yapo mahusiano kati ya mazingira na uchumi, mazingira na umaskini, lakini kiuhalisia utekelezaji wake umefanya kwa kiwango kidogo mno.

Mheshimiwa Naibu spika, katika taarifa ya Wizara mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, imeonesha udhaifu katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2014/2015. Kimsingi, matokeo ya udhaifu yameonekana zaidi katika athari za kimazingira ambazo zimeendelea kutokea nchini, lakini pia suala la fedha za maendeleo katika uhifadhi wa mazingira bado haijawa kipaumbele kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi na hili linajithibitisha kwa viwango ambavyo vinatengwa kwa miradi ya maendeleo. Katika jumla ya shilingi bilioni 61.1 ambazo Bunge liliidhinisha ni kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 7.5 tu ambazo zilitengwa kwa miradi ya maendeleo katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopokelewa na Wizara kuanzia tarehe 1 Julai, 2014 hadi 31 Machi 2015 ilikuwa ni jumla ya shilingi bilioni 36.3. Fedha ambazo ni takribani nusu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka mzima. Huu ndiyo umekuwa utamaduni wa Serikali hii ya CCM kudharau maagizo ya Bunge katika bajeti na kuonesha kutokuwajibika katika utekelezaji wa Bajeti kila mwaka. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshauri kwa takribani sasa miaka mitano mfululizo juu ya nidhamu ya bajeti kwa Serikali bila mafanikio yoyote.

Kazi yetu kama UKAWA ni kusema ukweli. Mwalimu Nyerere katika Kitabu chake cha TUJSAHIHISHE anasema "... ukweli una tabia moja nzuri sana, haujali mkubwa wala mdogo, haujali adui wala rafiki, kwake watu wote ni sawa. Pia ukweli una tabia ya kujilipiza kisasi kama ukipuuzwa." Mwisho wa kunukuu. Hivyo basi, jukumu letu ni kusema kweli, pia kuwafahamisha Watanzania iliyosababu na kwa kuwa Mwalimu anasema ukweli haupendi kupuuzwa puuzwa hata Watanzania hawapendi kupuuzwa na Serikali yao. Sasa ni wakati mwafaka kwa Watanzania kufanya uamuzi sahihi kwa maslahi ya Taifa letu ifikapo Oktoba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya miradi ya maendeleo peke yake iliyoidhinishwa na Bunge ambayo imeainishwa katika kitabu cha Waziri cha taarifa yake kwa Kamati ya Bunge juu ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya ya mwaka 2015/2016, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa jumla ya shilingi bilioni 6.5 na fedha zilizokwishatolewa kwa Wizara hadi kufikia mwezi Machi 2015 ni jumla ya shilingi bilioni 2.2, sawa na asilimia 33 ya bajeti nzima. Tafsiri ndogo ni kwamba, hadi kufikia mwezi Machi ni asilimia 33 tu ya fedha za miradi ya maendeleo zilikuwa zimetolewa katika Ofisi ya Rais. Tumejenga

utamaduni huo wa kutotekeleza bajeti na mipango yetu kama Taifa na utamaduni huu umeasisiwa na Chama cha Mapinduzi kwa kuwa na ahadi zisizotekelezeka, pia kujenga utamaduni wa kuwalaghai wananchi kwa lugha tamu zisizoweza kutekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utamaduni huu wa kutotekeleza ahadi na mipango ya Serikali pasipo kuchukua hatua za kurekebisha, Taifa hili litaendelea kuwa maskini milele. Mwandishi na Mchambazi wa Siasa na Profesa wa Uchumi, Ndugu Bryan Caplan wa Chuo Kikuu cha George Mason anasema; "Wanasiasa wengi hawatekelezi ahadi kwa kuwa hakuna adhabu zinazochukuliwa kwa kushindwa kwao kutekeleza ahadi, lakini pia huwa hawaoni haja ya kutekeleza baada ya kushinda uchaguzi.

Kimsingi, anatoa suluhu kwa wapiga kura kuchukua hatua za kuwawajibisha viongozi wa aina hii." Kwa mujibu wa Katiba yetu hakuna mahali ambapo wananchi wanayo haki ya kuwawajibisha viongozi au kiongozi ambaye hatimizi wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri Serikali katika masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Tanzania ni moja ya nchi ambayo tunashuhudia matokeo ya mabadiliko ya tabianchi hususan uwepo wa ukame wa muda mrefu unaojirudia rudia unaombatana na athari kubwa katika kilimo, usafirishaji, nishati, biashara na sekta mbalimbali za uchumi kwa jamii. Hivi karibuni tumeona athari za mafuriko katika nchi yetu ambapo wananchi wamepoteza maisha, baadhi ya maeneo wananchi wamekosa maji kwa matumizi ya kila siku kutokana na ukame na mambo ya kimazingira yenye kuhitaji majibu ya kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wananchi wakipoteza maisha katika maafa ya kimafuriko ambayo ni athari za kimazingira, bado Serikali ipo usingizini kwa kutokuwa na majibu ya kuliona tatizo hilo na kuchukua hatua mahususi za kunusuru roho za Watanzania wanaopoteza maisha siku hadi siku kutokana na mafuriko. Na ni furaha ya Serikali hii ya CCM kutenga bajeti kila mwaka za maafa na kuwadhulumu waathirika wa maafa yatokeapo bila kuwa na suluhisho ambalo ni la kudumu kwa kupunguza au kuondoa kabisa athari za majanga ya aina hii kutokea nchini. Wakati yaitokea majanga, kilimo katika maeneo husika kinadorora au kusimama kabisa, mifugo mingi na wanyama wa porini wanakufa kwa kukosa chakula na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo usemi usemao; "*The devil lies in the details*"; yaani mzimu upo katika maandishi. Ukitoma katika majibu ya Serikali kwa Kamati ya Bunge, Serikali inasema, Kampuni ya Dar Rapid Transport (DART), ilipewa hati ya mazingira tarehe 30 Juni, 2009 yenye Namba ya Usajili EC/EIS/146 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi yaendayo kwa kasi eneo la Jangwani." Serikali imeendelea tena kusema tena, DART imetekeleza masharti mengi iliypewa ikiwemo kufanya ujenzi katika maeneo yanayoruhusiwa tu, kupanua miundombinu, kuruhusu maji ya mvua kupita kwa kasi. Hoja hapa ni je, hali iliyojitekeza hivi karibuni hadi kupelekea kufungwa kwa barabara ya Jangwani ndiyo utekelezaji wa masharti ya Kampuni ya DART kutoka kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira? Serikali iwaambie Watanzania ukweli juu ya athari hizi za uzembe wa kuwepo kwa Miradi iliyotanguliza masilahi ya watu binafsi na siyo Watanzania ambao wanaambulia kupoteza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya Serikali inayojitaa siku ni haya yanayotokea sasa. Kwa asili tulizoea watu kuhama au kuwa wakimbizi kutokana na mapigano ya vita, lakini sasa wahamiaji wengi wanatokana na mabadiliko ya tabianchi na kwa lugha iliyozeoleka ni wakimbizi wa kimazingira (*environmental refugees*). Kimsingi, hili limekuwa tatizo sana kwani kutokana na watu kuhama maeneo yao ya asili kwa ajili ya ukweli kwamba maeneo hayo hayawezi kuwawezesha kuishi kwao na hivyo inawalazimu kuhamia maeneo mengine ili

kuendelea na maisha yao; jambo ambalo limetokea sana hasa kwa wafugaji na wakulima na athari yake kubwa sasa ni mauaji kati ya wakulima na wafugaji.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeishauri Serikali hii ya CCM kwa muda mrefu sasa. Kwa umri huu inatosha kusema CCM sasa imekuwa mtu mzima kama siyo mzee. Waswahili wanasema, mbwa mzee hafunzwi adabu. Kimsingi, Watanzania wameona kilichoitwa udhaifu wa viongozi wa sasa, udhaifu wa CCM na uzembe wa Bunge katika kuisimamia Serikali. Ikiwa leo ni mwaka wa mwisho wa Serikali hii ya CCM, tutakuwa tukimpigia mbuzi gitaa au kumfunza mbwa mzee adabu. Nitoe wito kwa Watanzania, sasa tukatae vifo vya wananchi maskini katika mafuriko, kwani hakuna hata kiongozi mmoja aliyekufa katika mafuriko zaidi ya watu maskini tu. (Makof)

NAIBU SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Mchungaji subiri kidogo.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kupata ufanuzi kuhusu utaratibu, Kanuni ya 64(f) na (g) ya kwamba Mbunge hatasema vibaya ama kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwininge ye yote, ama hatatumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhesimu sana Mchungaji ni Mtumishi wa Mungu, anapaswa kuishi katika kuonyesha mifano iliyo sahihi. Ni kweli usemi huu unaweza kuwa upo na unaweza kuwa haupo kwamba mbwa mzee hafunzwi adabu, lakini qualification ya usemi huu inakwenda kuwataja viongozi wa chama na viongozi wa Serikali sasa wanafananishwa na mbwa mzee anayetakiwa kufunzwa adabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni udhalilishaji, kwa Kiongozi kama Mchungaji na naomba Watanzania watusiki vizuri; kwa Kiongozi tena Mtumishi wa Mungu, kuwanafananisha binadamu wenzake na mbwa, hii haiwezi kukubalika!

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo na usemi huo, angeutumia kwa namna inavyotakiwa usemi utumike sawa, lakini ku-*qualify* usemi huo kwa kuwaita viongozi wanafananishwa na mbwa mzee ambaye hafundishiki adabu; huu ni upeo wa udhalilishaji na hatutaweza kuukubali.

Naomba mwongozo wako; kwa nini Mchungaji Natse asiondoe maneno haya, yasiwemo katika Taarifa yake na yasiwemo kwenye Hansard ya Bunge? Ni udhalilishaji mkubwa, ninaomba Mwongozo katika jambo hili. (Makof)

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE - MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, niseme Chief Whip asiwe na pressure, huu ni usemi ambaao tafsiri yake ni nzuri haina shida. Naendelea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji, kwa kweli hotuba yako imejaa na siyo hilo tu lililosemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini maneno mengine mengi tangu mwanzo nimefanya kuvumilia tu hapa, ni vizuri sana tukawa na hotuba ambazo zinajenga, zinaelimisha, zinaelekeza, zinasimamia Serikali, kuliko hotuba ambazo zina maneno yasiyochujwa. Napata taabu zaidi unapoyasoma wewe mwenyewe Mchungaji ni mtu mwenye heshima kubwa. Kwa hiyo, naomba uendelee lakini hebu uwe mwangalifu kidogo, yale maneno mengine mengine yale hebu jaribu kuweka maneno ambayo yanakubalika zaidi. (Makof)

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam ni moja ya Majiji machafu katika nchi za Afrika Mashariki. Miundombunu ya maji taka imekuwa mibovu katika maeneo mengi ya Jiji na hivyo kusababisha harufu mbaya katika Jiji, ambayo ni hatari kwa afya ya binadamu. Pili, kusababisha maji kushindwa kusafiri wakati wa mvua na kusababisha mafuriko ambayo yamekuwa yakileta maafa katika Jiji hususan maeneo ya mabondeni. Wakati wananchi wakipata matatizo haya ya mafuriko katika maeneo mengi, Serikali bado imeshindwa kutoa misaada ya haraka kwa wahanga ikiwa ni wajibu wa Serikali kuwasaidia wananchi wakipata matatizo yanapotokea haya nchini. Bado madhara haya yaktokea wananchi wameendelea kupata adha ya uchafu katika maeneo yao pamoja na kusababisha magonjwa ya mlipuko, lakini Serikali ya CCM inaona ni pafyumu katika Jiji na kubaki bila kuchukua hatua stahiki.

Kambi Rasmii ya Upinzani Bungeni, inawataka Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, sasa siyo wakati wa kuomba ombo msaada kwa Serikali kwani takribani mfululizo wa miaka kumi sasa ya Utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne, mambo haya yameshindikana kupatiwa suluhu ndani ya Serikali yake. Hivyo ni ukweli kwamba, mazingira bora ya kiafya katika Jiji la Dar es Salaam yatapatikana kwa kuwa na Serikali inayowajibika kwa wananchi na kutambua kero za wananchi waliowaweka madarakani; na hapa jibu ni UKAWA ifikapo 25 Oktoba 2015. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge hili mara kadhaa tumeoji juu ya ujenzi holela na ni ukweli kwamba miradi yote nchini kabla ya kuanza utekelezaji wake ni lazima kwanza ufanyiwe tathmini (*Environmental Impact Assessment*) na kupata cheti cha kuuwezesha uendelee kama ulivyopangwa. Cha kushangaza, miradi ambayo inamiliikiwa na Serikali imekuwa haipati cheti cha thamani na hivyo imekuwa ikileta usumbu mkubwa sana kwa wananchi au watumiaji na hivyo kuwa kero kwa Serikali yenyewe na kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nadharia hiyo, hivi karibuni katika Jiji la Dar es Salaam yalipotokea mafuriko barabara ya jangwani ya mabasi yaendayo kasi, ilijaa maji na kufungwa. Ukweli ni kwamba, Ofisi ya Kampuni inayojenga miundombinu ya mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam (*Strabag*) ilipewa Hati na Serikali ya kumiliki eneo hilo la Jangwani na hivyo tayari wamejenga Ofisi zao za Kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kuhoji utolewaji wa hati kwa Kampuni hiyo, tunahoji Je, tathmini ya mazingira ilifanyika? Kama ilifanyika, matokeo ya sasa hata kama tathmini hiyo ilifanyika ni kwa vipi au upo mkakati gani wa kuondoa kero zinazojitokeza sasa kwa wananchi? Kitendo cha kujenga hapo ni kurudisha maji katika maeneo jirani na kuzidisha maafa. Aidha, kama Kampuni hiyo imepewa hati miliki, ni kwanini waliokuwa wamejenga katika eneo hilo walihamishwa na kupelekwa nje ya mji? Yote haya yalihojiwa na Serikali hii ya CCM imetoe majibu mepesi na kujisifu kuwa Serikali siku ilhali ikiendelea kufurahia mafuriko na maafa ya wananchi masikini?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usafi wa mazingira na kudhibiti utupaji taka ovyo pamoja na Halmashauri kusimamia suala la usafi, ni jukumu la Wakurugenzi wa Halmashauri zinazohusika. Utupaji wa taka ovyo umekuwa kikazwo. Mkurugenzi wa Halmashauri ndio mwenye wajibu wa kuhakikisha Halmashauri yake inakuwa safi. Kwa bahati mbaya sana suala la usafi limekuwa likifanywa kama kete ya kisiasa na Wakurugenzi kutumika kufanya siasa za Vyama. Katika Halmashauri kadhaa nchini wananchi wameanza kuchangishwa fedha kwa ajili ya Ushuru wa Taka kwa maamuzi ya Halmashauri na Mkurugenzi ili kugombanisha wananchi na Vyama vyia Siasa vyenye mamlaka katika maeneo husika.

Kwa mfano, katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, kwa kuwa CHADEMA ilishinda Kiti cha Udiwani mwaka 2014 Februari; kabla ya hapo suala la usafi katika Kata ya Njombe ilikuwa chini ya Mkurugenzi, mara tu baada ya ushindi wa CHADEMA suala hilo limekuwa likikwepwa na Mkurugenzi na kutupiwa mzigo kwa Diwani wa Kata ya Njombe Mjini, suala ambalo limeufanya Mji wa Njombe kuwa mchafu, tukijua ni Mji wa Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muhimili Mkuu wa wa Bunge na Jimbo lake kuendelea kuwa chafu. Lakini pia hali inaendelea...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa tuvumiliane kidogo. Unaweza ukakaa kwenye kiti kwa dakika chache, dakika zako ninazitunza. Mheshimiwa Waziri nimekuona!

MWONGOZO WA SPIKA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwa heshima niliyonayo kwa Mchungaji, ni bora angelelewa utaratibu wa kikanuni na angeheshimu matakwa ya kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi tena kwenye kanuni ile ile ya 64; Kanuni hii inakataza Mbunge kuzungumzia mienendo na shughuli za Viongozi wetu Wakuu akiwemo Spika. Sasa anapokuja kuoanisha suala hili la uchafu katika Mji wa Njombe, akimuingiza na Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwa sababu kumwingiza Spika ni kumzungumza Spika kama Kiongozi wa Taasisi kubwa na mwenendo wake wa kishughuli kama Kiongozi na afadhali angeishia kwa kumtaja jina kama Mbunge wa Jimbo la Njombe na siyo Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni uvunjaji wa kanuni. Kama alikuwa anamtaka Mbunge wa Njombe, angamtaja Mbunge wa Njombe, lakini anapomtaja Spika, hazungumzii tena Ubunge wa Mbunge wa Njombe, anazungumzia Taasisi hii ya Bunge. Mheshimiwa Spika ni Kiongozi Mkubwa kwenye taasisi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwombe Mheshimiwa Mchungaji Natse, hebu kwa heshima aliyopewa ya Uchungaji, Kiongozi Mkubwa wa Dini aone kuna umuhimu wa kuheshimu Kanuni na kuheshimu viongozi. Narudia kusema, sina tatizo kama angetumia mfano huo akintaja Mbunge wa Jimbo na siyo Kiongozi wa Bunge. Ukiphasema "Spika," unazungumza na Kiongozi wa Taasisi kubwa. Taasisi hii ya Bunge ni Taasisi kubwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. Mchunganji huyu maneno haya ya kichochezi aachane nayo, ama ayafute ama uamuru *Hansard* yako haya maneno ya kudhalilisha viongozi wetu yaondoke katika speech hii. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mbunge wa Muhamwe!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nilikuwa nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwa sababu na sisi Kanuni tunazo. Uzuri ame-sight kanuni ambayo ni sahihi kabisa kwamba hurusiwi kuzungumza mwénendo binafsi wa mtu; lakini mtu kama ni Mbunge na Kanuni hii inasema, isipokuwa kama kumetolewa hoja mahususi kuhusu jambo hilo.

Sasa hapa sisi tunazungumza mambo ya mazingira; sasa Spika kuwa Spika haituzui sisi kuzungumza au Mzungumzaji wa Kambi yetu kuzungumza mambo ya Njombe yanayohusu mazingira. Kanuni haijakataza hilo jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa angekuwa anazungumza mambo binafsi, Spika amekwenda Disco, Spika sijui anafanya nini; hayo ndiyo mambo binafsi. Lakini kuzungumzia mazingira, namna gani Diwani wa Kata fulani ametupiwa mzigo, kanuni iko wazi. Sasa nashindwa kuelewa ni mwenendo gani ambao anauzungumza hapa.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther nilisikia taarifa!

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasi vilevile tunajua kanuni. Msemaji aliyejita alikuwa anataka kupotosha taarifa ambayo ameitoa Mheshimiwa Jenista kuhusiana na matumizi ya neno "Spika." Unapozungumzia mwenendo wa mtu binafsi, haihusiani na hoja ambayo ameitoa Mheshimiwa Natse. Ndiyo maana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Uratibu na Bunge), alichosema, hana shaka kama angetumia kumhusisha kwa position yake kama Mbunge wa Jimbo, kwa sababu speech hii haina connection na utendaji kazi wake kama Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndiyo hoja ambayo ameitoa Mheshimiwa Jenista. (Makofij)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mkosamali anataka kupotosha. Mwenendo binafsi, ni wa mambo yetu ya nje huko na kutumia hiyo nafasi vibaya kama ambavyo imetumika hapa. Amesema wazi hana shaka na kuzungumzia kama Mbunge wa Jimbo, tatizo letu sisi kutumia nafasi yake ya Spika kuihusisha na taarifa ambazo yeeye hazimhusu. Ahsante. (Makofij)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana nakushukuru sana. Mchungaji Natse ni nafasi yako kurekebisha na nikuombee amani. Nataka arekebishe kwanza halafu nitoe maamuzi yangu.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hata dada yangu Mheshimiwa Jenista ananiita Mchungaji wala haniiti Mbunge wa Karatu, ni vizuri. Kwa hiyo, hili ambalo tunalizungumza la Spika na Mbunge wa Njombe, sina shida nalo. Naomba aelewe ni kama Mbunge wa Njombe.

NAIBU SPIKA: Nakuomba utoe tu hayo maneno ili usonge mbele kwa amani.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Naam!

NAIBU SPIKA: Yatoe tu hayo maneno ya Spika na nini...

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Nimesema Mbunge wa Njombe.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima kama Viongozi tuonyeshe utii katika Kanuni na katika taratibu za uendeshaji wa Shughuli za Bunge. Mara ya kwanza tumeomba mwongozo, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amefanya ujanja hajataka kutamka hapa kuondoa neno la kwanza. Kama anakubaliiana na hoja hii, aseme hapa na Hansard i-record Watanzania wasikie kwamba anaondoa maneno hayo yaliyopo hapo na harahusiwi kuyaweka maneno mengine kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mchungaji Natse, Mheshimiwa Mbunge, mwasilishaji wa hotuba hii ya Kambi ya Upinzani aondoe maneno yafuatayo:-

"Kata ya Njombe Mjini suala ambalo limeufanya Mji wa Njombe kuwa mchafu, tena Mji wa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mkuu wa Muhimili wa Bunge." maneno hayo yaondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno hayo yaondoke kwa sababu Kanuni iko wazi kabisa. Hapa unapomzungumzia kama anavyosema Mheshimiwa Mkosamali; Mheshimiwa Mkosamali anataka kulipotosha Bunge na Watanzania. Hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, ni mwenendo; siyo mwenendo binafsi, ni mwenendo wa Mbunge, Jaji au mtu mwingine yeьте anayeshughulikia utoaji wa haki, isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahususi kuhusu jambo husika. Sasa jambo husika hapa linahusiana nini na uchafu wa Spika wa Bunge la Jamhuri Muungano wa Tanzania.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Natse, nilikuomba katika taratibu za kibunge kiti kinapokuomba urekebishe jambo ili uweze kusonga mbele, sidhani kama ni jambo kubwa kiasi hicho. Mkikumbuka Waheshimiwa Wabunge nikwamba leo muda hauko upande wetu kabisa. Kwa hiyo, tunakuwa tunauchezza muda amba ni muhimu kweli kwa jambo ambalo kwa kweli mimi sioni kama ni la kuvutana sana. Kiti kinakushauri ufute yale maneno usonge mbele kwa nia njema.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Sawa. Nimeondoa maneno kama olivyosema Chief Whip, yaani Spika wa Jamhuri ya Muungano, Mkuu wa Muhimili nimefuta. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Gazeti la Mwananchi la Augosti 16, 2013, lilinukuu habari Serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko yote ya plastiki ili kutokomeza kuenea kwa taka zinazotokana na mifuko hiyo kwenye mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tamko hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa wakati ule Dkt. Terezya Huvisa, alisema ametoa muda wa miezi mitano kuanzia mwezi huo Agosti hadi Januari mwaka 2014 na ikifika Februari, mosi wataanza msako rasmi kwa watakaoendelea kuuza aina hiyo ya mifuko. Wakati Serikali ikichukua uamuzi huo, bado iliendelea kuruhusu uwepo wa aina hiyo ya mifuko katika soko ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukithiri kwa uchafuzi wa mazingira, unaosababishwa na mifuko hii laini ya plastiki na Serikali kushindwa hadi sasa kulishughulikia suala hili zaidi ya kufanya sanaa ya kudai hatua zinachukuliwa; huu ni ushahidi tosha kuwa Serikali ya CCM imechoka, ni Serikali ambayo haiwezi kusimamia matamko yake yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya utekelezaji wa mipango na bajeti kwa mwaka 2014/2015 ilionyesha maagizo ya Kamati ya Bunge na utekelezaji wake, moja ya maagizo ni kutekeleza agizo la kusimamia kanuni ya kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki mapema iwezekanavyo ili kuondoa tatizo sugu la uchafuzi wa mazingira ambalo linaitia nchi aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma katika majibu ya Serikali, inasema bado inaendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya umuhimu wa kutumia mifuko mbadala ambapo kanuni zimekuwepo tangu mwaka 2006 hadi sasa. Ni takribani miaka kumi, hakuna utekelezaji wowote wa kuzuia utengenezwaji na uuzwaji wa aina ya mifuko hii ya plastiki. Huu ni ushuhuda mwingine wa kuchoka kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijifunze kutoka Rwanda Mji wa Kigali, hakuna kuingia na mfuko wa plastiki. Ukifika uwanja wa ndege wa Kigali, unaacha aina yote ya mifuko ya plastiki ndipo unaruhusiwa kuingia katika mji huo. Kama inawezekana Rwanda, kwa nini kwetu tushindwe? Ndiyo maana tunadharauliwa na wenzetu kwa kushindwa kufanya mambo madogo madogo kwa manufaa ya nchi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Nyumba katika kingo za mito na fukwe za bahari. Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika mchango wake wa Hotuba ya Waziri Mkuu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi, alizungumza juu ya *master plan* ya Jiji la Dar es Salaam. Msingi wa hoja yake ni pamoja na kuwepo kwa athari za kimazingira.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Naomba mlinde muda wangu...

Pale mji unapokuwa na majengo yaliyojegwa kiholelea bila kuzingatia mipango na kuona athari zinazoweza kujitokeza, kama Bunge na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tumekuwa tukishauri utoaji wa vibali vya ujenzi katika maeneo ya kingo za mito na fukwe za bahari kuwa siyo vyema kwa mazingira. Ukituwa Taarifa ya Wizara kwa Kamati juu ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na maagizo ya Kamati, Serikali inasema; imeshindwa kubomoa nyumba Na.2019/2020 iliyopo Kawe kutokana na pingamizi liliopo Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa siyo kuingilia uhuru wa Mahakama, siku zote tunasema Serikali ya CCM ni dhaifu na ukweli huu hauwezi kufutwa tu kwa kusema siyo dhaifu au kwa kusema hii ni siasa. Ukweli huu utabaki kuwa ukweli kwanza, nyumba hii imepewa Namba na Serikali kwa kutambua kuwa ni nyumba halali; pili Serikali hii ya CCM ndiyo iliyotoa kibali cha Ujenzi wa nyumba hii; tatu Serikali hii ya CCM ndiyo ilipima viwanja eneo hilo la Nyumba na kuvitoa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujisahihishe Watanzania. Mwalimu aliwahi kusema maneno haya, "hatulazimiki kuendelea na uongozi huu mbovu wa Chama na Serikali" kwa wakati huo tukiwa ndani ya mfumo wa Chama kimoja, alitaka kufanyike mabadiliko ya Uongozi wa Chama na Serikali. Mpaka leo, Chama ni hicho hicho hakijabadilika kimfumo wala kiuongozi. Sasa ni wakati wetu wa kuamua kutoendelea na Uongozi huu mbovu wa Chama na Serikali yake. Yale ambayo tumekuwa tukishauri, sasa tukayafanyie kazi wenyewe kwa maslahi ya Taifa letu na UKAWA ndiyo Tumaini letu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika moja ya maagizo ya Kamati ya Bunge kwa Serikali kwa hoja ya Serikali kuwezesha kifedha Idara ya Mazingira na Baraza la NEMC, hapa bajeti haitoshi. Serikali itenye fungu maalum la pekee kwa ajili ya Idara ya Mazingira na hiyo ijulikane wazi kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya matumizi katika Fungu 31 hujumuisha mgao wa kibajeti wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Katika majibu ya Serikali inasema, hili lipo kwenye mchakato na kuendelea kufanya ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchimbaji wa Madini endelevu ni muhimu ili kulinda mazingira na maendeleo endelevu. Ni muhimu kutambua na kutumia njia bora za utunzaji wa mazingira katika uchimbaji madini. Sekta ya Madini inachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi. Shughuli za uchimbaji madini husababisha uharibifu wa mazingira. Baraza la Taifa la Usimamizi wa mazingira lipewe mamlaka ya kusimamia na meno katika kufanya maamuzi mazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uchafuzi wa mazingira katika migodi mbalimbali nchini kwa kutupa taka hovyo, kusambaza kemikali ambazo ni sumu kwa uhai wa viumbi hai na binadamu pale inaposambazwa katika vyanzo vya maji na ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri katika migodi ya Nyamongo, Bulyankulu, Geita Gold Mine na mingine kwa kutaja. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kuwataka wananchi wanaoishi pembezoni mwa migodi hiyo ambao wamepata madhara kutokana na

uchafuzi wa mazingira, waone ni kipindi chao cha mpito kwani hali hiyo itakoma mara tu baada ya utawala huu kukoma mwezi Oktoba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme juu ya misitu, mali na mazao ya misitu; mbao na mkaa. Siyo vizuri Serikali ikaacha holela tu mazao ya misitu kama ambavyo iko sasa, badala yake Serikali iendelee kurasimisha mazao ya misitu na mkaa ili kuweza kupata mapato. Maana mkaa utaendelea kutumika kwa biashara ya wakubwa, mazao ya misitu kukatwa na Serikali kuendelea kukosa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba hatuna chanzo mbadala kwa Watanzania.

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Natse.

**MSEMAJI MKUU KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)
(MHE. MCH. ISRAEL Y.NATSE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yangu yote iwekwe kwenye Hansard. Ahsante sana.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA
UPINZANI BUNGENI MHE MCH ISRAEL YOHANA NATSE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO
YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS
MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA
2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99 (9), ya Kanuni za Kudumu
za Bunge Toleo la Mwaka 2013)

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kulihutubia Bunge pamoja na watanzania kwa ujumla.

Pili ninaishukuru Familia yangu kwa kunipa moyo na kunifanya niifanye kazi yangu ya Kibunge kwa ufanisi zaidi, Niwashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Karatu kwa kunipa ushirikiano mkubwa kwa kipindi chote cha miaka mitano hadi sasa.

Pia ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mh Freeman A Mboge kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya ndani na nje ya Bunge, watanzania wanaona tumaini kubwa kutoka kwa upinzani, pia natoa pongezi kwa Viongozi wakuu wa vyama vinavyounda UKAWA, Wenyeviti na Makatibu Wakuu pamoja na sekretarieti ya UKAWA, Kazi yao nzuri imeendelea kufuta machozi kwa watanzania wakiwa na matumaini ya kuuondoa utawala wa kifisadi wa CCM ifikapo October, 2015 kwani mbadala wake ambao wamekuwa wakiomba kwa muda mrefu sasa umepatikana.

Mheshimiwa Spika, Katika llani ya CCM ya Mwaka 2010 kifungu cha 34 kinachoainisha maswala ya Wanyamapori na Misitu, llani imeonesha Umuhimu wa wanyamapori na misitu unazidi kuongezeka siyo tu katika kuvutia watalii, bali pia katika kutunza mazingira. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010–2015), Serikali ya CCM itachukua hatua zifuatazo:-

- (a) Kuendelea kuelekeza nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha na kuvuna maliasili kwa manufaa ya Taifa letu,
- (b) Kuzipa serikali za mitaa nguvu zaidi na kuwawezesha wananchi kumiliki na kunufaika na maliasili,
- (c) Kuongeza msukumo katika kuendeleza ufgaji wa nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta kibiashara,
- (d) Kuvutia wawekezaji katika kuanzisha viwanda vya kusindika asali na nta,
- (e) Kuhimiza mijji ianzishe bustani za ufgaji wa wanyamapori (zoos) kwa maonyesho,
- (f) Kuweka utaratibu shirikishi wa upandaji wa miti, uvunaji na udhibiti wa moto. Ushirikishaji huo utakuwa wa sekta binafsi, NGOs na vijiji.

Mheshimiwa Spika, Uharibifu wa mazingira ni tishio kwa maendeleo ya Taifa. Matumizi endelevu ya mazingira ni muhimu kwa maslahi ya kizazi cha sasa na kijacho, llani yao imeendelea kusema kuwa, ili kuendeleza hifadhi ya mazingira, Serikali ya CCM itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kusimamia na kuendeleza mpango wa hifadhi ya mazingira katika maeneo ya ardhi, bahari na ukanda wa pwani.
- (b) Kuendeleza kazi ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi, ili kuimarisha utunzaji na hifadhi ya mazingira katika maeneo yao.
- (c) Kuendeleza kazi ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya makazi, viwanda na mahoteli.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la Majukumu ya Wizara (Assignment of Ministerial Responsibilities Notice), la mwezi Januari, Mwaka 2011, majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yameainishwa kama ifuatavyo:- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Hifadhi ya Mazingira, Kufuatilia na kuratibu Shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (National Environment Management Council-NEMC). Aidha, kutatua changamoto zinazohusiana na uharibifu wa Mazingira ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali na maliasili.

Mheshimiwa Spika, ukisoma katika llani ya CCM juu ya uhifadhi wa mazingira nchini na ukasoma pia katika mwongozo wa kiwizara katika majukumu ya ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira utaona kama upo mkakati wa kuhakikisha swala la kimazingira nchini linafanyiwa kazi kwa kuzingatia taaluma na weledi kuhakiki nchi inakuwa salama katika utunzaji wa mazingira na kuweza kuwawezesha uchumi kukua ikizingatiwa kuwa yapo mahusiano kati ya mazingira na uchumi, mazingira na umaskini, lakini kiuhalisia utekelezaji wake umefanyika kwa kiwango kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, Swala la uharibifu wa mazingira katika nchi zinazoendelea ni kati ya sababu zinazofanya nchi hizo ziendelee kuwa maskini, UPO uhusiano mkubwa kati ya mazingira na umaskini kwa maana kwamba, uharibifu wa mazingira unachangia kuongezeka kwa umaskini na kwamba kadri hali ya umaskini inavyoongezeka inasababisha uharibifu wa mazingira, kwa msingi huo umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira nchini unachochewa zaidi na ukweli kwamba mazingira ni mhimiili wa sekta za uzalishaji kama vile kilimo, utalii, uvuvi na madini. Changamoto iliyopo ni kuhakikisha mazingira na maliasili za Tanzania zinatumika katika njia endelevu kwa kuzingatia uwiano mzuri kati ya matumizi ya maliasili, hifadhi zake na uwezo wake

wa kuendelea kutoa huduma, ili kusimamia masuala ya hifadhi ya mazingira kwa ufanisi ni lazima kudhibiti shughuli za kibinadamu zinazoathiri mazingira, masuala ya kijamii na kiuchumi kama vile ongezeko la watu, na shughuli za kiuchumi zinazoendana na matumizi yasiyo endelevu ya mazingira zinazoweka shinikizo kubwa katika mazingira na kusababisha uharibifu.

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015 NA MWELEKEO WA BAJETI 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Katika taarifa ya waziri mbele ya kamati ya kudumu ya bunge ya Ardhi Maliasili na Mazingira, imeonesha udhaifu katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2014/2015, Kimsingi matokeo ya udhaifu yameonekana zaidi kwa athari za kimazingira ambazo zimeendelea kutokea nchini, lakini pia swala la fedha za maendeleo katika uhifadhi wa mazingira bado halijawa kipaumbele kwa serikali hii ya sasa ya chama cha mapinduzi, na hili linajithibitisha kwa viwango ambavyo vinatengwa kwa miradi ya maendeleo, katika jumla ya shilingi Bilioni 61.1 ambazo Bunge liliidhinisha ni kiasi cha jumla ya shilingi Bilioni 7.5 tuu ambazo zilitengwa kwa miradi ya maendeleo katika Ofisi ya Makamu wa Raisi.

Mheshimiwa Spika, Fedha zilizopokelewa na wizara kuanzia Tarehe 01 Julai, 2014 hadi 31 Machi 2015 ilikua ni jumla ya shilingi Bilioni 36.3 fedha ambazo ni takribani nusu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka mzima, huu ndio umekuwa utamaduni wa serikali hii ya CCM kudharau maazimio ya Bunge katika bajeti na kuonesha kutokuwajibika katika utekelezaji wa Bajeti kila mwaka. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshauri kwa takribani sasa miaka mitano mfululizo juu ya nidhamu ya bajeti kwa serikali bila mafanikio yeyote. Kazi yetu kama UKAWA ni kusema kweli, Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha TUJSAHIHISHE anasema” **Ukweli una tabia moja nzuri sana. Haujali mkubwa wala mdogo; haujali adui wala rafiki. Kwake watu wote ni sawa. Pia ukweli unayo tabia ya kujilipiza kisasi kama ukipuuzwa”.....** mwisho wa kunukuu, hivyo basi jukumu letu ni kusema wazi pia kuwafahamisha watanzania iliyo kweli na kwa kuwa mwalimu anasema Ukweli haupendi kupuuzwapuuzwa hata watanzania hawapendi kupuuzwapuuzwa na serikali yao, sasa ni wakati wa watanzania kufanya uamuzi sahihi kwa maslahi ya Taifa letu ifikapo Octoba 2015.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya miradi ya maendeleo pekee ambayo iliidhinishwa na Bunge ambayo imeainishwa katika kitabu cha Waziri cha taarifa kwa kamati ya Bunge juu ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya bajeti ya mwaka 2015/2016, Fungu 31 Ofisi ya Makamu wa Rais Fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa jumla ya shilingi Bilion 6.5 na fedha zilizokwisha tolewa kwa wizara hadi kufikia mwezi machi 31,2015 ni jumla ya Shilingi Bilioni 2.2 sawa na asilimia 33 ya bajeti nzima kwa mwaka, tafsiri ndogo ni kwamba hadi kufikia mwezi Machi ni asilimia 33 tuu ya fedha za Miradi ya maendeleo zilikuwa zimetolewa katika ofisi ya Rais. Tumejenga utamaduni wa kutotekeliza bajeti na mipango yetu kama Taifa, na utamaduni huu umeasisiwa na chama cha mapinduzi kwa kuwa na ahadi zisizo tekelezeka, pia kujenga utamaduni wa kuwalaghai wananchi kwa lugha tamu zisizo weza kutekelezwa na serikali.

Mheshimiwa Spika, Utamaduni huu wa kutotekeliza ahadi na mipango ya serikali pasipo kuchukua hatua za kurekebisha,Taifa hili litaendelea kuwa maskini milele, Mwandishi na Mchambuzi wa siasa na Profesa wa Uchumi Ndg Bryan Caplan wa Chuo Kikuu cha George Mason anasema, wanasiwa wengi hawatekelezi ahadi kwa kuwa hakuna adhabu zinazochukuliwa kwa kushindwa kwao kutekeleza ahadi, lakini pia huwa hawaoni haja ya kutekeleza baada ya kushinda uchaguzi, Kimsingi anatoa suluhu kwa wapiga kura kuchukua hatua za kumwajibisha kiongozi wa aina hii, kwa mujibu wa katiba yetu hakuna mahali ambapo wananchi wanayo haki ya kumwajibisha kiongozi ambae hatimizi wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, Kimsingi Serikali hii haijawahi kufikia asilia mia za utekelezaji wa bajeti, inahitaji kupewa adhabu, tena adhabu kubwa hata ya kutumikia kifungo cha maisha, ni wakati

sasa watanzania kupima kati ya kupewa ahadi hewa ambazo kamwe hazifiki utekelezaji wa kiwango hata cha asilimia angalau hamsini, kwa nini sasa serikali isikiri mapungufu kiungwana na kutaka kupumzika kwa hiari? Kwa nini watanzania sasa wasione haja ya kuwapumzisha kwa nia njema ya mustakabali wa taifa letu?

MABADILIKO YA TABIANCHI

Mheshimiwa Spika, Kwa mara kadhaa kambi rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri serikali katika maswala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, Tanzania ni moja ya nchi ambayo tunashuhudia matokeo ya mabadilko ya tabia nchi, hususani uwepo wa ukame wa muda mrefu unaojirudia rudia ambaa unaambatana na athari kubwa katika kilimo, usafirishaji, nishati, biashara na sekta mbalimbali za uchumi kwa jamii, Karibuni tumeona athari za mafuriko katika nchi yetu ambapo wananchi wamepoteza maisha yao, lakini baadhi ya maeneo wananchi wamekosa maji kwa matumizi ya kila siku kutokana na ukame, ni mambo ya kimazingira yenye kuhitaji majibu ya kimazingira.

Mheshimiwa Spika, Wakati wananchi wakipoteza maisha katika maafa ya kimafuriko ambazo ni athari za kimazingira, serikali bado ipo usingizini kwa kutokuwa na majibu ya kuliona tatizo la kimazingira na kuchukua hatua za kunusuru roho za watanzania maskini wanaopoteza maisha kila siku kutokana na mafuriko, furaha ya serikali hii ya CCM ni kutenga bajeti kila mwaka za maafa na kuwadhulumu waathirika wa maafa yatokeapo bila kuwa na suluhisho ambalo ni la kudumu kwa kupunguza au kuondoa kabisa athari za majanga ya aina hii kutokea nchini, wakati yaitokea hayo kilimo katika maeneo husika kinadorora au kusimama kabisa, mifugo mingi na wanyama wa porini wanakuwa kwa kukosa chakula katika maeneo yenye ukame na kukosa na maji, na wakati mwingine kusombwa na mkondo wa maji yaliyofurika.

Mheshimiwa Spika, upo usemi usemao '**The devil lies in the details**' yaani mzimu upo katika maandishi, ukisoma katika majibu ya serikali kwa kamati ya bunge. Serikali inasema," Kampuni ya DART (Dar Rapid Transport) ilipewa hati ya Mazingira Tarehe 30/06/2009 yenye namba ya usajili EC/EIS/146 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi yaendayo kasi eneo la Jangwani" serikali imeendelea tena kusema "..... **DART imetekeliza masharti mengi iliopewa ikiwemo; kufanya ujenzi katika eneo linaloruhusiwa tu, kupanua miundombinu kuruhusu maji ya mvua kupita kwa urahisi,....** Hoja hapa ni je hali iliyojitokeza hivi karibuni hadi kupelekeea kufungwa kwa barabara ya jangwani ndio utekelezaji wa masharti wa kampuni ya DART kutoka kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira? Serikali iwaambie watanzania ukweli juu ya athari hizi za uzembe na kuwepo kwa miradi iliyotanguliza maslahi ya watu binafsi na sio watanzania ambaa wanaambulia kupoteza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitahadharisha serikali kwa kuonesha Baadhi ya viashiria vya uwepo wa mabadiliko ya tabianchi katika nchi yetu, ambavyo ni pamoja na vifo vya mifugo viliviyokithiri kutokana na ukame kwa wakati huo, hasa maeneo ya kaskazini mwa Tanzania kama vile Monduli na Longido wakati wastani wa mvua kwa mwaka ukiwa umepungua kwa asilimia 25.

Pia Utokeaji wa mafuriko unaosababishwa na ongezeko la mvua zisizotabirika katika maeneo makame yasiyo na mimea na hivyo maji kutiririka kwa kasi zaidi na kusababisha madhara maeneo yanapoelekea, Pia Ongezeko la joto duniani linasababisha ongezeko hatari na utokeaji wa magonjwa mapya kwa mamillioni ya watu, hasa yale yanayoenezwa na vimelea na bacteria kwa maeneo ambayo kwa asili hayakuwepo, Tafiti mbalimbali zilizohusu mwelekeo wa joto wa muda mrefu katika ziwa Viktoria,Tanganyika na Nyasa zikionesha ongezeko la joto katika maji ya kina kirefu kati ya nyuzi za sentigredi 0.2 mpaka 0.7 kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1900(Taarifa za Serikali ya mwaka 2009).

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya serikali inayojitaa sikiivu ni haya yanayotokea sasa Kwa asili tulizoea watu kuhama au kuwa wakimbizi kutokana na mapigano ya vita, lakini kwa sasa wahamiaji wengi wanatokana na mabadiliko ya tabianchi na kwa lugha iliyozoleka ni Wakimbizi wa Kimazingira "environmental refugees", Kimsingi hili limekuwa tafizo sana kwani kutokana na watu kuhama maeneo yao ya asili kwa ajili ya ukweli kwamba maeneo hayo hayawezi tena kuwezesha kuishi kwao na hivyo inawalazimu kuhamia maeneo mengine ili kuendelea na maisha yao jambo ambalo limetoka sana kwa wafugaji na wakulima na athari zake sasa ni mauaji kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni imeishauri sana serikali hii ya CCM kwa muda mrefu sasa, Kwa umri tuu inatosha kusema CCM sasa imekuwa mtu mzima kama sio mzee, Waswahili wanasema..."**Mbwa Mzee hafunzwi adabu**"... Kimsingi watanzania wameona kilichoitwa udhaifu wa Viongozi wa sasa, udhaifu wa CCM na Uzembe wa Bunge katika kuiisimamia serikali, ikiwa leo ni mwaka wa mwisho wa serikali hii ya CCM tutakuwa tukimpigia mbuzi gitaa au kumfunza mbwa mzee adabu,

Nitoe wito kwa watanzania, sasa tukatae vifo vya wananchi maskini katika mafuriko kwani hakuna hata kiongozi mmoja aliyekufa kwa mafuriko zaidi ya watu maskini tuu kufa, au kwa kuwa viongozi hawapati adha hii ndio maana hawaoni haja ya kutafuta suluhu ya majanga ya aina hii? Serikali hii imechoka sasa, hajui wajibu wake na wapi inawajibika, ni vema sasa tukafikiri kuwa na serikali inayowajibika kwa wananchi, inayoishi na kutambua wajibu wake kwa umma.

October 25 ndio siku maalumu kwetu watanzania kubadilisha mfumo wa uongozi wa nchi yetu na kuweka viongozi sahihi watakaoondoa kero za wananchi, na UKAWA ndio jawabu la watanzania.

UBOVU WA MIUNDOMBINU YA MAJI TAKA JIJI LA DAR ES SALAAM.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam ni moja ya majiji machafu katika nchi za Africa Mashariki, miundombunu ya maji taka imekua mibovu katika maeneo mengi ya jiji na hivyo kusababisha, kwanza harufu mbaya katika jiji la Dar es Salaam ambayo ni hatari kwa afya ya binadamu, pili kusababisha maji kushindwa kusafiri wakati wa mvua na kusababisha mafuriko ambayo yamekua yakileta maafa katika jiji hususani katika maeneo ya mabondeni, wakati wananchi wakipata matatizo ya kufikiwa na mafuriko katika maeneo ya mabondeni serikali bado imeshindwa kutoa misaada ya haraka kwa wahanga ikiwa ni wajibu wa serikali kuwasaidia wananchi wakipata matatizo, wakati yote haya yaktokea nchini, Serikali pamoja na kuona madhara haya yaktokea na wananchi kuendelea kupata adha ya uchafu katika maeneo yao pamoja na kusababisha magonjwa ya mlipuko, bado serikali hii ya CCM inaona ni pafyumu katika jiji na kubaki bila kuchukua hatua stahiki.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inawataka wakazi wa jiji la Dar es Salaam, sasa si wakati wa kuomba omnia msaada kwa Serikali kwani ni takribani mfululizo wa miaka kumi sasa ya Utawala wa Mh.Kikwete mambo haya yameshindwa kupata suluhu ndani ya serikali yake, Hivyo ni ukweli kwamba mazingira bora ya kiafya katika jiji la Dar es Salaam yatapatikana kwa kuwa na serikali inayowajibika kwa wananchi na kutambua kero za wananchi waliowaweka madarakani - Jibu ni UKAWA ifikapo 25 Oct 2015.

UJENZI HOLELA MIJINI

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili mara kadhaa tumeoji juu ya ujenzi holela nchini, Ni ukweli kwamba Miradi yote hapa nchini kabla ya kuanza utekelezaji wake ni lazima kwanza ufanyiwe tathmini (Environmental Impact Assessment-EIA) na kupata cheti cha kuwezesha uendelee kama ulivyokuwa umepangwa, na tukasema katika bunge hili lakini cha kushangaza miradi ambayo inamiliikiwa na Serikali imekuwa haipati cheti cha Tathmini na hivyo imekuwa ikileta usumbu mkubwa sana kwa wananchi au watumiaji na hivyo kuwa kero kwa Serikali yenewe na kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika nadharia hiyo, hivi karibuni katika jiji la Dar es Salaam yalipotokea mafuriko barabara ya jangwani ya mabasi yaendayo kasi ilijaa maji na kufungwa, ukweli ni kwamba, Ofisi ya Kampuni inayojenga miundombinu ya mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam (Strabag) ilipewa Hati na Serikali ya kumiliki eneo hilo la Jangwani na hivyo tayari wamejenga ofisi zao za Kudumu. Mbali na kuhoji utolewaji wa hati kwa Kampuni hiyo, tunahoji Je tathmini ya mazingira ilifanyika? na kwa matokeo ya sasa hata kama tathmini ilifanyika ni kwa vipi au upo mkakati gani wa kuondoa kero zinazojitokeza sasa kwa wananchi? Kitendo cha kujenga hapo ni kurudisha maji kwa maeneo jirani na kuzidisha maafa. Aidha, kama Kampuni hiyo imepewa hati miliki ni kwanini waliokuwa wamejenga eneo hilo walihamishwa na kupelekwa nje ya mji? Yote haya yalihojiwa na serikali hii ya CCM ilitoa majibu mepesi na kujisfu kuwa ni serikali sikivu ilhali ikiendelea kufurahia mafuriko na maafa ya wananchi maskini.

UCHAFU KATIKA HALMASHAURI

Mheshimiwa Spika, Katika swala la usafi wa mazingira kwa kudhibiti utupaji taka ovyo pamoja na halmashauri kusimamia swala la usafi katika halmashauri zao, swala hili limeendelea kuwa ni tatizo katika halmashauri nyangi nchini kwa kushindwa kuweka miji safi wakati wote na kusimamia utupaji taka ovyo, Mkurugenzi wa halmashauri ndiye mwenye wajibu wa kuhakikisha halmashauri yake inakuwa safi, kwa bahati mbaya sana swala la usafi limekuwa likifanywa kama kete ya kisiasa na wakurugenzi kutumika kufanya siasa za vyama, Katika halmashauri kadhaa nchini wananchi wameanza kuchangishwa fedha za ushuru wa taka kwa maamuzi ya mkurugenzi ili kugombanisha wananchi na vyama vya upinzani vyenye mamlaka katika maeneo husika, Mfano katika Hamshauri ya Mji wa Njombe kwa kuwa CHADEMA ilishinda kiti cha Diwani mwaka 2014 February, kabla ya hapo Swala la usafi katika kata ya Njombe Mjini lilikuwa chini ya Mkurugenzi, mara tuu baada ya ushindi wa CHADEMA swala hilo limekuwa likikwepwa na Mkurugenzi na kutupiwa mzigo kwa Diwani wa kata ya Njombe Mjini swala ambalo limeufanya Mji wa Njombe kuwa mchafu tena mji wa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mkuu wa Mhimili wa Bunge, na Jimbo lake likiwa chafu kupindukia, Lakini pia hali ikaendelea kuwa mbaya mara tuu baada ya CCM kushindwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwezi Desemba 2014 na kuangushwa na CHADEMA, Kimsingi huku ni kutumika kwa watendaji wa serikali kisiasa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inawataka watendaji wa serikali kuacha kutumika kisiasa na kufanya kazi zao za utendaji kwa kufuata sheria hususani Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, Katika gazeti la Miwananchi Mwezi Agosti 16, 2013 liliukuu habari ya Serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko yote ya plastiki ili kutokomeza kuenea kwa taka zinazotokana na mifuko hiyo kwenye mazingira, tamko hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa wakati huo Dk Terezya Huvisa alisema wametoa muda wa miezi mitano kuanzia mwezi huo wa Agosti hadi Januari mwaka 2014 na itakapofika Februari Mosi wataanza msako rasmi kwa watakao endelea kuuza aina hiyo ya mifuko, wakati serikali ikichukua uamuzi huo bado iliendelea kuruhusu uwepo wa aina hiyo ya mifuko katika soko ndani ya nchi, Kutokana na kukithiri kwa uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na mifuko laini ya plastiki na serikali kushindwa hadi sasa kulishughulikia swala hili zaidi ya kufanya sanaa ya

kudai hatua zinachukuliwa, Huu ni ushahidi tosha kuwa serikali ya CCM imechoka, serikali ambayo haiwezi kusimamia matamko yake yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Katika taarifa ya utekelezaji wa mipango na bajeti kwa mwaka 2014/2015 inayoonesa maagizo ya kamati ya bunge na utekelezaji wake, moja ya maagizo ni pamoja na kutekeleza agizo lake kusimamia kanuni ya kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki mapema iwezekanavyo ili kuondoa tatizo sugu la uchafuzi wa mazingira ambao unatia aibu nchi, na ukisoma katika majibu ya serikali inasema bado inaendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya umuhimu wa kutumia mifuko mbadala ambapo kanuni zimekuwepo tangu mwaka 2006 hadi sasa ni takribani miaka kumi hakuna utekelezaji wowote wa kuzuia utengenezwaji na uuzwaji wa aina hii ya mifuko ya plastiki, Huu ni ushuhuda mwingine wa kuchoka kwa serikali, Serikali ijifunze kutoka Rwanda Mji wa Kigali hakuna kuingia na mfuko wa plastiki, ukifika uwanja wa ndege wa Kigali unaacha aina yote ya mifuko ya plastiki ndipo upate kibali cha kuingia katika mji huo, kama imezekana Rwanda kwa nini sisi tushindwe? Ndio mana tunadharauliwa na wenzetu kwa kushindwa kufanya mambo madogo kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni vema sasa watanzania wakatambua ukweli wa serikali hii ya chama cha mapinduzi, serikali iliyo na mipango mingi isiyo tekelezeka, mipango yenye mvuto kwa watanzania, hatuwezi kufikia malengo ya kufanya mazingira yetu kuwa masafi kwa kuwa na mipango ambayo hakuna jithiada zozote zinazochukuliwa katika kutekeleza kwa vitendo na kuishi bali kwa kauli tuu katika maandishi, natoa wito kwa watanzania wote kutaka mazingira safi ifikapo October 2015 kwa kuing'oa CCM na UKAWA kuchukua Usukani wa Kuliongoza Taifa hili ili tuweze kunufaika na rasilimali tulizonazo kwani hii ni nchi ya Asali na Maziwa.

UJENZI WA NYUMBA KATIKA KINGO ZA MITO NA FUKWE ZA BAHARI

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika mchango wake wa hotuba ya Waziri Mkuu juu ya makadirio ya mapato na matumizi alizungumza juu ya masterplan ya mji wa Dar es Salaam, msigi wa hoja yake ni pamoja na kuwepo kwa athari za kimazingira pale mji unapokuwa na majengo yaliyojegwa kiholelea bila kuzingatia mipango na kuona athari zinazoweza kujitokeza kimazingira, Kama Bunge na Kambi ya Upinzani tumekuwa tukishauri juu ya utoaji wa vibali vya ujenzi katika maeneo ya kingo za mito na fukwe za bahari kuwa si mwema kwa mazingira, Ukisoma taarifa ya wizara kwa kamati juu ya utekelezaji wa maazimio ya bunge na maagizo ya kamati, serikali inasema imeshindwa kubomoa nyuma Na.2019/2020 iliyopo Kawe kutokana na pingamizi lililopo mahakamani.

Hoja hapa si kuingilia uhuru wa mahakama, siku zote tunasema serikali ya CCM ni dhaifu na ukweli huu hauwezi kufutwa tuu kwa kusema si dhaifu au kwa kusema hii ni siasa, ukweli huu utabaki kuwa ukweli kwanza Nyumba hii imepewa Namba na serikali hii ya CCM kwa kutambua kuwa ni Nyumba halali, Pili serikali hii ya CCM ndio ilitoa kibali cha Ujenzi wa Nyumba hii, Tatu serikali hii ya CCM ndio ilipima viwanja eneo hilo la Nyumba na kuvitoa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, TUJISAHIHISHE, Watanzania TUJISAHIHISHE, Mwalimu Aliwahi kusema ".... Hatulazimiki kuendelea na uongozi huu mbovu wa chama na serikali....." kwa wakati huo tukiwa ndani ya mfumo wa chama kimoja, akitaka kufanyike mabadiliko ya uongozi wa chama na serikali, mpaka leo chama hichohicho hakijabadi lika kimfumo wala kiuongozi, sasa ni wakati wetu wa kuamua kutoendelea na uongozi huu mbovu wa chama na serikali yake, yale ambayo tumekuwa tukishauri sasa tukayafanyie kazi wenyewe kwa maslahi ya taifa letu. UKAWA Ndio Tumaini Letu.

UWEZESHWAJI WA IDARA YA MAZINGIRA NA BARAZA (NEMC)

Mheshimiwa Spika, Katika moja ya maagizo ya kamati ya bunge kwa serikali ni pamoja na kuwezesha kifedha idara ya mazingira na baraza la mazingira ili liweze kufanya kazi kwa ufanisi ya uhifadhi wa mazingira, katika hoja mahususi ya kamati, kamati ilitaka serikali kupitia wizara ya fedha ione umuhimu wa kuipatia idara ya mazingira na baraza – NEMC Fungu la pekee ili kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya idara ya Mazingira kijulikane wazi kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa fungu 31 hujumuisha mgao wa kibajeti wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Katika majibu ya serikali inasema swala hili lipo kwenye mchakato wa kuangalia uwezekano wa kufuata ushauri huu wa kamati.

Mheshimiwa Spika, Majibu haya ya serikali kwa kawaida ya Bunge hili yamekuwa yakitolewa na serikali hii ya CCM kwa maana ya utimizaji wa wajibu wa kujibu maswali na si kutoa suluhi ya matatizo katika utendaji, huu ndio mwaka wa kukamilisha utekelezaji wa llani ya CCM ya miaka mitano, kwa ushauri wa miaka mitano mfululizo hatutegemei jipya, na kama leo malaika atawashukia serikali hii ya CCM ikabadilika, basi wazingatie ushauri tuliookwisha utoa hapo nyuma na watanzania wanaweza kuona uungwana wa serikali hii na kuwasamehe kwa uzembe wa kutofanya hayo kwa miaka yote iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Uchimbaji wa madini endelevu ni muhimu ili kulinda mazingira na kuleta maendeleo endelevu, ni muhimu kutambua na kutumia njia bora za utunzaji mazingira katika uchimbaji madini, Sekta ya madini hasa uchimbaji mkubwa hapa Tanzania ni sekta inayouka kwa kasi na inayochangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi, Shughuli za uchimbaji madini husababisha uharibifu wa mazingira, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limepeewa mamlaka ya kusimamia shughuli za utunzaji wa mazingira nchini chini ya sheria No. 20 ya Utunzaji na Usimamizi wa Mazingira (EMA) ya mwaka 2004 Ibara ya 17 (1) na 25, Kumekuwa na uchafuzi wa mazingira katika migodi mbalimbali nchini kwa kutupa taka ovyo, kusambaza kemikali ambazo ni sumu kwa uhai wa viumbe hai na binadamu pale inaposambazwa katika vyanzo vya maji na ardhi, na ni dhahiri yaktiteka katika migodi ya Nyamongo, Bulyankhulu, Mererani, Geita Gold Mine michache kwa kuitaja.

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kuwataka wananchi wanaoishi pembezoni katika migodi ambaa wamekuwa wakipata madhara kutokana na uchafuzi wa mazingira, waone ni kipindi cha mpito kwao na hali hiyo itakoma mara tuu baada ya utawala huu kukoma mwezi Oktoba 2015. Tukiwa madarakani kama UKAWA tutalipa meno Baraza la Mazingira Nchini ili kuweza kudhibiti swala la uchafuzi wa mazingira katika migodi ili wananchi na viumbe visiendelee kuathirika na sumu na athari za kimazigira migodini.

SEKTA NDOGO YA MISITU NA NYUKI

Mheshimiwa Spika, Kwa mara kadhaa Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni imeendelea kuishauri serikali juu ya uimarishaji wa sekta ndogo ya misitu na Nyuki, kwa mujibu wa kitabu cha "**Transforming the informal Sector, How to overcome the Challenges**" (ESAURP). Kinaainisha takwimu za ukubwa wa eneo la misitu Tanzania ikiwa ni hekta million 33.5 za misitu ambayo ni sawa na asilimia 38% ya eneo la ardhi yote nchini, pia kinaainisha mchango mkubwa unaoweza tolewa na sekta ya misitu katika uchumi kwa kuirasimisha sekta hiyo kuweza kuweka mazingira bora ya ajira kwa wananchi ikizingatiwa shughuli za misitu ni moja ya chanzo kikubwa cha kipato kwa wananchi wa maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, na kwa mujibu wa taarifa za TRAFFIC 2007 zinaanisha kuwa ni asilimia 4 tu ya mazao ya misitu huvunwa kihalali na asilimia 96 huvunwa bila kupata vibali rasmi na serikali kukosa mapato kwa uvunaji mkubwa unaofanywa kutokana na kutorasimisha biashara ya mazao ya misitu na kuwa na utaratibu ulio rasmi wa kufuatailia uvunaji wa mazao haya ya misitu,

Kambi rasmi ya Upinzani bungeni katika bunge hili tuliitaka serikali kuona umuhimu wa kuona asilimia kubwa ya wananchi wanaotegemea bidhaa za misitu kuendesha maisha yao kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika hizo asilimia 96 ambazo huvunwa bila ya kupata kibali, kuna miti ambayo inavunwa kwa ajili ya uchomaji wa mkaa, kwa mujibu wa tafiti zilizokwishafanyika, sekta ya mkaa huingiza zaidi ya dola milioni mia sita na hamsini sawa na zaidi ya shilingi trillioni moja kwa mwaka na kuajiri mamilioni ya watanzania hususani waishio vijijini. Ni wazi kuwa sekta hii imeachwa bila mikakati na sheria unganifu. Tanzania tunapaswa kujifunza kutoka Brazil ambayo inazalisha mkaa asilimia 11% na Tanzania pekee inazalisha asilimia 3% ya mkaa wote unaozalishwa duniani. Sekta hii ikiwekewa mikakati mizuri ya makusudi itaweza kuzalisha mkaa kwa njia ya kisasa huku ikipunguza hewa ya ukaa na kuifanya sekta hii kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Brazil huzalisha asilimia 11% ya mkaa wote unaozalishwa duniani. Kwenye miaka ya 1990 asilimia 60.3% ya uzalishaji wa mkaa Brazil ulifanywa kutoka kwenye uvunwaji wa misitu ya asili baadaye mkakati wa makusudi ulifanywa ili mkaa uzalishwe kutoka katika misitu ya kupandwa. Ingawa matumizi ya mkaa nchini Brazil ni kwa ajili ya viwanda vyta kufua chuma. Jambo la msingi ni kwamba uvunaji wa mkaa kwa misitu asili ilipungua kwa asilimia 82% kati ya mwaka 1989 hadi 1996. Makampuni makubwa yalipewa jukumu la kupanda miti, kuzalisha na kusambaza mkaa kwa ajili ya kuifanya iwe endelevu. Hapa nchini upo uwezekano kabisa wa kuboresha ubora wa mkaa kwa kuwajengea uwezo wazalishaji na kuifanya kuwa sekta rasmi huku tukiendelea kuboresha mazingira yetu. Hali hii ikiwezekana itasaidia sana katika kuboresha na kuhifadhi misitu nchini.

Ikiwa sekta ya mkaa itafanywa kuwa endelevu ni dhahiri kuwa athari zitokanazo na mkaa kama vile uharibifu wa mazingira, hewa ya ukaa iharibuyo tabia nchi na gesi ya ozone kupunguzwa kwa kiasi kikubwa.

Kambi rasmi ya upinzani iilishataka serikali kuanzisha mikakati ya makusudi ya kuweza kuifanya sekta ya mkaa iwe sekta rasmi na endelevu kwani ni nishati tegemewa na asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania, Pia, mchango wake wa zaidi ya shilingi trillioni moja katika ukuaji wa pato la Taifa ni mkubwa ukilinganisha na mazao mengine yatokanayo na misitu hivyo haiwezi kupuuzwa na kuachwa bila mkakati wowote.

Mheshimiwa Spika, Badala ya kuacha serikali iendelee kupoteza mapato kupitia watendaji katika halmashauri ambao wamekua wakitoza faini kwa bidhaa za misitu na mapato yake kutoingizwa katika mfuko wa serikali, na ukweli ni kwamba hata tusipo rasimisha mkaa utaendelea kutumika na itaendelea kuwa ni biashara ya wakubwa tu, na kama taifa misitu itaendeleka kukatwa na mapato tutaendelea kuyakosa. Kwani ukweli ni kwamba hatuna chanzo mbadala cha nishati kwa watanzania wa kipato cha chini. Hivyo basi, ni wakati muafaka kwa serikali kurasimisha biashara za misitu na kuwafanya wananchi waendelee kufanya kwa utaratibu maalumu na kuweza kuipa serikali sehemu ya mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, iliwhi kusemwa hapa Bungeni na Mch Msigwa Mbunge wa Iringa Mjini kuwa mwanamazingira mmoja duniani aliwhi kusema hivi, naomba kumnunguu Mch Msigwa tena kama alivyonukuu pia, **"To be poor and be without trees, is to be the most starved human being in the world"**, **Hakuishia hapo na akasema tena "To be poor and have trees, is to be completely rich in ways that money can never buy"** mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uharibifu wa misitu bado limeendelea kuwepo nchini na kuathiri juhudzi za utunzaji wa misitu nchini, itakumbukwa mnamo tarehe 19 April 2013, ilizungumzwa ndani ya bunge hili kuwa magogo yamekuwa yakisafirishwa nje ya nchi kupitia bandari ya Dar

es Salaam katika maswali kwa mawaziri huku tatizo la madawati kwa wanafunzi likiwa halijapata suluhi?.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaliangalia swala hili kwa maono ya mbali zaidi, lipo tatizo kubwa la uhaba wa madawati nchini kwa watoto wetu mashulen, na ujisadi mkubwa ukifanyika katika sekta ya misitu, jambo kubwa hapa ni kusimamia sera na taratibu rasmi wa serikali katika kulinda misitu nchini, itakumbukwa kuwa takwimu zinaonesha kuwa ni asilimia 4 tu ya misitu yetu ambayo huvunwa kwa vibali halali na asilimia 96 ni kwa njia isyo halali, hii ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na chama cha waandishi wa habari za mazingira (JET)- "Biashara haramu ya mazao ya misitu yaisumbua Serikali".

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukishauri sana kuwa kutokana na ubadhirifu huo katika sekta ya misitu serikali inakosa mapato yatokanayo na uvunaji wa misitu, pia wananchi wa pembezoni mwa misitu wanashindwa kujikwamua katika umaskini, kwa kurejea taarifa ya shirika la mazingira la TRAFFIC ya mwaka 2007 ilioa takwimu zilizoonesha hasara inayoipata serikali kwa mwaka kutokana na biashara haramu ya misitu ikiwa ni shilingi bilioni 75, pamoja na kuonesha hasara hiyo ya mapato ya serikali pia ilieleza uhusikaji wa viongozi wa serikali katika ubadhirifu huo.

Mheshimiwa Spika, Mh. Waziri Mkoo, moja ya vipaumbele vyake na ofisi yake ni Ufugaji Nyuki hata sasa amekuwa maarufu kwa jina la "**Bwana Nyuki**", lakini bado sekta hii ipo nyuma ikilinganishwa na matamshi ya kuonesha kuwepo kwa juhud kubwa katika kuiwezesha sekta hii kukua na kuwa na tija kwa uchumi wa nchi na jamii husika, swala la kipaumbele chochote cha serikali si kufanya kwa malengo ya kutangaza nia kwa wananchi kwa maslahi ya kisiasa, kuna haja ya serikali kuhakiki inatekeleza vipaumbele kwa kuonesha utendaji halisi hasa kufanya sekta ya nyuki kuwa na manufaa kwa wananchi wanaoingia katika biashara hiyo, takwimu zinazotolewa na taarifa za serikali juu ya kuiwezesha sekta ya ufugaji nyuki si za kuridhisha kutokana na rasilimali nyuki tulionayo nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inatoa rai kwa wananchi sasa Kuchagua viongozi wakweli viongozi wenyewe uwezo wa kutekeleza ahadi kwa watananzia, hii ndio itakuwa dawa kwa matatizo yaliyodumu kwa zaidi ya miaka hamsini chini ya utawala wa CCM kama tutaamua kwa pamoja kuweka madarakani vyama mbadala vyenye maono mapya yaani UKAWA.

HITIMISHO.

Mheshimiwa Spika, Nimalize kwa kumshukuru Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe(Mb), Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Mwenyekiti Mwenza wa UKAWA, kwa kunihamini na kunithea kuongoza Wizara hii kama Waziri Kivuli Mazingira Ofisi ya Rais.

Pia Wenyeviti wenza wa UKAWA Mh Prof. Ibrahimu Lipumba, Mh Emmanuel Makaidi, na Mh James Mbatia (Mb), kwa kazi kubwa wanayoifanya ambayo imeshaanza kuzaa matunda kwa watananzia na hivyo ifikapo Mwezi Oktoba 25, 2015 watakapo fanya uamuzi wa kweli kwani tayari wametambua UKAWA ndio tumaini lao pekee. Mwenyezi Mungu Ibariki UKAWA, Mwenyezi Mungu Ibariki TANZANIA, Ameni.

Mch. Israel Y. Natse (Mb)

**Msemaji Mkoo Kambi Rasmi ya Upinzani - Ofisi ya
Makamu wa Rais, Mazingira, 2015**

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana, ahsante sana kwa hotuba yako.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye hatua inayofuata ambayo ni ya uchangiaji wa Mbunge mmoja mmoja; na kama mtakavyokumbuka dakika zetu ni saba, siyo zaidi. Narudia tena, ni dakika saba kufuatana na makubaliano ya jana.

Sasa naomba atuanzishie mjadala Mheshimiwa Mariba Chacha Nyangwine, atafuatiwa na Mheshimiwa Hilda Ngoye.

MHE. NYAMBALI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipatia nafasi ili na mimi niweze kutoa maoni kuhusu Ofisi hii ya Makamu wa Rais. Kwa kwenda kwa haraka haraka, naomba niweke mambo sawa, kwamba hawa wenzetu wa Upinzani, hasa ukifuatilia hotuba ya Mheshimiwa Tundu Lissu, yeye yuko nyuma ya wakati sana kuhusu kero za Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kero hizi za Muungano nyingi zimeshatatuliwa; na hata kwenye Kamati, Mheshimiwa Waziri alikuja akaeleza; na Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwepo kwenye Kamati. Sasa leo anakuja kutudanganya kwamba hizi kero hazijatatuliwa! Kweli, napata wasiwasi sana, asijaribu kuwadanganya Watanzania kwa kuwadanganya.

Hali kadhalika, hakushiriki katika kutunga Katiba inayopendekezwa ambapo sehemu kubwa ya Katiba inayopendekezwa, imetatua kero hizi za Muungano. Nawaomba Watanzania kokote kule waliko, waipitishe, waipigie kura Katiba inayopendekezwa ili iweze kuondoa kero zote hizi zinazoukibili Muungano wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba Muungano wa Tanzania ni moja ya miungano ya kuigwa katika dunia. Watu mbalimbali wanajifunza kuhusu Muungano wetu, amba ni wa kipelee. Umuhimu wake umeleta umoja, amani, mshikamano na undugu katika jamii zetu zote. Hizi kero mimi naamini kwamba zitawezza kutatulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kwamba kuna haja zaidi ya Watanzania kueleweshwa juu ya umuhimu wa Muungano wetu. Kwanza historia yake na sababu zilizofanya tuungane, mambo ya Muungano na mambo yasiyokuwa ya Muungano na sababu zake na mafanikio yake na hata changamoto zinazoukibili Muungano na jinsi zinavyotatulika. Viandikwe vitabu, majarida, vipeperushi na hata vipindi katika redio na television vitasaidia sana.

Vile vile nasisitiza kwamba Muungano wetu umefika hapo ulipo kwa sababu ya lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili imetuunganisha, ni vizuri kokote kule tunapojadili kuhusu masuala ya Muungano tuisahau kipatia kipaumbele lugha ya Kiswahili. Tuweze kufanya hayo.

Naomba sasa niingie katika suala la mazingira ambapo nitaongelea sana suala la Mgodi wa North Mara. Huu mgodi umeleta kero sana kwa wananchi wa Tarime hasa Nyamongo na kwa sababu wananchi wa pale wanapata athari kubwa sana kutokana na mazingira ya huo mgodi.

Mhehsimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, unakumbuka kwamba kulikuwepo na matatizo ya ule mto Tigite, wewe mwenyewe uliongoza Kamati kwenda kule na mpaka sasa hivi hamjawahi kutoa au kuwaeleza Watanzania athari hizo zimefikia wapi. Nyumba zinabomoka ovyo, milio ya baruti kila siku, vumbi na yule mwekezaji ameshindwa kuwalipa wananchi wanaozunguka ule mgodi.

Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, Naibu Waziri, nawafahamu kwamba ninyi ni wachapa kazi. Nawashauri kwamba fungeni ule mgodi kwanza ili tuweze kutatua matatizo haya.

Tusipoufunga, siyo kwamba natishia, katika kipindi hiki hiki, tutachukua hatua za haraka sana ili wananchi wetu waweze kupata haki. Kwa hiyo, nashauri kwamba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri mfike kule kuangaliia tatizo la ule mgodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile ripoti naiomba ili wananchi wa Tanzania na wananchi wa Nyamongo waweze kuelewa kwamba ile ripoti ya mto Tigite ambaa ulikuwa na maji ya sumu imefikia wapi na wananchi wa Nyamongo kwa nini wasipate fidia zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nasisitiza kwamba yule mwekezaji ni tapeli. Kwa sababu ni tapeli, anafanya mambo kihuni, nafikiri tufunge ule mgodi. Hiyo itakuwa ni suluhisho kubwa sana kwa wananchi wa Tarime ili waweze kupata haki zao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza kwamba hilo suala ni muhimu tulizingatie. Kwa kweli natoa onyo kubwa sana kwamba tusipochukua hatua za haraka, kwa wale wananchi wangu wa Tarime, kwa kweli tutafanya kitu ambacho kwa kweli hatutakuwa tumekitarajia, lakini tusifike huko. Mimi nashauri na natoa onyo kwa mara ya mwisho leo kwamba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, mwondoke mkafunge ule mgodi kabla hatujachukua hatua yoyote ile. Kama mtashindwa kufanya hivyo, basi mwalipe fidia wale wananchi wanaozunguka ule mgodi ambaa wanaishi ndani ya mita 30, mita 50 au na zile shule ambazo ziko karibu na ule mgodi, zihamishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusisitiza kwamba hayo yote yafanyiwe kazi. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mhehsimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime. Sasa namwita Mheshimiwa Hilda Ngoye, atafuatiwa na Mheshimiwa Chomboh.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi nami nichangie machache katika Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuungana na Kamati kutoa pale kwa kifo cha kijana wao Robert, ambaye alifariki ghafla siku chache zilizopita. Natoa pole hizi kwa Ofisi, lakini vilevile kwa Mkurugenzi Mkuu wa NEMC na familia ya kijana huyu, kwa sababu nilifanya naye kazi, nilimfahamu alikuwa ni mchapakazi kweli kweli. Kwa hiyo, ni pigo kubwa sana kwa NEMC.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nami nichangie machache kuhusu suala zima la mazingira. Katika miji yoyote ile Tanzania au ukienda huko nchi nyingine duniani, miji yoyote ambayo utasema ni mizuri, ni ile iliyopangwa vizuri, yenye miundombinu mizuri, mifereji na kadhalika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija Tanzania, ukaangalia miji yetu, kwa kweli sifa hiyo hatuna, bado hatuna kabisa. Miji yetu imeendelea kuwa shaghalabaghala, haina mipangilio. Kwa hiyo, ni lazima Serikali hivi sasa ichukue hatua. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mafuriko yaliyotokea siku chache zilizopita Jijini Dar es Salaam, mambo makubwa, athari kubwa, vifo viliviyotokea vilitokana hasa na ubovu wa miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam na hata majiji mengine ambapo athari hizi zimetokea kama huko Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika wakati sasa tuache kuendelea kuyafurahia haya majengo marefu, maghorofa yanayojengwa usiku na mchana bila kuangalia miundombinu. Siyo sifa hata kidogo kwa mji wowote kuonekana kuna maghorofa mpaka ghorofa 30, 40

kwenda juu, kama wakati wa mafuriko hali itatokea kama ilivyotokea Dar es Salaam. Haipendezi hata kidogo! Kwa hiyo, naomba nihimize, nishauri Serikali, sasa basi ikae chini ianze kuamua kuchukua hatua za kuweza kurekebisha hali hiyo. La sivyo, hakuna faida yoyote kuita Jiji la Dar es Salaam ni Makao Makuu ya nchi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati takataka zilipoonekana kutokana na mafuriko, kulijitokeza uchafu mwangi sana ambao ulilundikana katika maeneo mbalimbali ya makazi, barabarani na maeneo ya wazi. Kwa kweli ilikuwa ni tatizo! Hasa kulijitokeza wimbi kubwa sana la uchafu wa mifuko ya plastic.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Serikali katika kipindi kilichopita, iliwahi kuongeza kiwango cha unene wa mifuko ya plastic ambayo inatakiwa kuitengeneza, kutoka micron ya chini mpaka micron 30, lakini mpaka sasa ninavyozungumza, viwanda na wengine wanaoingiza mifuko kutoka nje, wamneendelea kuleta mifuko myepesi ambayo haiwezi kudhibitiwa; ndiyo hiyo inapeperuka huku nchini kote, yaani nchi zima imejaa mifuko na hasa mifuko myeus. Haipendezi hata kidogo! Haifurahishi, kwa sababu zaidi zaidi unaona ni kama takataka tu zilizozagaa kila mahali. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba hata kama wanongeza microns zikafika 50, bado kuna haja ya kusimamia sheria. Sheria hazisimamiwi hata kidogo! Sheria zipo na jithada zinafanyika kubwa sana na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, yaani NEMC; wanafanya kazi nzuri sana, lakini taasisi ile inafanya kazi kwa mazingira magumu sana. Hawana rasilimali watu wala hawana rasilimali fedha, wanafanya kazi sijui kwa kiwango gani ambacho sielewei. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali ijaribu kuliangalia hili tatizo kwa kuipa taasisi hii, pamoja TAMISEMI ambao nao pia wanaishi na hayo mazingira ya kila siku, nao wawezeshwe, wafanye hiyo kazi ya kurekebisha miundombinu hapa nchini. (Makof)

Kwa hiyo, naomba sana sasa Serikali ichukue hatua kali ya kusimamia sheria, ndani ya NEMC kwa kuipa uwezo, lakini vilevile kwa Local Government, ambao hata kitengo chenyewe cha mtu wa kusimamia mazingira, hawana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nilitaka niligusie ni suala zima la mabati aina ya asbestos. Mabati aina ya asbestos ni mabaya, yalisapigwa marufuku huku duniani hayatumiki tena, lakini sisi hapa nchini bado naona kuna majengo ambayo bado wanaezeka mabati ya asbestos.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wanatuambia, yale mabati ubaya wake, athari zake ni kuleta magonjwa kama ya kansa. Kwa nini tuendelee kuyatumia yale mabati? Ukienda kwenye majengo ya Serikali, Wizara ya Maji, ukienda huko Lugalo, mabati ya asbestos, hayana faida kuendelea kuyatumia. Naomba mabadiliko haya yafanyike, nadhani Serikali inanisikia, naomba kushauri strongly kabisa kwamba mabati yale yaondolewe. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nihimize uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa Mazingira. Mfuko huu ungekuwepo, ungeweza kusaidia hata katika kusimamia hizi Sheria na Kanuni na hasa tunapozungumzia NEMC kutokuwa na fedha; mfuko huu ndio ambao ungesaidia sana katika kutatua matatizo ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viwanda vingi sana vinavyojengwa majengo hapa nchini, vinaleta uchafuzi mwangi sana. Kwa nini kodi wanayolipa isitumike katika kuanzisha huu

mfuko au Hazina wenyewe wakawa ni kichocheo? Lakini kwa sababu tunaliona suala la mazingira ni kama by the way, athari zake ndiyo hizo tunazoziona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tubadilike katika mtazamo wa kulianglia suala la mazingira kama kipaumbele katika nchi hii. Endapo tutaendelea kulipuuzia suala la mazingira, kwa kweli tunajipuza wenyewe, athari ndiyo hizo tunaziona; wakati wa mafuriko watu wanahangaika huku na huko, tunaona huko Mitaani hali ni mbaya. Basi naomba sana hali hii tuikebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Muhammad Chomboh, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii name nitoe mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu ya Rais (Muungano).

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita zaidi kwenye suala la Muungano hasa kwa kufuatia hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani; amezungumzia sana leo suala la Muungano hasa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Utakumbuka Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuanzia kipindi chote cha Bunge cha miaka mitano alichointingia hapa, alikuwa analizungumzia suala la Muungano, hasa kwa kipindi cha kwanza ilikuwa ni kuuponda Muungano huu na kusema kwamba Zanzibar inaionea sehemu ya pili ya Muungano. Alianza kwanza mwaka 2011, akaja mwaka 2012, akasema Zanzibar inapata kila kitu inachotaka ilimradi na Serikali ya Muungano wa Tanzania inairidhia kwa sababu inaitaka ibaki katika Muungano. Leo hii amekuja kujifanya yeye ndio anayeumwa sana na Zanzibar, jambo ambalo siyo kweli. Ni mwongo, ni mnafiki! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho tunashukuru sasa Watanzania ambao tuna akili timamu, siyo kama yeye, tunamwelewa huyu mtu anachokizungumza. Ni wale tu ambao walikuwa kama akili zao ni kama yeye alivyo...

TAARIFA

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chomboh, yupo Mheshimiwa hapa amesimama.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa Msemaji kwamba hii taarifa ni taarifa ya Kambi ya Upinzani na aliyetoa hapa ni Waziri Kivuli ama Msemaji wa hii Wizara kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Sasa unaposema ni mwongo, ni mnafiki, sema uongo wake ni nini na unafiki wake ni nini; ili isije ikageuka wewe ukawa ndiye mwongo na ukawa ndiyo mnafiki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chomboh, unapokea taarifa hiyo!

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuanza kumpa uongo na unafiki wa Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitu kibaya duniani, au kitu chenye thamani zaidi, hakuna kuliko wakati. Wakati ni muhimu sana! Mtu anapokuibia wakati wako, basi huyo mtu hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, UKAWA kwa maana ya Kambi ya Upinzani, walipewa wakati wa kuja kuwatetea wananchi hasa Wazanzibar, ndugu zangu wale na wakakimbia hapa. Walitumwa na Wazanzibar kuja kutetea maslahi ya Zanzibar, wakalaghaiwa na wenzao wakatoka nje, wakawaibia wakati wao. Hawa watu ni wabaya sana! Wezi wa wakati hawa! Wanzanzibar wenye akili timamu wanawalaani mpaka hivi leo kwa kuwaibia wakati wao, kwa sababu wakati ukishaibiwa huupati tena! Mtu akikuibia pesa unaweza ukamshitaki au anaweza akakulipa, akikuibia wakati, utaupata wapi? Huo ndio ubaya wa UKAWA! (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sana wananchi wa Tanzania, UKAWA ni watu wabaya na wezi wa wakati na ndio mpaka hivi leo wanajaribu sana kuwalaghai Wazanzibar, eti wao hawapati maslahi yao. Toka lini Mheshimiwa Tundu Lissu akawa yeze ni mpenzi sana wa Zanzibar; na akawa yeze ndiye msemaji mzuri sana wa kuwatetea Wazanzibar? (Makofij)

Ndugu zangu Wanzanzibari ambao wameungana Kambi ya UKAWA, hawa Mwenyezi Mungu alijaalia, alikuwa ameshaona. Hawa tulikuwa nao na wakakimbia; tukajaribu kuwasihii na taasisi mbalimbali; Maaskofu, Mashehe na mpaka Vyama vingine sisi kama CCM tulikwenda tukawasihi ndugu zetu warudi hao. Lakini kumbe Mwenyezi Mungu alikuwa anajua kwamba hawa watu ni wabaya, ni wezi wa wakati, akawalaani hawakuja mpaka hivi leo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, imepitishwa Katiba ambayo inatetea maslahi ya Zanzibar hapa, leo wanajuaje kama Zanzibar walichokitaka chote kimepatikana kwa Katiba Iliyopendekezwa? Nataka kuwaambia Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla, katika watu wabaya, watu wezi wa wakati ni UKAWA, na msiwape maslahi, wala msiwape madaraka katika nchi hii.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chomboh, subiria kidogo.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1), Kuhusu Utaratibu, ikisomwa sambamba na Kanuni ya 64(1) (f), kwamba "Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi, hatasema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwininge yeoyote."

MBUNGE FULANI: Sawa kabisa!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji ambaye anaendelea kusema, amesema kwamba UKAWA ni wezi wa wakati. Neno "wezi" siyo neno la staha. Naomba Kiti chako kimwamuru aondoe neno hilo kwa sababu hapa hakuna mtu mwizi. Kama UKAWA ni wezi, tunamtaka athibitishe namna gani UKAWA ni wezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama lugha hiii itaruhusiwa, inawezekana wakati mwininge ikasababisha hali ambayo siyo nzuri, tunaomba ayaondoe maneno haya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Machali, hebu msaidie kidogo, badala ya kusema mwizi wa wakati sasa atumie neno gani hapo ili ujumbe wake ule ule ufike?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, neno "mwizi" ni mwizi wa wakati, ni mwizi wa vitu, ni mwizi wa jambo lolote, siyo lugha ya staha mahali hapa. Ina maama sisi ni wezi!

NAIBU SPIKA: Naomba umsaide lugha ya staha sasa asemeje?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema ayaondoe maneno hayo kwa sababu siyo maneno ya afya. Ayaondoe maneno hayo!

NAIBU SPIKA: Si unaona hata wewe umepata taabu eeh! Mheshimiwa Chomboh endelea! (Kicheko)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ayaondoe maneno haya! Hawezi kutuita wezi!

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mswahili na nakijua sana Kiswahili. Namshangaa yeye mtu aliyetoka Kigoma atanifundisha mimi Kiswahili!

Mheshimiwa Naibu Spika, mwizi wa wakati au mwizi wa kitu, ni yule mtu aliyepewa dhamana; nakupa dhamana hii, itunze na ukikosa kuitunza wewe ni mwizi. Mlipewa wakati na wananchi ninyi, mje mtumie wakati wao hapa kuja kuwatetea; mkaondoka zenu hapa mkaenda kulanda barabarani tu! Si wezi, ni nani? Mmewaibia wakati wao wananchi wa Tanzania; na wanawajua na hawatakupeni nchi ng'o! Kwa sababu ninyi ni wezi wa wakati! Mtawapoteza kabisa wakati wao waliowapeni. (Makof)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu!

NAIBU SPIKA: Sijawaruhusu! Mheshimiwa Mbarouk nilikuona umesimama!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli.

NAIBU SPIKA: Lakini nimekuwa naangalia Kanuni zangu kwamba Mheshimiwa Mbarouk hivi ni Mbunge wa Bunge hili au siyo? Mheshimiwa Mbarouk endelea! (Kicheko)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakushukuru kwanza kwa hilo. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwambia kaka yangu na kumpa taarifa kwamba kama ni wizi, basi wizi ulifanywa na wale tuliowaita Intarahamwe wakati wa Bunge la Katiba. Wao ndio ambao walibadilisha mapendekezo hata yale yaliyotolewa na Tume ya Jaji Warioba.

Ninyi ndio wezi; na kama ni ufisadi, ufisadi na ufataki mliufanya ninyi ambao mlikuwa ni Ma-Intarahamwe. UKAWA walitumia haki yao kutoka nje. Hata sasa hivi hapa, Mawaziri hawa, Waziri Mkuu hayupo. Ina maana yeye hajaiba muda wa Bunge huyu Waziri Mkuu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk...

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Kwa hiyo, ninyi ambao mlikuwa ni Maintarahamwe ndio mafisadi na mafataki, siyo UKAWA! (Makof)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk, ahsante nashukuru. Basi imeshasemwa pande zote wezi wezi, hiyo topick imekwisha. Mheshimiwa Chombo malizia hotuba yako.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Naibu Spika, nakwambieni Watanzania, hakuna kitu chenyeh thamani kuliko wakati. Msije mkathubutu hata siku moja, mkija kuwaamini UKAWA; hawana njia, hawana jinsi ya kuweza kuwatetea. Wametoka hapa; wezi wakubwa wa wakati hawa! Hamtaupata tena wakati walioupoteza, hamtapata maisha yote hamtaupata. (Makofi)

Mhakikishe kwamba wanaotunza wakati wenu na wanaotunza dhamana zenu ni Chama cha Mapinduzi, ndicho kinachothonamini wananchi na mwachague na mhakikishe kwamba mnawapitisha na Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaendelea kushinda na kushinda daima milele. Hawa ndio watakaotunza wakati wenu na ndio watakaotunza maslahi yenu kwa nchi hii, siyo UKAWA.

Ndugu zangu, mimi nawaambia Wazanzibar, hawa watu katika uongozi wenu wa UKAWA wamechukua asilimia 60 ya uongozi, ninyi mna 30; na ninyi Chama chenu kikubwa! Mtawapa mangapi? Kama mmewapa, mtawapa mangapi? Ndugu yangu, Mheshimiwa Rajab!

MBUNGE FULANI: Keshapigwa chini huyo!

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Ndiyo sababu, UKAWA unatoa kila kitu, wakakukataa. Utoe vitu ambavyo vina maslahi nao. Mheshimiwa Rajab, usitoe kila kitu na chako na cha wenzako; vingine siyo vyako, ni vya wenzio! Vingine siyo vyako, umepewa dhamana tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni dhamana, watanza dhamana wenzako walikukabidhi, acha kuwachukulia vitu vyao ambavyo siyo vyao. Maana nikisema wizi itakuwa ni ukakasi. Msivitumie wakati vibaya. (Kicheko/Makofi)

Mmeutumia wakati vibaya sana. Wakati amba wao waliuthamini na wamepoteza nguvu zao kuwachagua ninyi na matokeo yake ndiyo ninyi mliokuwa mmedhaminiwa leo mmerudishwa hamna kitu. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa pole ndugu zangu. Mimi sijui kama nitarudi au sirudi, lakini natetea maslahi ya Wazanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chombo amesema kwa mafumbo, mimi sijamwelewa kabisa. Kurudi au kutokurudi; kwani kumetokea nini? Sasa namwita Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Habib Mnyaa.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wanasema, ya Ngoswe mwachie Ngoswe; ya Zanzibar siyajui! Aka niko bara na mazingira! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuchangia. Masikitiko yangu makubwa, Wizara hii miaka yote imekuwa ikitengewa fedha ndogo. Kamati tumeshauri, Wizara ina mawaziri wazuri, wachapakazi, lakini wanakwamishwa kwa sababu hawapewi fedha. Hilo naomba niliongee kwa kifupi na Serikali katika siku zinazokuja waongezewe fedha ili waweze kutimiza wajibu wao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko makubwa naendelea kuzungumzia ujenzi holela kwenye fukwe zetu kinyume na taratibu. Napongeza katika nyumba walizobomoa NEMC, lakini zimebomolewa baadhi ya nyumba za dagaa, mapapa mmewaacha, wengine wako humu Bungeni sijui kushoto, sijui kulia na athari yake ndiyo mafuriko yanayoendelea Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi, wamejenga kwenye maeneo ambayo hakuna kiwanja. Ripoti ya Mheshimiwa Chiligati alipokuwa Wizara ya Ardhi, eneo hilo wamesema siyo kiwanja, halina hati, watu wameambiwa wasijenge, wamepewa onyo tangu likiwa kiwanja; wameshusha majengo yao, leo Serikali mnashindwa kubomoa! Watu wawili watatu wanawagharimu mabilioni ya fedha! Leo hii chanzo cha mafuriko 2012 kilichoharibu daraja la Mto Mbezi ni hizo nyumba, zimeziba njia ya mto kwenda baharini, tunao humu ndani, wanakimbilia Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mawaziri kuna baadhi ya watu wanawaponza. Kabomoeni! Mbona hizi 24 mmebomoa? Tunapozungumza, hatuna shida na ghorofa la mtu; kwani nani hapa Mbunge anashindwa kujenga ghorofa. Tunachosema, sheria zifuatwe. Hatuna nongwa! Wanaoathirika ni wananchi wa kawaida. Leo hii daraja la Mto Mbezi lina ufa; kisa kuna watu tu wamejenga katika viwanja hewa. Chukueni ripoti ya Mheshimiwa Chiligati, mtaona! Hakuna kiwanja pale! Utapeli tu! Utapeli!

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anajenga, wengine viongozi, tena wa dini, halafu tunyamaze kimya! Mwisho wa siku Serikali ya Chama changu inalaumiwa! Mtu mmoja tu anachafua chafua hapa, halafu tunamwacha. Mheshimiwa Keissy ananiamba na huko Ziwa Tanganyika ni hivyo hivyo! Hatuwezi kufumbia macho; kunakuwa na *double standard*. Wengine msumeno unakata, wengine msumeno unakuwa butu, why? Kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mnafanya kazi kuna mambo mengine mnayaacha na wameshaona mchezo siku hizi wa kukimbilia Mahakamani; hatuwezi kukubali vitu vya namna hii. Bomoeni jumba lile la Shilingi bilioni moja sijui milioni mia 800 ili mwokoe mabilioni ya kukarabati daraja. Ni hesabu ndogo tu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongea haya mambo yanakera. Mafuriko mengine yanatengenezwa na watu wachache tu, halafu wana viwanja lukuki, lakini bado kabisa anakwenda kujenga katika njia ya mtu. Tumweleweje kama siyo kuitafutia Serikali nongwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama viongozi ni lazima tuseme, hii tabia inakera. Tunawaomba mchukue hatu; hizi 24 mmechukua, kwa nini hizo nyingine mna kigugumizi nazo? Tuna taarifa hata hizo 24 nyingine zilikuwepo kesi Mahakamani; hii ina nini? Daraja lile limeanza kujenga ufa; mafuriko yaktokea, walala hoi ndio wanahangaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia hapa jambo lingine. NEMC inafanya kazi, inaishauri Serikali, maeneo mengine hawafuati ushauri wake. Leo mradi ule wa mabasi yaendayo kasi, wamekwenda kujenga pale Ofisi, halafu tunawafukuza wale wananchi. Mmeweka kituo. Maji yakijaca, yanaingia kwenye Ofisi za DART na kwenye nyumba za wananchi. Ndiyo maana leo watu hawana guts ya kuwaambia ondokeni. Wale wataondoka, na hii Ofisi mliyojenga? *Double standard!* Ooh, masharti ya mwekezaji. Masharti gani ya mwekezaji msiyomwambia mazingira ya nyumbani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wameshauri, rushwa tu! Mtu mmoja anafanya maamuzi tofauti na wataalam ambao wamesomesha na Serikali hii, wamewaambia. Aibu! Maji yakijaa hakuna magari ya mwendo kasi wala taratibu pale Jangwani.

Sasa haya lazima tuseme. Watu wamepewa dhamana wafanye kazi kwa maslahi ya Taifa hili. Wataalam tumewasomesha, wanashauri. Hao hao NEMC na hizo hizo hela ndogo ambazo wanapewa, wanashauri, wanafanya kazi chini ya hao Mawaziri. Lakini kuna Wizara nyininge zinawakwamisha. Hao hao mnaowaona akina Mheshimiwa Masele, Mheshimiwa Mama Samia wanafanya kazi! Wataalam wao ni wazalendo! Kwa nini huko kwingine mnashindwa kufanya kazi vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani kwa akili ya kawaida, pale Jangwani unawekaje kabisa Ofisi na Kituo? Kwanza *distance* ya kutoka tu pale *Fire* mpaka Magomeni, ukiweka hivyo hata wale wa Mabondeni mnawaambia kaeni, si mmewawekea wenyewe kituo? Sasa sisi tunasema tunahitaji mazingira ya jiji pamoja na wananchi yaendelee kuwa safi. Tusibebane! Tusimung'unye maneno kwenye mambo ya msingi kwa kubeba watu wasiokuwa na *impact* na Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mama yangu pia huwa namwambia; nakuheshimu lakini hapa umebugi, unatutia aibu!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninyi Mawaziri nawaomba, mnaafanya kazi, hawa watu wachache wasiwharibie. Mheshimiwa Mama Samia nakujua, unafanya kazi vizuri, Mheshimiwa Mahenge pale ni mzalendo; haya mambo yanayowachafua yaondoeni. Baadaye nitasimama nihitaji maelezo ya kutosha kwenye kifungu mpaka nitakapopata majibu ya msingi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya, tunakushukuru sana. Nilisema Mheshimiwa Habib Mnyaa atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante. Kuna msemo wa Kiingereza unaosema, “never argue with a fool, people might not notice the difference.” Kwa hiyo, nitakwenda moja kwa moja katika hoja za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni Wizara ya Makamu wa Rais inayoshughulikia Muungano na Mazingira niwape pole kwanza Watanzania wote waliopata tatizo la kimazingira kutokana na mvua kubwa zilizoharibu miundombinu na mambo mengine wakiwemo wananchi wa Kisiwapanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo ya kero za Muungano yamekuwa ni monotonous, zimeshatuchosha hata kuzungumza tena kwa miaka mingi, hasa hizo tulizozizoea, na hazijatutuka kama ambavyo wengine wanavyosema wanatatuwa; na kero zile ambazo zinahusu uchumi na maslahi ya Wazanzibar kiuchumi, hakuna hata moja iliyotutuka. Ni *bla bla* ambayo inazungumzwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuulize, kuna hii hoja ambayo kwa kweli inahusiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje lakini na Wizara ya Muungano. Sasa kwa kuwa muda wa kuchangia ndio hivyo, bora tuizungumze hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anayehusika na mambo ya Muungano, nataka kujua kwa nini Balozi zetu takriban zote za nje, ukienda pale unaikuta picha ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, lakini hakuna picha ya Karume na hizi ni Ofisi za Muungano?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni nini kinachosababisha kwamba upande mmoja picha ya Mzee Karume, Waasisi wa Muungano isiwepo? Nenda Ofisi za Zanzibar zote utakuta pana picha ya Mzee Karume, picha ya Mwalimu Nyerere, picha ya Rais wa Jamhuri ya Muungano hivi sasa Jakaya Kikwete; na picha ya Mheshimiwa Shein. Mbona picha za Mzee Karume haziko katika Ofisi za Bara? Nani anayevunja Muungano? Nani anayeteka haya mambo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tukizungumza, wanasema ooh, wanataka kuvunja Muungano, lakini dalili zote za kuvunja Muungano ziko upande wa Tanganyika. Watujibu, kwa nini Ofisi za Balozi hakuna picha ya Karume?

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika ni chache, huu mradi wa MIVARF ambaa ameuzungumza Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 12, Ibara ya 24; amesema kuna Dola za Marekani milioni 169.5, ambazo hizo kwa pesa zetu tunazozijuia sisi siyo chini ya Shilingi bilioni 317. Katika hiyo miradi ya Masoko na Barabara katika hizo Halmashauri 18, ni kwa nini katika hotuba yake asitueleze Zanzibar zimekwenda; kuna masiko kadhaa yamejengwa, kuna barabara kadhaa, kuna hili, kuna hili na thamani iliyopelekwa Zanzibar ni kundi hili; na hizi zimetumika Tanzania Bara. Kwa nini habagui? Sasa tukisema Zanzibar tunaonewa, mpige makelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii mifano halisi ya kuidhulamu Zanzibar iko miaka na miaka. Hizi pesa, kwa mfano hizo alizotaja katika speech ya Kiongozi wa Kambo ya Upinzani, ambaye mimi nampongeza na wasishangae watu wanabadiili, hata kama Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa anaikandia Zanzibar miaka ya nyuma, amebadili, ameona ukweli na ninyi leo mnauna ukweli; na ukweli uko wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika pesa za budget support ambazo Waziri wa Fedha katika makabrasha yake ameonesha, zimepatikana Sh. 100,000,001,583/=, Zanzibar imipelekwa Shilingi bilioni saba, ni sawa na asilimia 0.45. Penye uhalali kwa mujibu wa hayo makubaliano kama ni asilimia 4.5 zilikuwa zipelekwe Shilingi bilioni 71. Hazikupelekwa Shilingi bilioni 71, zimepelekwa Shilingi bilioni saba. Shilingi bilioni 64 ziko wapi? Huu ni mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, zimepatikana au hazikupatikana? Aeleze zilizopatikana ni ngapi? Mbona huku zimepelekwa nyingi? Ni zaidi ya hizo! Atueleze, mtindo huu uko miaka yote! Kwa miaka 51 trend ndiyo hii. Kwa nini tuendelee kusema kwamba tunataka mfumo huu wa Serikali mbili? Mfumo wa Serikali mbili umepingwa kwa sababu hizo. Sasa leo wenzetu wa Tanzania Bara, sasa hivi mnayaona zile dhuluma za wazi wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 2007 mara ya mwisho sherehe za Muungano kufanya Zanzibar, tuna miaka minane zinafanya upande mmoja wa Jamhuri. Sherehe zikifanya, Rais wa Jamhuri ya Muungano siku za Sherehe za Uhuru na Muungano, anasamehe wafungwa upande mmoja. Hizi ni Sherehe za Muungano! Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Januari 64 anasamehe kule. Huku wanasemehe siku ya Uhuru, anasamehe siku ya Sherehe ya Muungano. Kwa nini? Kwa nini asamehe upande mmoja tu? Hiyo siyo kero?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mfuko wa Jimbo, hizo pesa zinazopelekwa kwenye Mfuko wa Jimbo zinapelekwa kwa Majimbo ya Zanzibar takriban Sh. 24,800,000/= Tulibadilisha sheria kwamba mpaka pesa ikifika Jimboni, Sh. 500,000/= haipo, kila Jimbo! Kwa Majimbo 50 ni Shilingi milioni ngapi hizo? Leo bado zinapelekwa; pana Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Kwa nini pasiwepo na utaratibu na pesa hizi zinatoka katika Jamhuri ya Muungano; na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri ndiyo ya mwanzo kuzipokea, kwa nini direct asipeleke Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar halafu zikaenda Majimboni moja kwa moja? Kwa nini kila pesa ikienda, Shilingi laki

nne, laki tano, laki tatu, inatoweka? Kwa nini tuiseme? Sasa tukisema hatutendewi haki, kwa nini watu wengine mchukie? Twendeni katika data za namna hiyo, tutapata kuona nani anamnyonya mwenzake?

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi kero tunazoambiwa, wengine wanasema aah, Katiba imetatua! Kimetatuka nini? Katika mfumo wa Serikali mbili matatizo ya Muungano hayawezi kutatuka. Mfumo ambao unaweza kupunguza kwa asilimia 90 kutatua matatizo ya Muungano ni mfumo wa Serikali tatu tu. Hiyo wanayosema aah, tumewapeni mafuta, chimbeni data, seismic data ziko wapi? Kwa nini zimeuzwa? Je, fedha zote zilizouzwa seismic data kwa makampuni, Zanzibar itafidiwa? Hamyaoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, huo mfuko wa pamoja wa fedha tutazame leo difference, Zanzibar imenyonywa kiasi gani na tulipwe; ikiwa tutaweza kulipwa kuanzia mwaka 1965, mpaka leo miaka 51, fedha tulizodhulumiwa Zanzibar, basi tutautaka mfumo wa Serikali mbili: Je, mko tayari kuzilipa zote? Zilipeni basi hizo kama mna uwezo.

Kwa hiyo, tukisema tunadhulumiwa hapa kila siku, kwa nini mpige makelele na ukweli ndio huo. Kama yuko Mzanzibari ambaye tunatetea maslahi ya Zanzibar tunavyodhuluiwa kiuchumi, halafu yeye hapa akawa anawa-support hawa wanaotudhulumu kiuchumi, huyo kweli ndiye anayeumwa na Zanzibar au anataka Chama cha Mapinduzi kishinde tu, japo wananchi wake wanakufa! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo haki hata kidogo! Tukiendelea hivi, tutaona katika Uchaguzi wa 2015, hiyo tofauti tutaiona baina ya wewe unayedhulumu kila siku, unayetetea dhuluma ziendelee na sisi tunaotetea maslahi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulieni kidogo, Mheshimiwa Eng. Mnyaa ni mkali sana kwa sababu ya mazingira maalum. Mheshimiwa Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim. (Kicheko/Yowe/Makofi)

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, lakini nianze kwa kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwona Mzanzibar ambaye anatetewa maslahi ya Zanzibar, lakini hayuko tayari katika kutetewa maslahi hayo, basi nina walakini na Uzanzibari wake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nikubali na nikiri kwamba Tanganyika na Zanzibar haina Muungano wa kweli, bali kuna Tanganyika ambayo imeikalia Zanzibar kama sehemu ya koloni lake, kama alivyosema Mheshimiwa Tundu Lissu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema hivyo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna mgawo wa pesa zinazotolewa na Mataifa ya nje Shilingi bilioni 1,555.319. Zanzibar inapata Shilingi bilioni 27.681. Hii inaonyesha kwamba huu siyo Muungano wa kweli baina ya Tanganyika na Zanzibar. Kwa hiyo basi, nawaomba Wanzanzibar wenzangu ambao inapotokea kutetewa Zanzibar, wao wanamaka kwa sababu ya maslahi ya Ubunge na kwa maslahi binafsi wanakubali kuipeleka Zanzibar pabaya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo Mheshimiwa Mnyaa amelizungumza na watu wakikaa hapa; ndio, nimetoka huko kuja kuitetea Zanzibar; nimetoka huko haraka kwa sababu uchaguzi umepita kuja kuitetea Zanzibar! (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kombo, wanasema uwape taarifa!

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Eeh!

NAIBU SPIKA: Unasikia sauti zao, wanasema uwape taarifa tu.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Taarifa wameshazipata na wao wasubiri zao. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba kama kweli tunataka Muungano wa kweli kwa maslahi ya Tanganyika na Zanzibar, uwepo muundo wa mfumo wa Serikali tatu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumekutana hapa, Wizara karibu 26 lakini ni Wizara sita tu ndizo za Muungano ambazo sisi Wazanzibar tunapaswa kuzijadili humu. Wizara 20 ni Wizara zinazoihusu Tanganyika. Leo tukisema kwamba kuna Serikali ya Tanganyika inayojificha ndani ya kivuli cha Jamhuri ya Muungano, isikataliwe. (Makofi)

Kwa hiyo, nawaambia Wazanzibar, ni lazima tukubali kuitetea Zanzibar yetu na endapo watatokea wenzetu hata kama ni Wapinzani ambao wanaitetea Zanzibar, basi tuwaunge mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa hajafahamu, lakini alipofahamu namna Zanzibar inavyonyonywa na Tanganyika, sasa yuko mstari wa mbele katika kuitetea Zanzibar. (Kicheko)

Ndiyo! Amefahamu leo! Wewe uliyekuwa umefahamu muda mrefu, hujafanya hivyo na leo bado unaendelea kuikandamiza Zanzibar na wewe unajiita Mzanzibar! (Makofi)

MJUMBE FULANI: Huyo anataka Ubunge! (Kicheko)

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna fedha ambazo zimesemwa eti Wazanzibari tunapewa asilimia 4.5 lakini asilimia hizo ambazo tulipaswa kupewa Shilingi bilioni 84, Shilingi bilioni 62.568 zimekatwa. Kama alivyosema Mheshimiwa Eng. Mnyaa, ukichukulia data hii ya Shilingi bilioni 62.568 kwa miaka yote ya Muungano huu unaotajwa ni Shilingi bilioni ngapi ambazo Wazanzibar wanastahili wapewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba bado vikao vinavyotajwa kwamba vinakaliwa na SMZ na SMT havina ufanisi wowote. Ndani ya kipindi cha miaka 10 kunakaliwa vikao tu; ni vikao gani hivyo vinavyokaliwa ndani ya kipindi cha miaka 10 ambavyo havijaleta ufanisi? Ni vikao gani? Vikao hivi vinaelekea ni vigonjwa, vinaumwa na havina afya. Sasa umefika wakati ni lazima mabadiliko juu ya haki ya Zanzibar yapatikane. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru! (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kombo. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar.

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami nitoe mchango wangu katika Wizara ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo kuwa mzima wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Samia Suluhi Hassan, Mama yangu, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuitetea Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezaliwa mwaka 1964, Muungano nasema siujui, nimeukuta tu. Lakini toka muda huo kwa umri niliokuwa nao sasa hivi miaka 50, nasema tuna maslahi mazuri ya Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikia watu wanapiga kelele, wanasesma Zanzibar tunaonewa; lakini najiuliza, Mzanzibar gani huyo mnayemtazama ninyi mkaona anaweza kuonewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wazanzibar kweli ni wa kuonewa? Sisi tunajitetea wenyewe mahali popote ikiwa mchana au usiku, tunajitetea wenyewe. Muungano huu, jamani mahali popote wanapokaa wawili hata wake wenza au uwe na mwenzako ndani, lazima matatizo yatakuwepo tu, hayaachi kutokea. Yatakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yanatatulika hatua baada ya hatua. Nami nasema huu Muungano, matatizo ni sisi wenyewe Wazanzibar. Tulidai hapa Katiba, tukaletewa; tukaingia humu, tukakaa, tukazungumza; lakini tulipotaka kuitetea Zanzibar, wenzetu wakatoka na pale ndiyo palikuwa mahali muafaka pa kuitetea Zanzibar. Yale tunayoyasema yote yangetatuliwa humu kwa sababu ile Katiba bado inaendelea na itapigiwa kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhi Hassan, Mwanamama huyu ni mkakamavu, shujaa wa Zanzibar, huyu ndiye mtetezi wa Zanzibar. Tena nawaomba ndugu zangu, wifi zangu Makunduchi kule msije mkamwacha, hii ni hazina! Huyu mwanamke ni shujaa, jabali!

MJUMBE FULANI: Jembe!

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Ni jembe hili la kuotea mbali!

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema bado wenzetu hawajawa na agenda wanayoitakia Zanzibar. Wamesema wee mpaka sasa hivi hawana la kusema wanaanza kumpa Mheshimiwa Tundu Lissu. Mheshimiwa Tundu Lissu haitetei Zanzibar! Mheshimiwa Tundu Lissu anatuangamiza Zanzibar, nasi Wapemba tunasema tuna maslahi makubwa zaidi Bara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mpemba, nasema jamani tusjidhalilishe. Tuseme ukweli, kwa nini tunasema uongo? Mbona tumetawala kila pembe na kila uchochoro, nasi ndio wasemaji wakuu kila siku, tunaonewa, tunaonewa. Kipi tunachoonewa, mbona hatukisemi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema, hatuonewi wala hatunyonywi! Kwa hapa tulipofika toka Muungano siujui mpaka sasa hivi ni miaka 51, basi hatutaonewa tena kuanzia hapa, ni sisi wenyewe tu! Kila kitu tumeachiwa, tutafanya wenyewe. Katiba mpya ina majibu! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Rais aendeleze Katiba mpya ipigiwe kura na wananchi tunawaomba muipigie kura ya Ndiyo, hususan ndugu zangu na wazee wangu wa Pemba, muipigie kura za Ndiyo Katiba hii kwani ina kila kitu na ndiyo Mwarobaini wa Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye mazingira. Nampongeza Waziri wa Mazingira kwa kazi zao nzuri wanazozifanya. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri wewe ni mpole, mtaratibu na tunakuja ni mchapakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nchi yetu ni sehemu gani itakayoipa kipaumbele cha usafi? Maana yake kama Dar es Salaam ni kioo cha jamii, lakini jamani Dar es Salaam tunaona sote tunatembea asubuhi na jioni, mji umekuwa mchafu; hujui unapokwenda, hujui unaporudi. Ukitoka mjini kama Kariakoo unakwenda llala saa 10.00 basi unafika saa 12.00 ya usiku kwa uchafu na mafuriko ya maji.

Mheshimiwa Waziri tunaomba hicho unachokipata, basi ukielekeze sehemu moja, kama ni Dar es Salaam, basi uielekeze Dar es Salaam. Kwa sababu mazingira sote yanatugusa kila upande, Wizara zote zinaguswa na mazingira; na hiyo ni lazima mkae pamoja mshirikiane kutatua tatizo hilo ili mji wetu uwe safi. Tusingeme jamani Moshi kusafi; wamefanya vipi? Ni Tanzania hii, lakini tuseme Dar es Salaam tunafanyaje? Kile ndiyo kioo. Nami nasema, inawezekana kwa sababu siku wanazokuja wageni, mji mbona unakuwa msafi? Tena unakuwa safi sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tukauomba, tunajua mchapakazi, unapata kidogo, hicho hicho kielekezee kumoja. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wenzangu walisema kuhusu migodi; kuna migodi michafu sana na NEMC hatusikii habari zao. Hivi karibuni nilisikia mgodi mmoja tu wa Wachina umefungwa, lakini hatukujua mwanzo wala mwisho umeishia vipi. Tuwe na uzalendo wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni sisi tulitembelea Afrika Kusini, Afrika Kusini wenzetu wana bahari na bahari hiyo ina mmomonyoko, lakini wameijengea ukuta. Leo sisi tunaporudi Zanzibar kuja Dar es Salaam kuna majumba kule nafikiri karibuni yataangukia baharini, tunafanyaje mazingira yale ya bahari? Ni machafu sana!

Kwa hiyo, Mheshimiwa tunakuomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim, tunakushukuru sana.

Naomba vijana wanao wanaoshughulika na viyoyozi, Waheshimiwa Wabunge wanalamika, baridi kali sana humu ndani. Kwa hiyo, naomba mwangalie hali ya hewa kidogo!

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Fakharia Shomar na Mheshimiwa Dkt. Mbassa ajiandae.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa mbele ya hadhara hii ya Bunge, lakini pia kumpongeza Mama Samia Suluhu, Waziri wa Mambo ya Muungano kwa uwezo wake na juhudzi zake na kuangalia kutanzua kero za Muungano. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumpongeza na Waziri wa Mazingira na pia nina haki ya kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye kinara wa Ofisi hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal. Namwomba aendeleze juhudzi zake za kazi na tunamwona jinsi anavyoituma na tunamtakia kila la kheri na ninampa hongera. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamezungumzwa mengi kuhusu Zanzibar upande wa Kambi yetu ya Upinzani; lakini leo nimeshangaa kumwona Mheshimiwa mwenzetu, ye ye alikuwa mstari wa mbele kuibughudhi Zanzibar, alikuwa hataki kuiona wala kuisikia; lakini leo akawa anaionea huruma kwamba inayonywa. Hivi kweli Zanzibar inayonywa ama anatafuta kura za Wazanzibari? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kura za Wazanzibari hazipatikani kwa njia ya kuhubiri. Ufanye kazi uonekane na uaminike ndiyo utazipata. Kwa sababu wakati wa kuitetea Zanzibar ni wakati ule wa Bunge la Katiba na wenzetu walichukua mpira wakatia kwapani wakatoka. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Naam! (Makofi)

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Leo unasema, kweli una uchungu wa Wazanzibari? Si unapiga kelele tu hapa! Ukweli kutaka kutugombanisha baina ya Bara na Visiwani na hilo nakwambia haliwi ng'o! Kwa lugha ya nyumbani yahuju! (Makofi)

MJUMBE FULANI: He! Hebu rudia tena!

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Tutashikana na kukamatana! Mbili zatosha, tatu za nini? (Makofi)

MBUNGE FULANI: Ndiyo!

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria. Wakati tunatengeneza Mabadiliko ya Sheria, Mjumbe huyo huyo alisema Wazanzibar wasiitwe kuwa Wajumbe wa Bunge la Katiba amba ni Wawakilishi. Sisi Wabunge wenyewe tunatosha. Sasa imeendaje leo kuwa anawaonea huruma naye alikuwa ameshawatoa? Akawaambia Wazanzibar wana Katiba yao, iko Unguja. Sasa leo mtu huyo huyo anakuja hapa kutudanganya! Ina maana amekuja hapa kupiga kelele kutafuta kura za Wazanzibari na Wazanzibar ni werevu na wanafahamu na wanaelewa. (Makofi)

MJUMBE FULANI: Tumeshtuka!

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Tena tumeshituka mapema tu! Maana tumeshituka mapema, ndiyo tukakaa ndani tukaitetea Katiba mpaka tukatoka na tunavyotaka Zanzibar ipi iwe na kipi kiwe na Umma tunaoumba, wakati Kura ya Maoni itakapopigwa, Wazanzibari nendeni kifua mbele, mnakwenda kutetea wajibu wenu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa nane Ibara ya 18 imenifurahisha na kilichonifurahisha ni pale Mama Samia kaizungumza Tume ambayo itaratibu mambo ya migogoro ya Muungano. Sasa kama kweli tunapenda hizi kero ziondoke na Tume ipo naimeingia ndani ya Katiba na ilikuwa ndiyo wenzetu waje tuwepo ndani ya Bunge la Katiba tuitetee hii iingie ndani ya Katiba ili hii migogoro au kero tunazoita ziondoke. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tena la mwisho lililokuwa zuri, kama zile kero hazikutanzuka baina ya upande mmoja na wa pili, Mahakama ipo, tutapata suluhisho Mahakamani. Tena Mungu atupe nini Watanzania? Kitu kimeingia ndani ya sheria na kama kuna tatizo mmeshindwa kuelewana, chombo cha sheria kipo mtakwenda, kuna tatizo tena la kusema tunanyonywa, tunafanywa nini? Jamani nyie, Wazanzibar wenzangu, nami ni Mzanzibar tena kindakindaki, lakini hayo siyo kweli mnayozungumza. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna misemo hawa wenzetu wanaizungumza na hapa ilizungumzwa picha. Picha hazikuwekwa, mnatuvunja Muungano, tumekwenda; hayo ni mambo ya kuzungumzwa! Unakwenda Wizara zinazohusika, unaonana na anayehusika, unamwambia nini tatizo lilokuwepo. Siyo kuja kupita hapa kutafuta kura, kusema unaipenda Zanzibar kwa sababu picha hazikuwekwa. Picha midhali zipo na umeshaona kasoro iliyokuwepo, sasa ni kuwaona wahusika; na ukiwaona wahusika kila kitu kitakaa sawa; lakini najua ni kutafuta umaarufu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine, kuna maneno yanazungumzwa sana hapa na hasa nyumbani. Zanzibar haina Mikoa. Mikoa yote imekwenda kwenye Muungano, siyo kweli! Kweli Mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini penye utendaji, Zanzibar anachukua Mikoa yake anafanya kazi zake. Kama kutatokea uvamizi, ndio Rais wa Jamhuri kwa sababu mipaka yote ya Tanzania ipo chini ya Jamhuri ndio anachukua Mikoa yote. Hata kama ingekuwa ni Mzanzibari amekuwa Rais wa Jamhuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa!

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Fakharia Shomar. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Dkt. Mbassa na atafuatiwa na Mheshimiwa Ismail Rage.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa moyo wa dhati kwa kunipa nafasi angalau nami niweze kuchangia machache jioni hii ya leo nami nitajikita katika suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongea mazingira ni suala mtambuka na linahusu Wizara zaidi ya moja kwa kadri ninavyoliangalia suala hili. Hili ni suala ambalo limekuwa likiumiza vichwa vyta watu kama Wizara hii haina Watendaji au haiwezi kushirikiana na Wizara nyiningine ili kuweza kutatua kero hizi ambazo zimekuwa zikijitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyigi tumekuwa tukiongea hapa kuhusu masuala yote ya upimaji wa ardhi, viwanja, maendeleo ya ujenzi katika maeneo mbalimbali ya miji yetu. Lakini naweza kusema ni suala ambalo kimsingi halitiliwi maanani. Linapofika mahali likaleta madhara, ndipo tunaanza kumtafuta mchawi ni nani ilhali wakati suala hili linatendeka wote tulikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike mahali sasa Serikali ione jinsi ya kufanya kazi kwa kushirikiana na siyo Watendaji Wakuu wetu kuendelea kubaki Ofisini ilhali madhara yakitokea ndio wote tunaanza kukimbizana kuona jinsi tutakavyotatua hayo madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la ujenzi. Wananchi wetu ni kweli wanahitaji kujenga, lakini wanapoengya kwa mtaji wao mdogo na hawa wataalam wetu wa mazingira wapo Ofisini au kwenye maeneo husika, ni nani alaumiwe? Kama wangewaona hao watu wanaanza ujenzi wakaenda kuwakemea au wakuchukua hatua stahili, nani atakayewalaumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati sasa wa Serikali kuliangalia suala hili ili watu hawa wa mazingira waweze kutoka na wafanye kazi na Wizara mbalimbali ili mradi waweze kuepusha hizi athari ambazo zinajitokeza baada ya mambo hayo kuwa yametendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi yanayoendelea katika ujenzi. Kuna maeneo mengine tayari yamepimwa, lakini kuna migogoro ya viwanja baina ya Halmashauri na watu waliopimiwa. Migogoro hii haitatuliwi! Migogoro hii inapoenda Mahakamani, basi kila kitu kina-cease. Haiwezekani tuendelee kwa utaratibu huu. Ndiyo maana watu wengine wanaamua tu kujenga kiholela na mwishowe haya mazingira yanajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naombe kwa yale maeneo ambayo yameshatambuliwa kwamba kuna ujenzi holela na kwa yale ambayo hayajapimwa, Wizara hii ya Mazingira washirikiane zaidi na watu wa Wizara ya Ardhi, waweze kupima maeneo haya na miundombinu itengenezewa utaratibu mzuri ili tuepushe haya maafa yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hilo hilo la mazingira, kuna hawa watu wanaitwa Wakala wa Misitu. Mimi sijui kabisa wanatakiwa kuwajibika chini ya Wizara ipi? Tunaongea uharibifu wa mazingira na hapa ndani lilitjokeza suala zima la matumizi ya mkaa na likapigiwa kelele na Wabunge wengi kweli, kwamba hakuna suala zima la nishati mbadala ambayo imewezeshwa kwa wananchi wetu wa maisha ya kawaida na definitely watatumia mkaa. Lakini Wakala hii ndio wa kwanza kutoa vibali kwa watu kukata mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa ndio wanaongoza! Unakuta kule kwetu pembezoni, nina-declare interest kwamba natokea Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Bihalamuro; wameweke barrier wanasimamisha malori kukamata mkaa na wengine kutoza fedha; zile fedha zinakwenda wapi na zinafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika programu yote ya utunzaji wa mazingira sijawahi kusikia kwamba hawa watu wa TFS wamehamasisha angalau watu kupanda miti au wao wamepanda; hakuna! Lakini wanakuwa wa kwanza kutoa vibali. Kwa namna hii hatuwezi kuyaokoa wala kuyalinda mazingira yetu. Mkaa unatumika sehemu zote na maeneo yote; na sehemu ambako nishati ya umeme haijafika wala gesi; kimbilio lao kubwa sana litakuwa ni mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napata wasiwasi, kama hawa Wakala wa Misitu wapo na bado misitu inafyekwa, kuna faida gani ya hawa TFS kuwepo? Si bora tuwaondoe tu hawa watu? Kwa sababu wanalipwa mishahara lakini hakuna kinachofanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, imefikia mahali, hapa nilikuwa naeleza suala zima la migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya wanakijiji na maeneo ya hifadhi. TFS wana-raise issue kwamba, watu wanaishi kwenye eneo la hifadhi ilhalii mipaka imeshapimwa na wananchi wako kwenye vijiji halali ambavyo vimesajiliwa na Serikali hii na kuna Watendaji wa Vijiji wanaolipwa fedha ya Serikali hii na kuna miundombinu ya kila namna. Sasa kama hawa watu hawawezi kujua mipaka yao ya kazi, hawawezi kuhifadhi mazingira au hawawezi kufanya kazi yao, kuna faida gani ya kuwa na hawa Wakala wa Misitu? Naiomba Serikali iliangularie suala hili na tuweze kufanya kazi vizuri. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni suala zima la usafi katika miji au Halmshauri zetu. Suala la usafi ni hulka ya mtu binafsi, lakini tumekuwa na watu ambaa kimsingi wako kwa ajili ya kutusaidia katika suala hili. Wapo Maafisa Afya! Hivi ni nini nafasi ya Maafisa Afya katika suala hili? Maana yake ninachofahamu ni kwamba, kazi yao kubwa ni kuangalia masuala haya na

kuelekeza na kutoa ushauri. Lakini leo hii kama wote tutakuwa watu wa kukaa Ofisini, hatuwezi kwenda kwenye mazingira yetu (*field*) kuangalia ni nini kinaendelea, suala hili litaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiangazi kikifika, tunaona vumbi, mifuko ya *plastic* inaelea hakuna anayekemea. Hali hiyo, subiri mvua inyeshe, mifuko ile ndiyo itakayoziba mitaro na matokeo yake ni mafuriko. Sasa kama tunasubiri mafuriko yatokee ndiyo tujue mtaro umeziba wapi, hakika wote tutakuwa tumeangamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu, Watalamu wetu wa mazingira washirikiane na Wizara zinazohusika, wafanye kazi bega kwa bega, ninaamini haya mambo yanazuilia na mwananchi akielekezwa ataweza kufanya kwa utaratibu wake. Lakini tukisubiri kwanza hizi athari zitokee ndiyo tuanze kutafuta chanzo ni nini, hakika hatutawenza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba watu wanaohusika na masuala mazima ya ujenzi, tafadhali wafanye kazi kwa kushirikiana; siyo jengo limekwisha ndiyo watu wa mazingira wanakuja. Hapana, haitaleta tija! Siyo jengo limenyanyuka limefikia kwenye renter, Afisa Afya anasema hapa sijui kuna tatizo gani, hapana!

Mheshimiwa Naibu Spika, kile kibali cha ujenzi au mtu anapoanza kujenga, kinapita kwenye maeneo yote. Wekeni sheria zenu mezani mzisome na mzisimamie ili taratibu zote ziende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Rage na Waheshimiwa Mawaziri, mtafuatia.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, napenda kutoa pole kwa msiba mkubwa kwa wakazi wa Tabora; Mheshimiwa John McHele, Mjumbe wa NEC Jimbo la Tabora, amefiwa na mkewe leo asubuhi katika Hospitali ya Msasani, Peninsula. Naomba Mwenyezi Mungu amweke mahali pema Peponi Marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimesoma taarifa ya pande ya upinzani iliyosomwa leo na Mheshimiwa Tundu Lissu, nikafanya reference ya hotuba aliyoitoa tarehe 12 mwezi wa Tano, 2014, mwaka jana. Nilichogundua ni *copy and paste*, kilichobadilishwa ni tarakimu tu. Sasa nataka kumfahamisha kitaaluma kwamba kwa mfano, fedha inatolewa na *Millennium Challenge* kwa ajili ya mradi wa Tunduma – Sumbawanga, zile fedha huwezi ukagawa nusu ukapeleka Pemba au Zanzibar, haiwezekani! Huo ndiyo utaratibu uliopo katika mahesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sasa hivi Waziri wa Uchukuzi anahangaika kutafuta fedha kwa ajili ya *Central Railway Line Corridor*, akipata unasema 4.5% iende Unguja. Kuna reli Unguja kule? Kuna mambo ambayo yanatakiwa kwenda Unguja, ni yale ambayo yako kwenye general budget support ambayo inakuja pale na 4.5% ndiyo zinakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna mradi wa kujenga Chake Chake, fedha zinatolewa na *World Bank*; huwezi ukasema zile fedha zikienda Chake Chake nyingine zije Tabora. Haiwezekani hata kidogo! Kwa hiyo, ndugu zangu Wazanzibar, hasa Wapemba, muda mrefu mmekuwa mkilalamika humu ndani kwamba Zanzibar inaonewa. Siyo kweli hata kidogo! Humu ndani ya Bunge peke yake tukitaka kutoa mfano, Wabunge mnaotoka Visiwani Pemba kwenye Majimbo yenu watu hawazidi hata watu 2000. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninakotoka, Tabora kuna watu 450,000, tunapata sawa sawa, halafu unasema sisi Wazanzibari tunaonewa. Tena ninyi mmependelewa zaidi, licha ya kuwa na Wabunge, mna Wawakilishi. Halafu mnasema mnaonewa! Pale Tabora kuna sehemu moja inaitwa Ng'ambo, kuna Wapemba wako pale wana mashamba, ndio wanaoongoza kwa kulima mpunga. Kitu kikubwa ambacho nawashukuru Wapemba hawa, wameoa dada zangu, kwa hiyo, nina Wajomba zangu wengi pale. Ni waungwana sana kwa kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kila mtu anaelewa kwamba ardhi ya Unguja haitoshi kwa sasa. Lakini waniambie, kuna Mtanzania gani ana mashamba kule Unguja? Lakini wao wana mashamba mengi sana huku. Pale Kigamboni ukienda sasa hivi, hakuna hata Mzaramo mmoja, wamejaa wenyewe tu. Kwa hiyo, hii ndiyo faida ya Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimeshangaa sana Mheshimiwa mmoja anasema anataka kuona picha ya Mwasisi wa Zanzibar katika Ofisi ya Ubalozi. Jamani kuna kitu kinaitwa Muungano. Kiongozi wa Muungano anakuwa ni mmoja. Wakati ule alipokuwa Mzee Mwinyi huwezi ukaenda kule ukakuta tena picha ya Waziri Mkuu wa Tanzania Bara imewekwa kule, hapana! Inakuwa ni picha ya Mwinyi kwa sababu yule ndiye icon au kielelezo cha nchi. Haiwezekani nchi moja ikawa na icons mbili, jamani! Nchi inakuwa na icon moja. Tukishaungana, funakuwa na nchi moja na Serikali moja. Sasa hivi kwa bahati nzuri tuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakuja katika suala la majengo ambayo yanajengwa oyo Dar es Salaam. Kwa kweli inasikitisha sana. Tumwombe Mwenyezi Mungu isije ikatokea gharika yoyote pale Dar es Salaam. Tunajenga maghorofa bila kujua *infrastructure*, bila kufanya *Environmental Impact Assessment*. Wenzetu watu wa Johhannesburg baada ya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ISMAIL A. RAGE: Kengele ya kwanza hiyo?

MJUMBE FULANI: Endelea, endelea.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Aha! Baada ya kufanya...

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Rage, Mbunge wa Tabora.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Lahaula walakwata! Basi naunga mkono hoja hii bila wasiwasi. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nashukuru sana. Sasa tunageukia upande wa Serikali ili tuweze kupata majibu ya hoja mbalimbali.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rukia nimekuona!

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kusimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kwa sababu Mbunge aliyemaliza kusema, alikuwa anawataja watu kwa kuwabagua kwa makabila. Hii kweli inakubalika? Wapemba, maana yake nini? Tukianza kusema hapa mtaanza kupiga kelele. Kwanini anatubagua, anasema sijui Wapemba wako wapi; kwani sisi sio Watanzania kama wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapenda atuombe radhi, otherwise na sisi tutatukana sasa. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rage, umesikia ujumbe huo?

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani dada yangu hakunielewa. Mimi naheshimu sana kabilia, nami sikuongea ukabilia. Ninachojaribu kusema na ninarudia tena, kuna sehemu kutokana na umaarufu wa Wapemba haiitiwi tena Ng'ambo inaitwa Pemba kule Tabora. Sasa hii ni sifa kwake, ni lazima ajue hiyo. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, inatosha. Waheshimiwa Mawaziri, tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri Massele, dakika 10. Karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, napenda kutumia nafasi hii kujibu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri ambayo imelenga kuboresha utendaji kazi wa Wizara na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii pia kuwashukuru sana na kuwapongeza vijana wangu wa Stand United kwa kubakia Ligi Kuu na kuwashukuru sana wananchi wote wa Shinyanga kwa kuiunga mkono timu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nianze kwa hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Hilda Ngoye, sambamba na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, ambao wamezungumzia zaidi tatizo la miundombinu na maji yanayojaa katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba nchi yoyote ambayo inataka kuendelea kwanza kabisa ni lazima kuwe na utunzaji endelevu wa mazingira na Tanzania kama Taifa ambalo linataka kuendelea na kuwa Taifa la kipato cha kat, maendeleo endelevu ni lazima kuzingatia mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na matatizo mawili makubwa kama hoja ilivyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni shughuli za binadamu ambazo zimeongelewa kwa upana mkubwa sana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, wakazi wa Dar es Salaam wamekuwa wakivunja sheria mbalimbali za Mipango Miji pamoja na mazingira kwa kujenga katika maeneo ambayo hayaruhusiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mheshimiwa Ridhiwani amezungumzia eneo la Mikocheni. Eneo la Mikocheni limekuwa ni eneo linaloaja maji hata inaponyesha mvua ndogo tu. Ukweli ni kwamba zipo sababu kubwa mbili; sababu ya kwanza ni ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Mikocheni ndio njia ambayo maji yanayokusanywa kutoka maeneo mbalimbali ya mji yanapitia pamoja na Msasani kuelekea baharini. Wale waliokulia Dar es Salaam zamani wanafahamu eneo hilo ni eneo chepechepe ambalo lilikuwa linatumika kama mashamba ya mpunga na hivi sasa limegeuka kuwa makazi ya watu.

Kwa hiyo, shughuli za binadamu zinazoendelea kwenye eneo la Mikocheni kwa kujenga nyumba bila kuzingatia mifumo ya kudhibiti maji ya mvua na maji taka, inachangia kwa kiwango kikubwa kuongeza kiwango cha maji kinachobaki ardhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha maji cha Mikocheni ama Dar es Salaam kwa ujumla kiko juu sana kwa maana ya maji ya ardhini, hivyo maji ya mvua ama majitaka yanaposhindwa kudhibitiwa, hayaendi chini hayaendi chini, yanabakia juu na kusababisha mafuriko yasiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia uchafu ambao unatokana na matumizi ya binadamu katika makazi ya watu na viwanda, unaziba miundombinu ambayo ni chakavu na kusababisha mafuriko katika eneo la Mikocheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inatoa wito kwa mamlaka zote za Dar es Salaam, kwa maana ya Halmashauri zote tatu, kuhakikisha kwamba zinasimamia vizuri sheria, kanuni na taratibu zote za utunzaji wa mazingira na usafi katika maeneo yao ili kuondoa kero hizi ambazo zimekuwa ni tatizo kubwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kwenye eneo lile la *Shoppers Plaza* unaweza ukaona Halmashauri ya Kinondoni inafanya kazi nzuri ya kuzibua na kujenga upya mitaro yote inayopeleka maji machafu baharini na hivyo kuondoa tatizo ambalo limekuwepo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kiasili, Dar es Salaam maeneo yote ya mabonde, kwa mfano Bonde Msimbazi ni eneo ambalo linatumika kama sehemu ya kupumlia mji wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yote na uchafu unaotoka kwenye maeneo mengine yanakwenda kwenye bonde lile na kuelekea baharini.

Kwa hiyo, watu wote ambao wanajenga kwenye Bonde la Msimbazi wajue kwa namna moja au nyingine wanachangia kuharibu ama kusababisha matatizo ama majanga kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Ofisi yetu inasisitiza tena kwamba, maeneo ya Bonde la Msimbazi na mengine ambayo hayatakiwi wananchi kujenga ama kufanya shughuli zozote, mamlaka za Manispaa na Majiji zinazohusika ambazo zinatoa vibali vya ujenzi zisimamie na zisitoe vibali kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hoja imetolewa na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine. Kwanza namsihi rafiki yangu Nyambari, tumefanya naye kazi nzuri kwa miaka mitano; haya mambo ya kusema kwamba Serikali isipofunga Mgodi ataenda kuchukua hatua, jambo hilo aliondoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Tarime hasa kwenye Mgodi wa North Mara wa Acacia kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko ya mazingira hasa kwenye Mto Tigit na Ofisi yetu ya NEMC ilifanya utafiti mkubwa na imelichukua eneo lile kama ni pilot ku-study matatizo ya pale kwa ajili ya kuangalia na maeneo mengine kama wanawenza wakatumia mbinu mbalimbali kudhibiti hali ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgodi ule kuna kitu kinaitwa waste rocks ni sehemu ambayo wanatunza vifusi nya mawe ama mchanga ambao wanatumia kuchimba ardhini wakati wakichimba dhahabu. Kwa miaka ya nyuma mgodi haukutunza vizuri waste rocks zake na kusababisha kukaa muda mrefu na baada ya kunyeshewa mvua kupigwa na juu maji yakaanza kutiririka maana ilitengeneza matope, ambayo yalikuwa yana asidi ambayo ilitiririka kwenye mto ule na kusababisha madhara kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, NEMC na Kamati ambayo wewe mwenyewe uliongoza, mlizungukia eneo hilo na Serikali ilitoa maelekezo na maagizo kwa mgodi kuyatekeleza ikiwemo kufanya clean up ya waste rocks zote, lakini pia kuchimba visima kwa wananchi wa eneo la Nyamongo na vitongoji vingine nya Nyangoto na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali kupitia NEMC, Wizara ya Maji, Mkemia Kuu na Wizara ya Nishati na Madini pamoja na TMAA, Wakala huyu wa Nishati na Madini pamoja na OSHA wako katika maeneo yale na kila wakati wanakagua kemikali zilizoko kwenye maji kupitia Wizara ya maji; OSHA wanaangalia usalama na utendaji kazi wa wafanyakazi katika eneo la mgodi na NEMC wanaangalia athari za mazingira na kukagua pamoja na Mkemia Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kusimamia eneo hilo kwa karibu kabisa ili kuangalia uwezekano wa kudhibiti kabisa uchafuzi wa mazingira katika Mto Tigite na maeneo yote yanayozunguka Mgodi wa North Mara, lakini pia kuna tatizo la asili ambalo hili ni asili ya ardhi ya pale, kitaalam baada ya utafiti imeonesha kwamba, kuna kemikali ambazo zinatokana na mchanganyiko wa maji na udongo wa eneo hilo ambao pia unakuwa unaleta madhara kwenye maji, ambayo hii inatokana na asili ya pale ya udongo na mawe yaliyopo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, long term solution ya eneo la North Mara ni Serikali kwa kushirikiana na Mwekezaji kuhakikisha tunakamilisha mradi wa kuvuta maji kutoka Mto Mara na kuwasambazia wananchi ili wapate maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo mengine ya migodi Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia kwa mfano, kule Chunya Mgodi ule ulifungwa na Ofisi yetu kupitia NEMC tunaendelea kufanya kazi ya kila siku ya kukagua maeneo yote ya viwanda, mahoteli, migodi na miradi mbalimbali mikubwa ambayo inajengwa na kutoa ushauri na mapendekezo na kuzuia inapobidi miradi hiyo isiendelee na wanaovunja Sheria tumekuwa tukichukua hatua za kufungia miradi hii na kuwaelekeza kuchukua hatua muhimu za kutunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumepokea ushauri wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Mazingira, Ardhi na Maliasili, lakini pia tumepokea michango ya Waheshimiwa Wabunge na kuhakikisha kwamba tutahakikisha kwamba tunayasimamia. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge watupe ushirikiano wa kuhakikisha kwamba, tunasaidiana kujenga Taifa letu kwa kutunza mazingira, kwa sababu bila ya kutunza mazingira hakuna maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya na majibu haya, naomba kuunga mkono hoja. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Masele kwa majibu yako mazuri sana kuhusiana na hoja za Waheshimiwa Wabunge. Muda ulikuwa ni mdogo, lakini tunakushukuru sana.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, una robo saa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni mbalimbali ambayo wameyatoa na niwaahidi kwamba maoni yote ambayo wameyatoa tutayaafanya kazi Ofisi ya Makamu wa Rais na tutaandaa kitita cha maelezo ambacho kinatoa majibu katika maeneo mbalimbali, kwani muda huu unaweza usitoshe kabisa kutoa maelezo yote kulingana na walivyotoa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niwashukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili, Ardhi na Mazingira aliyesoma kwa niaba ya Kamati Mheshimiwa Ester Bulaya na nimshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mchungaji Natse kwa hotuba yake. Niendelee kusema kwamba maeneo yote ambayo yameainishwa tutayaainisha na kuyaelezea kwa undani na tutaleta majibu kwa Waheshimiwa Wabunge ili wawze kupata majibu yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa maelezo ya jumla. Waheshimiwa Wabunge wengi waliosimama na kuchangia ama kwa kuandika ama kwa kusema hapa Bungeni wameguswa sana na suala la uchafu wa miji mikubwa Dar es Salaam, Mwanza na Miji mingine. Nataka kutumia fursa hii kwamba hakuna linaloweza kutokea la ajabu kama hatuwezi kuwekeza kwenye mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba kama katika Halmashauri zetu za Majiji hatutaweza kuweka Bajeti kwa ajili ya shughuli za mazingira, Majiji yetu yataendelea kuwa siyo masafi. Ni sawa na mtu anahitaji kupata maziwa mengi kwa ng'ombe ambaye hampi nyasi za malisho ya kutosha. Naomba kutoa wito kwamba katika mipango ya Halmashauri ya Miji na Majiji wahakikishe wanaipa mazingira kipaumbele kama wanavyotoa kipaumbele shughuli za kilimo, shughuli za maji na maeneo mengine na kimsingi sekta zote zinagusa sekta ya mazingira.

Kwa hiyo, kama unapanga mipango ya sekta ya maji hakikisha vile vile unaangalia na masuala ya mazingira, kama unapanga mipango ya kilimo weka suala la mazingira, kama unaangalia usafi wa Jiji la Dar es Salaam basi ujue kwamba unatakiwa kuwa fedha kwa ajili ya usafi, kwa ajili ya kuwekeza katika mifereji. Hii ni shughuli ya Serikali za Mitaa, Serikali za Miji hii mikubwa kwani Ofisi ya Makamu wa Rais, kazi yetu ni kutoa miongozo kuhusu masuala mazima ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja, nilikuwa nafanya ziara Dar es Salaam ambapo nikwenda kukagua machinjio ya Yingunguti kwamba ile Manispaa inakusanya kwa mwezi milioni 24, lakini hakuna kiwango chochote cha fedha kinachorudi pale kwa ajili ya kuendeleza yale machinjio, ikiwa ni pamoja na kulipa wafanyakazi na usafi. Kwa hiyo, naomba kusisitiza kwamba hatuwezi kupata maajabu kama hatuwezi kuwekeza kwenye sekta ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limeongelewa sana na Wabunge wengi wakiwemo Mheshimiwa Mwanakhamis, Mheshimiwa Hilda Ngoye na Wabunge wengi. Nataka kuchukua nafasi hii kusema kwamba tushirikiane kuhimiza Halmashauri ziweke kwenye vipaumbele vyake masuala yote ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, limeongelewa sana kwenye Kamati upande wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Kamati iliyo somwa na mwenzetu wa Upinzani kwamba mradi wa mabasi yaendayo ya kasi hakuzingatia tathimini ya athari kwa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wenzangu Wabunge waelewe kitu kimoja kwamba, Serikali ilipoona tatizo la Dar es Salaam la usafiri ambapo kulikuwa kuna msongamano mkubwa wa magari na msongamano huu ulileta matatizo makubwa katika shughuli za uchumi, lakini siyo kwenye uchumi tu, ulileta matatizo makubwa kwenye uchafuzi wa mazingira, kwa sababu magari yanapokuwa yamesongamana sana yanatoa ule moshi amba ni hewa ukaa ambayo bado inachangia kuongeza zile ukaa ambazo huongeza mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Serikali ikafanya maamuzi kwamba, inahitaji mradi mkubwa amba utakuwa ni wa mabasi yaendayo kwa kazi na baada ya kufanya maamuzi hayo, ndiyo ikatafuta fedha na ujenzi wa mradi ule ukaanza na kabla ya kufanya ujenzi ule tathimini kwa athari ya mazingira ikafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, wafahamu kwamba, Serikali ina uwezo, pale inapokuwa imeamua na ule mradi ukiwa ni kwa *interest* ya Taifa, basi unakuwa na kipaumbele na kwa maana hiyo hakuna kitu kinachoweza kuzuia ule mradi kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kuona hili linahitajika pale Jangwani ilifanyika tathimini kwa athari ya mazingira na wala hakukuwa na suala la kwamba eti wataalam walizua, siyo kweli. Ukweli ni kwamba tathimini ya athari ya mazingira ilifanyika na ushauri wa wataalam ulielekeza ni vitu gani vifanyike ili mradi huu uweze kutekelezwa. Moja ya masuala yaliyoelekezwa ni kuwa na makalavati ya kutosha na kuweka vifusi ambavyo vingeweza kuruhusu maji yaweze kupita wakati wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kulinganisha uwezo wa Serikali kutekeleza matakwa ya tathmini kwa athari za mazingira zile *mitigation measures* na anavyoweza kutekeleza mtu binafsi ambaye hana uwezo, ndiyo maana watu binafsi wanashauriwa kuondoka kwenye yale maeneo lakini kwa Serikali ilikuwa inaamini kabisa kwamba yale matakwa ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kukibili masuala ya kukata miti yangeweza kutimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza yule Mkandarasi hakufanya vizuri, watu wangu wa NEMC walitembelea wakakagua na wakamwelekeza ayatekeleza, ameyatekeleza yote kama ilivyokuwa imekusudiwa. Kilichotokea juzi ni mafuriko ambayo yame tokea sehemu yote ya Jiji la Dar es Salaam na yameathiri siyo Jangwani tu, yameathiri na maeneo mengine ambayo pia kumetokea uharibifu wa barabara, uharibifu wa mifereji, uharibifu wa madaraja. Kwa hiyo, huwezi kuchukua kama hiyo ndiyo sababu kwamba ndiyo imesababisha mabadiliko ya tabianchi na kujaa maji pale Jangwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi ambalo tumeliona sisi kitaalam ni kwamba, yule Mkandarasi kaweka mifereji, lakini ile mifereji ilizidiwa wakati maji yamekuja kutokana na uchafu unaozalishwa maeneo ya upstreams yaani maeneo ya kule juu. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sote kuhakikisha kwamba hatuzalishi taka au hatutupi taka hovyo ambazo zitakwenda kuziba ile mifereji na hivyo kusababisha maji yaweze kujaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imeongozwa na Waheshimiwa Wabunge ni suala zima la mifuko ya plastiki. Ni kweli kuwa suala la mifuko ya plastiki limeongelewa sana na Waheshimiwa Wabunge kwa vipindi vingi na Serikali iliahidi kupiga marufuku, lakini kama unafuatilia, utaona agizo hili limekuwa linashindwa kutekelezeka muda hadi muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ni kwamba, sisi ni tofauti na Zanzibar, Zanzibar hawakuwa na Viwanda vya Plastiki na Rwanda hawakuwa na Viwanda vya Plastiki kwa wao ilikuwa ni rahisi kwa wao kupiga marufuku. Sisi tuliruhusu Viwanda vya Plastiki kuanzia miaka ya 1990 baada ya teknolojia hii kuanza. Kwa hiyo, leo hii inapotaka kupiga marufuku, ni lazima ushirikishe sekta hiyo ambayo wale watu wameruhusiwa na wana leseni na wanalipa ushuru Serikalini. Kwa kuheshimu hilo ili Serikali isipelekwe Mahakamani, tumefanya mambo yafuatayo:-

Kwanza, tumeamua kuongeza microns kutoka 30 kwenda 50. Kimsingi ukweli kabisa mifuko ya nailoni inayosambaa siyo ile ya microns 30, ni ile ambayo iko chini ya micron 30 ambayo inazalishwa siyo katika viwanda hivi ambavyo vimeruhusiwa. Aidha, mifuko hii inazalishwa kinyemela ama inaingizwa kwa njia ambazo hazistahili. Kwa hiyo, tunayo kazi kubwa ambayo naweza kuwaahidi Wabunge wenzangu hapa kwamba, ni ya kusimamia enforcement ambayo inatakiwa kufanywa na NEMC kuzuia uuzaji wa mifuko hii ambayo iko chini micron 30 kwa kupingana na Sheria na Kanuni ya mwaka 2006. Naamini kwamba Kanuni hii ya microns 50 ikipita basi kazi kubwa kwetu ni kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya maamuzi vile vile kwamba kwa kuwa sasa hivi ziko teknolojia za kujeresha tunacho kiwanda pale Mwanza Falcon ambacho kinarejeresta mifuko ya plastiki na kutengeneza mifuniko ya chemba za maji machafu, kinatengeneza madawati, kinatengeza viti, kwa hiyo tuna hamasisha wawekezaji na hasa hawa wenzetu ambao wako na viwanda hivi kwamba watafute mitambo kwa ajili kurejereza mifuko ya plastiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu tumeagiza maduka yote super market kwamba kuanzia sasa mifuko hii isitolewe bure, iwe inauzwa ili yule anayechukua ule mfuko ajue kwamba anaweza akautumia mara mbili au tatu kwa sababu ametumia fedha yake katika kununua. Juhudi zote hizi zinatupelekea kwamba tutafika mahali mifuko hii itaji phaseout yenyelewe lakini kwa kufuata taratibu ambazo tutakuwa tumeziweka na wawekezaji wetu tutakuwa hatujawafanya vitu ambavyo siyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nипитie baadhi ya maeneo machache ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Liko ambalo amechangia Mheshimiwa Hilda Ngoye la kuhusu matumizi ya bati aina ya Asbestos, nataka kuwashakikishia Watanzania kwamba bati hizi ni moja ya kemikali ambazo ni hatarishi na haziruhusiwi kutumika na ndio maana tulipiga marufuku na kukifunga kiwanda cha Wazo Hill kilichokuwa kinazalisha hizi plastiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, amesema kwamba Serikali isimamie usafi wa mazingira hususani katika maeneo ya mijini. Nadhani hilo nimelielezea kwa kushirikiana na TAMISEMI, Serikali za Mitaa tutalichukua na kulifanya kazi kama nilivyosema mwanzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ignus Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, Serikali imechukua hatua gani kulinusuru Ziwa Rukwa ambalo linakabiliwa na tishio la kukauka kutokana na uharibifu wa mazingira. Ofisi inahimiza utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa Hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari, ukanda wa pwani, maziwa, mito na mabwawa mwaka 2008 kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Mabonde.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limeongelewa sana ni suala la ubomoaji wa nyumba ambazo zimejengwa kwenye fukwe. Nataka kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tumekwishaanza kulitekeleza, wakati lilipoonekana suala hili limekuwa kubwa sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Kamati ambayo ilifanya tathmini na ikabaini nyumba 460 ambazo zimejengwa kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kando ya mito, kwenye sehemu za fukwe kule Ununio, Kawe na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Ardhi na aendeleo ya Makazi, Maliasili na Utalii, Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kuhakiki zile nyumba uhalali wa vibali vyake na pale tunapogundua kwamba vibali vyake siyo halali, basi tunachukua hata zinazostahili, ndiyo maana awamu ya kwanza tulibomoa nyumba 15 na sasa hivi mwezi wa tatu tu tumeweza kubomoa nyumba 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba kuna pengine vigogo tunawaacha kama alivyosema Mheshimiwa Ester Bulaya, siyo kweli kama kuna vigogo ambao tunawaacha, suala hapa ni kwamba tunao mhimili wa Sheria ambao pale mtu anapokuwa amekimbilia Mahakamani, basi inabidi hilo tuliheshimu ili haki iweze kutendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema nisingependa kugongewa kengele mara ya pili, yale yote ambayo Wabunge wameyasema, tutatengeneza kitita na tutayarudisha hapa ili waweze kuona kila mtu kwa namna ya pekee alivyochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuwashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Dkt. Binilith Mahenge.

Sasa naomba kumwita Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii na niseme kwamba tuna heshimu mawazo ya kila mmoja aliyechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yetu ilichangiwa na wachangaji 16 ambao wamepata fursa ya kuchangia kwa kusema na wachangiaji nane ambao wamepata fursa ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejikita katika kutoa majibu ya hoja au ufanuzi uliotakiwa, lakini nikiri kwamba hatutaweza kutoa majibu yote kwa sababu muda ni mchache, lakini niseme tu kwamba tutakwenda kuyafanya kazi kama alivyosema Waziri mwenzangu wa mazingira na tutaleta majibu ya hoja zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nijielekeze sasa katika hoja za Kamati kwa upande wa Muungano kwa sababu kwa upande wa Mazingira tayari hoja zilishatolewa ufanuzi.

Kwa upande wa Muungano Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala wametupa ushauri katika nyanja mbalimbali na niseme kwamba ushauri wote tunauchukua na tutakwenda kuufanya kazi ipasavyo. Baada ya ya hoja za Kamati nijielekeze sasa kwa hoja za Kambi ya Upinzani ambazo nazo nitajaribu kutoa ufanuzi jinsi nitakavyoweza na kama sikuzijibu zote, basi kama nilivyosema tutajibu katika maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza kwa Kambi ya Upinzani ni kwamba, kuna wasiwasi kwamba Zanzibar ni Koloni la Tanzania Bara. Sasa katika karne hii ukimwambia mtu

maneno hayo nadhani wewe unayesema atakutazana mara tatu, tatu kwa kujua hadhi ya Zanzibar na status yake ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kulikuwa kuna hoja kwamba mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha hajafanyiwa kazi, nataka niseme kwamba mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha yamefanyiwa kazi. Nimekuwa nikitoa majibu kila Bunge la Bajeti hatua kwa hatua mapendekezo yalipofikia. Tulipofikia sasa ni kwamba, sekta mbili za fedha za SMT n SMZ wameamua kuandika waraka wa pamoja ambao waraka huo utapitishwa na cabinet ya MST na Baraza la Mawaziri wa SMZ au Baraza la Mapinduzi la SMZ. Baada ya hapo ndiyo yatakuwa maamuzi ya Serikali zote mbili. Waraka upo tayari, upo kwenye majadiliano ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, kulikuwa na hoja ya gawio la 4.5 kwa misaada ya bajeti na mikopo kwa SMZ na kwamba zilitumika figure zilizotolewa kuchanganya watu. Ukweli ni kwamba tunesema kwamba bajeti iliyoombwa mwaka jana ilikuwa ni bilioni 44. Kati ya hizo, kuna fedha za misaada kibajeti ambayo wahisani wanatoa au tunaita GBS, kuna fedha kodi inayotokana na mishahara ya wafanyakazi Taasisi za Muungano 4.5; kuna fedha ya Mfuko wa Jimbo. Kwa mwaka huu pia kuna fedha ya gawio la faida ya Benki Kuu ambayo miaka yote tulikuwa hatujapata figure zake, lakini kwa mwaka huu tumeweza kupata figure yake. Gawio la faida za Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, papo hapo tulisema kwamba wakati wa sherehe za Muungano, Serikali ya Zanzibar ilitumia pesa yake kufanya uzinduzi wa sherehe, ambapo baadaye SMT ilikwenda kurudishia. Alichokifanya Msemaji wa Kambi ya Upinzani ni kuchanganya figures zote hizi na kusema zote ni GBS. Si ajali, lakini kwa sababu ukisoma kitabu kinasema kabisa figure iliyoombwa na mgawanyo wake.

Tunapokuja kwenye bilioni saba na milioni mia moja thelathini na saba, zilizotolewa na GBS, pesa hizi ni pesa ambazo wafadhili wanatoa. Wafadhili wakitoa mgao unafanyika. Wafadhili hawakutoa, mgao haufanyiki. Kwa mwaka huu ndiyo mwaka Zanzibar imepata pesa kidogo mno na hata Tanzania Bara kwa sababu wafadhili waligoma katikati kutoa misaada ya kibajeti na ndiyo maana inaonekana bilioni saba. Kwa miaka iliyopita tulikuwa tuna-range kwenye bilioni 25 mpaka bilioni 35 ama 33 wakati mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo hilo kuna jambo limechanganya tena kwa makusudi. Katika analysis ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, alikuwa anazungumzia gawio la 4.5 na kuchanganya figures akisema kinachopelekwa Zanzibar ni 2.8, lakini 2.8 hii ni figure ama tarakwimu ya kupotosha, lakini ukweli anaujua kwamba 4.5 inatoka kila kipembele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa nane wa hotuba yake, anasema kwamba sasa mambo yamegeuka, Zanzibar wamechukua 10% na Tanzania Bara imechukua 90%, which is even better! Kwa sababu kwenye gawio la kawaida Tanzania Bara inatakiwa ichukue 95.4% na Zanzibar ni 4.5%, lakini kama ni 10 kwa 90 which is even better for Zanzibar kwa analysis zake lakini sio analysis za kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililokuwa linasemwa hapa ni kutoa ripoti ya fedha zinazokwenda Zanzibar. Sasa hapa kuna mambo mawili, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amechanganya. Kuna fedha ambazo yeye alizungumza na Wizara ya Fedha au Waziri wa Fedha na akataka kujua fedha ambazo wanapokea za misaada ya kibajeti na za mikopo kwa Tanzania kwa muda wa miaka kumi. Hili hakuzungumza na Ofisi ya Makamu wa Rais. Sasa inashangaza leo kuzidai pesa hizi ndani ya hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tuliagizwa kuangalia fedha zinazotoka upande wa Tanzania Bara na kwenda Zanzibar. Miaka yote tumekuwa tukiripoti GBS, PAYE, Mfuko wa Jimbo, lakini kama nilivyosema awali mwaka huu tumeweka gawio la faida ya Benki Kuu lakini pia tumeweza kupata fedha za miradi mbalimbali inayokwenda Zanzibar na tumeonesha fedha zake katika ripoti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikiri kwamba kuna fedha za miradi mingine ambayo hatukuweza kupata. Kwa sababu hii kazi tumeanza mwaka huu na tumefanikiwa kupata tulichopata, lakini kama nilivyosema kwenye kitabu cha bajeti kwamba Ofisi itaongeza jitihada ya kukusanya takwimu zote na tunahakikisha kwamba tunasambaza kwa wananchi ili wajue. Hapa hakuna kificho wala hakuna dhuluma inayofichwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fadhaa iliyompata Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na hili limenishangaza na nilimwona Rajabu akimsaidia. Katika ukurasa wa kumi Maalim Seif Sharif Hamad amesema ni Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mpaka aliposaidiwa na Rajabu Mbarouk hapa ndiyo akatamka ni Makamu wa Kwanza. Kwa hiyo, ni moja kati ya fadhaa ambazo ndugu yangu hapa alikuwa nazo wakati anaandika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mikopo, kuna mikopo ambayo SMZ inakopa yenyewe, lakini kuna mikopo ambayo SMZ inakopa kwa kupata dhamana ya Hazina. Kwa hiyo, kwenye suala la mikopo hakuna suala la 4.5, ni mahitaji ya mikopo ya upande gani unakopa. Hata hivyo, hatuwezi kusema mikopo yote inayotoka nje na inayokuja kwa fedha za kigeni, hiyo ni pesa ya Muungano na lazima igaiwe kwa 4.5. Haiwezekani! Kwa sababu mikopo hii kama alivyosema Mheshimiwa Rage, inakwenda kwenye reli, afya, umeme, kilimo, maji na mambo mengi ambayo siyo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haiwezekani wenzetu wanakopa, mikopo ambayo siyo ya Muungano, sisi tusimame tuseme mikopo hiyo igawiwe kwa 4.5. Just kwa sababu ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwamba Kikatiba pesa yoyote ya kigeni inayoingia nchini na ikaingia Serikali hiyo ni pesa ya Muungano. Siyo kweli! Kuna pesa ambayo inakopwa kwa sekta ambazo haziko ndani ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tunasahau moja kwamba, mwaka 2012 tulikubaliana kwamba Zanzibar sasa itakuwa inakopa yenyewe ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, negotiations, kiasi gani, kwa mradi gani, Zanzibar inaamua yenyewe. Kinachofuata kama mkopo unataka dhamana Hazina ya Muungano ndiyo inatoa dhamana na kukamilisha process za kupatikana kwa mkopo wenyewe. Kwa hiyo, tusichanganye watu! Tumechukua factors chungu mzima, tumezichanganya tukagawanya kwa 4.5 tukadanganya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kubwa, kuna figure ambayo imetajwa ya dola za Kimarekani mia tano themanini na, ambayo wahisani waliahidi kutoa kwa mwaka huu wa fedha, lakini pesa hii haikutoka yote, pengine imetoka robo tu. Ndiyo maana nikasema Zanzibar wamepata bilioni saba na wenzetu wamepata walichokipata. Haikutoka yote! Pesa hii inategemea kama wahisani wanatoa basi pande zote mbili zinapata.

Mheshimiwa Spika, katika Kambi ya Upinzani kulikuwa pia kunakupuuzwa kwa maelekezo ya Kamati. Nataka niseme hapa tena kwa unyenyekevu mkubwa kwamba ofisi yetu hata siku moja hatutathubutu kupuza maelekezo ya Kamati. Kwa sababu maelekezo ya Kamati ndiyo yanayotufanya tufanye kazi zetu vizuri. Tunachukulia maelekezo ya Kamati kama ni masahihisho ya marekebisho kwenye kazi zetu. Kwa hiyo, tunajitahidi kufanya kazi zetu.

Maelekezo ya Kamati ndiyo yanatupa dira ya kufanya kazi zetu, kwa hiyo, hatuwezi kupuuza maelekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kutoka Kambi ya Upinzani ambalo limeshazungumzwa ni kuletwa mahesabu ya miaka kumi ambalo nimeshalizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa kuna suala pia la Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki ambalo ni kweli limeanza muda mrefu na halijamalizika, lakini kwa hatua iliyofika sasa hivi kama nilivyosema kwenye kitabu cha bajeti, kwamba sekta mbili za fedha, baada ya kupitia documents zilizotoka Bodi ya Sarafu Afrika Mashariki ambazo nazo zimechukua muda kupatikana, wote wawili wamekubaliana kuwashirikisha Wanasheria Wakuu wa Serikali mbili kwa sababu humo ndani kuna mambo ya kisheria, wao kama Mawaziri wa Fedha wasingeweza peke yao kuyafahamu na kuyatolea maamuizi.

Kwa hiyo, wanaomba kibali kupeleka documents zile ambazo ni za siri mno kwa Wanasheria Wakuu wa Serikali watoe ushauri wa kisheria kabla ya Waraka waliouandaa kwenda kwenye Kamati ya pamoja ya kuangalia changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma tena hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na kutoka ukurasa wa 22 kwenda mbele kulikuwa kuna mambo mengi ambayo yanapendekezwa pengine katika marekebisho ya Katiba, lakini kama walivyosema wengine kwamba wakati huu jamani tumeutupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nataka niwaambie ndugu zangu, katika karata mbaya mliyoicheza kisasa ni kutoka katika Bunge la Katiba, kwa sababu mngekuwepo mle, mnayoyazungumza leo hapa msingeyazungumza! Tungekuwa tumeyazungumza kule na wote kwa pamoja sisi na nyie tungerekebisha na kuiweka Zanzibar yetu pale mnapopataka. Sasa kama ngoma imepigwa, kucheza hucheki umeetoka, halafu uje kulaumu kwamba mlipiga ngoma mimi sikicheza, umeetoka mwenyewe! Kwa hiyo, ile ilikuwa karata mbaya sana kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niungane na Mheshimiwa Tundu Lissu, aliposema kwamba si busara kwa ye ye kujisifu kwa kazi ambazo amezifanya ndani ya Bunge hili Tukufu, kwa sababu katika michango yake Mheshimiwa Tundu Lissu ni mwelewa, ni Mwanasheria mahiri, Wakili mahiri, lakini anafanya michango ya makusudi tu kuwachanganya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nami naungana naye kwamba si busara kwa ye ye kujisifu kuwa anayoyafanya humu ndani Bungeni. Lile alilolishutumu kwa upande wetu, kwamba tunatumia nafasi hii kupambana au kuwapumbaza wajinga na kuwandanganya wasioelewa, ndani ya Tanzania sijui wajinga akina nani, wala wasioelewa ni akina nani. Sasa kama ye ye anatumia fursa hiyo kufanya hilo, kudanganya wajinga na kuwapumbaza wasioelewa, basi ni kweli kwamba asijisifu anachokifanya humu ndani. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka kwenye michango ya Kambi ya Upinzani, kulikuwa na michango ya wachangiaji mmoja mmoja na nianze na Mheshimiwa Lwanji, ambaye naye ametupa mapendekezo mazuri tu na nimhakikishie tu tutayachukua na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Muhammed Seif na ye ye pia alitupa ushauri kwamba ni vyema mitaala ya shule zetu ikaweka suala la Muungano. Nataka niseme kwamba tulijaribu kufanya hilo na Wizara ya Elimu wakasema kwamba tayari wana mambo hayo ndani ya somo linaloitwa civic education. Hata hivyo, kwa kuona kwamba halisomeshwi katika level ambayo labda tungependa lisomeshwe, tumekubaliana na makumbusho ya Taifa kwamba kazi hii wataifanya wao wakati tofauti tofauti kupitia wanafunzi wa shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine alikuwa anataka kujua ahadi ambayo Mheshimiwa Makamu wa Rais ameiweka. Nimhakikishie tu kwamba ahadi hizo tunazifanyia kazi na pale tutakapokuwa tupo vizuri, basi utaweza kutekeleza ahadi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ya Mheshimiwa Mnyaa ambaye kama ulivyomuona leo alikuwa mkali mno, lakini naye ametoa haja kadhaa ambazo Wabunge wengine walishazichangia, lakini na nyingine nilishazijibu wakati najibu hoja ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna moja hili specific la Mradi wa MIVARF. Mradi wa MIVARF ni kweli kwamba kwa sasa hivi sitawezu kukupa figure exactly kwa Zanzibar na Bara kwa sababu mradi huu upo chini ya Wizara ya Kilimo. Wizara ya Kilimo na Chakula watakapokuja watakuja kueleza kwa ukubwa zaidi. Mimi nimeitaja miradi kwa sababu ni mratibu tu wa mambo yanayofanyika huku na huku, ndiyo maana nimeeleza kwa ufupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, najua kwamba kuna njia kadhaa Unguja na Pemba zimejengwa, njia ambazo zinawafanya wakulima wapate urahisi wa kufikia masoko, lakini pia kuna masoko yamejengwa na maghala. Mradi huu ni wa muda wa miaka mitatu unaendelea kujengwa na tutegemee mazuri tu kutoka kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine alikuwa anasema tatizo lake kwamba, pesa za Jimbo zinavyoingizwa mpaka zikifika kwenye akaunti kuna laki tano zinapungua. Nimwahidi tu kwamba, hili totalifuatilia tuone zinapungua wapi, kama ni bank charges au vipi, lakini mimi mwenyewe experience yangu napata kitu chote kamili. Sina mikato huu toka tumeanza mpaka leo. Kwa hiyo, kama Pemba kuna tatizo hilo, niwaahidi Wabunge wa Pemba kwamba, nitalifuatilia ili tujue kwa nini kuna mikato hii. Kama sio mikato ya lazima, basi Mfuko ule usikatwe pesa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na michango kutoka kwa Mheshimiwa Kombo, naye pia alijielekeza zaidi kwenye suala la Katiba, lakini pia alikuwa na wasiwasi kwamba vikao havina ufanisi, vile vinavyokaa kutatua kero za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kombo kwamba vikao vina ufanisi. Kuna kero kadhaa tumezimaliza na sasa hivi Serikali zetu zinafanya kazi along those kero ambazo tumemaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nataka kukiri kwamba, kuna mambo mengine ni magumu hamuwezi kumaliza kwa muda mdogo, yanataka mazungumzo na mazungumzo. Kwa hiyo, katika kila negotiation kuna status tofauti za issues mnazozizingumza. Kwa hiyo, vikao vina ufanisi, lakini mambo yapo kwenye hadhi tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanakhamis, Mheshimiwa Fakharia pamoja na Mheshimiwa Chombo, nao wamezungumzia habari ya Muungano na wametoa mawazo yao na kama nilivyosema mwanzo, naheshimu mawazo ya kila anayezungumza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rage naye kwa upande wake alizungumza, lakini alikuwa mkali kidogo kwa sisi wenye asili ya Pemba, lakini nataka niseme tu kwamba Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano inamruhusu Tanzania kuishi popote pale anapohisi atafanya maisha mazuri na maendeleo yake yatapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu. Katibu!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 - Administration and Human

Resources Management... ...Shs. 5,079,085,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 - Administration and Human Resources

Management Division... ...Shs. 2,498,864,000/=

NAIBU SPIKA: Hapa nina majina maalum, kama haupo kwenye majina yangu basi pole sana. Tunafuata utaratibu wa ile kanuni yetu. Wa kwanza Mheshimiwa Suleiman Jafo kama yupo. Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMAN S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, napenda kupongeza majibu yote ya Mawaziri wote katika Wizara hizi mbili. Katika mchango wangu wa maandishi niligusa hasa sehemu ya uteketezaji wa bidhaa za sumu hususan mambo ya mbolea na madawa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba kama nchi tuna wakati mwengine tuna-import mbolea na *chemical* zingine mbalimbali, lakini inawezekana kuna vyombo mbalimbali huenda TBS au TFRA mamlaka ya mbolea inaweza ikabaini kwamba kuna bidhaa fulani zilizoingizwa ni feki, lakini bidhaa hizo zinatakiwa kuteketezwa.

Sasa kubwa zaidi nataka kujua, je, kama nchi tuna mipango gani kuhakikisha kwamba tuna utaratibu maalum wa kuteketeza bidhaa hizi tukijua wazi kwamba endapo utaratibu muafaka hautowekwa vizuri bidhaa hizi zinaweza zikaleta athari kubwa sana katika afya za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufanuzi kutoka Ofisi ya Mazingira katika eneo hilo. Ahsante sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Jafo kwa swali hili zuri. Tunao mkataba unaosimamia hizi taka ambazo ni sumu au bidhaa ambazo sizo nzuri zinatakiwa ziteketezwe. Kimsingi tunapokuwa na bidhaa kwa mfano tuna vitu ambavyo vinatakiwa vioke, viende nchi zingine kwa ajili ya kuharibiwa, ni lazima anayehusika atapeleka maombi yake Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Rais tutakwenda kukagua na ikijiridhisha ndyo inaweza ikatoa kibali ya hizo bidhaa kuweza kusafirishwa kwa ajili ya kuteketezwa, ama ndani ya nchi au nje ya nchi kwa kushirikiana na taasisi zingine, ikiwemo hiyo aliyoisema ya mambo ya vyakula.

MHE. SELEMAN S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, haja yangu ni kwamba, Serikali sasa iweze kujielekeza, maana yake hadi hivi sasa huwezi ukasema kwamba tuna site kadhaa, site 'x' ambazo bidhaa hizi tunasema Watanzania tunajua pale zinatekelezwa. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba, Serikali iweze kujipanga katika eneo hilo kwa sababu tukijua sasa hivi bidhaa nydingi zinaingia, kwa hiyo tuangalie ni jinsi gani bidhaa ambazo zitakuwa zimepigwa marufuku kutumika, basi tuwe na eneo maalum la kuziteketeza. Najua mkakati huo upo lakini ni lazima tuwe na site maalum, tunajua kwamba site hii ni site maalum kwa ajili ya uteketezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri kwa kumalizia.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, tutalizingatia na nashukuru kwa mapendekezo yake.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tuhamie upande wa CUF Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa!

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri kuhusu Mfuko wa Jimbo bado nina mashaka ambayo nataka atuweke sawa, kwamba hizi bilioni moja, milioni mia mbili arobaini na tatu, Majimbo hamsini ya Zanzibar ni wastani wa shilingi 24,800,000. Kwa mujibu wa Mfuko ule wa Jimbo kutegemea na poverty index ya Jimbo, ukubwa wa Jimbo, hatupitani sana, tupo 24,800,000, wengine 24,700,000, hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujaibadilisha sheria mpaka pesa ikiingia katika Mfuko wa Jimbo iliwa laki tano inatoka, kwa Majimbo hamsini, milioni 25 imetoweka. Tukalalamika tukabadilisha sheria. Sasa hivi katika fedha ile ikitumwa kama miaka miwili, mitatu sasa hivi inaingia sh. 24,300,000 au 24,400,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa laki nne hazimo kila Jimbo, Mheshimiwa Waziri kama katika Jimbo lake zinaingia kamili, milioni ishirini na nne na laki nane, ni ye ye tu labda wanamheshimu kwa kuwa ni Waziri, lakini zikatazamwe, CAG aende akaangalie, akaunti zote za NMB pesa zinapofikia ziliwa takribani milioni ishirini na nne na laki nne. Laki nne kwa Majimbo hamsini takribani milioni ishirini zinatoweka, hizo ni chaji gani za kibenki ziweze kupoteza pesa nydingi sana kama hivyo, ambazo zinapotea kila Jimbo milioni 20 takribani hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Ofisi ya Makamu wa Rais, Zanzibar inafanya shughuli gani ambapo kama hizi pesa zinakuja kwako Ofisi ya Makamu wa Rais na Waziri wa Muungano anahusika, kwa nini zisishughulikiwe moja kwa moja pale kwenda Majimboni, zipite katika process ambapo zinapungua kiasi kama hicho. Hizi instrument ambazo unasema huna, upate instrument gani tena Mheshimiwa Waziri, hebu fafanua hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, mambo mawili tunaruhusiwa, siku hizi yamepunguzwa yalikuwa matatu.

MWENYEKITI: Ni jambo moja mahsus.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Daah.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu wakati natoa ufanuzi wa hoja kwamba mimi kwangu sioni kama kuna makato makubwa kiasi hicho na sijapata malalamiko haya kutoka Majimbo mengi, lalamiko ndiyo nalisikia leo kwako. Kama nilivyosema kwamba ofisi inachukua, tutakwenda ndani tuangalie kuna sababu gani inayofanya pesa hizo zikatwe na halafu tutalifanya kazi. Kwa hiyo, sina lingine sasa hivi la kusema isipokuwa kwenda kulifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Ofisi ya Makamu wa Rais, Kikatiba siruhusiwi kufanya kazi na taasisi ya SMZ moja kwa moja. Masuala ya fedha ni lazima kwanza tuyaingize Hazina, halafu Hazina ndiyo inapeleka kwenye sekta zinazohusika. Nitakapopeleka moja kwa moja ina maana tatizo likitokea sitakuwa na wa kumuuliza ndani ya SMZ, itabidi niulizwe mimi ambaye nimefanya hiyo kazi ambayo siyo yangu. Kama kule kuna Hazina inabidi fedha zote zipelekwe Hazina na Hazina ndiyo wafanye mgawo. Ahsante.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ni hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopo Zanzibar inafanya kazi zipi ambazo ikiwa wewe unasema haiwezekani moja kwa moja? Vile vile kama kuhusu utaratibu mwengine, CAG wa Jamhuri ya Muungano amempa power CAG wa Zanzibar kukagua hizi. Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano Zanzibar inafanya kazi zipi na sisi Wabunge tunaweza tukaitumia kwa shughuli gani. Tufafanulie basi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MUUNGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja inakua, lakini niseme kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopo Zanzibar ina sehemu mbili, ina sehemu ya private ofisi, huduma za Makamu wa Rais, lakini pia ina sehemu inayowakilisha Ofisi ya Makamu wa Rais, inafanya kazi za uratibu na ku-feed Makao Makuu ya Dar es Salaam. Ahsante.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nahitaji nipate maelezo ya kina na nisiporidhika nakusudia kuondoka na shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria ambayo imepitishwa na Bunge lako Tukufu, kila mwaka Taifa linahitaji lipate taarifa ya mazingira. Taarifa ya mwisho ilitolewa mwaka 2008, tangu mwaka 2008 taarifa ya mazingira haikutolewa, imekuja kutolewa mwaka huu na kufanya hivyo ni kuvunja sheria ambayo sisi wenywewe Wabunge tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nahitaji maelezo ya kina, kwa nini kwenye hiyo miaka mingine taarifa zilikuwa hazijatolewa na ukizingatia uchafuzi wa mazingira unaendelea kukua kwa kasi, ukataji miti na mabadiliko ya tabianchi. Ni sababu gani ambayo imepelekea Wizara hii imeshindwa kutii sheria ambayo wao wanapaswa kuisimamia. Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Bulaya kwa sababu suala hili ameli-raise hata asubuhi wakati wa maswali, lakini sababu kubwa naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kweli kabisa taarifa ya kwanza ya ripoti ya mazingira ilitolewa mwaka 2008 na Sheria ya Mazingira inaanisha kwamba, ripoti itolewe kila baada ya miaka miwili na siyo mwaka mmoja. Ripoti ya pili imetolewa mwaka huu mwezi wa Nne ndiyo imezinduliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais katika sherehe ambazo Mheshimiwa Bulaya alihudhuria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zilizopelekea ripoti kuchelewa kutolewa ndani ya miaka sita, kwanza ni ufinyu wa fedha, kwa sababu kuandaa ripoti hii kunahitaji fedha na kuandaa ripoti hii maana yake unataka kuonesha tathmini au hali ya mazingira katika sekta zote. Uende Sekta za Madini, Maji, Misitu, mambo ya Taka za Kieletroniki na kila eneo ikiwemo mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, kutohana na ufinyu wa fedha ilishindwa kufanyika mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ambayo tunadhani ni ya kitalaam ni kwamba, kwa jinsi nilivyosema kwamba ina-cover maeneo yote, tunahisi siyo rahisi kutengeneza document ndani ya miaka miwili itakayoonesha uhalisia wa mabadiliko ya tabianchi au hali ya uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali ndani ya miaka miwili. Kwa hiyo, tumeliona hili na tumeanza majadiliano, tunaangalia ni namna gani nzuri zaidi bila kuathiri sheria lakini tuendelee kutoa taarifa ambazo ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mapendeleko tuliyonayo ni kwamba, pengine ndani ya miaka hii miwili tuwe tunachagua sekta, tusizichukue zote, tuchukue sekta baadhi mbili au tatu, lakini tuzifanyie ripoti nzuri ambayo inaweza ikatoka timely ndani ya miaka miwili na hivyo baada ya miaka kama mitano hivi mnakuwa na taarifa za kila sekta ambazo mmeziunganisha kwenye miaka miwili.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, najua uadilifu wake na uchapakazi wake na hayo ndiyo ambayo alitakiwa kunijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia unyeti na umuhimu wa Wizara hii na tunapoiomba Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha katika Wizara hii, kuna mambo ya msingi. Kwenye nchi za wenzetu mazingira taarifa yao wanatoa kila mwaka, lakini Wizara ya Mazingira wanaipa kipaumbele. Huwezi kuzungumzia Miundombinu bila kuzungumzia mazingira, huwezi kuzungumzia kupangwa kwa Miji bila kuzungumzia mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyokwambia hiyo ripoti yenye mpaka wafadhili wametupa fedha, ni aibu! Tuwaombe hela kwenye barabara, tuwaombe hela kwenye maji, mpaka kuandaa ripoti yetu ambazo tunatumia brain za watalaam. Ndiyo maana tunasema ni wakati muafaka wa Serikali kutenga fedha za ndani. Acha basi katika hayo mambo mengine tuwategemee, kuandaa ripoti na mabadiliko ya tabianchi yanatokea kila mara. Haya, tumeshindwa kuandaa ripoti watu anaendelea kujenga tu hovyo, watu wanaendelea kuchafua fukwe, takataka kila kona. Sasa watuambie hivi hii ni Wizara au ni Idara, kwa nini hamuipi pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko tunakokwenda hali itakuwa mbaya zaidi, nahitaji commitment ya Serikali tena hapa Waziri wa Fedha hayupo, tumezungumzia mambo mengi kuhusiana na kuipa fedha hii Wizara. Kutenga Fungu linalokwenda Zanzibar na Fungu la Mazingira, lakini wanaficha, wanaweka pamoja, mwisho wa siku upande wa mazingira hakuna pesa. Tunaipenda nchi hii na tunapenda mazingira haya yawe safi,

Mheshimiwa Mwenyekiti, naihitaji commitment ya Serikali kwa nini wasitenge fedha za ndani ili ripoti ya mazingira itoke kwa wakati, tusivunje sheria tunazozitunga. Tusimamie kwa maslahi ya mazingira ya nchi yetu na Taifa letu. Commitment ya Serikali naihitaji, kama siyo hivyo naondoa shilingi na Wabunge wachangie.

MWENYEKITI: Napata tabu kidogo Mheshimiwa Ester kwa sababu sidhani kama swali lako Mheshimiwa Waziri anaweza akalitolea ufanuzi, kwa sababu sisi Wabunge ndiyo tunaogawa rasilimali pesa. Kati ya sasa na atakaposoma Bajeti Waziri wa Fedha, tunayo nafasi hivi sasa kwa Mbunge mmoja mmoja kupitia Kamati zetu kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti, sisi tukaibeba hoja yako ambayo ni muhimu sana na ni nzuri sana kwa umoja wetu, tukaibana Serikali ili kusudi bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iweze kuangaliwa vizuri zaidi.

Nakubaliana kabisa na hoja yako, lakini ninachosema ni kwamba, ni jambo ambalo linatakiwa approach yake iwe na upana wetu sisi kwa pamoja, kwa kushirikiana, kuliko tukisema Mheshimiwa Waziri ajibu hili, itakuwa ni ngumu kidogo.

Mheshimiwa Ester nimekuona umesimama.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachofanya, natimiza wajibu wangu kama Mbunge na kama wewe mwenyewe ulishawahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, malalamiko haya ya hii Wizara kutengewa fedha na tunayosema hapa pia ni kwa faida yao wao na uchapakazi wao kuwafanya waendelee kuchapa kazi vizuri. Hapo pia tuna Waziri Senior, alichukue hili aende akaongee na Mawaziri wanaohusika ambaa ni Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona kwenye REA, hivi karibuni tumeona kwenye TEA, tunapitisha sheria fedha hazitengwi. Hatuwezi kukubali hii trend iendelee kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Ndiyo maana nasema kuna Waziri senior hapo, aichukue hiyo, wajipange upya, waliangalie hilo. Siwezi nikakubali kama sijapata majibu.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ester. Mheshimiwa Samuel Sitta naona hili linakulenga, karibu!

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru sana Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kuuliza hili. Ninachoweza kusema kwa sasa ni kwamba, malalamiko haya na hali hii anayoieleza Mheshimiwa Mbunge tumepokea. Cha kufanya hapa ni kwamba, tunahitaji muda kwa kweli, kwa sababu zipo taasisi mbalimbali zinahusiana kwa pamoja katika suala hili moja. Nyingine ni upande wa Ujenzi, nyingine ni upande wa Mazingira na pia sisi Uchukuzi upande wa Sera ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kumwahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tutafanya kila liwezekanalo tuje na jibu ambalo linatosheleza ndani ya muda mfupi na kwa vyovoyote vile siyo zaidi ya mwezi mmoja. Ningombaa Mheshimiwa Ester atupe nafasi hiyo ili tushauriane kwa pamoja ndani ya Serikali na kuweza kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tuendelee na Mheshimiwa Esther Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nakusudia kuzungumzia adha ya mazingira kwenye Mgodi wa Nyamongo na kama sijaridhika na majibu ya Waziri nitakusudia kutoa shilingi hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri anajibu alizungumzia kuhusu short term solution ya uchafuzi wa maji ya Mto Tigite. Kiukweli kuanzia mwaka 2011, Dkt. Huvisa akiwa Mazingira walisema kwamba wamechimba visima Acacia au Barrick kipindi kile, wamechimba visima vitano kila kijiji, lakini hadi leo hamna hata kisima kimaja. Wanachofanya wanagawa maji kwa kutumia gari, nafikiri na Mheshimiwa Naibu Waziri anajua kipindi hicho alikuwa Nishati na Madini kitu ambacho hakikidhi haja, kuendelea kuwepo na hiyo pollution ya watu kuendelea kuathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ambacho nashikia shilingi, mgodi unafanya kazi kabla ya kuhamisha watu wako ndani ya mita mia mbili, wakifanya zile blustering au kulipua miamba, wale Watanzania amba wapo ndani ya mita mia mbili na nimelizungumzia hili mara kwa mara wanaopata athari, siyo tu ya kelele, nyumba zao zingine zinabomoka, zingine zinapata nyufa, akinamama wajawazito mimba zao zimeharibika, wanapata athari ya vumbi na matatizo mengine mengi. Mgodi unafanya kazi wakati kuna watu wapo mita kumi, vitongoji vya Mjini Kati, Nyabikondo, Nyabichune na vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea Bunge lililopita mkasema mtalifanyia utatuzi, sasa nilitaka nijue tu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther nikuweke sawa kidogo tu, halafu utaendelea.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Sawa.

MWENYEKITI: Naomba ukae kidogo.

Katika kipindi hiki cha Mshahara wa Waziri tunakitumia zaidi kuzungumzia masuala ya kisera, tuki-deal na matukio itakuwa tabu kidogo. Kwa hiyo, naomba tu katika kukuweka sawa, ni sera ipi hasa unayoizungumzia ili Mheshimiwa Waziri aweze kuifafanua.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera yangu ni Sera ya Ustawi wa Jamii, sidhani kama ni dhahiri Serikali kuwaacha wananchi wake wanateseka, wanapata madhila, matatizo! Kwa sababu, Wizara ya Mazingira inatakiwa isimamie kuhakikisha maeneo yale, kupitia NEMC, kabla ya mgodi haujaanza ku-operate, wale watu wahakikishe wamehamishwa. Nafikiri hilo ni la kisera kabisa, sio Mgodi wa North Mara tu na migodi mingine, hata Kambi Rasmi ya Upinzani imeainisha! (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, iwapo migodi yote kabla hawa jafanya uchimbaji wanaondoa wale watu, ili wasiathirike na mazingira, nimeainisha! Kama ni fidia, walipwe wale watu waondolewe ndiyo mgodi uendelee. Sasa nahitaji kupata commitment ya Serikali kwamba, ule mgodi utaacha kwanza mpaka uwahamishe wale Watanzania amba wako ndani ya mita 200, wanaathirika! (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kwa hiyo, hoja yako ni kuhamisha wananchi amba wako karibu na migodi, ili wasiathirike na athari zinazotokana na shughuli za uchimbaji kwa maana ya migodi yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ufanuzi!

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge na Mbunge mwenzake wa Tarime kwa kuleta hoja hii mara nyingine. Ni kweli kwamba, matatizo ya mazingira kwenye Mgodi wa North Mara ni ya muda

mrefu na kwenye majibu ya hoja nilipokuwa nikieleza, nilieleza kihistoria matatizo ya Mto Tigite na namna hatua Serikali ilizochukua kufanya study ya kuona uchafuzi ule wa mazingira unasabishwa na nini hasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza hapa kwamba, unasababishwa na mchanganyiko wa kikemia wa mawe ambayo yanatoka chini baada ya kuchimba dhahabu, baada ya kukaa muda mrefu yakapigwa jua, yakanyeshewa mvua, yakasababisha tope ambalo lilienda kuleta athari kwenye mto ule. Serikali ilichukua hatua na hatua zile zilisaidia mto ule kurudi katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilieleza kwamba, hatua ya muda mrefu ni kuweka mradi wa maji kutoka Mto Mara na kusambaza kwenye maeneo ya Tarime kwa kuwa, kiasili ardhi ya Tarime imeonesha kisayansi baada ya kufanya utafiti kwamba, ina aina za kemikali zikichanganyika na maji zinasababisha kutengeneza asidi ambayo inakuwa sio nzuri kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili, Sheria ziko wazi na mgodi ili upewe leseni ya kuchimba, cha kwanza ni lazima upate pia, kibali cha mazingira. Pia, wanaleta na plan yao namna walivyo-design mgodi ikiwemo na hatua zote za kudhibiti mazingira. Kwa utaratibu siku ya kwanza mgodi unapoanza ndipo siku hiyo hiyo wanaanza na plan ya ufungaji wa mgodi, kwa maana ya kuangalia taratibu zote za maeneo ambayo hayatumiki na kuweza kuyarudisha katika hali ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kesi ya Nyamongo ni *special case* na wengi wetu tunafahamu kwamba, changamoto iliyoko Nyamongo ambayo mgodi umeshindwa kulipa kwa mujibu wa Sheria mpaka leo, kwa baadhi ya maeneo ambayo waliyafanya tathmini, ni kuwepo kwa majengo mapya yaliyojengwa katika eneo karibu kabisa na mgodi. Kwa hivyo, Wizara ya Nishati na Madini wanaendelea na majadiliano kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi pamoja na mgodi, ili kupata suluhu ya kudumu ya wananchi walioko katika eneo karibu na mgodi.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kweli, nitakusudia kutoa shilingi ili na Wabunge wengine wachangie. Nina imani hata Wabunge wa Kamati ya Mazingira walikwenda Nyamongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachorudia kusema na Naibu Waziri amesema hapa kwamba, NEMC wanatoa kibali, ina maana mgodi hauruhusiwi ku-operate kama haujahamisha hao watu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa tuangalie, kwa hiyo, kama Waziri anavyosema kwamba, kuna watu wengine majengo yamekuja mapya! Kitu ambacho, maana nimeshakwenda mgodini, nimeongea na wenge mgodi, nimeongea na wananchi! Kitu ambacho zaidi ya asilimia zaidi ya 90 siyo kweli. Kuna watu walifanyiwa tathmini mpaka leo haujahamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa iwapo, kama tukitembelea scenario yake hiyo hiyo kwamba, watu wamegoma. Kwa hiyo, kama watu wakigoma mgodi unaruhusiwa kufanya kazi kabla haujahamisha hao watu amba wamegoma, ina maana Serikali haithamini afya au uhai wa wananchi wake inathamini vitu vingine ambavyo sitaki kuvitaja hapa! Ndiyo mnataka mtuaminishe hivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ninachotaka kusema, nipate *commitment*, unless watwambie kwamba, NEMC walikuwa corrupted wakaruhusu mgodi ufanye kazi ilhali na watu wako pale kwenye mgodi. Kinyume cha hapo, Serikali itoe *commitment* na itwambie hapa

maana wamekuwa wakisema watashughulikia ndani ya muda mfupi, lakini ndugu zetu wale wanaendelea kuteseka! Itoe commitment mgodi ule wa North Mara ambaa umesema ni special case! Mshirikiane Wizara ya Ardhi, Nishati na Madini na nyie Mazingira, ndani ya muda mfupi. Hatuwezi kuendelea kuvumilia, ndugu zetu kule abortion zinaendelea na watu waathirika kupata vifua vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya muda mfupi, mgodi usitishe kwanza operation mtatue hilo tatizo la wananchi mpaka wahame kwenye hilo eneo, ili mwendelee na operation. Mji-commit ni muda gani mtatumia kuhakikisha kwamba, hilo mnatatua. Mwende site, mkae na wananchi, mkae na mgodi na nyie muangalie tatizo ni lipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani! Mpitie, kama walishafanya tathmini wana majina kamili ya watu waliowafanya tathmini, kama wameongezeka wengine watajua kabisa, tathmini imefanyika 2012, wewe umejenga 2014 ina maana ni disqualified! Hizo nyingine ni story, watoe commitment! Siwezi kukaa nikavumilia ndugu zangu wanaendelea kufa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa shilingi kama sijaridhika na nimetoa shilingi.

MWENYEKITI: Swali la Mheshimiwa Esther kabla halijajibiwa linataka kidogo ufanuzi na uelewa kwa watu ambaa tuko mbali kidogo na suala hili.

Mheshimiwa Machali, kaa kidogo!

Kwamba, mwekezaji ana eneo sawasawa na ukumbi wetu huu, ndilo eneo ambalo ana mandate nalo. Hivi yeye ana mamlaka gani na mtu ambaye amejenga kibanda hapo mita tano kutoka kwenye eneo ambalo yeye ndiyo amepewa? Yaani anaweza akamhamisha? Wakati yeye yule mtu yuko nje ya eneo ambalo yeye kapewa ambalo ndiyo anawekeza? Maana ndio swali lake la kuhusisha mgodi kuhamisha majirani, lakini kwa sababu, sijui vizuri, nilikuwa najiuliza tu! Tuache Waziri alifafanue!

Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Serikali na mimi binafsi sifurahii wananchi wa Tarime kupata madhara ya kiafya kutokana na shughuli za mgodi, lakini jambo hili na Mheshimiwa Mbunge anafahamu kabisa, kwanza suala la fidia liko chini ya Wizara ya Ardhi. Wao ndiyo wanaofanya tathmini ya ardhi na ndiyo ambaa wanasiimamia fidia kwa mujibu wa Sera ya Ardhi pamoja na Sheria zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Wizara ya Ardhi, mgodi na wananchi, kwa maana ya kuitia uwakilishi wao wa Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Tarime pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Tarime ndiyo ambaa wanapaswa kukaa na kujadili namna ya kutatua tatizo hilo kwa sababu, tatizo hilo halitatuliwi na upande mmoja tu wa Serikali. Anayepaswa kulipa fidia ile ni mgodi chini ya Sheria ya Ardhi na sisi wajibu wetu ni kuangalia, je, shughuli zinaendeshwa na masuala ya mazingira yanasiimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo linalozungumziwa ni eneo ambalo liko ndani ya leseni na wananchi hawa walikuwa wamefanyiwa tathmini na walistahili kwa mujibu wa Sheria kulipwa fidia. Sasa sababu gani zinafanya wasipokee fidia au sababu gani zinafanya mpaka leo

hawajalipwa, hizo ndiyo sababu ambazo Kamati Maalum hiyo, ndiyo inalifanyia kazi kupitia wadau wote husika, ili kupata suluhi ya kudumu.

MWENYEKITI: Aah! Kwa kuwa, hawa watu wako ndani ya leseni! Sasa hapo nimelielewa kwamba, wako ndani ya eneo ambalo ndiyo la mgodi kwa namna moja au nyngine.

Haya, nilikuona Mheshimiwa Susan!

MHE. SUZAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni mwenyekiti saa hizi eeh?

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante...

MWENYEKITI: Umechelewa kuja, ndio maana!

MHE. LIMBWENI A. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana! (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili, Mazingira na Ardhi na ni kweli, athari zipo kwa wananchi na naungana na Mheshimiwa Esther Matiko kwamba, anachokiongelea ni kweli. Ni muhimu Serikali ikajitathmini na kuwakomboa wananchi, yaani kuwanusuru wananchi wanaozunguka kwenye migodi, hususan, mgodi amba o nautambua wa Nyamongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea, Serikali wanachelewesha. Kwa mfano, ule Mgodi wa Nyamongo, pamoja na wengine hawajalipwa waliofanyiwa tathmini, lakini kuna eneo ambalo inaonekana mgodi wanataka kulichukua, lakini bado liko mikononi mwa wananchi. Kwa hiyo, ndiyo hilo wanalo sema kwamba, wananchi wanaendeleza! Sasa kama mnaona wale wanaliendeza na wao wanataka kulichukua na kama kweli wana nia ya kulichukua lile eneo kwa nini sasa wasilipe fidia wale wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili tatizo wako ndani ya leseni, lipo, lakini vile vile nje ya leseni kuna wananchi wanajenga nyumba kwa kasi kubwa kwa sababu, ni maeneo yao. Kwa hiyo, wakimaliza hili, linarukia lile lingine!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vema Serikali sasa inapokwenda kurasimisha migodi ikachukua Sheria zote za Mazingira, wakatathminia watu, wakalipwa, wakachukua eneo kubwa, ili wananchi wakae mbali na eneo la mgodi. Kwa kweli, hali za wananchi ni tete, hali ni mbaya! Ni vema sasa Serikali ikamjibu vizuri Mheshimiwa Esther Matiko kuonesha kwamba, wananchi wanaozunguka katika migodi wana athari kubwa za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni suala tete sana ndani ya nchi yetu na ndiyo maana hata Mheshimiwa Ester Bulaya amesema kwa uchungu mkubwa kwamba, hii mazingira hawapewi chochote! Hawana hata uwezo pengine wa kwenda kuzungukia kwenye hiyo migodi na kuangalia athari za mazingira! Kwa hiyo, hili ni angamizo la Kitaifa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunachekekacheka, lakini hii Tanzania itakuja kupotea kwa sababu ya kudharau suala la mazingira. Kwa hiyo, ninachokiomba, hoja ya Mheshimiwa Esther Matiko iko palepale na namuunga mkono, bora atoe shilingi au Serikali ilete Kauli mahususi ni namna gani watashughulikia haya matatizo ya wananchi na siyo kuweka mpaka hili Bunge liishe.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naunga hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Esther Matiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi swali la msingi ambalo pengine tunapaswa kujuliza Wabunge ni suala la *time frame*. Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza hapa kwamba, kuna Kamati ambayo iliundwa kwa ajili ya kushughulikia suala hilo Serikalini. Sasa Mheshimiwa Mbunge anachohojii anataka kujua ni lini sasa Kamati hiyo itakamilisha kazi, ili kusudi watu hawa waweze kuondokana na athari ambazo zinatokana na suala la *blustering* kwenye maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ambao ulikuwa umeutumia kwamba, inawezekana yule investor amepewa eneo fulani, halafu watu wako nje ya lile eneo, watu wa NEMC walipaswa kufanya *environmental impact assessment* kutokana na shughuli ambazo zitakuwa zinafanywa na wachimbaji wa madini! Walielewa bayana kwa sababu, kuna *environmental engineers*! Walielewa kwamba, pengine suala la ulipuaji wa milipuko ambayo itatumika katika kuhakikisha kwamba, wanafikia malengo yao, inaweza ikaja ikaleta athari nje ya eneo lile. Sasa ndiyo athari hizi ambazo tunazisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa hiyo, itamke kwamba, Kamati hiyo itakamilisha lini? Hatuwezi tuka-rely kwenye maelezo kwamba, inafanya kazi, inafanya kazi! Mwisho itapita hata miaka mitano mingine majibu yatakuwa ni haya! Kwa hiyo, Serikali itueleze kwamba, kazi itakamilika wakati gani?

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira na niliwahi kutembelea mgodi huu, nafahamu kiasi. Nakumbuka kuiona *EIA Report*, ipo, lakini *EIA Report* hiyo ni kubwa kuliko hii *Volume II* na *Volume IV* kwa pamoja! (Makofii)

Mheshimiwa Ester Bulaya!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhii, Maliasili na Mazingira na nilikwenda katika hilo eneo. Naelewa concern ya Mheshimiwa Esther Matiko pamoja na kaka yangu Nyambari na yeze amelizungumzia kwa uchungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimemsikiliza Mheshimiwa Masele, majibu yake ni mazuri na nikiri kwamba, Serikali katika maeneo mengine imefanya vizuri. Tumekwenda pia, Nzega tumeona walivyoweza kufanya vizuri katika suala zima la mazingira kwenye migodi na kuhakikisha wale wananchi ambao wanazunguka ile migodi basi hali zao zinakuwa salama na hawaathiriki katika namna moja au nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kikubwa hapa, tunajua Serikali ina nia njema, ndiyo maana ilikwenda kufanya tathmini, lakini hata Kamati tulisisitiza kwamba, lile zoezi la kulipwa fidia lifanywe haraka kwa sababu, kule kuna baadhi ya wananchi wanaendelea kujenga, wanaita tegesha. Sasa tungependia tu *commitment* ya Serikali, hiyo Kamati itamaliza lini ili kuhakikisha wale wananchi wa Tarime wanakuwa katika maeneo mazuri na vile vile uwekezaji unaendelea kwa sababu, hatuwezi kukataa Mwekezaji au kusema mgodi ufungwe kwa sababu, pia, uwekezaji una manufaa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa ili tutengeneze mazingira ya wote kuwa salama, Mwekezaji kuwa salama na wananchi kuwa salama, tuitake Serikali ituhakikishie lini hiyo Kamati

inamaliza kazi, wanaostahili kulipwa walipwe waondoke ili mgodi uendelee na shughuli zake na wale wananchi wasiendelee kuathirika. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Asante sana.

Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi!

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru michango ya Waheshimiwa Wabunge; Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Susan pamoja na Mheshimiwa Ester Bulaya kwenye hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi hapa ni ulipwaji wa fidia kwa wananchi walioko kwenye eneo la leseni ya North Mara, Acacia. Kama nilivyoeleza, wajibu wetu sisi, kama Ofisi ya Makamu wa Rais, ni kusimamia Sera yetu ya Mazingira pamoja na Sheria za Mazingira. Ripoti ya Tathmini ya Athari za Mazingira ilifanyika, kama ulivyokiri wewe mwenyewe na ilifanyika baada ya kuwa mgodi ule ulikwishakuwa umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowea kakisema hapa na narudia tena North Mara ni special case na Mheshimiwa Esther Matiko anafahamu kwa kina kwa nini nasema hivyo. Tukisema hapa tu-rush kutoa majibu, kusema kweli, hayawezi kuwa suluhu ya tatizo la pale! Tatizo la pale litasuluhishwa kwa ku-engage watu wote wanaohusika wakiwemo Viongozi wa Halmashauri ya Tarime, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tarime, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Ardhi na sisi kama wadau wa mazingira, kwa pamoja ndipo suluhu inaweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, wako wananchi waliokwishafanyiwa tathmini, lakini hawakuchukua malipo yao. Wapo wananchi waliofanyiwa tathmini, walipokea cheki zao za malipo; kwa hiyo, kwanza kuna mgogoro wa kukubaliana thamani halisi ya malipo hayo na kuna migogoro mingine ambayo nikisema niieleze yote hapa, muda hauwezi kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema kwamba, sisi hatuna mandate ya kuisemea Kamati ile, lakini ujumbe huu tumeupokea na tutawasiliana na wenzetu wa Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Ardhi pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Tarime pamoja na Acacia wenyewe, ili kuona jambo hili wanilikamilisha kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowea kusema tu kwamba, wote pande zote linawakera. Hakuna anayetaka jambo hilo liendelee kuwepo hivyo lilivyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther, rudisha shilingi!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, siirudishi shilingi yangu kwa nia njema kabisa kwa sababu gani? Mheshimiwa Naibu Waziri anasema anatambua Kamati ipo inayohusisha watu wa Ardhi na Waziri wa Ardhi yuko hapa, Waziri wa Nishati, Mazingira, Acacia na Mkuu wa Wilaya, ambapo natambua tarehe 4 baada ya wale wananchi kuathirika na ile blustering iliyotokea tarehe 2, Naibu Waziri Kitwanga alikwenda! Kilichoijiri, mtakuwa mnaelewa kwenye Serikali. Ndiyo maana nasema, ili hiki kitu kiwe serious na watambue kwamba, wale wananchi kule wanaathirika, Kamati mtwambie time frame ni lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama mnavyosema mgodi usimame! Una maeneo mengi ya ku-operate siyo kwamba, unasimama moja kwa moja! Hicho ni kieneo nilichokitaja, hivi vitongoji unavifahamu vizuri. Katika Vitongoji vine, hili ni eneo mojawapo. Kule kuna pit nyingi

za kuendelea kuchimba. Wakati Kamati inaendelea, ile sehemu husika wasimame kwanza, ili wamalize wawafidie hawa Watanzania waondoke!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema eti watu wamegoma, ndio hapo inaonesha ulegelege wa Serikali! Kama watu wamefanyiwa tathmini na miltuma task force ikaenda Tarime, maana mwanzoni ilikuwa hakuna task force ya kusimamia tathmini! Mmetuma task force, halafu leo mnatwambia Bunge kwamba, watu wamegoma kuhama, ila mnaona ni sawa mgodi uendelee kufanya kazi, wananchi waendelee kuathirika na kufa! Wanakufa leo, wengine kesho, wengine miaka mitano ijayo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupeni *time frame*! Watupe *time frame* kwamba, Kamati itamaliza shughuli hii na kukaa wamekaa wote na wananchi wapo, ndani ya mwezi au ndani ya wiki mbili, wananchi watakuwa wamelipwa! Nilivyokwenda Acacia walisema tayari wana hela! Kama Acacia wana hela, kigugumizi cha nini kuwalipa hawa watu ambao ndio wana uhalali, wameshafanyiwa tathmini 2011, 2012, 2013, kuacha hawa ambao mnasema wamekuja baadaye kujenga! Wawalipe hela waondoke mgodi u-operate!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe sikatai mgodi usifanye kazi kule! Kuweni serious, Acacia wana hela, kwa nini msisimamie wale watu walipwe? Mfuate Sheria, wananchi wale walipwe! Tuondokane na hii kesi! Maana tumezungumza tangu miaka mitano sasa!

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Esther. Hatua tuliyofikia ni ya kupiga kura. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba ushirikiano wenu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mbassa, hayupo. Wa mwisho ni Mheshimiwa Mchungaji Natse!

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hotuba yangu nilizingumzia jambo la ujenzi holela na maelezo mazuri aliyyoatoa Waziri nataka kupata ufanuzi zaidi katika jambo la ujenzi holela ambao unaenea kila mahali. Sheria iko wazi, kwenye kingo za mito mita 60, hata mia kwenye vyanzo vya maji na ufukweni kule. Nataka kufahamu kwa nini Serikali inapata kigugumizi kwa watu hawa kujenga ilhali ikifahamika kwamba *environment impact assessment* lazima ifanyike, itolewe cheti, baadaye ujenzi uanze.

Sasa kama ambavyo taarifa zipo nyumba zimejengwa ufukweni kule na sasa chache zimebomolewa, nataka kufahamu sheria zipo kwa nini hali inafikia hapo na baadaye watu kupata hasara ya kuvunjiwa nyumba zao na Serikali ipo? Nimeeleza kwenye taarifa yangu, watu wa ardhi wanatoa vibali, Serikali inatoa vibali, ruhusa ya kupima viwanja mpaka dakika za mwisho. Nataka maelezo ya kina kwa nini inatokea mpaka hali hiyo ya nyumba zinazovunjwa sasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba suala hilo ni kweli amelieleza kwenye hotuba yake na sasa analikumbushia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na yeye kwamba ni kweli upo uvunjifu wa taratibu na sheria katika maeneo mbalimbali na wanaofanya ni binadamu, wako ambao wanakwenda

kwenye maeneo ambayo yako wazi, wanachukua vifusi na kufukia ili wapate viwanja vyatubu. Wako ambao wanachukua vifusi na kufukia kwenye maeneo ya mito kama Mbezi, maeneo ya Ununio kule tumegundua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuliona hili, watu wangu wa NEMC ambao kazi yao ni kusimamia Sheria ya Mazingira walipoligundua ikaonekana kwamba upo udanganyifu wa watu wakidai kwamba wana vibali maalum. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu akaunda Kamati ambayo ilitakiwa ichunguze kwanza i-identify hayo maeneo na baada ya kupata hayo maeneo ichunguze uhalali wa vibali walivyovifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili limefanywa kwa ushirikiano na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri kama na TAMISEMI, wenzetu wa mipango miji ambao wanagawa vile viwanja. Baada ya kugudua wamebaini zaidi ya nyumba 460 ambazo ziko kwenye maeneo ambayo hayaruhusiwi. Nimeeleza kwamba hatua zimeanza kuchuliwa pale ambapo nyumba zile zinabainika kwamba document zake siyo sahihi basi zile zinavunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu kwa Watanzania usijenge nyumba ukisubiri uvunjiwe, unapata hasara. Kwa kweli kwenye eneo hili kuna corruption kubwa sana kwa sababu hata tunapokwenda kuvunja zile nyumba tunakwenda na waandishi wa habari, bado hata zile taarifa haziwafiki wananchi, nyumba zimebomolewa watu hawawezi kuona kinachoendelea.

Kwa hiyo, ni eneo ambalo tunataka tuwaombe Watanzania wote kwamba, usipoteze fedha zako kujenga kwenye eneo ambalo haliruhusiwi, kwa sababu kama haivunjwi leo, ipo siku itavunjwa hata kama kesi yako imekwenda Mahakamani, kuna siku ule mhimili utamaliza ile kesi na nyumba yako itavunjwa tu.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuweka mambo sawa. Nashukuru Waziri amekiri jambo la corruption katika mazingira hayo. Kwangu kwa sababu sheria ipo na tunakiri utawala wa sheria, mlipaswa kuvunja tu, maana unaangalia tu mita 60 pale, mita mia vunja tu, ye ye ndiye aende Mahakamani na siyo Serikali. Vunja nyumba, halafu ye ye akimbie Mahakamani tupambane naye, lakini kwa approach ambayo mnaifanya sasa mnadhalisha rushwa, ufisadi na kila aina ya uchafu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba commitment ya Serikali, maana hata hizo mlizovunja 27 zingine bado zipo, hamuoni kwamba ni uonevu kwa kuwavunja wengine na kuwaacha wengine? Kwa hiyo, naomba commitment ya Serikali, sheria zipo, sheria ni msumeno vunja wao waende Mahakamani.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri commitment!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mchungaji Natse kwamba tumekwishaanza kufanya kazi na nimewaaagiza NEMC kwamba zoezi hili liharakishwe na ndiyo maana mwezi Machi na Aprili tumevunja nyumba 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba hata wale waliokimbilia Mahakamani ni haki yao na hatuwezi kuvunja sheria, mtu amekwenda Mahakamani unakwenda kuvunja nyumba hapana. Tunaamini ule mhimili utatoa hukumu yake na mwisho majibu yakipatikana, kama inaonekana amevunja sheria, tutavunja hiyo nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotoa ushauri kwa Watanzania, tusiende huko, maeneo ambayo yametengwa tusianze kujenga tushirikiane Manispaa za Miji, wenzetu wa Ardhi kwa pamoja, kuona kwamba tunachokifanya ni kwa uendelevu wa nchi yetu.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Machali malizia, kutoka NCCR!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naamini kabisa kwamba ni Sera ya Serikali kuhakikisha kwamba mazingira yanatunzwa, lakini pia maslahi ya binadamu yanalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi, kulijitokeza jambo moja ambalo Mheshimiwa Waziri ambaye anashughulikia Mazingira na kwa sababu hili suala ni la kimazingira nalazimika kumuuliza kusudi aweze kutupa maelezo ya kina. Kumekuzungumzwa hapa issue hapa baadhi ya Watanzania maskini ambao wanaishi kwa kutegemea nishati ya mkaa kwa ajili ya kuweza kupika na kutengeneza vitu vingine ambavyo vinawasaidia kwenye maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali kama Serikali inaona ni halali kuwaambia kwamba watu waache kukata mkaa, nafahamu concern ya suala la utunzaji wa mazingira, ni jambo la msingi sana. Hata hivyo, binadamu pamoja na mimea tunategemeana, ni lazima mimea ipo kwa ajili yetu na sisi binadamu tupo kwa ajili ya mimea, hatuvezi tukasema kwamba, tunalinda mimea halafu tuhatarishe usalama wa wananchi ambao wanategemea mimea hiyo. Mimea itutunze na sisi tuitunze, sasa kuna mambo matatu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nafikiri Serikali mlikuwa mnapaswa moja m-encourage suala la upandaji wa miti na mki-encourage suala la kupanda miti pia ndiyo mtawezesha wananchi waweze kukata miti, kata miti panda miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kama mnataka wananchi hao wasiweze kukata miti wakatengeneza mkaa kwa ajili ya maisha yao, mnapaswa mhakikishe mmepeleka nishati mbadala kama vile matumizi ya gesi pamoja na umeme mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba commitment ya Serikali, bado pengine mafikiria kwamba wananchi hawa muwazuie wasikate mkaa ili wakaweza kupika chakula na wakatumia kwa matumizi mengine kwa ajili ya sustainability yao, eti kwamba wanaharibu mazingira, nini msimamo wa Serikali kuhusiana na suala la kuhakikisha kwamba pengine wanapeleka nishati mbadala kabla ya kuwazuia watu hawa kama ilivyotamkwa hapa asubuhi....

MWENYEKITI: Kwa hiyo, hoja yako Mheshimiwa Machali ni kwamba...

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sikupata majibu nakusudia kutoa shilingi kama sikupata ufanuzi.

MWENYEKITI: Hoja yako ni kwamba, mkaa uendelee kukatwa kama kazi enhe?

MHE. MOSES J. MACHALI: Ukatwe mkaa lakini kuwe na control ya Serikali. Serikali i-take control, lakini isiwaumize wananchi hawa, tunaomba commitment ya Serikali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Machali kwa swali hili zuri ambalo kimsingi linawagusa Watanzania wengi. Labda tu kwa wasiofahamu kwa sasa hivi, kila mwaka tunapoteza hektaa 400,000 za misitu zinatketea kwa shughuli kama alizozitaja za mkaa. Kwa hiyo, hali ni mbaya na

hii ndiyo inayoleta mabadiliko ya tabianchi ambayo ni mabadiliko ya mifumo ya hali ya hewa katika uso wa dunia na hii inasababisha majanga makubwa ya mafuriko ambayo tumekuwa tukishuhudia, jua kali na ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi kama msimamizi wa Sekta ya Mazingira, ningependa kabisa mkaa usitumike hata chembe. Kwa utafiti tuliofanya sisi wanaotumia mkaa siyo wananchi waishio vijijini, wananchi waishio vijijini wanatumia kuni, wanatumia yale majani yaliyoanguka ndiyo wanapikia. Mkaa unatumika na wale wanaoishi kwenye miji, kwenye mikusanyiko ya watu wengi, maeneo ambayo kuna umeme, ndiyo maana asubuhi, nilimsifu yule kiongozi wa kule Kibondo ambaye aliongeza ushuru, lakini Serikali haijapiga marufuku kuhusu utengenezaji wa mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichosifu sisi ni zile hatua ambazo zimeongeza ushuru, ili sasa mwananchi achague ajue kwamba kuna nishati nyininge ambayo ni nafuu kuliko ile ya mkaa. Kwa mfano majiko banifu, majiko banifu ni shilingi 25,000. Tulikwenda pale Lake Tanganyika kwenye Kambi ya Magereza, wanatumia kuni mbili kupikia chakula cha watu wa Magereza kwa sababu ya majiko banifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo tunahamasisha, watu waende kule na yale majiko banifu madogo yanauzwa sh. 25,000 ambayo mtu ye yeyote anaweza akanunua na akaweza kulitumia na hivyo akahifadhi uharibifu wa misitu. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Machali tukubaliane tu kwamba, tunataka hii misitu hata vizazi vijavyo viweze kuitumia kwa sababu ni rasilimali yetu wote.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali hili nalo ni la kuvutana kweli? Haya, Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti...

(Hapa Waheshimiwa walikuwa wanamrushia
maneno mzungumzaji)

MHE. MOSES J. MACHALI: Nyie kaeni kimya sikilizeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, concern yangu ni moja, sina tatizo na mtazamo wa Serikali, sina tatizo kabisa. Kwa mfano, anasema kwamba kuna *alternative solution* mfano, anarejea amekwenda kwenye gerezani fulani amekuta wanatumia kuni mbili kupika chakula, concern hii ni concern mbadala, kama ambavyo nilisema kwamba wapeleke gesi, umeme mijini na vijijini ili kuweza kuondokana na suala hili la ukataji wa miti ambao ni mkubwa.

Sasa naomba *commitment* ya Serikali kuhusiana na suala la kupeleka elimu hii ya matumizi ya majiko ambayo ni mbadala, kwa sababu kwenye bajeti yenu sijaona, pamoja na kuwa mnayajua haya kwamba yanaweza yakasaidia kuepusha watu kwenda kukata miti, sioni kitu hiki kama kwenye bajeti yenu mmetenga pesa na wakati huo huo bado mnaruhusu watu wengine wanaendelea kutaka magogo wanakwenda kuuza, watu wa mkaa mnaruhusu kwamba watozwe ushuru mkubwa, maskini wa kule kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati huu ambao bado mnategemea kuweza kupeleka elimu hiyo mji-commit hapa, hawa wananchi mnawasaidiaje ili kuweza kuondoka na ushuru mkubwa ambao wanatozwa, kwa sababu nyie hamjatimiza wajibu wenu, Serikali hamjatizima wajibu katika hili, nini kauli ya Serikali kuhusiana na mambo haya mawili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo, tupate ufanuzi wa Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nashukuru kwa uliyoyasema Waziri atajibu, lakini tuseme tu ukweli kwa kuvuna hekta 400,000 za mraba kila mwaka, kuna vijiji hata katika Jimbo langu, havina hata mti mmoja unaoweza kukata kwa ajili ya kutengeneza mkaa, maana mti wa mkaa lazima uwe na saizi Fulani. Viko vijijini vya namna hiyo, itafika wakati watu watapikia kinyesi cha mifugo, mazao mazao haya wakishavuna, mwaka huu mvua haikunyesha hata hayo mazao hakuna. Kwa hiyo, tutake tuisitake, lazima tuende kwenye hizi njia za kisasa hizi. Mheshimiwa Waziri utamalizia.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Machali kwamba elimu tumekwishaanza kutoa na ndiyo maana Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa ripoti ya mazingira katika nchi yetu ambayo ilitakiwa itolewe kila miaka miwili. Mle ndani tumeainisha kila sekta jinsi uharibifu ulivyo, chanzo cha uharibifu na hatua zilizochukuliwa na ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kudhibiti uharibifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasambaza hizi documents kwa sekta zote ikiwemo viongozi wetu wa TAMISEMI na tuna hakika kwamba itatumika, watatusaidia kuieneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuhusu kwamba tutoe tamko hapa kwamba tuwasaidie kule wananchi, hilo halitawezekana. Ninachowea kuwashauri, wale wananchi wanaoishi kwenye sehemu za miji waende kutumia nishati mbadala na sasa hivi Serikali imefanya mambo mazuri sana, imeamua kushusha gharama za kuingiza umeme mpaka 27,000 ambako umeme unapita, nadhani hizi fursa tuzitumie, kuna majiko mbadala na haitakuwa rahisi turuhusu kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – Finance and Accounts Shs. 414,648,000/=

Kif. 1003 – Policy and Planning Division Shs. 695,263,000/=

Kif. 1004 – Government Communication

Unit Shs. 219,283,000/=

Kif. 1005 – Internal Audit Unit Shs. 231,731,000/=

Kif. 1006 – Procurement Management

Unit Shs. 278,314,000/=

Kif. 1007 – Information and Communication

Tech. Unit Shs. 230,520,000/=

(Vifungu vilivytajwa hapo juu vilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1008 – Legal Services Unit Shs. 192,326,000/=

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi tu kwamba, msomaji, anatusomea kwa mfano milioni mia mbili thelathini nne, mia saba tisini na moja, ni mia saba tisini na moja elfu, kwa hiyo, kwa zote hizi amekuwa akiacha hiyo elfu, ambapo kwenye hansard itasomeka tofauti.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu tu...

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo kwenye kifungu hiki cha 1008, kifungu kidogo cha 208000, *Training Domestic tumeona hakikutengewa pesa kabisa na huku kunahusiana na*

MWENYEKITI: Rudia kidogo ishirini na mbili ngapi?

MHE. ESTER A. BULAYA: 220800...

MWENYEKITI: Ndiyo, endelea!

MHE. ESTER A. BULAYA: Na hapa pia pana husiana na masuala ya kisheria na kama unavyoja hata kwenye taarifa yetu tumezungumzia kuhusiana na elimu kwa umma na tunaona ni jinsi gani sheria ambayo zinavunjwa, sasa sijui wametumia vigezo vipi katika kupanga hapa. Nataka maelezo...

MWENYEKITI: Umeeleweka Mheshimiwa. Kifungu hicho kina sufuri, ufanuzi tu.

NAIBU WAZIRI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kiko hivyo kwa sababu ya ukomo wa bajeti.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – Union Secretariat...Shs. 23,110,653,000/=

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba atufafanulie kwenye 220600 ambapo miaka ya nyuma ilitengewa milioni 18, mwaka jana 2,000,000/= na safari hii 800,000 hizo Clothing, Bedding ni namna gani, hebu atufafanulie tufahamu, katika hii Sekretarieti ya Muungano.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahusu sare za wafanyakazi na wafanyakazi hawa huwa wanapewa sare karibu kila mwaka, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti mwaka tumeweka kiasi hicho.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 5001 – Environment...Shs. 5,686,766,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo peke yako!

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka ufanuzi katika kasma namba 270800, *current grant to non-financial public units* ambapo hapo nafikiri ni sehemu NEMC ilipo ambapo bajeti ya mwaka huu imepungua karibuni kulinganisha na bajeti ya mwaka jana karibu milioni 178.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikiangalia changamoto ya nchi yetu sasa hivi katika suala zima la NEMC inatakiwa ipewe nguvu, lakini pesa zimezidi kupungua, tukiangalia kwamba

viwanda vinajengwa, uwekezaji unaendelea, taarifa zinatakiwa, NEMC wanatakiwa wafanye kazi, pesa zinapungua. Kwa nini tunafikia maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni ukomo wa bajeti na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakitusaidia kupata bajeti ya kutosha.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 31 – OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Kif. 1001 – Administration and Human Resources
Management DivisionShs. 1, 100,000,000/=

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimamia kifungu sub-vote 6309, ujenzi wa ofisi pamoja na makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais. Mwaka 2013/2014 ilipangiwa sh. 211,124,487; mwaka 2014/2015 bajeti yake ilikuwa ni sh. 400,000,000 mwaka huu inaombewa tena 300,000,000.

Nataka kujua, jumla imekuwa milioni 911,124,487. Wakandarasi walikuwa wameshalipwa mpaka mwaka 2014/2015, tayari jengo lilikuwa limemalizika, yalikuwa bado matengenezo madogo madogo na hili nilishuhudia kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii na tulikwenda kuliangalia jengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachonishangaza hizi sh. 300,000,000 zinazoombwa sasa hivi ni kwa ajili gani au kidogo kunaanza kuwekwa fedha kwa ajili ya uchaguzi mkuu kwa ajili ya kuwafidia Wanamaskani? Naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ufanuzi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rukia wala asiwe na wasiwasi wa kuwa na pesa ya kuwapa Wanamaskani kwa uchaguzi. Wanamaskani ni wazalendo wanajua wajibu wao na watapiga kura kwa CCM. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinawekwa majengo yale ni kweli kwamba, kwa kiasi kikubwa yamemalizika, kulikuwa na matengenezo madogo madogo, lakini baada ya majengo kumalizika, kuna pesa ambayo tunaizua mpaka tuhakikishe Mkandarasi amefanya matengenezo yaliyobakia. Baada ya matengenezo yale, pesa ile ni lazima itoke. Kwa hiyo, tumeomba kulipa malipo ya mwisho kwa Mkandarasi kwa majengo mawili, Luthuli pamoja na Tunguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – Policy and Planning Division... ...Shs. 780,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 5001 – Environment Shs. 2, 638,847,000/=

MWENYEKITI: Watu wawili, Mheshimiwa Mnyaa na Mheshimiwa Jafo. Tuanze na Mheshimiwa Jafo! Hapana watatu na Mheshimiwa Pamba. Basi, ataanza Jafo kwanza halafu Mnyaa, halafu Pamba.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo, katika kifungu kidogo 6506 *lower Kihansi Environmental Management Project*, ambapo mwaka huu hawakutenga pesa, lakini nikijua kwamba Kihansi ndiyo sehemu ambapo vyura ambao wengine walisafiri kupelekwa nje ya nchi, wanaishi pale.

Sasa kama katika suala zima la kimazingira pale kuna viumbe lakini mwaka huu wote wa fedha hakuna pesa yoyote iliyotengwa hapa. Je, program ya mazingira tunaiwekaje? Nikisema hivyo na-declare interest, ni Katibu wa Chama cha TAPAC, tunaangalia suala zima la mazingira katika Bunge letu. Sasa nataka nataka nipate ufanuzi hapa jinsi gani wale vyura wa Kihansi tunaweza kuwa-manage kama hatukuweka fungu la bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ufanuzi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mazingira kuhusu vyura vya Kihansi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Jafo. Vipaumbele tunavyo vingi na safari hii tuliamua tutekeleze ambavyo tumeviainisha kulingana na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo safari hii chura siyo kipaumbele bwana. (Kicheko)

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye subvote 50301, *climate change*, hizi milioni 500 nataka kufahamu hili suala hata Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira alikuwa anasema Zanzibar itengewe Fungu lake maalum kwa sababu hatuzijui sasa pesa za mazingira, ile kasma iliyotengewa Zanzibar na akaomba na Mheshimiwa Waziri akajibu itafikiriwa maagizo ya Kamati kutengewa fungu lake.

Sasa hizi pesa kama zimetengwa hivi, sasa tutajuaje asilimia zinazokwenda Zanzibar ni zippi, ni amount gani ili tujuje kwamba, katika mambo ya mazingira kiasi kadhaa kwa mwaka huu kimetengwa kwa fedha ambazo zitakwenda Zanzibar?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani anataka kuelezea hii miradi ya *climate change*, tunayo miradi ambayo inatekelezwa mpaka Zanzibar na kwenye randama hii miradi ipo. Huu mradi unahusisha vile vile kujenga ukuta Pangani, kujenga Zanzibar, pale Ocean Road na pale Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya fedha za miradi hii ni milioni nne US Dollars. Tayari sasa hivi Wakandarasi wameshapatikana, mkataba ulisainiwa mwezi wa Kwanza tarehe 29, mradi unatekelezwa kati ya Januari 2015 na utakamilika mwezi wa Saba, 2017. Sasa hivi mradi unasimamiwa na UNOPS - United Nations Office Program Services ambao tayari wanafanya feasibility studies.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalijibu pamoja na Mheshimiwa Pamba, Mbunge wa Pangani, swali lake litakuwa ni hilo hilo tu, kwamba, tayari anafanya feasibility study na itakamilika mwezi wa Sita. Baada ya hapo tunautangaza mradi kwa ajili ya kupata upembuzi yakinifu mwezi wa Saba pamoja na kumpata Mkandarasi mwezi wa Nane. Tunategemea miradi hii yote itaanza mwaka huu kabla ya kwenda kwenye uchaguzi. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pamba swali lako limejibiwa kabla hata hujauliza. Mheshimiwa Pamba! (Kicheko)

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni suala ambalo lilikuwa linatukera sana, lakini wananchi wa Pangani wamepata faraja.

Kwa misingi hiyo, tunaomba kazi hii ifanyike haraka sana kwa sababu tumeshapoteza zaidi ya miaka mitatu kwa program hii. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali kwamba kazi hii sasa itaanza. Kwa hiyo, hoja yangu ilikuwa hiyo. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)
(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja taarifa!

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia makadirio ya matumizi ya Fedha za Ofisi ya Makamu wa Rais Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

*Makadirio ya Matumizi ya Ofisi wa Rais (Mazingira na Muungano) kwa Mwaka wa Fedha
2015/2016 yalipitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu naomba niwashukuru sana na niwatakie kila la heri Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha unaokuja. Nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkifanya katika mazingira magumu.

Tumejifunza kwamba fedha mnazopata ni kidogo lakini pamoja na mazingira hayo bado mnaendelea kuchapa kazi. Tunawaombea mfanye kazi bora zaidi kwa mwaka unaokuja.

Sasa matangazo; kuna tangazo la wageni ambaa wametoka *Our Hopeful Promotion Dar es Salaam*, karibuni sana. Ni Ndugu Mayor Adili, Kaimu Mratibu; Karista Mwanda Meneja wa Promotion na Ndugu Razidi Katundu Afisa Mahusiano. Karibuni sana. (Makofi)

Mwisho, kuna Tangazo la Kamati ya PAC linatangazwa na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Ismail Rage, anawaomba Kamati ya PAC baada ya Kikao hiki mwende Dodoma Hotel ambako mtakutana na Wataalam wa Controller and Auditor General. Baada ya Kikao hiki mnaombwa PAC mwelekee Dodoma Hotel.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana kwa jinsi ambavyo leo mmefanya kazi kubwa toka asubuhi lakini tunashukuru kwamba yale yote yaliyopangwa kufanyika yamekamilika. Kwa hiyo basi, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 1.50 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 20 Mei, 2015 Saa Tatu Asubuhi)